**7 FEBRUARI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

**Kikao cha Tisa – Tarehe 7 Februari, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**SPIKA:** Hati za kuwasilisha Mezani, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Kwa niaba yake Mheshimiwa Asia Halamga.

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**MHE. ASIA A. HALAMGA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 138

### Hitaji la Gari la Mkuu wa Wilaya ya Tarime

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka Gari la Mkuu wa Wilaya ya Tarime?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali ilitenga na kuidhinisha shilingi Milioni 504.7 kwa ajili ya ununuzi wa magari mawili aina ya *Toyota Land Cruiser Prado* kwa ajili ya Wakuu wa Wilaya ya Tarime na Musoma.

Mheshimiwa Spika, taratibu za malipo kwa ajili ya ununuzi wa magari hayo zimefanyika Januari, 2025 kupitia kwa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini *(GPSA)* na hatua za manunuzi zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuyapata magari hayo likiwemo gari la Mkuu wa Wilaya ya Tarime ndani ya mwaka huu wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, hata hivyo, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Tarime Vijijini ina Idara Tisa. Idara zenye magari ni mbili tu: Idara ya Miundombinu, Kilimo na Mifugo, Utawala, Maendeleo ya Jamii; lakini Mkaguzi wa Ndani, Sheria na TEHAMA hawana magari, na vitengo vyote havina magari. Je, ni nini utaratibu wa Serikali kuwawezesha watumishi hawa wa Serikali katika Halmashauri ya Tarime pia na nchi nzima ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi na wanapotakiwa kufika kwa wananchi wafike kwa wakati, watatue changamoto za wananchi wetu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kununua magari kwa ajili ya usimamizi, usambazaji na ufuatiliaji katika halmashauri zetu kote nchini. Katika mwaka wa fedha uliopita Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan alipeleka magari ya usimamizi wa huduma za afya katika Halmashauri zote 184, ikiwemo Halmashari ya Wilaya ya Tarime na magari ya Idara na Vitengo vingine yameendelea kupelekwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwanza, magari yanayokuwa kwenye idara moja au kitengo kimoja pia yanaweza kutumiwa na idara nyingine. Tunafanya kazi kwa ushirikiano ndani ya Halmashauri. Vile vitengo ambavyo havina magari, Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa awamu kwa ajili ya kupeleka magari ili usimamizi uwe na ufanisi mkubwa zaidi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, sasa aulize swali lake.

Na. 139

**Kutenga Dirisha la Mikopo kwa Wanaume**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatenga dirisha maalum la mikopo ya Wanaume waliovuka umri wa Kijana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, mikopo ya 10% inatolewa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 Kifungu cha 37A ya mwaka 2018 na Kanuni za usimamizi na utoaji wa mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu za mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria hii, mikopo ya 10% inatolewa kwa makundi maalum ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupata mikopo isiyo na riba. Makundi haya yana fursa ndogo ya kupata mikopo katika taasisi nyingine za fedha kwa kuwa yanakosa dhamana na uwezo mdogo wa kumudu riba.

Mheshimiwa Spika, aidha, umri wa ukomo katika mikopo kwa vijana umeongezwa kutoka miaka 35 hadi 45.

Mheshimiwa Spika, makundi mengine ambayo siyo walengwa wa mikopo hii wanashauriwa kupata mikopo kupitia taasisi nyingine za fedha, biashara na programu za kijasiriamali zinazohusisha makundi yote, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli kusema mikopo imeongezeka kutoka miaka 35 mpaka miaka 45 hilo nilikuwa silijui. Sasa kwa sababu imeongezeka, na huko vijijini wanasema umri wa vijana ni miaka 18 mpaka 30, je, ni lini sasa Serikali itatoa mwongozo kwa Halmashauri za Wilaya ili hawa watu wapate fursa ya kukopa, kwa sababu kuna *gap* kubwa kati ya watu 30 mpaka 35?

Mheshimiwa Spika, sasa tungependa kujua kama Serikali inaweza kuongeza hilo suala la kutoka miaka 30 hadi miaka 45. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali itoe mwongozo kwa Halmashauri za Wilaya ili suala hili liweze kutekelezeka kwa vijana, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa kanuni za mikopo ya 10% za mwaka 2024, miongozo tayari imeshatolewa na kupelekwa kwenye Halmashauri zote 184. Tangu mikopo imeanza kutolewa vijana wote wenye umri kati ya miaka 18 mpaka miaka 45 wanapewa mikopo.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuendelea kuwasisitiza Wakurugenzi wa Halmashauri kote nchini kuhakikisha wanaendelea kutoa elimu kwamba umri wa vijana umeongezeka kutoka kikomo cha miaka 35 mpaka kikomo cha miaka 45 ili wanufaika waongezeke na kupata hiyo fursa ambayo ipo kwa ajili yao, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, kundi la akina mama waliozaa watoto wenye ulemavu wamekuwa wakipata shida sana kuwalea, na kwa kuwa hawakopesheki kwa akina mama na wala hawakopesheki kwenye kundi la watu wenye ulemavu, je, ni lini Serikali itaona

umuhimu kwa hawa akina mama waliozaa watoto wenye ulemavu, waweze kuwekewa kifungu maalum ili wakopesheke japo kwenye kikundi cha walemavu, kwa sababu wengi wao wanaume wamewakimbia kwa sababu ya kuzaa watoto wenye ulemavu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, aakina mama ambao wanalea watoto wenye ulemavu, kwanza wanazo sifa ya kujiunga na vikundi vingine vya wanawake ili kupata ile mikopo ya 10%.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwanza tunawashauri hawa akina mama wajiunge na makundi mengine ya wanawake yaliyopo katika maeneo yao ili waweze kunufaika na mikopo ya 10%.

Mheshimiwa Spika, pili, tutaendelea kuona namna nzuri ya kuboresha mfumo na kuwapa zaidi kipaumbele wale ambao wanalea watoto au watu wenye ulemavu, ambapo walemavu wenyewe wasingeweza kufanya biashara, lakini walezi wanaweza kufanya biashara. Serikali imeendelea kuwapa kipaumbele katika mikopo ili waweze kutoa huduma hiyo ipasavyo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul, swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa mwongozo uliotolewa sasa hivi, Wenyeviti wa Vijiji na Madiwani hawaruhusiwi kushiriki katika zile Kamati za kutambua vile vikundi vinavyokopeshwa.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini hawa viongozi wametolewa wakati ndio wanaowafahamu hawa wananchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, katika muundo wa sasa wa mikopo ya 10%, kuna Kamati za Watalaam ambazo zinahusika na mikopo hiyo ngazi ya Kata na ngazi ya Wilaya, lakini viongozi ambao ni wanasiasa katika maeneo hayo nao wanahusika kwa namna moja au nyingine, hawako kwenye zile Kamati moja kwa moja, lakini wanahusika kuhamasisha, wanahusika pia kufuatilia vikundi kama vimepata mikopo? Pia wanahusika kufuatilia urejeshaji wa mikopo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, siyo kwamba wametolewa, ni utaratibu ulioboreshwa lakini wanaendelea kuhusika kuhakikisha kwamba vikundi vile vinanufaika na mikopo lakini marejesho yanarejeshwa kwa kadri ya utaratibu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki sasa aulize swali lake.

Na. 140

**Kukamilisha Nyumba za Walimu na Waganga Mkalama**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha maboma ya nyumba za Walimu na Waganga ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi – Mkalama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama ina jumla ya maboma 54 ya nyumba za watumishi wa Elimu na Afya

ambayo yanahitaji ukamilishaji. Kati ya maboma hayo, maboma ya nyumba za watumishi wa afya ni nane na elimu ni 46.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri imeendelea kutenga fedha za kukamilisha maboma ya nyumba za watumishi kupitia mapato ya ndani ambapo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2023/2024 jumla ya maboma sita ya nyumba za waganga katika zahanati za Endasiku, Mgimba na Kinankamba pamoja na nyumba za walimu katika shule za Ishenga, Kinyangiri na Mbigigi zimekamilishwa kwa gharama ya shilingi milioni 113.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mwaka wa fedha wa 2025/2026 Halmashauri inatarajia kutenga shilingi milioni 100 ajili ya ukamilishaji wa nyumba mbili *(three in one)* za watumishi wa Afya.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya nyumba za watumishi katika Sekta ya Afya na Elimu kwa awamu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali ambayo yanatia moyo, lakini ufanisi wake utakuwa mdogo, ukizingatia kwamba Halmashauri zetu hazifanani kwa mapato. Halmashauri yangu ya Mkalama ni Halmashauri mpya, mapato yake ni kidogo sana. Magofu haya ambayo wananchi wamejenga hizi nyumba kwa gharama zao za kilimo ni mengi. Je, Serikali haioni kwamba sasa majibu haya ya kusukumia Halmashauri, yanazidi kuchelewesha na zile nguvu za wananchi zinapotea?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa iweke bajeti maalum kwa ajili ya kumalizia magofu haya ili wananchi waweze kupata huduma stahiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Francis Isack Mtinga kwa swali lake zuri kabisa linalolenga kuhakikisha miundombinu mizuri na nyumba zinapatikana kwa ajili ya watumishi wetu katika kada ya afya na Elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hoja yake ni ya msingi na ndiyo maana Serikali kupitia Wizara ya Fedha imetoa tamko kwamba, hivi karibuni tutapokea fedha kwa ajili ya kwenda kukamilisha baadhi ya maboma ambayo yameanzishwa kujengwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hizi fedha zitakazotoka Wizara ya Fedha zinalenga pia kugusa ukamilishaji wa miundombinu ya nyumba kwa ajili ya watumishi wetu kwenye kada ya afya na elimu. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge akae kwa mikono ya kupokea kwa maana Serikali italeta fedha kuongeza nguvu katika ujenzi wa hii miundombinu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeahidi kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma, je, Mkoa wa Shinyanga pia utakuwa miongoni mwa mikoa hiyo itakayopata fedha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mnzava kwa kupambania sana maslahi ya Mkoa wake wa Shinyanga. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inadhamiria kugusa siyo tu Mkoa wa Shinyanga bali mikoa yote ya Tanzania Bara kwa ajili ya kuhakikisha inakuja kuunga mkono jitihada za wananchi walioanzisha ujenzi wa miundombinu mbalimbali iliyofikia katika

ngazi ya maboma, kwa kuongeza nguvu ili kukamilisha maboma haya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali kwa kifupi.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza nyumba za watumishi katika Hospitali ya Mji wa Nanyamba, ambapo kwa sasa kuna nyumba moja tu ya mtumishi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Chikota kwa maana amekuwa akifanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kuhakikisha kwamba watumishi wanapata mazingira bora ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inatambua umuhimu wa watumishi kuwa na mazingira mazuri ya kufanyia kazi na ndiyo maana Serikali imeanza kujenga nyumba za watumishi mbalimbali kwenye kada ya afya na elimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na jitihada hizo ili kutengeneza miundombinu itakayotosheleza watumishi wetu kufanya kazi na kuwa na mazingira mazuri ya kuishi na kufanya kazi katika mazingira bora zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu naona swali langu ni kama ameshalijibu, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, sasa aulize swali lake.

Na. 141

**Ujenzi wa Miundombinu ya Shule Shikizi za Msingi – Kilolo**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa miundombinu ya Shule Shikizi za Msingi zilizoanzishwa kwa nguvu za Wananchi – Kilolo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo ina jumla vituo shikizi 18 vilivyoanzishwa kwa nguvu za wananchi ambavyo ni Kichangani, Msombwe, Mlewela, Madizini, Igingilanyi, Mabondwa, Kware, Mapangali, Muungano, Lugolofu, Ilangamoto, Ubandusi, Barabarambili, Kidumka, Lulindi, Kitemela, Kisanzala na Masimike.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024/2025, Serikali ilipeleka shilingi milioni 701 kwa ajili ya ujenzi wa shule mbili mpya za mkondo mmoja katika vituo shikizi vya Kichangani na Msombwe. Ujenzi wa shule hizi upo hatua ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha za kukamilisha ujenzi wa miundombinu katika vituo shikizi vilivyoanzishwa kwa nguvu za wananchi kadri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, pia napenda kuishukuru Serikali kwa kuleta fedha za kujenga shule mbili, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Pamoja na shule shikizi, lakini ziko shule chakavu ambazo zimejengwa miaka mingi iliyopita kama Shule ya Msingi ya Idete, Shule ya Msingi Boma la Ng'ombe na Shule ya Msingi ya Ilole, hali zake ni mbaya sana. Je, Serikali ina mpango gani maalum wa kupeleka fedha ili shule zile ziweze kukarabatiwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Shule shikizi mojawapo ya Lugolofu ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameitaja hapo, wananchi wameikamilisha, wamejenga madarasa mawili na vyoo, na watoto wanatembea kilomita 20 kufika shuleni. Je, Serikali iko tayari kupeleka walimu haraka ili wale watoto wadogo wa Darasa la Kwanza na la Pili, waanze kusoma pale na kuepuka usumbufu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Justin Nyamoga kwa kuendelea kupaza sauti kwa ajili ya wapiga kura wake wa Jimbo la Kilolo.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Serikali imetenga fedha katika mwaka huu wa bajeti kwa ajili ya kufikia shule ambazo zimechakaa na miundombinu yake inahitaji kuboreshwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakaa mimi naye, nafahamu tayari alishaleta maombi, nitamweleza mchakato umefikia hatua gani?

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Mbunge awaambie wapigakura wake wa Kilolo kwamba, Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ipo tayari kwa ajili ya kuhakikisha inaboresha miundombinu hii muhimu katika shule hizi alizozitaja.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na uhitaji wa walimu naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari Serikali imetangaza ajira za walimu 10,015 na michakato ya usahili inaendelea. Walioomba wanafanyiwa usahili, watapatikana

walimu watakaopangwa katika maeneo tofauti tofauti kwa ajili ya kwenda kuanza kufundisha. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutazingatia maombi aliyoyatoa ili kwenye hizo shule alizozitaja ziweze kupata walimu wa kuwafundisha wanafunzi wetu.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Prof. Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Katika Jimbo la Moshi Vijijini, shule nyingi za msingi zilizojengwa kabla ya uhuru na mara baada ya uhuru zimechakaa sana. Naomba aniambie Serikali ina mpango gani wa kuzikarabati shule hizi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Prof. Ndakidemi kwa kazi nzuri ya kuwasemea wananchi wake na kuwapambania katika changamoto zao. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali katika mwaka huu wa fedha imetanga fedha kwa ajili ya ukarabati wa shule chakavu.

Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuzifikia shule alizozitaja kwa ajili ya ukarabati ili wanafunzi wapate mazingira mazuri ya kusomea na walimu wapate mazingira mazuri ya kufundishia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni haja ya kupeleka shule ya mkondo mmoja katika Kijiji cha Maweni ili kupunguza msongamano uliopo katika Shule ya Msingi Ng'oboko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Leah Komanya kwa kupaza sauti yake kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wananchi katika jimbo lake wanapata elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatekeleza mradi wa *BOOST* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inapunguza msongamano katika shule za msingi ambazo zina wanafunzi waliozidi, na pia inapunguza umbali mrefu wa wanafunzi kufika shule.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mbunge kwamba, Serikali inatambua uhitaji alioueleza na Serikali itaendelea kufika katika maeneo mbalimbali, ikiwemo katika jimbo lake kwa ajili ya kujenga shule hizi ili kupunguza msongamano.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Serikali imetenga fedha kwa ajili ya shule chakavu na shule kongwe, nami kwenye Jimbo langu kuna Shule ya Mchinga moja, hii ni shule ya tangu mwaka 1948 na imechakaa sana. Je, ipo miongoni mwa hizo fedha zilizotengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Salma Kikwete, kwa kweli amekuwa akifuatilia sana ili kuhakikisha kwamba wapigakura wake wanapata elimu iliyo bora kwa kuwa amekuwa akiwasemea changamoto zao katika sekta hii muhimu ya elimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake, naomba nimhakikishie kwamba, ni dhamira ya Serikali kufikia shule chakavu na kuweza kuzikarabati ili ziwe na mazingira mazuri kwa ajili ya wanafunzi kusomea na walimu kufundishia.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mimi naye tutakaa, tutazungumza, tutapanga, lakini lengo ni kufikia shule hizi zinazotajwa ambazo ni chakavu ili ziweze kuboreshwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya waheshimiwa Wabunge. Tunaelekea na Wizara ya Nishati.

Waheshimiwa Wabunge, tulishatoa katazo humu ndani la kuzungumza na simu ukiwa Bungeni. Milango iko mingi, kama ni lazima uzungumze, huwezi kuandika ujumbe, nenda nje ukazungumze na simu. Wewe ni Mheshimiwa, wewe kwanza liheshimu Bunge.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu sasa aulize swali lake.

Na. 142

**Kushusha bei ya umeme Kata za Mangaka na Kilimanihewa Nanyumbu**

**MHE. ALLY Y. MHATA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itashusha bei ya kuunganisha umeme katika Kata za Mangaka na Kilimanihewa kama maombi yalivyowasilishwa Wizarani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali halisi ilivyo nchini, kuna maeneo ya vijiji na vijiji miji ambapo maeneo ya vijiji yanaunganishwa umeme kwa gharama ya shilingi 27,000/= na maeneo yenye sura ya vijiji miji, yanaunganishwa kwa gharama ya shilingi 320,960/=. Kwa maeneo ya Kata ya Mangaka na Kilimahewa yenye sura ya vijiji miji yanaunganishiwa umeme kwa gharama ya shilingi 320,960/=. Serikali inaendelea kuangalia kama kuna uwezekano wa kufanya maboresho kutokana na tathmini iliyofanyika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Yahya Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY Y. MHATA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, maeneo ya Kata hii ya Mangaka, yote yana sura ya vijiji na siyo vijiji mji.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kufuatana nami akaone hali halisi ya kata zangu ili maamuzi haya yafanyike kwa haraka iwezekanavyo kwa sababu wananchi wana hamu sana ya kupata umeme huu?

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya yangu tunavyo vitongoji 105 ambavyo mpaka sasa hivi havijapata umeme. Je, Waziri anatoa kauli gani kuhusu vitongoji hivi 105, kwamba ni lini vitapata umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa maswali mazuri ya Mheshimiwa Mbunge, na ninaomba niyajibu kwa Pamoja kwamba, kuhusu kuambatana na Mheshimiwa Mbunge, nitafurahi kwenda kwenye Jimbo la Nanyumbu na Mheshimiwa Mbunge ili tukayaangalie maeneo hayo. Kwa hiyo, nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya Bunge tutajipanga kwa ajili ya ziara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na vitongoji 105 ambavyo havina umeme, kwa sasa Serikali ina miradi ambayo inaendelea

ikiwemo vitongoji 15 vya Mbunge. Hata hivyo, kwa mradi ambao tutauanza mwaka huu wa fedha, tutaongea vitongoji vingine 38 ili kupunguza idadi hii ya vitongoji 105 ambayo imebakia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni dhamira ya Serikali kuhakikisha tunaendelea kupeleka umeme kwenye vitongoji, na tumejipanga hivyo hata kwa mwaka huu wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuishukuru Serikali kwa kutujengea kituo cha kupozea umeme Wilayani Urambo eneo la Uhuru, je, ni lini kituo cha kupozea umeme kitaanza kufanya kazi ili tuachane na tatizo la umeme tulilonalo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, Kituo hiki cha Kupooza Umeme cha Uhuru katika jimbo la Mheshimiwa Mbunge tayari kimeshakamilika. Tunasubiri kukamilisha njia ya kusafirisha umeme ambayo ikikamilika ndipo kituo kitakapoanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, njia ya kusafirisha umeme tayari imefika asilimia nzuri. Wakandarasi kwa sasa wako *site* na wanafanya kazi hii kwa haraka sana ili kuhakikisha kwamba tunamaliza *transmission* line ili Kituo hiki cha Uhuru kianze kufanya kazi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Madini, Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda sasa aulize swali lake.

Na. 143

**Kupitia Upya Tozo kwenye Uchimbaji na Uchenjuaji wa Dhahabu**

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapitia upya tozo zilizopo kwenye mnyororo wa uchimbaji na uchenjuaji wa dhahabu zinazowaelemea wachimbaji wadogo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Madini, majibu.

**WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mkakati wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Nchini (MKUMBI) imefanya utafiti wa tozo 66 zinazotozwa na halmashauri katika shughuli za madini ikiwemo madini ya dhahabu. Tozo zilizobainika katika shughuli za uchimbaji na uchenjuaji wa dhahabu ni pamoja na ushuru wa karasha, ada ya ukaguzi, *VAT leaching,* Mialo, ushuru wa kusafirisha miamba ya madini na visusi (mabaki ya miamba baada ya kuchenjuliwa).

Mheshimiwa Spika, katika kutatua changamoto hizi Wizara iliitisha kikao mwezi Agosti, 2024 Mkoani Singida ambacho kilishirikisha Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Wizara ya Fedha; Tume ya Madini; *STAMICO*; Halmashauri za Wilaya za Ikungi, Chunya, Kahama, Msalala, Meatu, Shinyanga, Mtama na Lindi; *FEMATA;* na *TAWOMA*. Rasimu ya mapendekezo ya maboresho tayari imeshaandaliwa na ipo katika hatua ya kufanyiwa mapitio na tathmini, ambapo matokeo ya tathmini hiyo yatatusaidia katika kupanga tozo rafiki kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto za kikodi nchini, Mheshimiwa Rais ameunda Tume ya Maboresho ya Kodi ili ifanye tathmini ya mfumo wa kodi na kuleta mapendekezo ya namna ya kuboresha mfumo wa kodi. Ni imani yetu kuwa

maboresho hayo yataangazia changamoto za kikodi zinazoikabili Sekta ya Madini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, swali la nyongeza.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali kuhusu tozo nyingi ambazo zinaambatana na mnyororo wa uchenjuaji wa dhahabu. Nina maswali mawili ya nyongeza: -

(a) Je, kwa vile wachimbaji wadogo wameendelea kulipa fedha hizi na mirabaha mingi kwenye uchenjuaji huu wa dhahabu, hamwoni sasa ni wakati mwafaka kwa Wizara ya Madini na TAMISEMI kukaa mapema ili hizi rasimu zinazosemwa zikamilike mapema ili wananchi (wachimbaji wadogo) waweze kupata unafuu?

(b) Je, Wizara ya Madini hawaoni kwamba ni muda mwafaka sasa wa kwenda kwenye mazingira ambayo kuna uchimbaji wa madini kuwasaidia watu wenye leseni na maduara ambao wanaendelea kubisha kila siku namna ya kugawana baada ya kupata mali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa swali kwanza tayari tumeshakaa na wenzetu wa TAMISEMI katika hatua ya awali, na hivi sasa jambo hili liko katika ngazi ya Makatibu Wakuu, baada ya hapo litawasilishwa ili tuweze kulitolea maamuzi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili linalohusu wenye leseni na wenye maduara, naomba nitumie fursa hii kuliarifu Bunge lako kwamba katika utatuzi wa changamoto hii tumetunga kanuni ambayo hivi sasa inapitiwa na wadau, ambayo inalenga kuhakikisha kwamba mwenye leseni na wenye maduara waingie makubaliano ili kuepusha migogoro.

Mheshimiwa Spika, sheria inataka kila anayepewa leseni achimbe yeye, asipangishe. Ukikubali kumwingiza mchimbaji mdogo kwenye leseni yako, ni lazima pia uingie naye makubaliano, ambapo ndiyo kanuni hiyo inasema ili tuondoe migogoro hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 144

**Hitaji la Mahakama ya Wilaya – Momba**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Mahakama ya Wilaya Momba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania, imeendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa Mahakama kwa kuimarisha majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kujenga majengo mapya na kukarabati yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango huo, ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Momba utatekelezwa kwa bajeti ya mwaka 2024/2025. Kwa sasa mradi huo upo hatua ya mwisho ya manunuzi ya kupata mkandarasi wa ujenzi. Hivyo, ujenzi unatarajiwa kuanza ndani ya mwezi Februari, 2025, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza. Kwa kuwa mwezi huu ndiyo mwezi wa Pili sasa, na majibu yake yanaonesha kwamba ujenzi unaanza mwezi huu wa Pili, nataka kujua, je, wameshampata mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi huu?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Changamoto iliyopo Wilaya ya Momba ndiyo changamoto kubwa iliyopo Wilaya ya Ileje. Nataka kujua, Serikali mna mpango gani wa kujenga Mahakama nzuri na ya kisasa yenye hadhi ya wilaya ndani ya Wilaya ya Ileje?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kumhakikishia kama mkandarasi amepatikana, katika jibu la msingi nilisema wako katika hatua za mwisho za kumpata mkandarasi. Baada ya mkandarasi kupatikana, atakabidhiwa *site* na kwa mujibu wa Mahakama, mwezi huu ndiyo anatarajiwa kukabidhiwa *site*. Kwa hiyo, dada yangu Mheshimiwa Mbunge awe na uhakika kwamba litatekelezwa na vinginevyo mimi na yeye tutafuatilia ili kuona kwamba lengo hilo linafikiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwepo wa ujenzi wa Mahakama ya aina hiyo Ileje, kama nilivyowahi kusema katika nyakati tofauti, Mahakama ina mpango mkakati wa miaka mitano mitano. Katika mpango mkakati huu wa awali, Ileje haikuwemo, lakini katika mkakati unaofuata tunatarajia Wilaya ya Ileje itaingia, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Angelina Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Ilemela ilitenga kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo ya Sangabuye ili kuitoa katika lile eneo ambalo wana mwingiliano na Kituo cha Afya cha Sangabuye. Je,

ni lini sasa Mahakama itakwenda kujenga katika kiwanja walichotengewa ili kuwapa uhuru Kituo cha afya kipanuliwe? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri ya Ilemela, moja, kwa kuhakikisha kwamba kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama kinapatikana. Nami nashukuru kwa taarifa hiyo nzuri.

Mheshimiwa Spika, tutakachokifanya kwa sasa niitake Mahakama, hasa Mtendaji Mkuu wa Mahakama na wataalamu wake wafuatilie kuona kiwanja hicho ili wakimiliki, kwanza kiwe chini ya Mahakama, na baada ya hapo, kiingizwe katika mpango wa ujenzi wa Mahakama inayohitajika pale Ilemela, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Je, ni lini Mahakama ya Wilaya ya Uyui itajengwa, kwa sababu mchakato peke yake umechukua miezi sita?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika mwaka huu wa fedha ambao tunaendelea nao, Mahakama za Wilaya 18 zinatarajiwa kujengwa ikiwemo Mahakama ya Wilaya ya Uyui.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yetu kwamba, Mahakama itakamilisha mchakato wa manunuzi; na kwa uhakika wamenihakikishia kuwa mwezi huu wa pili michakato itakuwa imekamilika ili kuwakabidhi wakandarasi *site* waweze kuijenga.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutafuatilia ili kuona kwamba ahadi ya kujenga

Mahakama hiyo katika mwaka huu wa fedha inatekelezwa. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Eric J. Shigongo, Mbunge wa Buchosa, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Oliver Semuguruka.

Na. 145

**Kufufua Kiwanda cha Kuchambua Pamba cha Nyakarilo – Buchosa**

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA K.n.y. MHE. ERIC J. SHIGONGO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itafufua kiwanda cha kuchambua Pamba cha Nyakarilo, Buchosa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bodi ya Pamba *(TCB)* mwaka 2020 ilifanya tathmini juu ya hali ya viwanda vya kuchambua pamba nchini. Tathmini hiyo imewezesha ukarabati wa baadhi ya viwanda hivyo. Viwanda vilivyokuwa vinahitaji ukarabati mkubwa ni pamoja na kiwanda cha kuchambua pamba cha Nyakarilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Benki ya Kilimo ilianzisha utaratibu wa dirisha maalum la kuvikopesha viwanda husika. Baadhi ya viwanda vilivyopata mikopo, kukamilisha ukarabati na kuanza kufanya kazi ni pamoja na *Chato Cooperative Union,*

*Mbogwe Cooperative Union, Kahama Cooperative Union* na Sola. Kwa kutumia utaratibu huo, Serikali itahakikisha pia kiwanda cha Nyakarilo kinakarabatiwa ili kuongeza tija katika mnyororo mzima wa sekta ya pamba. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa majibu mazuri ya Jimbo la Buchosa. Sasa ninalo swali dogo la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani katika kuimarisha Kiwanda cha Maruku cha Chai kilichopo Bukoba Vijijini ambacho kinafanya kazi kwa kusuasua?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Oliver kwa swali zuri la Sekta ya Kilimo na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo ikiwemo chai.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda hiki cha *Kagera Tea Company* ambacho kiko Maruku ni moja ya viwanda katika sekta ya chai. Kama tunavyojua, sekta ya chai ina changamoto kidogo, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imeshaweka nia thabiti na mikakati ya kuhakikisha kwamba sekta ya chai inakua, kwanza kwa kuviwezesha na kuhakikisha kuwa viwanda vyote vya chai vinafanya kazi vizuri, pamoja na kuhakikisha kwamba tunapata soko kwa sababu changamoto iliyopo kwenye sekta ya chai ni soko linalosuasua.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kwenye vile viwanda ambavyo vina changamoto zaidi, tutakaa na wenye viwanda ili tuone namna ya kuwasaidia kwa sababu hivi viwanda ni vya sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutakuja pale Maruku tukae na huyu mwekezaji ili tuone namna ya kumsaidia pale ambapo ana

changamoto katika uchakataji wa chai katika Kampuni hii ya *Kagera Tea Company.*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wakulima wa Kata ya Doma, Msongozi na Mlali ni wakulima wakubwa sana wa zao la nyanya, je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kutafuta mwekezaji wa kujenga kiwanda kidogo cha kusindika nyanya ili kuokoa wakulima hawa kwa hasara wanayoipata ya kutafuta soko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nampongeza Mheshimiwa Jonas, ni kweli kama nilivyosema, lengo la Serikali ni kuona mazao yote ya kilimo yanaongezwa thamani ili kuongeza pato kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, moja ya maeneo ambayo tunaangalia ni hili la nyanya na maeneo mengine ya *horticulture*. Kwa hiyo, tutahakikisha katika eneo hilo nako tutatafuta wawekezaji ili tuweze kuwaleta waweze kuongeza thamani kwenye nyanya ambazo zinapotea *(postharvest losses),* nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba Kiwanda cha Chai cha Kilolo kinafufuliwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Grace kwa swali zuri. Kama nilivyojibu kwenye swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver, Sekta ya Chai ina changamoto, lakini mipango ya Serikali ni kuhakikisha tunakwamua sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, moja ya mikakati ambayo tumeiweka ni kuhakikisha wakulima wa chai Kilolo, kwanza wamewezeshwa. Hatua inayofuata ni kuwatafutia sasa sehemu ya kuongeza thamani na tunapeleka kwenye Kiwanda cha Mufindi *Tea Company* ambacho kitaongeza thamani kwa maana ya kuchakata chai yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha tunawawezesha wakulima hawa kwa kufufua mashamba yale ambayo tayari tumeshaanza kupitia Wizara ya Kilimo. Baadaye tutaenda kupeleka kuzalisha au kuchakata chai kwenye viwanda vya jirani ikiwemo kiwanda cha Mufindi *Tea Company*, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara ya Viwanda kule Makambako kulikuwa na eneo la Soko la Kimataifa, mlilipa fidia, lakini watu 18 hawakulipwa, je, ni lini Serikali itawalipa hao 18 waliobaki? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Deo Sanga kwa swali hili muhimu, lakini kama ambavyo Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshafanya katika maeneo mengi kulipa fidia, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika eneo hili la Soko la Kimataifa nako tutaenda kumalizia wale wachache waliobaki kwa sababu ilikuwa ni changamoto ya tathmini na ndiyo maana walikuwa wamerukwa. Hata hivyo, tunapitia na kuhakiki upya madeni yao ili tu na hao waliobakia tuweze kuwalipa fidia.

Mheshimiwa Spika, nadhani katika mipango ya Serikali, ni mwaka wa fedha unaokuja. Kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge, tutapitia wale waliobakia ili nao tujue thamani ya

malipo yao katika eneo hili la Soko la Kimataifa pale Makambako. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Asia Abdukarim Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 146

**Kutoa Hati za Ardhi - Hanang**

**MHE. ASIA A. HALAMGA** aliuliza:-

Je, lini Wananchi waliolipia upimaji watapewa Hati za umiliki wa Ardhi - Hanang?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, jumla ya mashamba 5,506 yamepimwa katika Kata za Gitting, Masakta, Ishponga, Dirma, Balangdalalu, Gehandu na Mogitu. Aidha, jumla ya viwanja 11,440 vimepimwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Hanang katika kata za Ganana, Endasiwold, Nangwa, Bassotu, Dumbeta, Katesh na Balangdalalu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya upimaji kukamilika, wananchi wameandaliwa nyaraka za umiliki wa ardhi zao ambapo jumla ya Hati za Hakimiliki za Kimila 1,360 zimeandaliwa na kutolewa kwa wananchi wa kata za Gitting (150), Masakta (210) na Ishponga (1,000). Aidha, jumla ya Hatimiliki 1,505 zimeandaliwa na kutolewa katika Kata za Gitting (355), Masakta (205) na Ishponga (950).

Mheshimiwa Spika, zoezi la kuandaa Hatimiliki na Hati za Hakimiliki za Kimila bado linaendelea kutegemeana na ukamilishwaji wa masharti ya umiliki wa ardhi kwa wananchi husika. Aidha, Serikali inaendelea kushughulikia changamoto na malalamiko ya wananchi yanayoendelea kujitokeza wakati wa zoezi la umilikishwaji ardhi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri na niende sasa kwenye maswali yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwa muda mrefu sasa ni zaidi ya miaka miwili Kata ya Masakta, Ishponga, Dirma, Balangdalalu, Mogitu, Gitting bado wananchi hawajapata hati zao huku wakiwa wamepata watu wachache tu, je, ni lini Serikali itakamilisha utoaji wa hati kwa kuwa limekuwa ni suala la muda mrefu?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili ambalo ni sawa na ombi: Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kwenda sasa Wilaya ya Hanang ili kwenda kutoa hati hizo kwa wananchi wa kata nilizozitaja pamoja na maeneo mengine ya Wilaya ya Hanang?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wa haki za wananchi wa Hanang. Kwa kweli tunakiri kwamba ni mfuatiliaji mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye majibu ya maswali yake mawili; moja, ni kwamba zoezi la kutambua maeneo haya linaendelea na mpaka sasa mkononi katika hatua za mwisho za

kukamilisha tunazo karibu hati 300 ambazo wakati wowote zinaenda kutolewa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja yake ya pili kwamba lini naweza kwenda huko, kwanza nikiri kwamba nitakwenda na hizo hati ninaenda kutoa mimi mwenyewe ili kuzungumza na wananchi vilevile katika suala zima la kuwashukuru kwa uvumilivu wao wakati wa zoezi hili. Ni kweli ni muda mrefu na ni miaka miwili, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Emmanuel Peter Chereheni, Mbunge wa Ushetu, sasa aulize swali lake.

Na. 147

**Hitaji la Gari Ofisi ya Uhamiaji – Kahama**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka gari Ofisi ya Uhamiaji Wilaya ya Kahama ili kuboresha utendaji kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Uhamiaji Wilaya ya Kahama kwa sasa ina gari moja yenye namba za usajili STL 1022 aina ya *Ford Ranger pick - up double cabin* ambayo ni chakavu. Aidha, Serikali kupitia Idara ya Uhamiaji imetenga kiasi cha fedha shilingi 3,259,987,000 katika mwaka wa fedha 2024/2025 kwa ajili ya ununuzi wa magari 18 kwa ajili ya kuimarisha misako na doria nchini. Pindi magari yatakaponunuliwa, yatasambazwa kwenye wilaya zenye uhitaji mkubwa ikiwemo na Wilaya ya Kahama, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Wilaya ya Kahama ina halmashauri tatu; Msalala, Kahama pamoja na Ushetu, lakini imekuwa ndiyo lango la nchi jirani; Congo, Burundi, Rwanda na Uganda.

Mheshimiwa Spika, hawa watu hawana gari zaidi ya miaka minne leo, lakini pia wana pikipiki mbili za kudhibiti uhamiaji kitu ambacho ni hatari sana kwa askari wetu.

Mheshimiwa Spika, nataka nipate *commitment* ya Serikali kwa sababu nimekuwa nikiahidiwa kila mwaka, na mwaka 2024 gari zilipatikana zikapelekwa pale mkoani. Kwa hiyo, hali ya Kahama siyo nzuri, naomba nipate *commitment* ya Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wa gari la uhamiaji kwa Ofisi ya Kahama. Ni kweli Wilaya ya Kahama ina Halmashauri tatu kwa maana ya Ushetu, Msalala pamoja na Kahama yenyewe.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, tayari tulishapata kibali kwa ajili ya kununua magari 18. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika mgao huu utapata gari kwa ajili ya wilaya yake ya Kahama, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kuhakikisha kwamba inapeleka gari kwenye Ofisi ya uhamiaji Tarime pamoja na Ofisi ya Kipolisi ya Nyamwaga na Tarime ambazo hazina magari kabisa ili kurahisisha utendaji?

**SPIKA:** Ngoja Mheshimiwa swali ni moja. Uliza mojawapo kati ya hayo uliyouliza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kuhakikisha kwamba inapeleka gari kwenye Ofisi ya Uhamiaji Tarime ili kurahisisha utendaji, maana hamna gari kabisa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, tumeagiza magari 18 na tunaanza na wilaya zile za mpakani kwa ajili ya kuimarisha misako na doria. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwenye mgao huu Wilaya ya Tarime pia itakuwa mojawapo kwa sababu ipo pia mpakani, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako. Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 148

**Udhibiti wa Pembejeo Feki**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA** aliuliza:-

Je, ni Mkakati upi Serikali imeuweka kudhibiti uingizaji wa pembejeo feki za mazao ili kuwasaidia wakulima wasipate hasara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti uingizaji wa pembejeo feki za mazao nchini, Serikali kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania *(TPHPA),* Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu

Tanzania *(TOSCI)* na Mamlaka ya Udhibiti Ubora wa Mbolea Tanzania *(TFRA)* imeweka mikakati ifuatayo:-

(i) Kutambua na kusajili waagizaji wote wa pembejeo nchini ili kudhibiti uingizaji holela wa pembejeo nchini;

(ii) Kufanya ukaguzi wa kila shehena ya pembejeo za kilimo inapofika bandarini au mpakani na kuchukua sampuli kwa ajili ya uchambuzi wa kimaabara;

(iii) Kutoa elimu kwa wakulima na wauzaji wa pembejeo za kilimo kuhusu utambuzi wa pembejeo feki, utunzaji na matumizi bora ya pembejeo; na

(iv) Kufanya kaguzi za mara kwa mara katika maghala na maduka ya pembejeo na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika ikiwemo kuwafutia leseni za kuuza pembejeo zote wale wote wanaobainika kuuza au kusambaza pembejeo feki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza. Mheshimiwa Mwandabila alikuwa hajasimama, kwa hiyo, nikafiri hana swali la nyongeza. Kumbe unayo? Haya, Mheshimiwa Cecilia Paresso halafu nitakurejea.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na utaratibu uliopo wa Serikali wa kutoa hizo mbegu za ruzuku lakini mawakala wanakuwa wachache sana. Kwa mfano, Jimbo la Karatu mawakala ni watatu tu kwa wilaya nzima, je, Serikali ina mpango gani wa kupanua wigo ili wananchi wengi wafaidike na hizo mbegu za ruzuku? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba mawakala tumetoa fursa kwa wafanyabiashara wote wanaotaka kuingia katika biashara ya mbegu pamoja na mbolea kuja kujisajili. Wanajisajili *TFRA* halafu wanapewa hicho kibali cha kuuza

mbolea. Kwa hiyo, ni *room* ya kila mtu ambaye anahitajika kufanya hivyo. Kwa hiyo, niseme tu kabisa kwamba wale wote wanaohitaji kufanya hiyo biashara waje na sisi tutawapa hiyo ruhusa ya kufanya biashara hiyo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, samahani nilikuwa nimepitiwa kidogo.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kufahamu, kwa kuwa Serikali imeweka njia mbalimbali ambazo ni thabiti za udhibiti wa uingizaji wa pembejeo, lakini wakulima wanakutana na pembejeo feki. Je, Serikali haioni kuwa kuna mahali imefeli katika udhibiti huo wa uingizaji wa pembejeo feki?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Je, ni fidia zipi hutolewa kwa wakulima ambao huathirika na matumizi ya pembejeo feki? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nikubaliane na Mheshimiwa Neema kwamba, kweli kuna changamoto kwenye baadhi ya maeneo hususan maeneo ya mipakani hasa kwa zile mbolea ambazo zinapitishwa kutoka nchi jirani kuingia ndani.

Mheshimiwa Spika, jukumu letu sisi kama Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, tumeendelea kuongeza udhibiti wa kuongeza Watendaji ambao wamekuwa wakifanya *patrol* za mara kwa mara. Kwa hiyo, kikubwa tu ni sisi kuendelea kuongeza huo udhibiti ili kuhakikisha kwamba tunafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la fidia kwa wakulima ambayo inatokana na mbolea feki, moja, kwa hatua ya sasa ambayo tumekuwa tukiifanya, wale wote ambao wanatambulika ama kubainika wamepeleka mbolea feki, tunawachukulia hatua za kisheria ikiwemo kuwapeleka Mahakamani, kuwafutia leseni na

kuendelea. Baada ya hapo maana yake Mahakama ndiyo itakayoamua maamuzi ya mwisho juu ya hatua gani za kisheria pamoja na za kifidia ambazo mwananchi anapaswa kulipwa. Kwa hiyo, hiyo ndiyo hatua tuliyopo kwa sasa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Madaba ni miongoni mwa wananchi walioathirika sana na mbegu feki ambazo zilisambazwa msimu uliopita. Wapo wengi wamepata hasara kabisa katika mashamba yao, na kwa vile yule ambaye alisambaza hizo mbegu feki alishakamatwa.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha kwamba hasa wakulima waliopata hasara kwa kutumia zile mbegu wanafidiwa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilikuwa najibu katika swali ambalo lilitangulia, ni kwamba, baada ya yule msambazaji wa mbegu feki au pembejeo feki kukamatwa, sisi kama Wizara hatua ambazo tumechukua ni kumfutia leseni ya kushiriki katika shughuli zote za mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili, tumeshapeleka Mahakamani, na jambo hili lipo katika hatua za kisheria. Kwa hiyo, baada ya hatua za kisheria, ninaamini sasa tunaweza tukawa na neno la kusema kuliko kuingilia Mahakama, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, Mbunge wa Nachingwea, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Ally Kassinge.

Na. 149

**Kujenga Skimu za Umwagiliaji – Nachingwea**

**MHE. ALLY M. KASSINGE K.n.y. MHE. AMANDUS J. CHINGUILE** aliuliza:-

Je, lini Skimu za Umwagiliaji zitajengwa katika Kata za Ruponda, Mramba, Mbondo, Matekwe na Kilimarondo – Nachingwea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kuchimba visima na kuweka miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo ya Ruponda, Mandawa, Marambo, Mnerongongo na Ntila. Aidha, maeneo ya Matekwe, Mbondo, Kilimarondo na Mitumbati kwa pamoja yatapewa kipaumbele katika mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza, lakini pia naishukuru Serikali kwa majibu ambayo yanakwenda kutoa matumaini kwa wananchi wa Nachingwea.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Kwa kuwa maeneo ambayo Mheshimiwa Chinguile ameyaainisha yapo katika bajeti ya 2025/2026, nini *commitment* ya Serikali kuhakikisha kwamba skimu hizi zinakwenda kujengwa na hazitachukua muda mrefu kama ambavyo ilikuwa huko awali?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kupitia mpango huu wa kujenga visima katika maeneo ya mabonde ya umwagiliaji, pale

Wilayani Kilwa kuna Bonde la Makangaga katika Kata ya Kiranjeranje. Nini *commitment* ya Serikali kujenga kisima kwa ajili ya umwagiliaji katika Bonde la Makangaga? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Niwathibitishie tu wananchi wa Nachingwea kupitia swali la Mheshimiwa Kassinge kwamba *commitment* ya Serikali iko palepale, ndiyo maana jambo hili tumeliweka katika bajeti yetu kwamba tumedhamiria kulifanya na tutalifanya kwa kadri pesa zinavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri Wizara ya Fedha imekuwa ikitoa ushirikiano kuleta fedha ili kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati na wananchi wanapata huduma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *commitment* ya kuchimba kisima katika Bonde la Makangaga katika Jimbo la Kilwa Kusini, nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hilo tutalitekeleza kwa sababu lipo katika mpango wa mwaka wa fedha unaokuja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa za Serikali za kupeleka wataalamu katika Maporomoko ya Likingu kule Mdunduwalo, je, Serikali sasa itaanza lini ujenzi wa skimu ili wasomi vijana wa kule waanze kulima zao la mpunga? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba tayari tumeshapeleka wataalamu katika maporomoko ya Likingu ambao wameenda kwa kazi moja tu ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na hatua zilizopo sasa hivi ni kumalizia michoro na baada ya hapo tutangaze hiyo tenda kwa ajili ya

kumpata mkandarasi ambaye atapewa hiyo kazi. Kwa hiyo, wananchi wa Jimbo la Peramiho, Songea Vijijini wakae mkao wa utayari kwa ajili ya kazi hiyo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Spika, Skimu ya Nyendara iliyojengwa katika Jimbo la Muhambwe haikukamilika na hivyo kuacha eneo ambalo ni hatarishi kwa maisha ya binadamu na watoto mara nyingi wanatumbukia. Je, ni lini Serikali italeta fedha ili tukamilishe Skimu ya Nyendara ili watoto wasiathirike zaidi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba hatua ya awali ambayo tulikuwa tumeipanga kibajeti katika Skimu ya Lingala, tayari tumeshaifanya, na hatua ya pili ni kufanya *expansion* ambayo sasa hivi watu wa tume wanaendelea na hatua za mwisho za kufanya ile tunasema *feasibility study* ili kukamilisha mchoro na kuanzisha ili tuweze kuwasaidia zaidi wakulima katika eneo la jimbo lako, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Vwawa.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa skimu ya umwagiliaji kwenye Mto Myovizi kwenye Kata ya Mlangali ambayo ni eneo muhimu sana kwa uzalishaji? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Hasunga, Mbunge wa Jimbo la Vwawa, kwamba Mto Myovizi ni moja ya mto ambao una faida kubwa sana kwa wananchi katika jimbo lake na ni sehemu ya miradi ambayo sisi Wizara ya Kilimo tunaipa kipaumbele na ndiyo

maana wataalamu wetu sasa hivi na wenyewe wanafanya *feasibility study* ili tukamilishe ule mchoro, tutafute fedha ili tujenge mradi ambao utasaidia wananchi wa Kata ya Mlangali kulingana na *standard* za kisasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge wathibitishie wananchi wa eneo hilo kwamba Serikali iko kazini na tutalifikia hili jambo kama ambavyo nimeahidi hapa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu, sasa aulize swali lake.

Na. 150

**Soko la Zao la Alizeti**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta Soko la uhakika la Zao la Alizeti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha uwepo wa masoko ya uhakika ya mazao ya kilimo ikiwemo zao la alizeti kwa kuhamasisha kilimo cha kibiashara kinachozingatia mahitaji ya soko; kuhamashisha uanzishwaji wa viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na kuwaunganisha na wakulima; ukamilishaji wa kanuni za kilimo cha mkataba; na kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko *(COPRA)* kukaa na wadau na kupendekeza bei elekezi ya kununua alizeti kwa kilo pale inapohitajika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa mikakati mizuri ya Serikali. Kwa kuwa, soko la alizeti liko juu sana nchi za nje, pamoja na viwanda vilivyopo nchini, je, Serikali haioni haja ya kumtafuta mwekezaji ambaye atawekeza kufikia soko la nje ili kuleta ushindani katika bei ya alizeti kwa wakulima?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, mpaka sasa Wilaya ya Meatu hawajapelekewa mbegu za alizeti, je, Serikali haioni haja ya kuwapelekea mbegu za alizeti zenye tija zitakazowatolea mafuta mengi ili wakulima kujiongezea kipato?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kuona umuhimu wa wawekezaji nchini. Wizara ya Kilimo tumeshafanya majadiliano na balozi zote za nje ya nchi zinazowakilisha Tanzania kwamba watafute wawekezaji ambao wanaweza kuja kuwekeza hapa nchini katika kuongeza thamani ya zao la alizeti.

Mheshimiwa Spika, vilevile, sisi kama Wizara tumeendelea kutoa wito kwa wawekezaji wa ndani waweze kuwekeza katika zao hilo ili kuongeza thamani na tupate mafuta ya kutosha kwa ajili ya wananchi, kwa sababu bado mahitaji ya ndani ya mafuta ni makubwa sana tofauti yalivyo kule nje. Kwa hiyo, mahitaji ya ndani ya mtakuta ni makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mahitaji ya alizeti katika Jimbo la Meatu, niwaelekeze tu, *Agent* wetu *ASA*, Mamlaka ya Uzalishaji wa Mbegu, kwamba wapeleke mbegu katika Halmashauri ya Meatu kwa sababu wanazo mbegu za kutosha za alizeti, hivi ninavyozungumza nina uhakika na hiki ninachokisema, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Abubakari, Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, sasa aulize swali lake.

Na. 151

**Fidia kwa Wananchi Waliopisha Ujenzi wa Barabara ya Mchepuko – Kilombero**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itawalipa fidia wananchi waliopisha ujenzi wa Barabara ya Mchepuko kutoka Ifakara, Kikwawila, Mbasa hadi Lipangalala?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa Barabara ya Mchepuo ya Mji wa Ifakara yenye urefu wa kilometa 10. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, taratibu za kufanya tathmini ya mali zote zitakazoathiriwa na ujenzi zinaendelea. Mara baada ya kukamilika kwa tathmini, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi wote wanaostahili kwa mujibu wa sheria.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naishukuru Serikali kwa kukubali kwamba inatafuta fedha kwa ajili ya kuijenga barabara hiyo. Wananchi wanasubiri fidia kwa zaidi ya miaka sita katika barabara hiyo na wanaambiwa kwamba tathmini inaendelea. Je, ni lini tathmini hiyo itakamilika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika barabara ya Ifakara Kidatu ambayo Mheshimiwa Rais aliizindua mwaka 2024 mwezi

wa Nane, tathmini imeshafanyika, imegundulika kuna wananchi bado wanadai kihalali. Je, wananchi hao nao watalipwa lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli hii barabara ya Mchepuo ya Ifakara tathmini ilifanyika muda na ndiyo maana sasa hivi kinachofanyika ni kuihuisha kwa sababu imeonekana hii barabara ilitakiwa ijengwe mapema kwa sababu ya ukuaji wa Mji wa Ifakara, na barabara iliyoko katikati imekuwa haitoshelezi tena mahitaji ya Mji wa Ifakara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Ifakara – Kidatu wale wote waliokuwa wanastshili kwa mujibu wa sheria walilipwa, lakini kupitia Kamati inayoshughulikia malalamiko chini ya Mkuu wa Wilaya, ilionekana wengine pia waliathirika kutokana na ujenzi ambapo ama barabara ilisogea, ama baada ya kukata magema walionekana wanatakiwa waondoke, kwa hiyo, wanatakiwa walipwe.

Mheshimiwa Spika, tayari tulishapokea taarifa zote za hao watu ambao baada ya kupitia hiyo Kamati ambayo inaongozwa chini ya Mkuu wa Wilaya wanastahili walipwe, na wananchi hao watalipwa hizo fidia zao, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Norah Mzeru, swali la nyongeza.

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua na kuboresha barabara za mikoa zinazopita Morogoro Mjini ili kupunguza ajali za mara kwa mara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Mpango wa Serikali kwa sasa, nadhani swali hili nililijibu juzi, kwamba sehemu zote za mji na hasa Mji wa Morogoro upo kwenye mpango wa kujenga barabara zaidi ya nne ili kupunguza msongamano katika

mji huo. Kwa hiyo, tayari tumeshaandaa *master plan* kwa miji yote kuhakikisha kwamba pale ambapo tunahitaji barabara zaidi ya mbili tujenge barabara nne na Mkoa wa Morogoro ni kati ya mikoa hiyo ambayo itanufaika na mpango huo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, swali la nyongeza.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, wapigakura wangu wa Bungu na Nyamisati wanataka kujua, lini barabara ile ya Bungu – Nyamisati itajengwa ukizingatia kwamba upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umeshakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tulishaanza hatua ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na ninamwomba Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa tuonane, kwa sababu kipindi hiki ndiyo tunaandaa mipango kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti inayokuja ili tuweze kuingiza kwenye mipango hii ya 2025/2026, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali imefikia wapi taratibu za ujenzi wa Barabara ya Mtwara Pachani kwenda Lusewa – Magazini mpaka Nalasi – Tunduru? Maana Mwenyekiti mmoja wa kijiji…

**SPIKA:** Mheshimiwa hiyo ni barabara moja?

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo, ni barabara moja, ila inapitia kwenye Kata za Lusewa - Magazini...

**SPIKA:** Haya, uliza swali lako sasa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itajenga Barabara ya Mtwara – Pachani – Nalasi ambayo inapitia katika kata hizo?

Mheshimiwa Spika, juzi nilielezwa na Mwenyekiti wa Kijiji kimoja kwamba mwezi wa Nne niwe nimeanza kuijenga barabara hiyo au watanishughulikia. Je, Serikali inawaeleza nini? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa...

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ngoja kwanza. Mheshimiwa Mbunge maelezo ya sehemu ya pili ya swali lako kidogo yatakuwa nje ya utaratibu wa yale anayoweza kujibu Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa hiyo, ili umweke sehemu nzuri, hebu mwulize swali lako kwa yale anayoweza kuyajibu yeye kama Naibu Waziri wa Ujenzi. Ile sehemu ya pili mwondolee ili asilazimike kukujibu.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali imefikia wapi kuhusu utaratibu wa kuijenga barabara ya Mtwara - Pachani mpaka Nalasi – Tunduru ambayo inapita kwenye Kata za Mkongo, Ligera, Lusewa, Magazini mpaka Tunduru? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna uhitaji mkubwa sana wa kuijenga hii barabara kwa kiwango cha lami. Tulichofanya kama Serikali, kwanza ni kuisanifu barabara yote wakati tunatafuta fedha kuijenga hiyo barabara ambayo ina urefu wa kilomita 300.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tulichomwahidi Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, wakati tunaendelea kutafuta fedha, maeneo yote korofi katika hiyo barabara ambayo huwa yanaleta changamoto tutahakikisha kwamba tunayaimarisha kwa kuyajenga kwa zege ama lami ili wananchi hao wasikwame

wakati Serikali inatafuta fedha. Hivyo, mpango huo upo, ndiyo maana tumefanya usanifu kwa barabara yote, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Afya, Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 152

**Huduma Bure za Matibabu kwa Wazee na Watoto**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatunga sheria itakayolinda utoaji wa huduma za matibabu bure kwa wazee na watoto?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imetunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ya Mwaka 2023, ambayo imeanzisha mfuko wa kuhudumia makundi ya watu wasio na uwezo yakiwemo makundi ya wanawake wajawazito na watoto chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, kuanza kutekelezwa kwa sheria hii kutawezesha makundi yote yakiwemo ya wazee na watoto kupata huduma za matibabu pasipo kuwepo kwa vikwazo vya fedha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, swali la nyongeza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, Sera ya Afya ya nchi yetu inatamka wazi kwamba, wazee na watoto

wanapaswa kupata huduma ya afya bila malipo. Nakubaliana na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba kuna Sheria ya Bima ya Afya ambayo haijatekelezwa mpaka sasa hivi. Nia yangu kuuliza swali hili ni kutaka kujua, wazee kama hawakupata huduma stahili kutoka kwa mtoa huduma, ni ipi kinga yao? Yaani wanaweza kwenda kulalamika wapi ili waweze kusaidiwa kuhakikisha huduma yao inatolewa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Magonjwa ya wazee ni mengi. Ukitaka kuyakwepa, ufe haraka. Mengi yanahitaji wataalamu kama ilivyo kwa watoto. Nashukuru katika nchi yetu watoto wanapata huduma zao na wana madaktari wao, sasa ni lini Serikali itahakikisha kwamba wazee wanapata madaktari wao ambao ni wataalamu bobezi kuhusu magonjwa ya wazee? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge, kwa Mkoa wake wa Kagera, lakini kwenye eneo hili la kuwatetea wazee, amekuwa akifanya kazi nzuri, ndiyo maana natamani kumwambia Tundu Lissu ahakikishe huyu mama anarudi humu Bungeni tena kwa mara ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ameuliza maswali mawili ya msingi sana. Swali lake la kwanza ni kuhusu wazee na huu mfuko. Kwanza hili suala la Bima ya Afya kwa Wote siyo kwamba halijatekelezwa, ni bado Bunge mnaendelea kutushauri kuhakikisha tunafanya vizuri hili jambo likae vizuri.

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusu wazee, ni kwamba wanahudumiwa, ndiyo maana nilisimama hapa Bungeni nikasema Serikali inatumia shilingi bilioni 661 kwenye eneo hili la *exemption.* Maana yake wazee wakiwa ni moja ya sehemu, lakini kwenye mfuko wetu wa Bima ya Afya inatumika shilingi bilioni 187 kutibu wazee, na hao wazee hawachangii kwenye Mfuko wa Bima ya Afya.

Mheshimiwa Spika, hivyo, nakubaliana na Mbunge kwamba hatuwatibu wazee kwa 100%. Ni kweli hatujafikia 100% ndiyo maana tumekuja na Muswada wa Bima ya Afya kwa wote ili kutenga lile kundi la watu wasiojiweza 26%, ili tukishaingia kwenye Bima ya Afya tuwezeku-*cover* tufike 100% kama ambavyo anasisitiza Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunachukua wazo la Mheshimiwa Mbunge na tutaendelea kuchakata na wakati wowote tutaongeza nguvu kwenye eneo hilo kama ambavyo ametamani liwe.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kwamba wazee wanahitaji madaktari maalumu, ni wazo zuri mno kwa sababu kwanza tunakwenda kwenye *Samia Scholarship* ambapo sasa hivi Mheshimiwa Rais wetu ametoa *scholarship* kwa ajili ya madaktari. Kuna madaktari ambao wanakwenda, na wanaenda pia ku-*specialize* kwenye eneo hilo la kuwahudumia wazee.

Mheshimiwa Spika, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba magonjwa ni yale yale, hata ma-*specialists* (madaktari bingwa tulionao) magonjwa ya madaktari bingwa ni hayo hayo, lakini wazee wanahitaji uangalizi maalumu kisaikolojia na kisosholojia na ndicho anachokisema. Tutakwenda kuwekeza kwenye eneo hilo na tutaweka rekodi kwamba ni mojawapo ya mambo ambayo dada yangu au mama yangu amehakikisha yanatokea kwenye eneo letu la afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu. Subiri, kuna Mbunge amesimama kule nyuma. Mheshimiwa Janeth Mahawanga, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni kwa namna gani Serikali inashughulikia malalamiko ya wazee na watoto wanaokosa huduma za bure katika baadhi ya vituo vya afya na hospitali za umma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kuna utaratibu wa kuhakikisha yule ambaye hawezi kulipa kuna utaratibu uliowekwa ndani ya hospitali ambao unafuatwa na kuhakikisha wanapata huduma. Kama ambavyo Mheshimiwa anasema kwamba ni watoto, ni kweli sheria yetu inawataka watoto wote walipiwe na wale ambao watashindwa kulipiwa kuna utaratibu ambao uko ndani ya hospitali ambao unafuatiliwa.

Mhehimiwa Spika, nitumie tu fursa hii kuwaambia madaktari wetu na hospitali zetu za umma asiwepo Mtanzania anayekosa huduma eti kwa sababu hana fedha au jambo lolote.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, changamoto ni kwamba mnaanza kusimama wakati unapaswa usimame akiwa anasimama mwenye swali ili nikishakuona napanga idadi hapa. Sasa mkianza kuchomoka kama uyoga hivyo, mnanichanganya hata hapa mbele. Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na wazee, Sera ya Afya inataka watoto wachanga na akina mama wakati wa kujifungua wapewe huduma bure, je, hilo linahitaji sheria mpya ili litekelezwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, hilo halihitaji sheria mpya ili litekelezwe. Ndiyo maana toka mwanzo kama mnakumbuka nilisema hapa kwamba tunatenga dawa shilingi bilioni 200, lakini kuhudumia tu eneo hilo la akina mama na watoto linahitaji shilingi bilioni 227. Ndiyo maana hapa nimezungumzia kwenye kusamehe *(exemption)* maana ya kutibu hilo kundi unalolisema tunatumia shilingi bilioni 661 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kusema, ni kweli hawahudumiwi kwa 100%, ndiyo maana tumekuja na Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote ili tuweze kwenda kufikia malengo ambalo ninyi Wabunge hapa mnatamani lifikiwe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Riziki Lulida, swali la nyongeza.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, nami nashukuru. Hata ukisikiliza majibu ya Mheshimiwa Waziri, hakutaja watu wenye ulemavu hasa watoto chini ya miaka mitano hawamo katika jumuishi ya matibabu hayo.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha hili kundi maalumu la watu wenye ulemavu wakiwemo watoto wa chini ya miaka mitano wanakuwemo katika jumuishi na kupata haki ya matibabu bure? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli katika fedha zote ninazozitaja hapa za *exemption,* hata unapozungumzia mama na mtoto unamaanisha na mtoto chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, hili eneo nataka kuwaambia, linafanyiwa kazi vizuri na ndiyo maana unaona Mheshimiwa Rais wetu ameleta mashine maalumu ambazo zimesaidia watu ambao wamekuwa miaka sita mpaka kumi ya nyuma na watoto ambao wamezaliwa bila kusikia, sasa wanasikia na uliona walitibiwa bure pale Muhimbili. Makamu wa Rais alikwenda na akabonyeza kitufe na wakaanza kusikia wote kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, eneo hili wakati wote linazingatiwa na kwenye hospitali zetu zote tunaendelea kuhakikisha sasa hivi zile *process* na vitu vyote vinavyoweza kuwasaidia walemavu zinafanyika na tunaweka utaratibu mzuri wa kuwasaidia hao walemavu na wao waweze kuishi maisha kama watu wengine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Edward Olelekaita, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wazee hawa (wastaafu) wamekuwa na taabu nyingi za kuja

kuhakiki taarifa zao za *NHIF*, kwa nini msiweke mpango mwafikie hawa wastaafu maeneo walipo, wajikusanye na mkawapa taarifa maalumu? Nakushukuru *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Olelekaita ameandika barua Wizara ya Afya akilielezea hili eneo kwamba wazee wanatakiwa wasije hapa Dodoma au kwenda kwenye ofisi za mikoa kuhudumiwa kule.

Mheshimiwa Spika, tumeiona barua yake, nami ni kuwaambia sasa wale wazee wa Kiteto wakusanywe, na wataalamu wataenda Kiteto. Itakuwa hivyo kwa Waheshimiwa Wabunge wote sasa, watu watashuka kuwafuata wazee kule waliko. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 153

**Minara ya Simu Newala – Vijijini**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga minara ya simu katika maeneo mbalimbali yenye changamoto ya mawasiliano - Newala Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Newala Vijijini linaendelea kunufaika na Miradi ya Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* ambapo mnamo tarehe 30 Agosti, 2022 Serikali kupitia *UCSAF* iliingia makubaliano na Kampuni ya Simu ya Halotel kwa ajili ya kujenga mnara wa simu katika Kata ya Chitekete kupitia mradi wa mipakani na maeneo maalum wa Awamu ya Sita ambao ulikamilika na wananchi wananufaika na huduma.

Mheshimiwa Spika, aidha, kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidigitali Awamu ya Kwanza ambao mkataba wake ulisainiwa tarehe 13 Mei, 2023, Kata ya Makukwe katika Jimbo la Newala Vijijini, ilijumuishwa na kupata mtoa huduma Kampuni ya *Yas* (zamani ikijulikana kama *TIGO*) na kwa sasa *Yas* wameshapata kibali cha ujenzi na mkandarasi anajiandaa kwenda kuanza ujenzi wa mnara huo. Kwa mujibu wa taarifa za *Yas*, mnara unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Machi, 2025.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali kupitia *UCSAF*, itafanya tathmini katika maeneo mbalimbali ya Jimbo la Newala Vijijini ili kubaini maeneo yenye changamoto ya mawasiliano ya simu kama alivyowasilisha Mheshimiwa Mbunge ili kubaini mahitaji halisi na kuyaingiza katika mpango wa kuyafikishia huduma katika utekelezaji wa miradi ijayo ya mawasiliano ya simu kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naishukuru Serikali kwa majibu mazuri na kwa yale yote ambayo yanaendelea kufanywa katika jimbo letu la Newala Vijijini, lakini nina masuala mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza ni ombi, kwa sababu Serikali imeshaahidi kwamba itaenda kufanya tathmini katika

maeneo mbalimbali yenye changamoto ili kubaini na kupanga bajeti. Ombi langu ni kwamba, hiyo tathmini ifanyike kwa haraka ili wananchi wa Newala Vijijini nao wapate huduma zinazostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni swali. Kwa dunia tuliyonayo leo, suala la mafunzo ya TEHAMA haliepukiki kwa wanafunzi wetu wote walioko shuleni na tunatambua kwamba zipo shule ambazo zipo katika maeneo ambayo yana changamoto ya mawasiliano, hivyo wanakosa kusoma masomo ya TEHAMA kwa vitendo, wanasoma kwa nadharia. Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuwakwamua wanafunzi hawa ili na wenyewe waweze kusoma masomo ya TEHAMA kwa vitendo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kupokea shukrani, kwa kweli Mkoa wa Mtwara maeneo mengi tayari tumeweza kuyafikia, ni eneo la Mheshimiwa Mbunge la Newala pamoja na Nanyumbu tu, tunaendelea kuja kulifikia.

Mheshimiwa Spika, masuala ya TEHAMA shuleni ni kipaumbele ndani ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa Mradi wa Mkongo wa Taifa. Maeneo mengi tayari mmeweza kujionea namna ambavyo mkongo umeweza kuwafikia na kurahisisha spidi na gharama nafuu ya mawasiliano ya *data* kwa maana ya *internet*.

Mheshimiwa Spika, shuleni, kwa mpango wa Serikali tutafikisha huduma hii ya Mkongo wa Taifa. Hivyo nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo ya Newala Vijijini pia tunatarajia kufikia Desemba 2025 iwe imeweza kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kwa mawasiliano kwa ujumla maeneo ya mipakani ninafahamu usikivu wa redio unakuwa ni tatizo. Mheshimiwa Mbunge tumeshaongea mara nyingi katika

hili, nikutoe hofu, *TBC FM* pia mtakuja kufikishiwa na usikivu utakuwa imara kabisa. Mtaacha kusikiliza redio za jirani na kusikiliza redio yetu ya *TBC FM* na nyingine nyingi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mliosimama, mko wengi. Wote ni minara! Si tulishaletewa taarifa za minara humu ndani! Au zile taarifa hazijasaidia sana?

Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, ni lini Serikali itajenga minara ya simu katika Kata za Kiteto zenye changamoto ya mawasiliano zikiwepo Kata za Makame, Ndedo na Njoro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuhusu minara ya Kiteto, kazi zinaendelea. Nimtoe hofu Mheshimiwa Rahhi kwamba tuendelee kuvuta subira. Ninaamini watoa huduma wetu wote wataendelea kukamilisha minara hii kwa wakati, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia Mtamba, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili kuuliza swali dogo la nyongeza. Kata ya Tangazo, Naumbu, Kijiji cha Namgogoli, hakuna kabisa minara ya mawasiliano. Je, ni lini Serikali itapeleka minara ya mawasiliano katika maeneo hayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kata hizi zote alizozitaja Mheshimiwa Shamsia ziko katika mpango wa kuhakikiisha wanajengewa minara kwa lengo la kupata mawasiliano ya uhakika. Kwa hiyo, tukishindwa

kwa mwaka huu wa fedha, mwaka ujao wa fedha tutaendelea kuwafikia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ni takribani miaka miwili toka nimeomba mnara katika Kata ya Uru Kusini na hadi leo hatujapatiwa. Je, ni lini sasa tutawekewa mnara katika kata hiyo ili tuache kukaa kwenye miti kupiga simu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, suala la kata hii aliyoitaja Mheshimiwa Shally Raymond, naomba niwe nimelipokea na kwenda kulifanyia kazi kuona wamefikia hatua gani? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nami nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Serikali ilikuwa na mkakati wa kujenga mnara wa mawasiliano katika Kata ya Uru Kusini ambapo hakuna mawasiliano kabisa, na mkakati huu ulisitishwa.

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itajenga mnara katika kata hii ili wananchi waweze kupata mawasiliano? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kata hizi zote zimeshafanyiwa tathmini na kazi ya tathmini inaendelea. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Njau, kadiri tunavyoendelea kupata fedha tutaendelea kuhakikisha maeneo haya yote wananchi wanapata mawasiliano ya uhakika kwa ujenzi wa minara, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, kata zetu zilizo mpakani na nchi mnayoifahamu, mawasiliano yake yanaingiliwa sana na mawasiliano kutoka kwenye nchi hiyo na hatupati *signals* kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Kata za Kirua Vunjo Magharibi, Marangu Magharibi, Kilema Kaskazini, Mamba Kaskazini na Mwika Kaskazini hazina mawasiliano mazuri kabisa. Kwa hiyo, tulikuwa tunatarajia kwamba ule mgao wa minara wa awamu ya pili tungepata minara. Je, ni lini mgao huo utafanyika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, nimtoe hofu Mheshimiwa Dkt. Kimei kwamba maeneo yote ya mipakani tayari tumeweka mpango maalumu na mahususi kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanakuja kujengewa minara ili waweze kupata mawasiliano ya ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hata kwenye usikivu wa redio, tayari tuko kwenye mkakati wa kuhakikisha maeneo yote ya mipakani wanaacha kusikiliza redio kutoka nchi za nje na waendelee kupata usikivu kutoka redio zetu za ndani. Kwa hiyo, tayari kama Wizara tunaendelea kulifanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Hali ya usikivu wa Redio yetu ya *TBC* katika Wilaya ya Kishapu ni ya chini sana. Sasa, nataka niulize swali, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wananchi wa Kishapu wanaendelea kupata taarifa za uhakika kutoka *TBC* katika kipindi hiki cha mwaka huu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniphace Butondo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu usikivu wa *TBC FM* kuwa chini, naomba niwe nimelipokea ili tuwasimamie wataalamu wetu waje kuona namna ya kuuboresha mnara huo na mawasiliano ya *TBC FM* yaweze kupatikana vizuri kabisa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, Serikali ilituahidi katika awamu ya kwanza minara 700 na zaidi kujengwa katika Kijiji cha Kintanula, Kata ya Mwamagembe, Halmashauri ya Itigi, ni lini mnara huu utajengwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, minara hii 758 utekelezaji unaendelea. Katika eneo hili la Itigi kijiji alichokitaja Mheshimiwa Massare nalo tutalifuatilia kuona wapi imekwama ili tuweze kutoa msukumo na mnara huu uweze kujengwa ndani ya wakati. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itajenga minara ambayo tuliiomba kwenye eneo la Getanyamba, Changanyikeni, Mewadan, Haydarer na Endahagichan na Qamtananat? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, maeneo haya aliyoyataja Mheshimiwa Flatei Massay kwa kweli yote yapo katika mpango na tutahakikisha

tunaendelea kuyatekeleza na kusimamia watoa huduma wote waliosaini mikataba wakajenge minara hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, swali la nyongeza.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kata za Ntaba, Kambasegela, Kabula pamoja na Mpata zina changamoto kubwa sana za kimawasiliano. Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini mtapeleka mawasiliano katika kata hizi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fredy Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, haya maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mwakibete na yenyewe pia tutaendelea kuyapa kipaumbele kuona minara inakuja kujengwa na kuimarisha mawasiliano.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Matwebe katika Jimbo la Rungwe kumekuwa hakuna kabisa mawasiliano ya simu mpaka uende kwenye sehemu za miinuko. Ni lini Serikali itapeleka minara maeneo hayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, eneo hili la Matwebe na lenyewe pia, tunatamani Tanzania nzima na ndiyo maana tukaweka ile minara

758. Tuna minara 636 na tuna *project* nyingi ambazo tayari zipo katika mpango.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kusema, nchi nzima tutakwenda kuifikia na kuona kwamba mawasiliano yanaimarishwa. Kwa hiyo, minara hii ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge itajengwa. Nawaomba tu kuwa na subira na mwendelee kutuunga mkono. Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari tuna nia njema ya kuhakikisha maeneo yote nchini tunakwenda kuimarisha mawasiliano.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Kombo, swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Micheweni usikivu wa *TBC FM* ni mdogo sana. Je, Mheshimiwa Waziri ni lini nasi utatujengea mnara katika Wilaya ya Michweweni ili kuwawezesha wananchi kuisikiliza redio yao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, nafikiri ni miezi miwili tu imeisha toka nimeweza kufanya ziara Zanzibar. Nimeacha maagizo maeneo haya yote yaweze kushughulikiwa. Hivyo na eneo hili la Micheweni naomba niseme nimelipokea kwa ufuatiliaji zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 154

**Ujenzi wa Minara ya Simu Kata ya Kikolo na Kagugu – Mbinga Mjini**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga minara ya simu katika Kata za Kikolo na Kagugu - Mbinga Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* itafanya tathmini katika kata hizi mbili za Kikolo na Kagugu ili kubaini maeneo yenye changamoto na kutambua mahitaji halisi ya huduma za mawasiliano ili tuweze kuyaingiza maeneo hayo katika zabuni za miradi inayofuata ya mawasiliano kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jonas Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru Serikali kwa kukubali kufanya tathmini katika Kata ya Kikolo na Kagugu kwa kuwa zina changamoto kubwa ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, swali langu la nyongeza, baada ya kufanya tathmini, je, Serikali inaweza ikanihakikishia kwamba mpango huo utaingizwa katika bajeti ya mwaka 2025/2026?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Jonas Mbunda kwa kuishukuru Serikali kwa kazi ambayo tunaendelea kuifanya katika eneo hili la Mbinga Mjini. Pia, nampongeza kwa ushirikiano ambao tunaendelea kufanya baina yako na sisi Wizara.

Mheshimiwa Spika, nataka kukuhakikishia ni dhahiri baada ya tathmini kukamilika, basi itaingizwa kwenye bajeti ijayo na kuja kuhakikisha minara inajengwa na usikivu unaimarishwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa minara iliyojengwa na Kampuni ya *TTCL* katika vijiji vya Nandete, Pungutini, Mwengei na Chapita, haifanyi kazi kwa ufanisi wa kutosha. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha mawasiliano katika minara hiyo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Francis, amekiri minara imejengwa vijiji hivi vyote alivyovitaja. Kwa hiyo, tutafuatilia nini tuweze kufanya ili minara hii iliyokamilika iweze kuboreshwa na itoe huduma iliyokusudiwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 155

## Wasichana Wanaoendelea na Masomo Kunyonyesha Watoto Wao kwa Wakati

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA** aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha watoto wachanga wa wasichana wanaoendelea na masomo wananyonya maziwa ya mama kwa wakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kulingana na mwongozo wa wanafunzi wanaorejea shuleni baada ya kujifungua, hawaruhusiwi kwenda shuleni na watoto wao na badala yake, mwongozo unawataka wazazi kusaini makubaliano na uongozi wa shule ya kuwajibika kuwalea watoto wa wanafunzi wanaorudi shuleni. Hata hivyo, kupitia elimu nje ya mfumo rasmi, wanafunzi wenye watoto wachanga wanaruhusiwa kunyonyesha kwenye kituo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeendelea kuweka mazingira rafiki katika vituo vya elimu nje ya mfumo rasmi, kwa kujenga chumba maalumu cha watoto katika vituo vyote vipya vinavyojengwa kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari kwa njia mbadala, ambapo katika vituo hivyo, kuna mlezi anayekaa na Watoto, na mwanafunzi mwenye mtoto anapata nafasi ya kunyonyesha mtoto wake kwa wakati, pindi anapohitajika kufanya hivyo. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Najma Giga, swali la nyongeza.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba kuuliza Serikali, je, haioni umuhimu wa kuwapa muda wa miaka miwili watoto hawa ambao wamejifungua wakiwa shuleni ili wale watoto waweze kupata haki ya msingi ya kiafya kwa kupata maziwa ya mama?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Je, Serikali haioni umuhimu wa kurasimisha vituo hivi kwa sababu hili jambo tayari limeshakuwa rasmi katika nchi yetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza, Mheshimiwa Giga anatoa ushaui kwa Serikali tuweze kuona namna bora ya kufanya iwapo tutatoa nafasi ya miaka miwili. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumepokea ushauri wake kama Serikali, tutakwenda kuufanyia tathmini ili kuweza kuona ni namna gani tunaweza kutekeleza katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili anazungumzia suala la namna ni gani tunaweza kuruhusu watoto wetu kulelewa kwenye maeneo ya shule. Naomba kumweleza Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali inaendelea kuangalia namna bora ya kufanya kwa kuanzisha au kuimarisha vituo vile vya kulelea watoto kwa maana ya zile *daycare centres* aidha, ndani ya shule au karibu na shule, ili kuhakikisha kwamba, watoto wetu hawa wanaozaliwa wanaweza kupata malezi bora vilevile na kuweza kuangalia afya zao pindi wanapopata maziwa ya mama. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, na Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Manonga, sasa aulize swali lake.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Sasa naomba Serikali kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Manonga…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge unayepita hapo, naomba uketi, maana kuna Mheshimiwa Mbunge nyuma yako kule anauliza swali. Mheshimiwa Mbunge wa Manonga, endelea.

Na. 156

**Ujenzi wa Majosho Wilayani Igunga**

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI** aliuliza: -

Je, ni lini Kata za Ntobo, Ngulu, Igoweko, Ugaka na Sungwizi ambazo zinaongoza kwa mifugo nchini zitapatiwa fedha za ujenzi wa majosho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025, Wizara haikuweka katika mpango wa bajeti ujenzi wa majosho maeneo mbalimbali hapa nchini, ili kutoa fursa ya uwepo wa kampeni kubwa ya chanjo ya Kitaifa ambayo itahusisha uchanjaji wa magonjwa ya homa ya mapafu ya ng'ombe *(CBPP)*, sotoka ya mbuzi na kondoo *(PPR)* na ugonjwa wa kideri au mdondo kwa kuku. Kampeni hii inatarajiwa kuanza mwezi Februari, 2025 kwa kuwa, taratibu zote zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuweka katika Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2025/2026 ujenzi wa majosho nchini, yakiwemo majosho ya Kata za Ntobo, Ngulu, Igoweko, Ugaka na Sungwizi. Hata hivyo, Wizara inaielekeza Halmashauri ya Igunga kutenga fedha zinazopatikana katika mapato yake ya ndani ili kujenga majosho kwa ajili ya kuwasaidia wananchi katika maeneo husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Seif Gulamali, swali la nyongeza.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuweza kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa, Wizara imekuwa ikitoa fedha za ujenzi wa majosho na kuipeleka katika Mfuko wa Halmashauri na kusababisha wakati mwingine majosho haya kutokukamilika, je, kwa nini fedha hizo msiwe mnazipeleka kwenye akaunti za vijiji husika, zinazojenga majosho hayo ili kuhakikisha kwamba, miradi hiyo inakamilika kama ambavyo Serikali inataka, ama ambavyo Wizara nyingine, kama Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inavyofanya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Wilaya ya Igunga ni moja ya Wilaya zenye mifugo mingi sana Tanzania. Ni nini mkakati wa Wizara katika kuhakikisha kwamba, inaboresha sekta ya mifugo Wilayani Igunga, hususan Jimbo la Manonga? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kuna umuhimu gani wa kupeleka fedha kwenye halmashauri badala ya kijijini moja kwa moja?

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zinapotoka Wizara ya Mifugo, kwenye Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa maana ya halmashauri, zinakwenda kwa mujibu wa sheria. Miradi inapokwenda kutekelezwa huko, inatekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi.

Mheshimiwa Spika, sasa urahisi wa Wizara ya Mifugo kutoa fedha kupeleka TAMISEMI ni kwa sababu ya Sheria ya Manunuzi ambayo inatulazimu kupeleka mahali ambapo mchakato wote wa manunuzi ya umma unaweza ukafanyika. Kule kijijini bado Kamati za Manunuzi hazijakamilika, ndiyo maana fedha inatoka Wizara ya Mifugo inakwenda moja kwa moja halmashauri ambako kamati na michakato yote ya manunuzi inaweza kufanyika kwa kufuata sheria bila uvunjifu wowote wa Sheria ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaendelea kupeleka fedha kwenye halmashauri. Kikubwa zaidi ni kwa sababu Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe wa Kamati za Utawala na Fedha kule, ili kuhakikisha kwamba, fedha tunazozipeleka kwenye maeneo hayo zinasimamiwa inavyotakiwa. Kama ni fedha, kwa ajili ya majosho, ziende zikafanye kazi, kwa ajili ya majosho katika maeneo ya halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, la pili, anataka kujua mkakati wa Wizara ya Mifugo. Mikakati iko mingi na Mheshimiwa Mbunge bahati nzuri ni shahidi. Mkakati mmojawapo wa kuboresha sekta ya mifugo, ni kwamba tumeshagawa madume bora 20 katika Jimbo lake la Igunga.

Mheshimiwa Spika, sasa madume hayo yatafanya kazi ya kuzalisha mbegu bora, baada ya hapo yatakwenda kwenye

maeneo mbalimbali na kwenyewe kwenda kuzalisha mbegu bora ya madume.

Mheshimiwa Spika, mikakati iko mingi ikiwa ni pamoja na kuendelea kuboresha miundombinu ambayo ipo kwa ajili ya ufugaji wetu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe, sasa aulize swali lake.

Na. 157

**Kumaliza Migogoro ya Mipaka Kati ya Wananchi na Hifadhi za Misitu Nchini**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza migogoro ya mipaka kati ya wananchi na hifadhi za misitu nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua na inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kutatua migogoro baina ya hifadhi na wananchi nchini. Hatua kubwa ambayo imechukuliwa ni uamuzi wa Mheshimiwa Rais kuunda Kamati ya Mawaziri wa Kisekta toka Wizara nane kubaini na kushauri kuhusu utatuzi wa migogoro hiyo nchini. Kamati hiyo ilibainisha migogoro 975 ambapo migogoro 438 ilibainishwa kuhusu hifadhi za misitu.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua migogoro hiyo, tayari Wizara kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania imefanya

marejeo ya migogoro hiyo, ambapo migogoro 416, sawa na 95% ya migogoro iliyokuwa imebainishwa imetatuliwa. Migogoro 22 sawa na asilimia tano ipo katika hatua mbalimbali za utatuzi, hususan ile inayohitaji wananchi kuhamishwa kupisha uhifadhi katika maeneo yaliyoonekana yabaki na hadhi ya uhifadhi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kavejuru Felix, swali la nyongeza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa juhudi na jitihada kubwa za kutatua migogoro. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Kitongoji cha Gatoto kinachopatikana katika Kata ya Kagera Nkanda na Kitongoji cha Gachele kinachopatikana katika Kata ya Rusesa, vyote katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, ni vitongoji ambavyo sasa ni miaka miwili tangu Serikali ipange kuvihamisha na maeneo yao kuwa sehemu ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, wananchi wa vitongoji hivi wanategemea kilimo kama shughuli zao za kiuchumi; katika msimu huu wa kilimo, *TFS* wameharibu mazao yao, ikiwa ni pamoja na tumbaku. Kwa kuwa, Serikali bado haijatekeleza agizo la kuwahamisha, kwa nini isiwaachie mazao yao wakavuna?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Serikali ilitoa hekta 10,000 kutoka kwenye Hifadhi ya Msitu ya Makere Kusini, sehemu ambayo ilikuwa imepoteza sifa ya uhifadhi, ikatoa kwa Halmashauri ya Kasulu. Mpaka sasa hivi yapo malalamiko ya wakulima wadogo wadogo katika Vijiji vya Nyachenda, Kitagata na Mgombe ambavyo havikupata kabisa…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, uliza swali.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali iko tayari kufuata mpaka ngazi ya chini ili kuangalia mgawanyo wa hizo hekta 10,000? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, vitongoji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge kimsingi ni maeneo yaliyoanzishwa kwenye hifadhi. Vitongoji hivi viliacha vijiji mama vikaenda kuanzishwa ndani ya hifadhi. Kwa hiyo, uamuzi ulikuwa vitongoji hivi virejee kwenye vijiji mama. Maeneo haya ni kitalu cha uwindaji kinachosimamiwa na halmashauri na kwamba, shughuli zote za doria zinafanywa chini ya usimamizi wa halmashauri kwa kutumia askari wanaowapata wao.

Mheshimiwa Spika, mara ya mwisho jambo hili lilipokuja tulilifuatilia na kukawa na makubaliano kwamba, hakuna mazao ya wananchi yatakayofekwa na kwamba, halmashauri itafanya kazi ya kupanga maeneo haya ambayo wananchi wanatakiwa kuhamishiwa ili wananchi wahamishwe.

Mheshimiwa Spika, taarifa tulizonazo ni kwamba, katika kipindi hicho tangu tumetoa majibu yale, hakuna mazao ya wananchi yaliyofekwa, na kwamba sasa hivi halmashauri inakamilisha upimaji wa maeneo yale ili wananchi waweze kuhamishiwa eneo linalotakiwa.

Mheshimiwa Spika, rai yetu kama Wizara ni kwamba, kwa sababu, jambo hili liko chini ya usimamizi wa halmashauri, halmashauri ikamilishe kwa haraka upimaji wa maeneo yale ili wananchi waweze kuhamishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, ni kweli kwamba, Wizara tulipokea ombi la kugawa hekta 5,000 kwa ajili ya halmashauri hii. Tuligawa eneo hili na mara baada ya kugawa eneo hili, milki inahama kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, inahamia kwa halmashauri husika. Wao sasa ndio wana jukumu la kugawa ardhi hii kulingana na mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, rai yetu, na ni kwa sababu jambo hili limepigiwa kelele muda mrefu, tunaiomba Serikali ya Mkoa na ya

Wilaya ilishughulikie jambo hili, ili wananchi waweze kupata maeneo kwa ajili ya kufanya shughuli zao.

Vilevile kwa sababu, ni jambo ambalo limekuwa likijotokeza mara kwa mara, Wizara itatuma timu mara moja ili kwenda kushauriana vizuri na wenzetu wa Serikali ya Mkoa na Halmashauri, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. *Chief Whip*, upande wa kujibu maswali tumefikia hatua nzuri baada ya kuondoa yale maneno "kwa niaba", ili tuokoe wakati, tukomboe wakati, lakini bado kuna changamoto eneo la kumtaja tena upya Mheshimiwa Mbunge.

Ninapokuwa mimi tayari nimeshamtambulisha kwa mtu anayejibu maswali hapa, inatupotezea muda.

Kwa hiyo, nanyi kwenye vikao vyenu mwangalie namna ya kuliweka sawa, ili kila mtu anayekuja kujibu maswali hapa tuwe wote tumeelewana kuliko niwe narudiarudia hilo jambo kila wakati, linakuwa halipendezi.

Nikishamtambua Mheshimiwa Mbunge, wewe jibu swali moja kwa moja, hata kama unaanza na pongezi na chochote, lakini nenda moja kwa moja kwenye kujibu swali lake. Huna haja ya kumtaja tena kwa sababu, mimi nakuwa nimeshamtaja. Kwa hiyo, tunarejea sisi wenyewe. Yaani tunajirejearejea na tunapoteza muda mwingi.

Waheshimiwa Wabunge, ninaye mgeni ambaye yuko Jukwaa la Spika, huyu anaitwa Dkt. Mathew Mndeme, ni Mhadhiri wa Kitivo cha TEHAMA kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine waliokaa Jukwaa la Spika, amba oni wageni wanne wa Mheshimiwa Deogratias John Ndejembi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Tutaanza na Mhandisi Antony Sanga, Katibu Mkuu, karibu sana.

Wengine ni Ndg. Lucy Kabyemera, Naibu Katibu Mkuu, karibu sana. Ndg. Hamad Abdallah, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Nyumba la Taifa, karibu sana. Pia, yupo Ndg. Mathew Nhonge, Kamishna wa Ardhi, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni mbalimbali ambao ni wageni wetu hapa Bungeni. Tutaanza na wageni 30 wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, Waziri wa Viwanda na Biashara, hawa ni wadau wa maendeleo kutoka Wilaya ya Kisarawe, Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni sita wa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Waziri wa Madini. Hawa ni Kamati ya Utekelezaji ya Jumuiya ya Wazazi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana.

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Jerry William Silaa, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, huyu ni Ndg. Hamisi Mkali, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi, Kata ya Gongolamboto Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 29 wa Mheshimiwa Aeshi Hilaly, ambao ni Watumishi wa Halmashauri ya Sumbawanga Mjini, Mkoani Rukwa, karibuni sana.

Wageni 105 wa Mheshimiwa Pauline Gekul, Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi; Walimu, wafanyabiashara, marafiki zake na wafanyakazi wa Paleii kutoka Jimbo la Babati Mjini, Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo Wageni 27 wa Mheshimiwa Festo Sanga, hawa ni washiriki wa Tuzo za Wanafunzi wa Vyuo vya Kanda ya Kati, Mkoa wa Dodoma, Singida, Iringa na Morogoro, karibuni sana.

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Yustina Rahhi, ni Diwani wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dorothy Mbogo, kutoka Hanang Mkoa wa Manyara, karibu sana.

Wengine ni wageni wanne wa Mheshimiwa Issa Mtemvu, ambao ni Jumuiya ya Watanzania waishio nchini China *(DITAG)*, wakiongozwa na Ndg. Alawi Abdallah Rwegoshora, karibuni sana.

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Martha Mariki, ambaye ni Mwenyekiti wa Machinga Mkoa wa Katavi, Ndg. Marko Ernest, karibu sana.

Tunao wageni 36 wa Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana.

Wageni nane wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, ambao kwanza ni wanufaika wa Mradi wa Vizimba vya Kufugia Samaki, Wilaya ya Nyamagana, Mkoani Mwanza, ahsante sana.

Vilevile, yupo Mratibu wa Jumuiya ya Maridhiano ya Amani Tanzania kutoka Mkoani Mwanza na Ndg. Ivan Kilaga Mlata na pia, viongozi wa Taasisi ya *Youth Success Foundation* kutoka jijini Dar es Salaam, karibuni sana.

Wengine ni wageni watatu wa Mheshimiwa Kavejuru Felix, ambao ni wapigakura wake kutoka Jimbo la Buhigwe, Mkoa wa Kigoma, karibuni sana.

Pia, wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Capt. Abbas Ali Mwinyi, ambao ni marafiki zake kutoka jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, hilo ndilo tangazo la wageni, wengine watatangazwa kadiri watakavyoingia hapa Bungeni. Tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024**

**na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira Kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ni Hoja za Kamati, na tutaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Timotheo Mnzava, karibu.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA (MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niwasilishe Taarifa hii ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, aidha, natumia nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa namna walivyojitoa kikamilifu kutekeleza majukumu kwa moyo na weledi mkubwa, hivyo kuwezesha Kamati kukamilisha taarifa kwa wakati na kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, naomba taarifa yote ya Kamati iingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa mapema leo asubuhi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba sasa kuwasilisha taarifa ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii zilizotekelezwa na Kamati kwa

kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Februari 2024 hadi Januari, 2025.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne kama ifuatavyo: -

(i) Sehemu ya kwanza inatoa utangulizi wenye kueleza muundo na majukumu ya Kamati, na kuanisha shughuli zilizotekelezwa na Kamati katika kipindi hicho

(ii) Sehemu ya pili inafafanua namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake na yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa majukumu hayo;

(iii) Sehemu ya tatu inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati; na

(iv) Sehemu ya nne inahitimisha taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa yaliyobainika: Katika kipindi cha kuanzia Februari, 2024 hadi Januari, 2025, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilifanikiwa kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati kwa 2023/2024: Katika taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati iliyowasilishwa Bungeni tarehe 08 Februari, 2024, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ililiomba Bunge lako Tukufu kukubali na kuridhia mapendekezo mbalimbali kwenye Sekta za Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na ile ya Maliasili na Utalii kuwa Maazimio ambayo yangetekelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inalishukuru Bunge lako Tukufu, kwani kwa kauli moja, liliridhia mapendekezo yaliyowasilishwa na

hivyo kuwa maazimio ya Bunge. Kamati ilipata muda wa kufuatilia utekelezaji wa maazimio hayo na kupokea taarifa ya utekelezaji kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maazimio kwa upande wa Sekta ya Maliasili na Utalii: Bunge lilitoa maazimio kumi ambayo yalitakiwa kutekelezwa na Serikali katika Sekta ya Maliasili na Utalii. Serikali iliwasilisha mbele ya Kamati taarifa ya utekelezaji wa maazimio hayo. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, sehemu kubwa ya maazimio imetekelezwa pamoja na kuwa kuna changamoto ya utekelezaji kwenye baadhi ya maazimio.

Mheshimiwa Spika, katika Azimio la Serikali kuruhusu Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)* na Mamlaka ya Usimamizi wa Eneo la Ngorongoro *(NCAA)* kubaki na sehemu ya Makusanyo yake, Kamati ilitarifiwa kuwa Serikali ilifanya maandalizi yote kwa ajili ya utekelezaji wa Azimio hilo katika mchakato wa kupitisha bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya Mwaka 2024/2025 iliyowasilishwa Bungeni tarehe 31 Mei, 2024. Hata hivyo, wakati wa kupitisha Bajeti Kuu ya Serikali, Serikali haikutekeleza Azimio hilo.

Mheshimiwa Spika, maazimio mengine ambayo Kamati haikuridhika na utekelezaji wake ni pamoja na lile la kuitaka Serikali kuandaa na kuleta Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania *(TAWA)* na Serikali kuhakikisha inapandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania *(TFS)* kuwa Mamlaka.

Mheshimiwa Spika, maazimio haya siyo mapya, kwani kwa takribani miaka mitano iliyopita, Bunge limekuwa likiagiza Serikali kutekeleza maazimio haya kwa lengo la kuimarisha Sekta ya Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Kamati ilitoa mapendekezo nane ambayo Bunge lako Tukufu liliridhia na kuwa maazimio ya Bunge. Katika maazimio hayo, Kamati inapenda kulijulisha Bunge lako

Tukufu kuwa Serikali imetekeleza kwa ukamilifu maazimio matatu na maazimio matano yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kwani utekelezaji wake ni endelevu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, baadhi ya maazimio kasi ya utekelezaji wake hairidhishi. Mathalani, utekelezaji wa kasi ya kusambaza mfumo wa e-Ardhi ni ndogo sana na ipo nyuma ya wakati, kwani katika Halmashauri zote 184 nchini, Wizara imefanikiwa kusambaza mfumo huo kwenye Halmashauri 20 sawa na 10.9% tu. Hii ni kinyume na ahadi iliyotolewa na Wizara katika hotuba ya bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 ambapo, Wizara iliahidi kuwa itakuwa imesambaza mfumo huo kwa Halmashauri zote nchini kufikia mwezi Juni, 2024.

Mheshimiwa Spika, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilipanga kufanya ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ipatayo saba iliyopo katika Mikoa ya Lindi, Pwani, Dar es Salaam na Tanga.

Mheshimiwa Spika, utekeleaji wa miradi ya maendeleo katika sekta zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii na ile Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ni kama inavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati ukurasa wa 10 mpaka ukurasa wa 14.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitekeleza jukumu hili la kuchambua na kupitia bajeti za Wizara zote mbili na taasisi zake, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa mujibu wa fasili ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Utekelezaji zaidi wa jukumu hili ni kama ulivyoonekana kwenye ukurasa wa 15 mpaka wa 16 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka kati ya Julai mpaka Desemba, 2024. Kamati ilipata fursa ya kuchambua utekelezaji wa bajeti za Wizara zote mbili kwa kipindi cha nusu mwaka kuanzia Julai hadi Desemba, 2024. Katika uchambuzi huo, Kamati ilijikita katika kuangalia ukusanyaji

wa maduhuli na fedha za matumizi zilizotolewa kwa Wizara na Taasisi zake. Uchambuzi ni kama unavyoonekana kwenye ukurasa wa 17 hadi ukurasa wa 21 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kufuatilia utekekelezaji wa shughuli zinazotekelezwa na Wizara, kwa mujibu wa Kanuni ya 7(1)(d) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023 inazitaka Kamati za Kisekta kufanya ufuatiliaji wa shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara zinazosimamiwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilifanya ziara za ufuatiliaji kwa lengo la kujiridhisha na tija inayopatikana katika miradi na *program* zinazotekelezwa na Wizara zinazosimamiwa na Kamati. Kutokana na ziara hizo, Kamati iliweza kuwianisha taarifa zinazotolewa na Serikali kuhusu tija na mafanikio na hali halisi iliyopo kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, yaliyobainika wakati wa ufuatiliaji wa sekta. Katika kipindi cha kuanzia Februari, 2024 hadi Januari, 2025, Kamati ilipokea na kujadili taarifa 40 ambapo taarifa 15 ni za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na taarifa 25 ni za Wizara ya Maliasili na Utalii. Lengo la kupokea na kujadili taarifa hizi ni kuiwezesha Kamati kulisaidia Bunge kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Maliasili na Utalii. Katika Wizara za Kisekta, Wizara ya Maliasili na Utalii imepewa dhamana ya kusimamia kisheria maeneo yenye ukubwa wa kilometa za mraba takriban 307,800. Eneo hili ni sawa na 32.5% ya eneo lote la nchi yetu ikuhusisha uhifadhi wa wanyamapori, milima mbalimbali, misitu, ardhioevu, nyuki, malikale na Makumbusho ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa uliofanywa na Kamati, umewezesha kubaini mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Maliasili na Utalii kwenye

miradi na taasisi zake kama inavyoonekana katika ukurasa wa 23 mpaka ukurasa wa 21 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara hii ndiyo iliyokasimiwa majukumu ya kuratibu na kusimamia Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 (Toleo la Mwaka 2023 na ile ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000).

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu haya ya Kisera, Wizara inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vya Serikali vilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa mwaka 2021/2022 - 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati. Kamati imebaini mafanikio na changamoto katika sekta ya ardhi kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa 41 mpaka ukurasa wa 52 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Mapendekezo. Yafuatayo ni maoni ya Kamati kuhusu shughuli zilizotekelezwa katika kipindi cha kuanzia Februari, 2024 hadi Januari, 2025 ambayo yanabainisha mtazamo wa kile kilichojiri wakati Kamati ikitimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Maliasili na Utalii:-

(i) Serikali iweke mikakati ya kulinda maeneo yaliyohifadhiwa na kuweka alama za kudumu na zenye kuonekana ili kudhibiti uvamizi wa shughuli za kibinadamu;

(ii) Serikali ichukue hatua madhubuti za kutoa elimu na kuwashirikisha wananchi katika shughuli za uhifadhi wa rasilimali za misitu ili kunusuru misitu yetu nchini; na

(iii) Serikali iweke mkakati wa kuvitambua, kuviendeleza na kuvitangaza vivutio vyote vya utalii nchini ikiwa ni pamoja na utalii

wa malikale, utalii wa fukwe za bahari, uvuvi, utamaduni na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Ardhi: -

(i) Serikali ibuni njia zitakazowezesha utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini ili kusudi sekta ya ardhi iongeze mchango katika pato la Taifa na kustawisha wananchi;

(ii) Serikali ibuni mbinu mbalimbali za kuhamasisha wananchi kulipa kodi za ardhi, kama vile kufanya matangazo kwenye mikusanyiko mbalimbali; na

(iii) Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuzingatia mpango wa matumizi ya ardhi sambamba na ushirikishwaji wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo. Utaratibu wa Kubaki na Makusanyo Katika Taasisi za *TANAPA* na *NCAA:*-

KWA KUWA, taasisi hizi zinakabaliwa na uhaba wa fedha katika utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi kutokana na ukomo wa bajeti na kuchelewa kupokea fedha kutoka Hazina;

NA KWA KUWA, hali hiyo inazorotesha ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya kuwezesha shughuli za uhifadhi na utalii jambo ambalo linaweza kupunguza mchango wa sekta kwenye uchumi wa nchi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ilete Marekebisho ya Sheria ya Fedha kwa lengo la kuzifanya taasisi hizo kubaki na sehemu ya makusanyo yake ili kuzisaidia kutekeleza majukumu yake ya uhifadhi na kuhudumia utalii kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA):-*

KWA KUWA, miradi ya kimkakati ya ujenzi wa Hoteli ya Nyota tatu ya Burigi, Chato na utengenezaji wa kiwanja cha *golf* katika Hifadhi ya Serengeti eneo la *Fort* Ikoma imechelewa kukamilika;

NA KWA KUWA, Ucheleweshaji huo, unaongeza gharama ya miradi kuliko ilivyokadiriwa awali; na unakwamisha uwezekano wa Taifa kunufaika ipasavyo na fursa zilizopo katika sekta ya utalii;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali, ifanye tathmini ili kubaini sababu za miradi hiyo kutokukamilika kwa wakati na Serikali ijipange kukamilisha miradi hiyo kabla ya tarehe 30 Juni, 2025.

Mheshimiwa Spika, Mchakato Mrefu wa Malipo ya Kifutamachozi na Kifuta Jasho:-

KWA KUWA, Serikali imefanya uamuzi wa kutoa kifuta machozi na kifuta jasho kutokana na athari zinazowapata wananchi kwa sababu ya migongano kati ya wanyamapori wakali;

NA KWA KUWA, mchakato wa malipo ya kifuta machozi na kifuata jasho umekuwa ukichukua muda mrefu hivyo kuongeza madhara kwa wananchi wanaokutwa na kadhia hiyo ikiwemo ulemavu, kuharibiwa mali na kupoteza maisha;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa inaboresha na kurahisisha mchakato wa malipo kwa wananchi walioathirika na migongano hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokutekelezwa kwa Azimio la Bunge Kuhusu Uendeshaji wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania *(TAWA)* na Mchakato wa kupandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania *(TFS)*:-

KWA KUWA, utekelezaji wa majukumu ya taasisi za TAWA na TFS ufanisi unaweza kupungua kutokana na changamoto ya muundo wa undeshaji;

NA KWA KUWA, athari za changamoto hizo zilizingatiwa na Bunge kwa kupitisha azimio mwaka 2023 na 2024 ili kutatua hali hiyo, lakini utekelezaji haujafanyika;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ilete maelezo kwa Katibu wa Bunge kuhusu maazimio hayo ikifafanua mkakati uliopo wa kutekeleza maazimio hayo ifikapo 10 Machi, 2025.

Mheshimiwa Spika, Kutangaza vivutio vya Utalii Nchini kwa Njia ya Kidijitali:-

KWA KUWA, Serikali imetumia gharama kubwa katika ujenzi wa Kituo cha Kutangaza Utalii Kidijitali *(DDMCC);*

NA KWA KUWA, kituo hicho hakijaanza kufanya kazi licha ya kuwa kimekamilika takribani miaka mitatu, hivyo Taifa kushindwa kunufaika na manufaa ya kituo hicho;

KWA HIYO Basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye tathmini na uchuguzi wa kina ili kubaini sababu ya Kituo hicho kushindwa kufanya kazi na iwasilishe taarifa kwa Katibu Wa Bunge kabla ya tarehe 10 Machi, 2025.

Mheshimiwa Spika, Taasisi za Mafunzo zilizo Chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii:-

KWA KUWA, taasisi hizi zinakabiliwa na changamoto za ufinyu wa bajeti, wanafunzi wake kukosa ufadhili katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na kutofahamika miongoni mwa wananchi wengi;

NA KWA KUWA, hali hii inapelekea vyuo hivi kushindwa kuboresha miundombinu na kushindwa kufikia malengo ya udahili wa wanafunzi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali, iandae mpango maalumu wa kuboresha miundombinu ya kufundishia na

kujifunzia inayoendana na mahitaji ya sasa ya Kidijitali. Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ifanye tathmini ili kuwasaidia wanafunzi wanaodahiliwa katika vyuo hivi kunufaika na fursa ya mikopo ya elimu ya juu. Serikali iandae mpango madhubuti wa kuvitangaza vyuo hivi ili kuvutia wanafunzi wengi kujiunga na vyuo hivi.

Mheshimiwa Spika, Uchelewaji wa Maandalizi ya Kongresi ya 50 ya Shirikisho la *APIMONDIA*:-

KWA KUWA, uchelewaji huo unaweza kupelekea Tanzania kupokonywa nafasi ya kuwa mwenyeji wa Mkutano huo;

NA KWA KUWA, hali hiyo itaathiri nafasi ya nchi yetu katika mtandao wa Kimataifa na kukosa ujuzi toka nje kwa watalaam wa sekta ya nyuki nchini;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ikamilishe taratibu za maandalizi ya Mkutano huo ikiwa ni pamoja na kupata fedha na eneo kwa ajili ya ujenzi wa Ukumbi. Taarifa ya hatua iliyofikiwa katika maandalizi hayo iwasilishwe kwa Katibu wa Bunge kabla ya tarehe 10 Machi, 2025.

Mheshimiwa Spika, uchelewa kwa tekelezaji wa Mradi wa REGROW:-

KWA KUWA, utekelezaji wa shughuli zinazotekelezwa chini ya mradi huu umechelewa kukamilika kwa wakati;

NA KWA KUWA, ucheleweshaji huo unaathiri mradi kwa kuongeza gharama za utekelezaji na kuchelewa kupatikana kwa manufaa yake katika sekta ya utalii nchini;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa shughuli zote zilizopangwa katika mradi huo zinakamilika hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2025. Serikali ichukue hatua za kimkataba wa Wakandarasi ambao hawajamaliza miradi ikiwa ni pamoja na kuwatoza gharama za upotevu wa muda ili kufidia

ongezeko la gharama za mradi kwa sababu ya ucheleweshaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF):-

KWA KUWA, mfuko huu unakabiliwa na uhaba wa bajeti na majukumu yake kutofahamika miongoni mwa wananchi wengi nchini;

NA KWA KUWA, changamoto hizo zinawanyima fursa wananchi wengi kupata manufaa ya Mfuko huo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe inausimamia Mfuko ili kuongeza uwezo wake wa kuhudumia maombi yote ya ruzuku yanayowasilishwa kwake. Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii ibuni mkakati wa kutangaza fursa zinazopatikana kupitia Mfuko ili kuongeza idadi ya wanufaika wa mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, Hoteli na *Lodge* zilizobinafsishwa na Serikali kwa Wawekezaji:-

KWA KUWA, imebainika kuwa kuna baadhi ya hoteli na *Lodge* za Serikali ambazo wawekezaji wamekiuka masharti ya ubinafsishaji;

NA KWA KUWA, hali hiyo imesababisha hoteli na *lodge* hizo kushindwa kufanya kazi kwa mujibu wa mikataba ya ubinafshaji na kupoteza manufaa ya kuwepo kwa hoteli hizo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae taarifa kuhusu hatua iliyofikiwa katika majadiliano yanayoongozwa na Wakili Mkuu wa Serikali kwa ajili ya mchakato wa kuzirejesha hoteli na *Lodge* hizo Serikalini. Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Ofisi ya Msajili wa Hazina, ifanye tathmini na ufuatiliaji kuhusu utendaji wa hoteli na *Lodge* zote zilizobinafsishwa nchini na kuwasilisha taarifa yake kwa Katibu wa Bunge kabla ya tarehe 10 Machi, 2025.

Mheshimiwa Spika, hali ya miundombinu katika maeneo ya hifadhi nchini:-

KWA KUWA, miundombinu ya barabara, madaraja na viwanja vya ndege katika maeneo ya hifadhi siyo nzuri na fedha zinazotengwa kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa miundombinu hiyo hazitoshi;

NA KWA KUWA, hali hiyo inaathiri utekelezaji shughuli za uhifadhi na kushindwa kuhudumia idadi ya watalii nchini inayozidi kuongezeka kila mwaka;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae mpango madhubuti wa muda mrefu kwa kutenga bajeti mahususi kwa ajili ujenzi na ukarabati wa kudumu wa miundombinu hiyo. Serikali ihakikishe inapeleka fedha za matengenezo na ukarabati wa miundombinu katika mpango wa muda mfupi ili kunusuru miundombinu hiyo kwa sasa.

Kwa upande wa *TANAPA* Serikali ihakikishe inaijengea uwezo kampuni ya ujenzi ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)* ili iweze kuwa inafanya ujenzi na ukarabati wa mara kwa mara katika miundombinu ya hifadhi nchini.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa makumbusho ya Marais:-

KWA KUWA, hatua za awali za usanifu wa mradi huu unaolenga kuendeleza uhifadhi katika urithi wa asili ulitakiwa kuanza ndani ya mwaka wa fedha 2024/2025;

NA KWA KUWA, mradi huo una faida ya kulifanya Taifa letu kuwa kitovu cha fikra na kutoa tafsiri ya maendeleo kupitia tawala za nchi yetu baada ya uhuru;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe inatoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo kama zilizoidhinishwa na Bunge ili usanifu wa mradi huo uanze mara moja.

Mheshimiwa Spika, Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi:-

KWA KUWA, imebainika kuwa zaidi ya 65% ya vijiji nchini havina mipango ya matumizi ya ardhi;

NA KWA KUWA, hali hii inachangia migogoro baina ya watumiajii wa ardhi nchini;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae Mpango Madhubuti ambao utaiwezesha Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kupata fedha kwa ajili ya kuandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi kwa vijiji vyote nchini.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa Maboresho ya Mfumo wa Usimamizi wa Ardhi Nchini:-

KWA KUWA, utekelezaji wa maboresho ya Mfumo wa Usimamizi wa Ardhi nchini umechelewa kwa zaidi ya mwaka mmoja;

NA KWA KUWA, ucheleweshaji huo umechangia kuendelea kuwepo kwa changamoto ya utunzaji wa kumbukumbu kwa wananchi kunakochangiwa na watumishi wasio waaminifu katika sekta hiyo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ijipange kukamilisha mfumo huo ili kutatua changamoto ya utunzaji wa kumbukumbu za taarifa katika sekta ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*:-

KWA KUWA, Shirika halijakamilisha baadhi ya miradi ya kimkakati kinyume na lengo la kuikamilisha kufikia mwaka 2025, huku kukiwa na malalamiko ya shirika kujenga nyumba za bei ghali;

NA KWA KUWA, hali hiyo inachangia miradi hiyo kutekelezwa kwa gharama kubwa na kupunguza manufaa ya miradi hiyo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali, ilisimamie Shirika hilo kukamilisha mradi wa Kawe 711 kufikia tarehe 30 Juni, 2026, kwani utekelezaji wake umefikia 50% tu. Serikali ihakikishe majadiliano kati ya Shirika na Wakandarasi katika miradi ya *Golden Premium* na Kiwanja Na. 300 R*egent Estate* yanafikia mwisho kufikia tarehe 30 Juni, 2025 ili kukwamua miradi hiyo ambayo utekelezaji wake umesimama tangu mwaka 2017.

Serikali ilipe madeni kwa Shirika ikiwa ni malimbikizo ya kodi ya pango na gharama ya huduma ya ukandarasi wa ujenzi wa majengo ya Wizara nane kwenye Mji wa Serikali Mtumba. Serikali ilisaidie Shirika kutimiza azma ya kujenga nyumba za gharama nafuu kwa kuondoa kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* kwa nyumba zinauzouzwa kwa bei isiyozidi Shilingi milioni 100 badala ya Shilingi milioni 50 ya sasa ili kuwafanya wananchi na wafanyakazi kuweza kumudu ununuzi wa nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa Vijiji 333 katika mwaka 2024/2025:-

KWA KUWA, muda wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025 umefikia 50% huku kukiwa hakujatolewa fedha za kutekeleza ya program hiyo;

NA KWA KUWA, hali hii inayoweza kufanya lengo la Programu hiyo lisikamilke kama ilivyopangwa;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itoe kiasi cha Shilingi bilioni tano kama ilivyoahidi ili kuhakikisha programu hiyo inatekelezwa kama ilivyopangwa.

Serikali itenge fedha zaidi katika bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 ili kufanya kazi ya mipango ya matumizi ya ardhi kuwa kazi endelevu.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi nchini:-

KWA KUWA, 70% ya halmashauri na taasisi zilizokopeshwa fedha kwa ajili ya kutekeleza program hii zimeshindwa kurejesha fedha hizo tangu mwaka 2018;

NA KWA KUWA, hali hiyo inakwamisha azma ya Serikali kupanga na kupima ardhi yote nchini;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ihakikishe inazisimamia Halmashauri zote kurudisha kiasi cha shilingi bilioni 22.5 walizokopeshwa kwenye mradi huu ili ziweze kutumiwa na Wizara ya kisekta katika kuendelea kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwenye Halmashauri zote nchini;

(ii) Serikali kupitia Wizara ya Ardhi ihakikishe inafanya uchambuzi wa maandiko ya halmashauri zinazoomba mikopo kupitia programu hiyo ili kujiridhisha kama zina uwezo wa kurejesha fedha hizo; na

(iii) Serikali kupitia Wizara ya Ardhi ihakikishe inalinda uhai wa Mfuko wa Mzunguko wa Maendeleo ya Ardhi *(Plot Development Revolving Fund)* ili uendelee kuwa chanzo cha uhakika cha fedha kwa ajili ya Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

KWA KUWA, Serikali iliamua ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi ufanywe na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na pango la Ardhi;

NA KWA KUWA, uamuzi huo umetoa matokeo hasi katika ufuatiliaji wa makusanyo hayo, kwani Wizara haina fedha za

kutosha kwa ajili ya shughuli hiyo na halmashauri ambazo zimepewa jukumu hilo hazilitekelezi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali irudishe jukumu la ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi katika Wizara ya Ardhi ambayo ndiyo ina nyenzo za kisheria na kimfumo katika kutekeleza jukumu hilo;

(ii) Serikali iiwezeshe kifedha Wizara ya Ardhi katika kutimiza jukumu hilo kwa kuruhusu ibaki na 20% ya makusanyo ya Kodi ya Pango la Ardhi kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika zoezi hilo;

(iii) Serikali kupitia Wizara ya Ardhi ihakikishe inaongeza nguvu katika kukusanya maduhuli ili kufikia lengo la makusanyo katika mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ardhi ya wawekezaji ambayo haijaendelezwa:-

KWA KUWA, imebainika uwepo wa uhaba wa ardhi kwa wananchi wanaoishi na kuzunguka baadhi ya maeneo ambayo yako chini ya wawekezaji wenye mashamba makubwa huku mashamba hayo yakiwa haijaendelezwa kwa mujibu wa sheria;

NA KWA KUWA, hali hiyo huchangia migogoro inayosababosha maafa, majeruhi na uharibifu wa miundombinu na mali kati ya wawekezaji na wananchi katika maeneo husika;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye tathmini ya wamiliki wa mashamba makubwa yote nchini ili kutambua ambayo hajaendelezwa na kuchua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu utatuzi wa migogoro ya ardhi katika Jiji la Dodoma:-

KWA KUWA, Jiji la Dodoma ni moja ya sehemu zenye migogoro mingi ya ardhi nchini;

NA KWA KUWA, migogoro mingi inachangiwa na uwepo wa watumishi wasio waaminifu na wasiozingatia sheria katika sekta ya ardhi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kuwa:-

(i) Serikali ihakikishe kuwa miamala yote ya ardhi katika Jiji la Dodoma inafanyika katika Mfumo wa *e-Ardhi* ambao tayari unafanya kazi katika jiji hilo;

(ii) Serikali ifanye tathmini na uhakiki wa huduma zinazotolewa na kila mtumishi katika Ofisi ya Ardhi Jijini Dodoma ili kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wasiowaaminifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1985, Toleo la Mwaka 2023;

KWA KUWA, Sera hiyo imebainisha changamoto ya kutokuwepo kwa mipango ya matumizi ya ardhi katika eneo la mipakani;

NA KWA KUWA, hali hiyo inawanyima wananchi wa mipakani fursa ya kupata manufaa yanayopatikana katika sekta ya ardhi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali iandae mpango wa matumizi ya ardhi katika maeneo ya mipakani kwa kuzingatia usalama wa nchi ili kuleta ustawi wa wananchi katika maeneo ya mipakani kupitia sekta ya ardhi;

(ii) Serikali ifanye uwekezaji wa miundombinu ya barabara katika maeneo ya mipakani ili kuchochea shughuli za

maendeleo na kurahisisha utekelezaji wa shughuli za ulinzi katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa namna ya kipekee napenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Mafanikio ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii katika kutekeleza shughuli zake kwa kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025 yametokana na juhudi, weledi pamoja na umahiri mkubwa wa Wajumbe katika kushiriki na kutoa maoni yenye tija wakati wote ambapo Kamati imekuwa ikifanya kazi ya kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba, ufanisi wa utendaji wa Kamati hii unatokana zaidi na ofisi yako kuwajengea uwezo Wabunge na kuwapa msaada stahiki wa kitaalam, na kiushauri wakati wote. Kwa heshima kubwa ningependa kuwataja Wajumbe wote wa Kamati. Hata hivyo, kwa sababu ya ufinyu wa muda naomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyoorodheswa kwenye Taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, na Naibu wake Mheshimiwa Geofrey Pinda, Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, na Naibu wake Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano walioуonyesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wote wa Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji

shughuli hizo na pia maoni na mapendekezo ya Kamati, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII KUHUSU SHUGHULI ZA KAMATI KWA KIPINDI CHA FEBRUARI, 2024 HADI JANUARI, 2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niwasilishe taarifa hii ya Kamati. Aidha nitumie nafasi hii, kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa namna walivyojitoa kikamilifu kutekeleza majukumu yao kwa moyo na weledi mkubwa na hivyo kuwezesha Kamati kukamilisha taarifa kwa wakati na ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii zilizotekelezwa na kamati kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Februari 2024 hadi Januari, 2025.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne (4) kama ifuatavyo:-

i) Sehemu ya Kwanza inatoa Utangulizi wenye kueleza Muundo na Majukumu ya Kamati, na kuanisha shughuli zilizotekelezwa na Kamati;

ii) Sehemu ya Pili inafafanua namna Kamati ilivyotekeleza Majukumu yake na yaliyobainika wakati wa utekelezaji huo;

iii) Sehemu ya Tatu inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati; na

iv) Sehemu ya Nne inahitimisha taarifa.

## 1.1 Muundo na Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ni miongoni mwa Kamati za Kisekta za Bunge lako Tukufu. Kamati hii inaundwa kwa kujumuisha aina mbalimbali za Wabunge kama inavyoelekezwa na kanuni ya 135 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** Majukumu ya Kamati za Kisekta, yamebainishwa katika Kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Majukumu hayo ni kama ifuatavyo: -

a) Kushughulikia Bajeti za Wizara au Taasisi inazozisimamia;

b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara hizo; na

d) Kufuatilia Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara na Taasisi zake.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu Kifungu cha 6(8) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati hii ina jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii. Aidha, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba

Kamati imetekeleza kikamilifu wajibu wake katika kuzingatia matakwa ya Kanuni hiyo.

### 1.2 Msingi wa Utekelezaji wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati umejengwa katika dhana ya Kikatiba kupitia ibara ya 8(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ambapo inaelekeza kuwa lengo kuu la Serikali ni ustawi wa wananchi. Ibara ya 62 na 63 zinasisitiza juu ya Wananchi kushiriki katika shughuli za Serikali yao kupitia chombo chao cha Uwakilishi ambacho ni Bunge. Katika ibara ya 96, Katiba inaelekeza Bunge kuunda Kamati mbalimbali ili kurahisisha na kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake ya kuisimamia na kuishauri Serikali. Hivyo, basi Kamati inapotekeleza majukumu yake inafanya kwa niaba ya Bunge zima na wananchi kwa ujumla katika kuhakikisha kuwa Serikali inatimiza wajibu wa kuleta ustawi wa watu wake.

### 1.3 Njia na Mbinu Zilizotumika

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha shughuli za Kamati, zinatekelezwa kikamilifu, ikiwa ni pamoja na kuzingatia Katiba na Kanuni za Kudumu za Bunge ili kufikia lengo la kuleta ustawi wa wananchi ambao ndio tunaowawakilisha, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilitumia mbinu na njia mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake. Njia hizo ni kama zifuatavyo: -

i) Vikao vya kupokea, kuchambua na kujadili taarifa za Wizara na taasisi zake kwa lengo la kufahamu utendaji wao, mafanikio na changamoto zinazowakabili wakati wa utekelezaji wa majukumu yao;

ii) Ziara za ukaguzi wa maeneo na miradi ya maendeleo kwa lengo la kujiridhisha hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wake kwa kulinganisha na taarifa iliyowasilishwa katika vikao vya Kamati; na

iii) Kushiriki mafunzo, semina na warsha mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na wizara, mashirika ya umma, taasisi binafsi, asasi za
Kiraia na wadau wengine katika Sekta zinazosimamiwa na Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kutumia mbinu hizi tofauti ni kuwawezesha wajumbe wa Kamati kujielimisha kwa kiwango cha kutosha katika sekta ambazo wanawajibika kuzisimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya Bunge na wananchi kwa ujumla.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA YALIYOBAINIKA

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Februari, 2024 hadi Januari, 2025, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilifanikiwa kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Miongoni mwa Shughuli ambazo zilitekelezwa na Kamati katika kipindi hicho ni hizi zifuatazo:-

(i) Kufanya Ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(ii) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti kwa Wizara ya Ardhi,Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na mwelekeo wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iii) Kupokea, kuchambua na kujadili taarifa za utendaji wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi zinazosimamiwa na Wizara hizo;

(iv) Kushiriki Semina na warsha za mafunzo; na

(v) Kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotokana na taarifa ya mwaka ya kamati.

## 2.1 Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati kwa 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** katika taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati iliyowasilishwa Bungeni tarehe 08 Februari, 2024, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ililiomba Bunge lako Tukufu kukubali na kuridhia mapendekezo mbalimbali kwenye sekta za Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na ile ya Maliasili na Utalii kuwa maazimio ambayo yangetekelezwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inalishukuru Bunge lako Tukufu, kwani kwa kauli moja, liliridhia mapendekezo yaliyowasilishwa na hivyo kuwa maazimio ya Bunge. Kamati ilipata muda wa kufuatilia utekelezaji wa maazimio hayo na kupokea taarifa ya utekelezaji kutoka Serikalini katika sekta inazozisimamia kama ifuatavyo:-

### 2.1.1 Sekta ya Maliasili na Utalii

**Mheshimiwa Spika**, Bunge lilitoa maazimio kumi (10) ambayo yalitakiwa kutekelezwa na Serikali katika Sekta ya Maliasili na Utalii. Serikali iliwasilisha mbele ya Kamati taarifa ya utekelezaji wa maazimio hayo. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, sehemu kubwa ya maazimio imetekelezwa pamoja na kuwa kuna changamoto ya utekelezaji katika baadhi ya maazimio.

**Mheshimiwa Spika,** Mathalani, katika azimio la Serikali kuruhusu Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Eneo la Ngorongoro (NCAA) kubaki na sehemu ya sehemu ya Makusanyo yake (Retention), Kamati ilitarifiwa kuwa Serikali ilifanya maandalizi yote kwa ajili ya utekelezaji wa Azimio hilo katika mchakato wa Kupitisha Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya Mwaka 2024/2025 iliyowasilishwa Bungeni tarehe 31 Mei,

2024. Hata hivyo, wakati wa kupitisha Bajeti Kuu ya Serikali, Serikali haikutekeleza Azimio hilo la Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, azimio hili lililenga kuongeza uwezo wa taasisi hizi katika kukarabati na kujenga miundombinu ya barabara na viwanja vya ndege. Katika utaratibu wa sasa ambapo taasisi hizi zinapangiwa ukomo wa bajeti na kusubiri mgawo wa fedha za uendeshaji kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, unazifanya taasisi hizi kuwa na uwezo mdogo wa kutekeleza majukumu yake kwa Ufanisi. Kwa upande mwingine, taasisi hizi zinachangia zaidi ya **asilimi 80** ya mapato yote yanayotokana na shughuli za utalii nchini lakini hazina miundombinu ya kuhimili ongezeko kubwa la Watalii hifadhini. Hali hii inaweza kupelekea kushindwa kupata tija zaidi kutokana na shughuli za utalii nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Maazimio mengine ambayo Kamati haikuridhika na Utekelezaji wake ni pamoja na Serikali kuandaa na kuleta Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA) na Serikali kuhakikisha inapandisha Hadhi ya Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) kuwa Mamlaka. Maazimio haya sio mapya kwani kwa takribani miaka 5 iliyopita (2019-2024), Bunge limekuwa likiiagzia Serikali kutekeleza maazimio haya kwa lengo la kuimarisha Sekta ya Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu nchini.

### 2.1.2 Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Mheshimiwa Spika,** katika sekta hii, Kamati ilitoa mapendekezo **nane (8)** ambayo Bunge lako Tukufu liliridhia na kuwa maazimio ya Bunge. Katika maazimio hayo, Kamati inapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imetekeleza kwa ukamilifu maazimio matau (3) na maazimio matano (5) yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kwani utekelezaji wake ni endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, baadhi ya maazimio kasi ya utekelezaji wake hairidhishi. Mathalani, utekelezaji wa kasi ya kusambaza mfumo wa e-Ardhi ni ndogo sana na ipo nyuma ya wakati kwani katika Halmashauri zote **184** nchini, Wizara

imefanikiwa kusambaza mfumo huo kwenye Halmashauri **20** sawa na **asilimia 10.9** tu. Hii ni kinyume na ahadi iliyotolewa na Wizara katika Hotuba ya Bajeti ya Mwaka wa fedha 2023/2024 ambapo, Wizara iliahidi kuwa itakuwa imesambaza mfumo huo kwa Halmashauri zote nchini kufikia Mwezi Juni, 2024.

## 2.2 Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilipanga kufanya ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ipatayo Saba (07) iliyopo katika Mikoa ya Lindi, Pwani, Dar es Salaam na Tanga. Miradi iliyotembelewa na kukaguliwa ni pamoja na:-

a) Mradi wa kuwawezesha Watalii katika Hifadhi ya Urithi wa Dunia ya Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara unaotekelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyapori (TAWA);

b) Mradi wa UVIKO -19 Pugu/ Kazimzumbwi unaotekelezwa na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS);

c) Mradi wa Kituo cha Kutangaza Utalii Kidigitali (Destination Digital Marketing Command Centre – DDMCC) unaotekelezwa na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB);

d) Mradi wa kukuza Utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Saadan;

e) Mradi wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi katika Halmashauri ya Ruangwa;

f) Mradi wa Kupanga Kupima na Kumilikisha Ardhi – KKK katika halmashauri ya Chalinze; na

g) Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Adhi (LTIP) katika Manispaa ya Kinondoni

### 2.2.1 Utekelezaji wa Miradi ya Sekta Maliasili na Utalii

**a) Mradi wa Kuwezesha Watalii katika Hifadhi ya Urithi wa Dunia ya Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songa Mnara unaotekelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA)**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulitekelezwa kwa thamani ya **Shilingi 1,449,387,245.00** zilizoidhinishwa na Bunge. Lengo lake ni kuwezesha shughuli za utalii katika Hifadhi ya Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara ambayo ipo katika Wilaya ya Kilwa Mkoa wa Lindi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa Mradi huu ni sehemu ya mkakati wa kuirejesha sekta ya utalii baada ya athari za **UVIKO -19.** Mradi huu umekamilika kwa **asilimia 100** na tayari umeanza kutumika.

***b) Mradi wa UVIKO – 19 Pugu/Kazimzumbwi Unaotekelezwa na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS)***

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulitekelezwa kwa jumla ya **Shilingi 658,267,957.19**. Utekelezaji wake ulihusisha ujenzi Barabara ya **kilometa 12** kutoka Kimani-Maguruwe na ukarabati wa barabara ya **kilometa 1** kutoka Minaki – Bwawani. Shughuli nyingine ni ujenzi wa **kilometa 7** za njia za watembea kwa miguu na Ujenzi wa lango la kuingilia kwenye ofisi, kituo cha taarifa za utalii, ofisi ya malipo na kibanda cha mlinzi.

**Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, mradi huo ulihusisha ujenzi wa makalavati na madaraja ili kulinda miundombinu hiyo dhidi ya mvua kubwa zinanyesha katika msitu wa Pugu/Kazimzumbwi. Aidha, Mradi huu umekamilika kwa **asilimia 100,** na tayari umeanza kutumika katika shughuli za uhifadhi na utalii.

***c) Mradi wa Kituo cha Kutangaza Utalii Kidigitali (Destination Digital Marketing Command Centre – DDMCC)***

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulitekelezwa na kupitia Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) ukiwa umegharimu jumla ya **Shilingi 1,372,256,210.07.** Lengo la Kituo hicho ni kutangaza vivutio vya Utalii nchini kidijitali na kutoa taarifa sahihi kuhusu fursa za uwekezaji katika sekta ya utalii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa utekelezaji wa mradi huu umekamilika kwa **asilimia 100** na ulihusisha ujenzi miundombinu ikiwemo chumba cha kurushia matangazo, ununuzi wa vifaa, samani na mifumo ya kurushia matangazo.

Hata hivyo, Kamati inapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kituo hiki hakijaanza kufanya kazi ili kupata manufaa yake kama ilivyoripotiwa katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kamati imegundua kuwa upo uwekezakano wa makusudi wa utendaji wa kituo hicho kuhujumiwa.

***d) Mradi wa Kukuza Utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Saadan***

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unalenga kuchochea ukuaji wa sekta ya Utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Saadani na unatekelezwa na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kwa jumla ya **Shilingi 2,023,128,519.23.**

Utekelezaji wa mradi huu ulihusisha ujenzi wa vyoo vya kisasa katika uwanja wa ndege wa Saadan na eneo la kupiga mahema, ukarabati wa barabara mbalimbali ndani ya hifadhi, ujenzi wa bwalo la chakula na kisima cha kuvuna maji ujazo wa lita 1000 pamoja na ununuzi wa samani kwa ajili ya matumizi ya hosteli.

Aidha, mradi huu umefikia **asilimia 80** na unatarajiwa kukamilika pale fedha zilizobakia zitakapopokelewa kutoka hazina.

### 2.2.2 Utekelezaji wa Miradi ya Sekta ya Ardhi

**a) Mradi Namba 4951: Upangaji wa Matumizi ya Ardhi**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa na Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ukihisisha Halmashauri za Wilaya 14 Nchini. Kamati ilitembelea utekelezaji wa mradi huu katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa ambapo mradi ulijumuisha kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi katika vijiji 16.

**Mheshimiwa Spika,** Vijiji hivyo ni Chikwale, Chiundu, Nambilanje, Mkaranga, Namkatila, Namkonjela, Nangandala, Nanjaru, Mbecha, Chikoko, Likwachu, Mibure, Chilangalile na Litama. Mathalani katika Kijiji cha Namkatila ambapo Kamati ilifika na kujionea utekelezaji wa mradi, Tume ilikuwa imefanikiwa kupanga Matumizi ya Ardhi yote ya Kijiji hicho na Kamati ilishiriki katika utoaji wa hati zipatazo 25 kwa Wananchi wa kijiji hicho.

***b) Mradi Namba 2326: Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi – KKK***

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa kwa utaratibu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutoa mikopo ya fedha isiyo na riba kwa Halmashauri nchini. Kamati ilitembelea Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze ambapo ilipokea Mkopo riba wa Shilingi **2,500,000,000.00.** Mkopo huo ulitumika kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika maeneo ya Msolwa na Chamakweza yenye ukubwa wa **ekari 440.34.**

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa mradi huu umekamilika na Halmashauriya ya Wilaya ya Chalinze inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 4,500,000,000.00** ambapo itapata faida ya **Shilingi 2,000,000,000.00** baada ya kurudisha kiasi walichokopeshwa. Hata hivyo, marejesho ya Mkopo huo bado yanasuausa kwani hadi Kamati inatembelea mradi huo, Halmashauri hiyo ilikuwa imerejesha kiasi cha **Shilingi 300,000,000.00** tu sawa na **asilimia 12** ya deni fedha inayotakiwa kurejeshwa.

**c) Mradi Namba 4953: Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP)**

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa mradi huu ulilenga kuboresha Usalama wa miliki na utoaji wa huduma za ardhi kwa wananchi katika Halmashauri 67 kwenye mikoa 15 nchini. Kamati ilitembelea eneo la Bunju katika Halmashauri ya Kindoni ili kukagua shughuli mbalimbali zinazofanyika katika utekelezaji wa mradi huo.

**Mheshimiwa Spika,** moja ya shughuli zilizokuwa zikiendelea ilikuwa ni uendeshaji wa Kliniki za Ardhi ambapo wananchi walipatiwa huduma za ardhi katika eneo moja. Huduma zilizokuwa zinatolewa ni pamoja na Kupanga, Kupima, Kumilikisha Ardhi; utatuzi wa migogoro ya ardhi; utolewaji wa hati za ardhi; na elimu kwa umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata nafasi ya kushiriki katika kusikiliza kero za wananchi kuhusu ardhi na kutoa hati za umiliki wa ardhi katika eneo hilo. Aidha, Kamati ilipongeza utaratibu huo na kutaka uwe endelevu kwa ajili ya utatuzi wa kero za ardhi katika maeneo mengine nchini.

### 2.2.3 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kutoa maoni ya jumla katika eneo la ukaguzi wa miradi kama ifuatavyo:-

a) Serikali ishirikishe Wananchi katika kutunza miradi iliyotekelezwa ikiwa ni pamoja na kufanya ukarabati ili kuzuia uchakavu na kuifanya miradi hiyo itumike kwa muda mrefu hivyo kupata tija iliyokusudiwa;

b) Bajeti ya Tume ya Mipango ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi iendelee kuongezwa ili kuiwezesha Tume kupanga vijiji vingi zaidi hali itakayopunguza migogoro ya ardhi nchini na kuongeza thamani ya Ardhi kwa wananchi, kukuza uchumi na kuongeza mapato ya Serikali kwa njia ya Kodi ya Ardhi; na

c) Serikali ihakikishe Kituo cha Kutangaza Utalii Kidijitali (DDMCC) kinaanza kufanya kazi mara moja ili kupata manufaa ya fedha zilizotumika katika ujenzi wa kituo hicho.

## 2.3 Kushughulikia Bajeti za Wizara

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitekeleza jukumu hili la kuchambua na kupitia bajeti za Wizara zote mbili na taasisi zake. Jukumu hili ni kwa mujibu wa fasili ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

### 2.3.1 Mpango wa Makadirio wa Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2024/2025

#### *i) Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69)*

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara inakadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 968,842,018,480/=.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 213,419,063,000/=** zitakusanywa na Idara za Wizara pamoja na baadhi ya taasisi na **Shilingi 755,422,955,480** zitakusanywa kutoka vyanzo vya Taasisi za TANAPA, NCAA na TAWA na kuwasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa matumizi, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ilitengewa na kuinidhishiwa na Bunge lako Tukufu kiasi cha **Shilingi 708,891,841,026/=** ikiwa ni ongezeko lako **asilimia 8.3** kulinganisha na mwaka wa fedha 2023/2024 ambapo Wizara ya Maliasili na Utalii iliidhinishiwa **Shilingi 654,668,208,000/=.**

Kwa upande wa fedha za kutekeleza miradi ya Maendeleo, Bunge liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 176,392,513,000/=,** kati ya hizo **Shilingi 100,225,838,000/ =** sawa na **asilimia 57** ya fedha zote za maendeleo ni fedha za ndani na Shilingi **76,166,675,000/=** sawa na **asilimia 43** ni fedha za nje.

**ii) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48)**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara iliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 250,000,000,000/=.** Makusanyo hayo yanategemea kutoka katika vyanzo mbalimbali ambavyo ni kodi ya pango la ardhi, tozo na ada za aina tofauti.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu kiasi cha **Shilingi 157,455,085,000/=** ikiwa ni pungufu ya asilimia 3.5 kulinganisha na mwaka 2023/2024 Wizara hii ilitengewa **Shilingi 163,169,880,000/=**. Aidha, katika fedha hizo, kiasi cha Shilingi **70,656,510,000/=** kilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo **Shilingi 10,601,757,000/=** ni fedha za ndani na Shilingi **60,054,753,000/=** zikiwa ni fedha za nje.

***iii) Tume ya Matumizi bora ya Ardhi (Fungu 03)***

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Tume iliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 1,018,000,000/=.** Makusanyo hayo yanategemea kutoka katika vyanzo mbalimbali ambavyo ni kodi pango ya nyumba za Tume zilizopo Tabora na michango ya wadau.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi katika mwaka wa fedha 2024/2025, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya **Shilingi 12,173,330,000/=** ikiwa ni ongezeko la **asilimia 32.6** kulinganisha na mwaka 2023/2024 ambapo iliinishiwa **Shilingi 8,202,628,000/=** kwa ajili ya kuiwezesha Tume kupima na kupanga ardhi ya nchi yetu. Katika fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 5,041,232,000/=** kilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo zote ni fedha za ndani.

### 2.3.2 Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka kati ya Julai-Desemba 2024

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kuchambua utekelezaji wa bajeti za Wizara zote mbili kwa kipindi cha nusu Mwaka

kuanzia Julai hadi Disemba, 2024. Katika uchambuzi huo, Kamati ilijikita katika kuangalia ukusanyaji wa maduhuli na fedha zilizopokelewa na Wizara na Taasisi zake.

*i) Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69)*

**Mshemiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2024, Wizara na taasisi zake ilikuwa imefanikiwa kukusanya maduhuli ya Serikali kiasi cha **Shilingi 638,500,494,403/=** sawa na **asilimia 66** ya lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Fedha za Matumizi toka Hazina, Wizara na taasisi zake ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi 320,842,436,482.12** ikiwa ni fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2024. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 45.26** ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** katika fedha hizo kiasi cha **Shilingi 281,203,787,834.80** ni fedha za matumizi ya kawaida ikiwa ni pamoja na mishahara na matumizi mengineyo sawa na **asilimia 52.81** ya lengo. Kwa upande mwingine, fedha za maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi 39,638,648,647.32** tu sawa **asilimia 22.5** ya lengo. Kwa kuzingatia umuhimu wa Sekta ya Uhifadhi na Utalii nchini katika kukuza uchumi, kuwa kinara katika kuchangia fedha za kigeni na mchango wake katika kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi, Kamati haijaridhishwi na mtiririko wa fedha za Maendeleo kutoka Hazina kwenda katika wizara na taasisi zake.

**Mheshimiwa Spika,** hali ya miundombinu katika maeneo ya vivutio vya utalii sio ya kuridhisha kwani baadhi ya barabara, viwanja vya ndege na madaraja hayapitiki. Pia, kuna upungufu wa hoteli na mabanda kwa ajili ya malazi ya watalii. Vivile, sehemu za vivutio vya mali kale vimechakaa na havijafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu. Ili kuweza kuhudumia watalii walioongezeka kutokana na juhudi kubwa za Serikali kukuza utalii, kuna haja ya kufanya jitihada za makusudi katika kuhakikisha

kuwa Wizara na taasisi zake wanapewa fedha zote za miradi ya maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge.

*ii) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48)*

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Disemba, 2024 Wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi bilioni 101** sawa na **asilimia 40.4** ya makusanyo yaliyoidhinishwa na Bunge ambapo ni **Shilingi bilioni 250.** Lengo hili ni pungufu ya **asilimia 9.6** kulinganisha na kipindi cha utekelezaji wa bajeti ambapo ilitarajiwa kuwa **asilimia 50** ya lengo kuwa limefikiwa yaani **Shilingi bilioni 125.**

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wake wa kina, Kamati imegundua sababu mbalimbali zilizosababisha Wizara kushindwa kufikia lengo la Makusanyo kwa kipindi cha nusu mwaka katika utekelezaji wa bajeti. Aidha sababu hizo ni pamoja na:-

(i) Muingiliano wa majukumu baina ya Wizara na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kukusanya kodi ya pango la ardhi;

(ii) Baadhi ya Mashirika na Taasisi za Serikali kushindwa au kuchelewa kulipa kodi ya pango la ardhi;

(iii) Uhaba wa vitendea kazi na watumishi katika utekelezaji wa zoezi la kukusanya maduhuli hasa kodi ya pango la ardhi,

(iv) Mwitikio mdogo wa wananchi katika kulipia kodi ya pango la ardhi kwa hiari; na

(v) Wananchi kuchanganya kati kodi ya pango la ardhi na ile ya kodi ya majengo inayolipiwa katika Ankara za umeme kwa njia ya LUKU.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi, hadi kufikia Disemba, 2024 Wizara ilipokea kiasi cha **Shilingi 69,652,301,863.86**. Kiasi hiki kilichopokelewa ni sawa na **asilimia 37.35** ya bajeti yote kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Katika fedha zilizopokelewa

kiasi cha **Shilingi 37,410,769,500.000** zilizokuwa ni fedha za ndani za Maendeleo. Aidha, Wizara na taasisi zake ilikuwa imetumia **asilimia 94** ya fedha zote ilizokuwa imezipokea toka hazina.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Wizara ilipokea kiasi cha **Shilingi 32,238,481,000/=** ikiwa ni fedha kwa ajili ya kulipa madeni mbalimbali ya Wizara. Kamati inapenda kuipongeza Serikali kupitia Hazina kwa kuhakikisha Wizara inapokea fedha hizi ili kulipa madeni yakiwemo ya wazabuni, wakandarasi na watumishi wake. Ongezeko la kiasi hiki cha fedha, kinafanya jumla ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2024/2025 kuwa kiasi cha **Shilingi 189,693,566,000/=.**

***iii) Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03)***

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Disemba, 2024 Tume ilipokea kiasi cha **Shilingi 5,117,722,500/=.** Kiasi hiki kilichopokelewa ni sawa na **asilimia 42** ya bajeti yote kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Katika fedha zilizopokelewa kiasi cha **Shilingi 2,205,722,500/=** zilizokuwa ni fedha za ndani za Maendeleo. Aidha, Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2024, Tume ilipokea na kutumia fedha kutoka Wakala wa Misitu Tanzania (TSF) na Frankfurt Zoological Society (FZS) jumla ya **Shilingi 486,855,055/=** ambazo zimewezesha shughuli za Upangaji wa Matumizi ya ardhi katika Halmashauri za Mlele, Sikonge, Urambo, Kaliua na Bariadi.

### 2.4 Kufuatilia Utekekelezaji wa Shughuli zinazotekelezwa na Wizara

**Mheshimiwa Spika,** fasili ya 7(1)(d) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023 inazitaka Kamati za Kisekta kufanya ufuatiliaji wa shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara zinazosimamiwa na Kamati. Aidha, Kamati pia ilifanya ziara za ufuatiliaji kwa lengo la kujiridhisha na tija inayopatikana katika miradi na program zinazotekelezwa na Wizara zinazosimamiwa na Kamati. Kutokana na Ziara hizo Kamati iliweza

kuwianisha taarifa zinazotolewa na Serikali kuhusu tija na mafanikio na hali halisi iliyopo kwenye maeneo husika.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Sekta ya Maliasili na Utalii, Kamati ilitembelea na kukagua shughuli zinazotekelezwa katika Mradi wa Kuboresha Usimamizi wa Maliasili na Kukuza Utalii Kusini mwa Tanzania (REGROW). Katika ziara hiyo, Kamati ilitembelea Mkoani Iringa ambapo ilipata nafasi ya Kukugua hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi katika Hifadhi za Taifa za Ruaha, Kituo cha Utafiti wa Wanyamapori na Kituo cha Kutangaza Utalii Kusini mwa Tanzania.

Vilevile, Kamati ilitembelea na kukugua utekelezaji wa shughuli za mradi katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi na ile ya Udzingungwa Mkoani Morogoro ili kujiridhisha kama utekelezaji wa mradi wa REGROW unafanyika kwa tija na ufanisi. Aidha, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea katika Mikoa ya Tabora na Singida ambapo ilikagua utendaji wa Chuo cha Nyuki Tabora sambasamba na shughuli zinazotekelezwa katika sekta ya Misitu chini ya Ufadhili wa Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF).

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwingine, Katika sekta ya Ardhi, Kamati ilifanya ziara katika Mkoa wa Arusha ili kukagua shughuli zinazotekelezwa katika Mradi wa Kupima, Kupanga na Kumilikisha Ardhi (KKK) katika eneo ambalo Uwanja wa Mpira kwa ajili ya Michuano ya AFCON itafnyika. Aidha, Kamati ilitembelea Mkoa wa Kagera, Wilaya ya Misenyi ili kubaini mapungufu ya kutokuwepo utaratibu maalum wa kisera na kisheria wa kusimamia maeneo katika mipaka ya Tanzania.

### 2.4.1 Yaliyobainika wakati wa ufuatiliaji wa Sekta

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Februari, 2024 hadi Januari, 2025, Kamati ilipokea na kujadili taarifa 40 ambapo taarifa 15 ni za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na taarifa 25 ni za Wizara ya Maliasili na Utalii. Lengo la kupokea na kujadili Taarifa hizi ni kuiwezesha Kamati kulisaidia Bunge kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Ibara ya 63 (2)

ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo imelipa Bunge mamlaka ya Kuisimamia na Kuishauri Serikali.

### *2.4.1.1 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Maliasili na Utalii*

**Mheshimiwa Spika,** Katika Wizara za Kisekta nchini, Wizara ya Maliasili na Utalii imepewa dhamana ya kusimamia kisheria maeneo yenye ukubwa wa kilometa za mraba takriban **307,800**. Eneo hili ni sawa na **asilimia 32.5** ya eneo lote la nchi yetu ikuhisisha Uhifadhi wa Wanyamapori, Milima mbalimbali, Misitu, Ardhioevu, Nyuki, Malikale na Makumbusho ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Hii ni sekta mtambuka ikiwa na manufaa Kiikolojia na Kiuchumi. Sekta hii ni muhimili katika uhifadhi wa mazingira, uoto wa asili, viumbe hai, vyanzo vya maji na kuhakikisha usawa wa Kiiokolojia nchini na duniani. Kwa upande wa kiuchumi sekta hii inachangia zaidi ya **asilimia 25** ya fedha za kigeni nchini ikiwa ndio sekta kinara katika mauzo ya nje, pato la Taifa kwa zaidi ya **asilimia 20** na kuchangia ajira zaidi ya **milioni 1.6.** Uchambuzi wa taarifa uliofanywa na Kamati, umewezesha kubaini mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya sekta ya Maliasili na Utalii kwenye miradi na taasisi zake kama ifuatavyo:-

#### *a) Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA)*

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) ilianzishwa kwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 14 ya 1975 kwa lengo la kusimamia eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Hifadhi ya Ngorongoro (NCA) ni eneo la matumizi mseto ya ardhi lililoanzishwa mwaka 1959 kupitia Sheria ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro namba 413 ya Mwaka 1959 ikiwa na ukubwa wa Kilomita za mraba 8,292. Eneo hilo liloorodheshwa katika Urithi wa Dunia na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kutokana na ikolojia ya asili ya eneo hili.

**Mheshimiwa Spika**, ili kulinda Ikolojia ya pekee ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro iliyoharibika kutokana na shughuli nyingi za kibinadamu kwa manufaa ya kizazi kilichopo na kizazi kijacho, mwaka 2022, Serikali ilifanya uamuzi wa kuwahamasisha wakazi wa eno hilo kuhama kwa hiari kwenda katika maeneo mbadala. Zoezi hilo lilitekelezwa kwa awamu ya kwanza kuanzia Februari, 2022 na awamu ya pili ilianza Julai, 2023 ambayo inaendelea hadi sasa.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Oktoba, 2024 kaya **1,655** zenye wakazi **9,679** na mifugo **40,397** zimehamia Msomera na maeneo mengine. Idadi hii ni sawa na **asilima 10** tu ya wakazi na **asilimia 4** tu ya mifugo katika eneo la Ngorongoro. Pamoja na umuhimu wa zoezi hili katika kuhakikisha uhai wa hifadhi ya eneo la Ngorongoro kasi ya utekelezaji wake sio ya kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, ili kutatua changamoto zinazolikabili na kuongeza ufanisi katika zoezi hilo, tarehe 1 Disemba, 2024, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alikutana na kuzungumza na viongozi wa kimila wa jamii ya Kimasai wanaoishi katika Eneo la Ngorongoro.

Katika mazungumzo hayo, Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan alitoa ahadi ya kuunda Tume mbili ambapo moja itachunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masuala ya ardhi yanayolalamikiwa na wakazi wa eneo hilo na nyingine itajikita mahsusi katika utekelezaji wa zoezi zima la Uhamasishaji Kuhama kwa hiari kutoka katika Eneo hilo kwenda maeneo mbadala.

**Mheshimiwa Spika,** Tarehe 23 Disemba, 2024, Rais, Dkt. Samia alitekeleza ahadi hiyo kwa kuunda Tume hizo. Tume inayoshughulikia maswala ya Ardhi inaongozwa na Mhe. Jaji Dkt. Gerarld Ndika na ile inayochunguza zoezi la kuhama kwa hiari inaongozwa na Mhandisi Mussa Iyombe. Kamati inampongeza Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassani kwa uamuzi wake huu ambao utahakikisha ustawi wa wananchi na uhai wa Ikolojia

hifadhi ya Eneo la Ngorongoro vinalindwa kwa maslahi ya Taifa letu.

### *b) Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA)*

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) lilianzishwa Mwaka 1959 kupitia Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura ya 412 (kwa sasa Sura ya 282). Shirika linasimamia hifadhi za Taifa ishirini na moja (21) zikiwa na ukubwa wa eneo la kilometa za **mraba 96,908.88** sawa na takribani **asilimia 10.2%** ya ardhi yote nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na utekelezaji wa majukumu yake ya msingi ya uhifadhi, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Shirika linatekeleza miradi miwili ya Kimkakati ambayo ni Kuendelea na Ujenzi wa awamu ya kwanza wa hoteli ya Burigi-Chato yenye hadhi ya nyota tatu iliyofikia **asilimia 70** na Ujenzi wa Uwanja wa Golf ndani ya Hifadhi ya Serengeti katika eneo la Forty Ikoma ilitofikia **asilimia 40.** Miradi yote hii inategemewa kukamilika mwezi Juni, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa miradi hiyo imechelewa na ipo nje ya muda. Mathalani, Ujenzi wa hoteli ya Burigi-Chato ambapo ulianza mwaka mwezi Aprili, 2020 ukiwa umepanga kukalimika ndani ya mwaka mmoja yaani Aprili, 2021 kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 11**, ambapo ulikuwa umesimama hadi Serikali ilipoamua kuukwamua mradi huo mwezi Aprili, 2024.

Aidha, Serikali iliahidi kuwa mradi huo ungekuwa umekamilika kufikia mwezi Disemba, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Ujenzi wa Uwanja wa Golf, awali Kamati ilijulishwa kuwa uwanja huo ulitakiwa kukamilka mwezi Juni, 2024. Hata hivyo, wakati Wizara inawasilisha taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka fedha 2024/2025, Kamati iliahidiwa kuwa mradi huo ungekamilika kufikia mwezi Disemba, 2024. Aidha, ucheleweshaji wa miradi hii inaongeza gharama na inapunguza tija.

### *c) Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS)*

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala Sura 245 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Namba 269 la Julai 30, 2010. Aidha, Wakala ulizinduliwa Julai 18, 2011 ukiwa na jukumu la kusimamia rasilimali za misitu na nyuki zilizochini ya Serikali Kuu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kufanya majukumu yake ya Usimamizi wa uhifadhi wa rasimali za Misituna nyuki nchini, Wakala unatakiwa kutekeleza mikataba ya mashirikiano pamoja na kushiriki mikutano ya Kimataifa. Aidha, Wakala unawajibu wa kushiriki na kuandaa mikutano ya Kimataifa iliyofanyika nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutimiza azma hiyo, Tanzania kupitia Wakala wa Huduma za Misitu ilishiriki Kongress ya 48 ya Apimondia nchini Chile iliyofanyika mwezi wa 8. Apimondia ni Shirikisho la Umoja wa Vyama vya Wafugaji nyuki Duniani ambalo hushughulikia rasilimali nyuki kimataifa likiwa na Makao Makuu yake Jijini Roma nchini Italia. Katika Kongresi hiyo, Tanzania iliwania na kushinda kuwa mwenyeji wa Kongresi ya 50 ambayo itafanyika nchini mwaka 2027 katika jiji la Arusha.

**Mheshimiwa Spika,** Mkutano huo unatarajiwa kuhudhuriwa na takribani washiriki 6,000 kutoka katika nchi 150 duniani. Ili kuhakikisha Mkutano huo unafanyika nchini, Serikali inatakiwa Kuwa na ukumbi wa mikutano wenye uwezo wa kuchukua zaidi ya watu **4,500** kwa wakati mmoja, eneo la maonesho lenye ukubwa wa zaidi ya mita za mraba **5,000,** eneo kwa ajili ya kujiandikisha lenye ukubwa wa mita za maraba **750.**

**Mheshimiwa Spika,** Shirikisho la APIMONDIA limeweka ukomo wa Tanzania kuwa na ukumbi wenye sifa hizo kabla au ifikapo Julai 31, 2025 kufuatia makubaliano ya nyongeza (***Adendum to the letter of Agrement***) ya pande zote mbili. Kamati ilipohoji kuhusu hatua iliyofikiwa katika maandalizi ya Mkutano huo, Wizara ilitoa taarifa kuwa Maandalizi ya Ujenzi wa Ukumbu huo unaotarajiwa kuitwa Mount Kilimanjaro International Conference Centre

yameanza kwa Kushirikisha Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mambo ya Nje na Afrika Mashariki na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Watu wenye Ulemavu kupitia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya PSSSF na NSSF.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na majibu hayo ya Serikali, Kamati hairidhiki na kasi ya uandaaji wa Mkutano huo. Aidha, Mkutano huo unatarajiwa kuwa na manufaa makubwa kwa sekta ya Utalii, Diplomasia na Uchumi nchini.

Ni maoni ya Kamati kuwa, Manufaa hayo yapo hatarini kupotea iwapo Shirikisho la APIMONDIA litafikia uamuzi wa kuiondolea Tanzania nafasi ya kuwa mwenyeji wa Mkutano huo.

***d) Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF)***

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) ni Mfuko ulioanzishwa chini ya Kifungu vya 79 na 83 vya Sheria ya Misitu Sura ya 323 kwa lengo la kukabiliana na changamoto za usimamizi wa rasilimali misitu hususan katika kuimarisha utekelezaji wa Sera na Sheria ya Misitu. Mfuko huu ulizinduliwa na kuanza kufanya kazi rasmi mwezi Julai 2010.

**Mheshimiwa Spika,** majukumu ya Mfuko ni kutoa uwezeshaji kupitia utoaji ruzuku kwa miradi inayochangia kuboresha uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu. Tangu kuanzishwa kwake Julai 2010 hadi Juni 2024, Mfuko umefanikiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 73,137,641,683.68.**

Kati ya fedha hizo **Shilingi 52,315,625,554.89** sawa na 72% zilitumika kutoa ruzuku kwa miradi **1037** inayotekelezwa katika wilaya **133,** mikoa yote **26** ya Tanzania Bara.

**Mheshimiwa Spika,** Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa viwanda sita (6) vya kuchakata na kufungashia asali katika mikoa minne ya Tabora, Katavi, Kigoma na Geita. Mfuko pia unawajengea uwezo na kuhamasisha upandaji miti shuleni kwa kuwezesha uanzishwaji wa vitalu vya miti katika shule za msingi na sekondari.

**Mheshimiwa Spika**; Katika kuhakikisha sekta ya Misitu na Nyuki inachangia katika kuleta ustawi wa wananchi wanaoishi pembezoni mwa misitu, Mfuko unawezesha wananchi kufuga nyuki na kuanzisha mashamba ya miti. Katika kuhakikisha kunakuwa na Maendeleo Endelevu wa sekta hii, Mfuko huu unagharamia Tafiti mbalimbali katika sekta ya misitu na nyuki na kuboresha mazingira ya mafunzo kwa kutengeneza na kukarabati miundombinu katika vyuo vya mafunzo ya misitu, viwanda vya misitu na ufugaji nyuki nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa pamoja na fursa zinazotokana na Mfuko wa Misitu Tanzania, mfuko huu haujajitangaza miongoni mwa wananchi hivyo kufanya wananchi wengi nchini kushindwa kunufaika na fursa hizo. Mfuko pia, unakabiliwa na changamoto ya rasilimali fedha hali inayochangia kushindwa kuhudumia maombi yote ya ruzuku inayopatikana.

### *e) Hali ya Utalii Nchini*

**Mheshimiwa Spika,** Kati ya mwaka 2019 na 2021 Dunia ilipitia mtikisiko kiuchumi na kijamii kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa **UVIKO-19.** Nchini kwetu sekta iliyoathirika zaidi ilikuwa Sekta ya Utalii hasa kutokana zuio la kutoka ndani (lockdown) na kufanyia kazi nyumbani kwani ugonjwa huo ulikuwa unasambaa wa njia ya hewa. Safari za Kimataifa zilisitishwa duniani na hakukuwa na watalii toka nje katika kipindi hicho.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa sababu hiyo, Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika ibara ya 67-70 ya Ilani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2020-2025 iliilekeza Serikali kuhakikisha inakuja na mbinu za kufufua na kukuza Sekta ya Utalii. Katia ibara hizo Serikali ilitakiwa kuhakikisha Watalii wanafikia **Milioni 5** na Kuingiza fedha za kigeni kiasi cha Dola za Marekani **bilioni 6** kufikia mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuhakikisha maelengo hayo ya Ilani yanafikiwa, mwaka 2021, Serikali ilipokea Mkopo wa gharama nafuu kutoka Benki ya Dunia kwa ajilli ya kushughulika na

madhara ya UVIKO-19 ambapo Sekta ya Utalii ilikuwa ni moja ya sekta za kipaumbele. Mikakati mbalimbali iliwekwa na Serikali iweze kurejea katika kukuza uchumi kuleta ustawi miongoni mwa wananchi.

Aidha, mwaka huo huo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alifanya uamuzi wa Kimapinduzi wa kutengeneza Filamu ya ***"Tanzania: The Royal Tour"*** huku yeye mwenyewe akiwa ndio muigizaji kinara wa filamu hiyo ambayo imetumika kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** katika kufuatilia mwenendo wa shughuli za utalii duniani, Kamati ilipitia taarifa za Shirika la Utalii Duniani (WTO) Mwezi Disemba, 2024 ambapo Shirika hilo limeripoti kuwa Tanzania imeshika nafasi ya sita **(06)** duniani na ya kwanza **(01)** Afrika katika kipindi cha Januari na Septemba, 2024 kwa ongezeko la Watalii wa Kimataifa. Ripoti hiyo inaonyesha zaidi kuwa, Tanzania imefanya vizuri kwenye kipengele cha nchi iliyopokea wageni wengi zaidi Afrika kwa **asilimia 50** ikifuatiwa na Mauritius, Morocco na Tunisia.

**Mheshimiwa Spika,** Kupitia uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa hadi kufikia Disemba, 2024, idadi ya watalii imefikia jumla ya watalii **5,360,247** ikiwa ni sawa asilimia **107.2** ya lengo la Ilani. Aidha, mapato ya fedha za kigeni kutokana na shughuli za Utalii yamefikia Dola za Marekani **Milioni 3.9** sawa na **asilimia 65** ya lengo la ilani. Maoni ya Kamati ni kuwa, Kama Wizara itaongeza nguvu ya usimamizi katika sekta hii, Malengo ya Ilani yanaweza kufikiwa katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani kilichobaki.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio hayo, Kamati inaona kuwa Serikali inatakiwa kutangaza vivutio vya utalii zaidi ili kuendelea kupata tija katika sekta hii. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kubuni mazao mapya ya utalii na kuhuisha sekta ya malikale, utamaduni na historia ili yaweze kuchangia katika mapato yanayotokana na utalii.

### f) Hali ya Miundombinu katika Vivutio vya Utalii Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Katika taarifa hii, Kamati imeonyesha na kupongeza Serikali kuhusu hatua iliyofikiwa katika jitihada zake za kufufua na kukuza sekta ya Utalii nchini kutokana na athari za mlipuko wa **UVIKO-19.** Pia, Kamati imebaini kuwa zaidi ya **asilimia 80** ya watalii nchini wanafanya utalii wa wanyamapori katika hifadhi zetu.

**Mheshimiwa Spika,** maeneo yaliyohifadhiwa yana miundombinu mbalimbali ikiwemo barabara, madaraja na viwanja vya ndege inayotumika kuboresha shughuli za uhifadhi na utalii. Maeneo hayo yana mtandao wa barabara zenye urefu wa jumla ya kilomita **33,805.70** na viwanja vya ndege **137.** Aidha, hali ya miundombinu katika maeneo yaliyohifadhiwa haikidhi mahitaji ya uhifadhi na utalii.

**Mheshimiwa Spika,** takriban jumla ya barabara zenye urefu wa **kilomita 6,950** zinahitaji ukarabati mkubwa kwa kiasi cha **Shilingi 197,951,397,052.00.** Mathalani, katika Hifadhi ya Serengeti, barabara ya Golini-Naabi-Seronera-Ikoma gate (98 KM) ambayo inaptisha magari **1000** kwa siku kwa sasa kutoka magari **500** kwa siku iliyokuwa ikipitisha 2019, na ndio uti wa mgongo wa shughuli za utalii katika hifadhi hiyo namba 1 barani Afrika. Barabara hii inahitaji ukarabati mkubwa na inatakiwa kutengewa takribani Shilingi bilioni **17** kwa mwaka kwa ajili ya ukarabati huo. Kama Serikali itaamua kujenga barabara hii kwa lami itagharimu **Shilingi 137,200,000,000/=** na itakuwa imeondoa adha ya marekebisho ya mara kwa mara.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa viwanja vya ndege, viwanja vinavyotumika kibiashara ni **72** na vingine **65** ni kwa ajili ya shughuli za utawala na doria. Hata hivyo, viwanja vingi vinahitaji maboresho ili kukidhi matakwa ya sheria na kanuni za usalama wa usafiri wa anga na pia kuendana na kasi ya ongezeko la idadi ya watalii. Aidha, **Shilingi bilioni 7.77** kila mwaka zinahitajika katika kukarabati viwanja vya ndege **72** ili viweze kukidhi utoaji wa huduma kwa ufanisi. Mfano, Kiwanja cha Seronera kipindi cha

watalii wanapokuwa wengi kinapokea ndege nyingi kuliko hata Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere. Hata hivyo, kiwanja hicho kimejengwa kwa changarawe.

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wa taarifa mbalimbali, Kamati imebaini kuwa pamoja na athari ya mvua zinaendelea kunyesha katika maeneo ya hifadhi, changamoto kubwa ni Ukomo wa bajeti unaotengwa kwa ajili ya taasisi za Uhifadhi nchini. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo hazipatikani kama zilivyotengwa kwenye bajeti licha kuwa kiasi kilichoidhinishwa ni kidogo.

**g) Mradi wa Usimamizi wa Maliasili Endelevu na Ukuaji wa *Utalii Kanda ya Kusini (REGROW)***

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Tanzania ilipata mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia kiasi **Shilingi 345,000,000,000/=** ili kutekeleza mradi wenye lengo la kuboresha usimamizi wa maliasili na kukuza utalii Kusini mwa Tanzania (REGROW). Awali mradi huu ulipangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka sita kutoka mwaka 2017 hadi 2023.

Hata hivyo kutokana na mlipuko wa janga la UVIKO-19 na mvua kubwa za el-nino, Serikali na Benki ya Dunia ziliongeza muda wa utekelezaji wa mradi huo hadi Februari, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Julai, 2024, mradi ulikuwa umepokea kiasi cha **Shilingi 288,172,857,709/=** sawa na **asilimia 83.5** ya fedha zote za mradi. Aidha, kiasi kilichotumika ni **Shilingi 180,574,632,326.40** sawa na **asilimia 62.7** ya fedha zilizopokelewa. Hii maana yake ni kuwa Serikali ina kiasi cha **Shilingi 107,598,225,382.60** ambacho hakijatumika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata nafasi ya kutembelea na kukagua baadhi ya shughuli zinazofanyika chini ya mradi ya REGROW katika hifadhi za Taifa za Ruaha na Mikumi. Aidha, Kamati ilitembelea ujenzi wa Kituo cha tafiti wa Wanyamapori na

jengo la Kutangaza vivutio vya Utalii Kusini wa Tanzania katika eneo la Kihesa mjini Iringa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa shughuli hizo ina changamoto ya kuwa nje ya muda licha ya ukweli kwamba fedha kwa ajili ya kuzikamilisha zipo. Wakandarasi wanaotekeleza ujenzi wa viwanja vya ndege, hosteli na mabanda ya malazi katika hifadhi wanafanya kazi kwa kasi isiyoridhisha hivyo kufanya utekelezaji wa jumla ya mradi kuwa nyuma ya muda.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa ujenzi wa Jengo la Kutangaza Utalii Kusini mwa Tanzania kasi ya mradi ipo chini ya asilimia 10 huku mkandarasi akiwa hadai fedha zozote. Kamati inapongeza kasi ya ujenzi ya mkandarasi wa ujenzi wa kituo cha utafiti wa wanyamapori kwani alikuwa amefikia asilimia 80 na kama Serikali itaendelea na usimamizi madhubuti anaweza kumaliza mradi ndani ya muda yaani
Februari, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Katika tathmini ya jumla iliyofanywa na Kamati inaonyesha kuwa, shughuli zinazotekelezwa na wakandarasi wa ndani ndio zipo nyuma ya wakati kwa kiasi kikubwa na wakati mwingine hazifikii ubora wa viwango vinavyotakiwa.

Licha ya ukweli kuwa katika mradi huu, fedha zimekuwa zikitolewa kwa wakati baada ya wakandarasi kupeleka hati ya malipo Serikalini lakini wakandarasi wa ndani miradi yao mingi ipo nje ya wakati na hawafanyi vizuri.

**Mheshimiwa Spika,** Hali hii inaweza kuifanya Serikali kuwa na kigugumzi katika utekelezaji wa dhana ya kuwapa kipaumbele wakandarasi wazawa (local content) nchini.

Aidha, ucheleweshaji wa miradi unafanya gharama za mradi kuwa kubwa kufutia mfumuko wa bei na wananchi kuchelewa kupata manufaa yaliyotarajiwa kutokana na miradi hiyo.

### h) Taasisi za Mafunzo zilizopo chini ya Wizara ya Maliasili *na Utalii*

**Mheshimiwa Spika,** Mafunzo ni nguzo muhimu katika kuhakikisha kunakuwa na uhifadhi na utalii endelevu wa rasilimali za wanyamapori, misitu na mali kale nchini. Katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025 Kamati ilifanikiwa kupokea taarifa za utendaji za vyuo saba **(07)** vya mafunzo vilivyochini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Aidha, Kamati ilifanikiwa kutembelea na kukagua miradi na kujionea utekelezaji wa majukumu katika Chuo cha Mafunzo ya Nyuki Tabora (BTI).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa vyuo vilivyo chini ya Wizara vyuo vikongwe kwani vingi vilijengwa zaidi ya miaka 50 iliyopita. Hali hii imefanya miundombinu ya kufundisha na kujifunzia kuwa chakavu na kuhitaji mkakati wa kufanya ukarabati mkubwa ili kuviweka vyuo hivi katika hali nzuri kwa ajili kujifundisha na kujifunzia.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mchango kubwa wa vyuo hivi katika uhifadhi na utalii, vyuo hivi bado havijajitangaza miongoni mwa watanzania wengi. Kamati imebaini kuwa, ni wanafunzi wachache wanaomaliza elimu ya kidato cha nne na cha sita wanaovifamu vyuo hivi. Hali imepelekea wakati mwingine vyuo kuwa na udahili mdogo kuliko uwezo wa vyuo husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa baadhi ya vyuo hivi kama vile Chuo cha Wanyamapori Mweka ada zake ni kubwa na zimekuwa kikwazo kwa baadhi ya wanafunzi kusoma chuoni hapo. Kamati inasikitika kwamba, pamoja na Sekta ya Utalii kuwa ni moja ya sekta kongwe za uzalishaji na kuchangia katika pato la Taifa, ajira na fedha za kigeni, Serikali haijazitambua taaluma zinazotolewa katika vyuo hivi kama taaluma za kipaumbele katika orodha iliyotolewa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB).

**Mheshimiwa Spika,** hali hii imefanya wanafunzi wasio na uwezo wa kugharamia masomo katika vyuo hivi kushindwa kujiunga na vyuo licha ya kuwa na ndoto ya kufanya kazi katika Uhifadhi

Maliasili na Utalii nchini. Pia, inapelekea kuendelea kuwa na idadi ndogo ya watalaamu katika sekta ya uhifadhi na utalii ambazo mahitaji yake katika soko yanaongezeka kufuatia ongezeko la idadi ya watalii nchini na mahitaji ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

### i) Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto ya *Wanyamapori Wakali na Waharibifu*

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yanapatikana kupitia sekta ya Maliasili na Utalii, migongano baina ya binadamu na wanyamapori ni moja ya changamoto kubwa inayoikabili sekta hii. Aidha, kati ya halmashauri **184** nchini, hailmashauri **91** zimekumbwa na changamoto hiyo huku halmashauri **44** zikiwa katika hali mbaya zaidi.

Madhara yanatokana na changamoto hiyo ni pamoja na wananchi kujeruhiwa hivyo kupata ulemavu, vifo na kuharibiwa mali kama vile mazao na miundombinu ya makazi, maji na barabara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini Serikali inachukua hatua mbalimbali kukabiliana na changamoto. Pamoja na hatua hizo zinazochukuliwa, Serikali imekuwa ikitoa mkono wa pole kwa maana ya kifuta machozi na kifuta jasho kufuatia madhara yanayoawapata wananchi. Mathalani, Julai, hadi kufikia Oktoba, 2024, Serikali ilikuwa imelipa **shilingi 1,128,280,500** kwa wananchi **4,142** katika Wilaya **14.** Aidha, uhakiki katika madai katika maeneo mengine unaendelea.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilitunga Kanuni za Kifuta Jasho na Kifuta Machozi za mwaka 2011 ambazo ziliweka utaratibu na kiwango kutokana na madhara yaliyomkuta muathirika. Kamati kupitia Bunge lako Tukufu liliitaka Serikali kupitia upya kanuni hizo kwa ajili ya kuzifanyia marekebisho. Kamati inapenda kulitaarifu Bunge kuwa, Serikali imefanya marekebisho ya Kanuni za Kifuta Jasho na Kifuta Machozi za Mwaka 2011 kupitia Tangazo la Serikali Na. 440 la tarehe 31 Mei 2024.

**Mheshimiwa Spika,** Katika marekebisho hayo viwango vya malipo vimeongezeka kwa **asilimia 50** kwa majeraha ya muda, uharibifu wa mazao na vifo vya mifugo na **asilimia100** kwa majeraha ya kudumu na vifo binadamu. Aidha, katika maboresho hayo bado mchakato wa mwananchi kuwasilisha madai yake na muda wa uhakiki wa madai hayo mpaka kulipwa umebaki kuwa kama ulivyokuwa awali. Wananchi walioathirika na changamoto hiyo wameendelea kulalamikia mchakato huo kwa kuchukua muda mrefu.

**j) Hali ya Hoteli na Loji Zilizobinafsishwa na Serikali kwa Wawekezaji**

**Mheshimiwa Spika,** Katika taarifa hii, Kamati imeonyesha mafanikio yaliyopatikana kufutia kukua kwa sekta ya utalii nchini. Hata hivyo, moja ya changamoto kubwa inayoikabili sekta hii ni uhaba wa malazi kwa watalii.

**Mheshimwa Spika,** kufuatia changamoto hiyo, Kamati ilikutana na aliyekuwa Msajili wa Hazina tarehe 24 Januari, 2023 Ndg. Mgonya Benedict ili kupata taarifa kuhusu hoteli za Serikali zilizobinafsishwa katika mchakato wa kubinafsisha mashirika ya umma. Aidha, Katika taarifa yake ya mwaka kwa shughuli za Kamati Mwezi Februari, 2023 ndani ya Bunge lako Tukufu, Kamati ilipendekeza Serikali kuwakuchukulia hatua za haraka wawekezaji wa hoteli na loji za Serikali ambao wamekiuka masharti ya uwekezaji. Bunge liliridhia pendekezo hilo na kuwa azimio rasmi la Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Katika taarifa yake ya mwaka iliyowasilishwa Bungeni tarehe 08 Februari, 2024, Kamati iliripoti kuwa azimio hilo halikutekelezwa. Hata hivyo, Kamati ilichukua hatua ya kupata ufafanuzi zaidi kutoka Serikalini kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina. Tarehe 21 Januari, 2024 Waziri wa Maliasili na Utalii akiwa na Kaimu Msajili wa Hazina Ndg. Lightness Mauki walifika mbele ya Kamati kuwasilisha taarifa juu ya hoteli hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitarifiwa kuwa Serikali imeunda timu ya majadiliano chini ya Wakili Mkuu wa Serikali ambayo inafanya

majadiliano na wawekezaji hao namna na kiasi cha fedha ambacho kinatakiwa kurejeshwa na Serikali ili iweze kurudisha umiliki wa hoteli. Msajili wa Hazina alitoa taarifa kuwa kuna tathimini na ufuatiliaji wa kina unafanyika kuhusu utendaji na uendelezaji wa hoteli hizo na inatarajiwa kukamilika ndani ya mwezi Juni, 2025. Aidha, taarifa ya awali inaweza kupatikana ndani ya mwezi Machi, 2025 na Kamati imemtaka Msajili wa Hazina na Wizara ya Maliasili na Utalii kuhakikisha taarifa hiyo inafika mbele ya Kamati kabla ya Mkutano wa 19 wa Bunge unaotarajiwa kuanza mwezi April, 2025.

***k) Shirika la Makumbusho ya Taifa***

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Makumbusho ya Taifa la Tanzania liliundwa kwa Sheria ya Makumbusho ya Taifa Sura 281 kama Taasisi ya kimkakati ya kuhifadhi na kuendeleza malikale. Lengo kuu la uhifadhi malikale hizo ni kutunza, kulinda na kuelimisha jamii juu ya urithi wa Taifa na historia ya nchi, chimbuko la mwanadamu na maendeleo yake kiutamaduni na kimaumbile, mahusiano ya binadamu na mazingira pamoja na mila, desturi na tamaduni za watu wa kale kwa faida ya vizazi vya sasa na baadaye.

**Mheshimiwa Spika,** Shirika pia linajukumu ya kuendeleza miundombinu ya utalii, kuimarisha programu za kielimu, matumizi makubwa ya matukio na matamasha ya uhifadhi, kubuni mbinu za masoko na utangazaji kwa kushirikisha wadau na jamii. Shirika linatakiwa kujiimarisha kiuchumi na kuboresha uwezo wa usimamizi wa Sekta ya malikale nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kuendeleza uhifadhi katika Urithi wa Asili, Shirika limepanga kujenga Makumbusho ya Marais nchini katika eneo la Mtumba jijini Dodoma. Mradi huo unaotarajia kutumia **Shilingi bilioni 34,** umepangwa kuanza katika mwaka huu wa fedha kwani umetengewa **shilingi bilioni 1** ili kuanza maandalizi ya awali usanifu wa ujenzi huo. Mradi huo umedhamiria kuweka alama katika Taifa letu na bara la Afrika kama chachu ya mabadiliko ya kifikra na tafsiri ya historia ya Taifa letu kupitia

mapito ya Tawala za Nchi yetu. Hata hivyo, sasa ni robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti na bado mradi huo haujaanza.

### 2.4.1.2 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Mheshimiwa Spika**, Wizara hii ndio iliyokasimiwa majukumu ya kuratibu na kusimamia Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 (Toleo la Mwaka 20230 na ile ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000. Pamoja na majukumu haya ya Kisera, Wizara inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vya Serikali vilivyoainisha katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025, Dira ya Taifa ya Maendeleo, 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa mwaka 2021/2022-2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, ardhi ni nyenzo kuu katika shughuli za uzalishaji na makazi. Shughuli za kilimo, ufugaji, madini, utalii, biashara, ujenzi, uchukuzi na mawasiliano zote zinafanyika juu ya ardhi.

Katika Taifa letu, sekta ya ardhi ni moja ya sekta ya kipaumbele, pamoja na kuwa inakabiliwa na changamoto za migogoro ya ardhi, ujenzi wa makazi holela, eneo kubwa la ardhi kutokupangiwa matumizi ya ardhi na kuwa na bajeti ndogo katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Februari, 2024 na Januari, 2025, Kamati imebaini mafanikio na changamoto katika sekta ya ardhi kama ifuatavyo: -

#### *a) Mipango ya Matumizi ya Ardhi*

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwaka 2020 ni Vijiji **1,852** saawa na asilimia 15 pekee ndio vilikuwa vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi kati ya Vijiji **12,333** vilivyopo nchini. Katika ukurasa wa 120 wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 iliitaka Serikali kuwa imeandaa mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa vijiji **4, 131** nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa hadi kufikia Disemba, 2024, Serikali ilikuwa imefanikiwa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji **2,437** sawa na **asilimia 59** ya lengo la Ilani. Vijiji hivyo vinafanya kuwa na jumla ya vijiji **4,289** vyenye mipango ya matumizi ya ardhi na kufanya **vijiji 8,044** vilivyobaki ili kukamilisha vijiji vyote **12,333** nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa kama Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ikiidhinishiwa kiasi cha Shilingi bilioni 120 kama fedha za maendeleo inaweza kukamilisha kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji vyote **8,044** vilivyobakia. Hatua hii ni muhimu ili kuweza kuondoa migogoro ya mipaka ya kiutawala na kati ya makundi ya uzalishaji hasa wakulima na wafugaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kama ardhi yote ya vijiji nchini itaandaliwa mipango ya matumizi, itaongeza thamani ya ardhi hivyo kuondoa umasikini miongoni mwa wananchi wanaomiliki ardhi vijijini. Aidha, Serikali itaongeza mapato kupitia kodi ya pango la ardhi tofauti na sasa ambapo wanaolipa ni wachache na wengi wapo mijini. Pia, itapunguza uvamizi wa maeneo ya hifadhi kwa ajili ya shughuli za kilimo, mifugo, uvuvi na uchimbaji wa madini.

### *b) Ardhi ya Wawekezaji ambayo Haijaendelezwa*

**Mheshimiwa Spika,** itakumbukwa kuwa mnamo tarehe 27 Agosti, 2024, Kamati Maalumu uliyoiunda kuchunguza mgogoro wa Ardhi kati ya mwekezaji ambae ni Kanisa la EFATA na wanakijiji wa Kijiji cha Sikaungu Wilaya ya Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa iliwasilisha taarifa yake Bunge. Wakati wa kuhitimisha hoja hoja hiyo, ulitoa maelekezo kwa Kamati hii kuhakikisha inapata taarifa juu ya uendelezaji wa mashamba ya wawekezaji katika maeneo mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza jukumu hili, siku ya tarehe 18 Oktoba, 2024, Kamati iliitaka Wizara kuwasilisha taarifa ya Uendelezaji wa ardhi kwa wawekezaji wakubwa kwenye sekta ya ardhi katika mikoa ya Manyara, Arusha, Tanga, Morogoro na

Iringa. Kamati ilibaini kuwa Viwanja na mashamba **77** vyenye ukubwa wa Mita za Mraba **869,608,387** vimemilikishwa kwa wawekezaji ajili ya matumizi mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake, Kamati iliendelea kubaini kuwa mashamba ambayo hayajaendelezwa ni **31** sawa na **asilimia 40** ya idadi ya maeneo yaliyomo katika mikoa mitano iliyoainishwa. Twakimu hiyo inaonyesha wazi kuwa kuna haja ya Serikali kuandaa mikakati ya kupitia ardhi yote isiyoendelezwa ili iweze kuchukua hatua stahiki za kisheria.

***c) Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)***

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 76 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 iliitaka Serikali Kuendelea kuboresha na kuimarisha Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ili litekeleze miradi kwa tija na kujenga nyumba, kwa gharama nafuu. Aidha, Ilani ililekeza Serikali kuhakikisha kuwa inaisimamia Shirika kujenga nyumba 1000 za gharama nafuu kwa ajili ya kuuza au kupangisha kwa wananchi na watumishi wa umma katika jiji la Dodoma. Aidha, Shirika lilitakiwa kukamilisha ujenzi wa nyumba za majengo makubwa ikiwemo Morocco Square, Kawe 711, Golden Premier Residence na Mradi wa Kiwanja Na. 300 Regent Estate katika jiji la Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, hadi kufikia Disemba, 2024, Shirika limefanikiwa kukamilisha mradi wa Morocco square pekee na kukwamua ujenzi wa miradi ya Kawe 711 na Golden Premier Residence ambayo ilikuwa imesimama kwa muda mrefu. Mradi wa Kiwanja Na. 300 Regent State bado majadiliano na mkandarasi yanaendelea.

**Mheshimiwa Spika,** katika ujenzi wa nyumba 1000 jijini Dodoma, Shirika limeanza kutekeleza mradi huo kupitia programu yake ijulikanayo kama Samia Housing Scheme katika Medeli/Njedengwa. Kwa upande mwingine Shirika limekuwa likilalamikiwa na wananchi kuwa linajenga nyumba za gharama kubwa.

***d) Proramu ya Kuandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi kwa Vjijiji 333 katika mwaka wa Fedha 2024/2025***

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2024/2025 Wizara ilipanga kutekeleza programu maalumu ya Kupanga vijiji 333. Programu hiyo ilipangwa kutumia kiasi cha **Shilingi 5,000,000,000.**

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Katika kikao cha kupokea utekelezaji wa bajeti ya Wizara Fungu 48, fedha hizo hazikuwa zimepokelewa toka hazina. Kamati ilikutana pamoja na Wizara ya Fedha na Wizara ya Ardhi siku ya tarehe 04 Februari, 2025 ili kupata majibu ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kikao hicho kilichohudhuriwa na Waziri wa Fedha na Waziri wa Ardhi, Serikali kupitia Waziri wa Fedha iliahidi kutoa kiasi hicho cha fedha hadi kufikia mwisho wa mwezi Februari, 2025. Kamati inaitaka Serikali kutimiza ahadi hiyo ili kuiwezesha Wizara kutekeleza programu hiyo kama ilivyokusudiwa.

***e) Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK)***

**Mheshimiwa Spika,** Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi Nchini (KKK) ni programu ya miaka 10 (2028/2029-2028/2029) inayotekelezwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Halmashauri mbalimbali nchini. Kupitia mradi huu halmashauri na mamlaka mbalimbali za Serikali hukopeshwa fedha bila riba ambapo zinatakiwa kupanga, kupima na kuuza viwanja kisha kurejesha kwa ajili halmashauri zingine kukopa fedha hizo.

**Mheshimwa Spika,** Pamoja na mradi huu kuwa na manufaa katika zoezi la Kuanga, Kupima na Kumilikisha ardhi nchini, utekelezaji wake umekumbana na changamoto ya Halmashauri na Mamlaka zingine zilizokopa kushindwa kurejesha fedha za mkopo au kurejesha kwa kiasi kidogo. Katika mamlaka za Serikali 57 za mitaa zilizokopa nchini, ni Halmashauri 17 pekee na

Sekretarieti ya Mkoa mmoja wa Iringa ndio zimerejesha kiasi chote cha fedha.

Aidha, vyuo vya Ardhi vya Morogoro, Tabora na Chuo Kikuu cha Ardhi vilikopeshwa jumla ya Shilingi **2,810,488,800/=** na hadi sasa vimerejesha kiasi cha Shilingi **450,000,000/=** sawa na asilimia 16 tu ya fedha hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini sababu zinazopelekea mikopo hii kutokurejeshwa. Sababu hizo ni:-

(i) Mipango na upimaji wa viwanja ulifanyika katika maeneo ambayo yapo mbali na miji hivyo gharama za viwanja zimekuwa kubwa kuliko thamani ya maeneo hayo kwa bei ya soko;

(ii) Baadhi ya Taasisi na Halmashauri zilizokopa zilichepusha matumizi ya fedha za mikopo hivyo kushindwa kupata chanzo cha marejesho. Kwa mfano Halmashauri ya Korogwe vijijini ilitumia fedha hizo kurasimisha makazi holela badala ya kwenda kupanga na kupima eneo jipya la mji;

(iii) Baadhi ya halmashauri zimeuza viwanja lakini zimetumia fedha hizo kwa matumizi mengine; na

(iv) Wizara kutoa mikopo kwa halmashauri na taasisi bila kutoa ushauri wa kitalaamu na kufuatilia namna zoezi zima la Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi linavyotekelezwa uwandani.

**Mheshimiwa Spika,** hali hii imepelekea Wizara kuwa imekusanya kiasi cha Shilingi **bilioni 27.5** pekee kati ya **Shilingi bilioni 50** zilizokopeshwa toka mwaka 2018.

Aidha, Hazina iliamua kutoa kiasi Shilingi bilioni 50 kuwa chini ya usimamizi wa Wizara kwa kuunda Mfuko maalumu unaoitwa Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi (Plot Development Revolving Fund-PDRF).

### *f) Marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995*

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 74 (Uk. 119) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025) inaitaka Serikali Kufanya mapitio na kuhuisha Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya Usimamizi na Utawala wa Ardhi kwa kushirikisha wananchi kikamilifu ili kuwawezesha kumiliki uchumi ikitambua kuwa ardhi ndio nyenzo kuu ya shughuli za Uchumi nchini. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara ilifanya mapitio na tathmini ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 ambapo ilibaini kuwepo kwa changamoto na upungufu kutokana na mabadiliko makubwa katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa katika sekta ya ardhi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kubaini changamoto hizo, Wizara iliandaa mapendekezo na kuyawasilisha katika mamlaka husika. Aidha, Mapendekezo ya Marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 yaliridhiwa na Baraza la Mawaziri tarehe 18 Agosti, 2023, na kuifanya sera hiyo kujulikana kama Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 (Toleo la Mwaka 2023). Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara kwa kufanya mabadilko hayo ambayo yanalengo la kuifanya sekta ya ardhi kuendelea kuleta ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kikao chake cha tarehe 19 Agosti, 2024, Kamati ilipokea taarifa ya marejeo na marekebisho ya Sera hiyo ambapo Serikali ilifafanunua mambo mbalimbali katika sera husika. Kupitia taarifa hiyo Kamati ilibaini kuwa kuna upungufu wa kutokuwepo utaratibu maalum wa kisera na kisheria wa kusimamia maeneo katika mipaka ya Tanzania na nchi jirani. Hali hii imepelekea kukosekana kwa mfumo endelevu wa uratibu na unufaikaji wa ardhi kwa wananchi wanaoishini katika maeneo hayo kiuchumi kwa kuzingatia usalama.

**Mheshimiwa Spika,** katika kujiridhisha na hali hiyo, tarehe 06 Januari, 2025, Kamati ilifanya ziara katika Wilaya ya Misenyi, Mkoani Kagera kwa ajili ya kuangalia hali ya matumizi ya ardhi katika mpaka wa Tanzania na Uganda. Katika ziara hiyo, Kamati iliona changamoto ya kukosekana kwa miundombinu wezeshi

kwa ajili ya shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na barabara na skimu za kilimo cha umwagiliaji. Aidha, maeneo hayo hayajaandaliwa mpango unaoainisha matumizi ya ardhi.

### *g) Maboresho ya Mfumo wa Usimamizi wa Ardhi*

**Mheshimiwa Spika,** Katika taarifa ya Shughuli za Kamati kwa mwaka 2023 iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu tarehe 8 Februari, 2024, Kamati Iizungumzia kuhusu Maboresho ya Mfumo wa Usimamizi wa Ardhi nchini. Aidha, Katika Ibara ya 74 Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025, Serikali ilitakiwa kuhakikisha inaboresha mfumo na kuusambaza katika halmashauri zote nchini.

**Mheshimiwa Spika,** awali Serikali ilikuwa imeitarifu Kamati kuwa mfumo huo unaoitwa e-Ardhi au zamani ILMIS ulikuwa unajengwa ili uweze kuchukua taarifa nyingi zaidi na kuhudumia wateja wengi zaidi. Mfumo huo ulikuwa umefikia **asilimia 88** mwezi Disemba, 2023 na inatarajiwa ifikapo mwezi Juni, 2024 mikoa mitano (5) ya Arusha, Tanga, Mbeya, Mwanza, na Dodoma kuwa wanahudumiwa na mfumo huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasikitika kuwa hadi kufikia Juni, 2024 mfumo huo ulikuwa haujaanza kufanya kazi. Kamati iliomba kupata maelezo ya hatua iliyofikiwa katika Ujenzi, Usambazaji na Matumizi ya Mfumo wa e-Ardhi nchini katika kikao chake na Wizara tarehe 21 Januari, 2025. Katika kikao hicho, Serikali iliitarifa Kamati kuwa uzinduzi wa awali wa mfumo huo ulifanyika mwezi Disemba, 2024 jijini Dodoma. Aidha, hadi kufikia tarehe 17 Januari, 2025, mfumo huo ulikuwa umeanza kuhudumia wananchi **6,954** pekee katika halmashauri **20** nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara iliitarifu Kamati kuwa changamoto ya uhaba wa fedha, wataalamu wa TEHAMA na ukosefu wa Mtandao na Miundombinu ya TEHAMA ndio sababu zilizofanya hadi sasa mfumo huo haujaanza kufanya kazi. Pamoja na sababu hizo zilizoelezwa na Wizara, kufuatia malalamiko ya wananchi wengi kuhusu uadilifu wa watumishi wa sekta ya ardhi nchini,

Kamati inadhani kuwa upo uwezekano mfumo huo una hujumiwa ili usifanye kazi.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, mfumo huo ukiweza kufanya kazi kwa ufanisi utakuwa na manufaa makubwa kwa Taifa kwani utaondoa kwa kiasi kikubwa muingiliano kati ya watoa huduma na wananchi katika miamala ya ardhi nchini. Hali itapelekea kupunguza malalamiko ya rushwa, uuzwaji wa viwanja mara mbili katika eneo moja kuongeza ufanisi na tija katika sekta ya ardhi nchini.

### *h) Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi katika Jiji la Dodoma*

**Mheshimiwa Spika,** Utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini ni moja ya jukumu msingi kwa Wizara ya Ardhi nchini. Hata hivyo, katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara inashirikiana na taasisi zingine za kisheria ikiwemo Mahakama ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia jiji la Dodoma kuwa miongoni mwa sehemu zenye migogoro mingi ya ardhi nchini, Kamati iliitaka Serikali kuwasilisha hatua ilizochukua kukabaliana na changamoto hii. Tarehe 15 Oktoba, 2024, Serikali iliwasilisha taarifa yake kwa Kamati kupitia Wizara ya Ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wa taarifa hiyo, Kamati ilibaini kuwapo kwa vyanzo mbalimbali vya migogoro hiyo kama ifuatavyo:-

(i) Utaratibu wa uendelezaji Mji kwa njia ya Maboresho uliotekelezwa na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA), ambao haukutambua ardhi tupu kuwa na thamani hivyo, kutwaa sehemu kubwa ya ardhi ya wenyeji bila kuwafidia;

(ii) Udhahifu katika usimamizi na utekelezaji wa miradi ya urasimishaji makazi, maboresho ya makazi na upimaji shirikishi ambapo kulikosekana uwazi baadhi wa miradi ya urasimishaji kwenye upimaji shirikishi hasa mgao wa **30%** kwa

**70%.** Wananchi wengi wanadai kudhulumiwa ardhi yao na baadhi ya watendaji walioendesha zoezi hilo;

(iii) Utwaaji, Upangaji na upimaji wa Ardhi katika miradi ya Serikali kufanyika bila kulipa fidia ambapo katika utekelezaji wa miradi ya uwanja wa mpira Nala, mradi wa barabara ya mzunguko (ring road) na Reli ya Mwendo Kasi (SGR) wananchi bado wanadai fidia ya maeneo yao; na

(iv) Baadhi ya Watumishi kutokuwa waadilifu ambapo wamekuwa wakifanya wakitoa milki pandikizi (double allocation) na kuchelewesha huduma za ardhi kwa wananchi ili kuvutia rushwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kutatua miggogoro hiyo. Serikali imetekeleza kampeni ijulikanayo kama Zero Migogoro Jiji la Dodoma mwaka 2021, Kuunda Kamati ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi mwaka 2022, Kuendesha zoezi la Kliniki za Ardhi mwaka 2023. Pamoja na hatua hizo kutatua sehemu ya migogoro bado, Jiji la Dodoma limeendelea kuwa na migogoro mingi ya ardhi.

Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa migogoro mingi ni zao la watumishi wa sekta ya ardhi wasio waamini wanaoshirikiana na walanguzi katika sekta ya ardhi ili kujitajirisha kinyume na sharia.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, yafuatayo ni maoni ya Kamati kuhusu shughuli zilizotekelezwa katika kipindi cha kuanzia Februari 2024 hadi Januari 2024 ambayo yanabainisha mtazamo wa kile kilichojiri wakati Kamati ikitimiza majukumu yake.

### 3.1.1 Wizara ya Maliasili na Utalii

(i) Serikali iweke mikakati ya kulinda maeneo yaliyohifadhiwa na kuweka alama za kudumu na zenye kuonekana ili kudhibiti uvamizi wa shughuli za kibinadamu;

(ii) Serikali ichukue hatua madhubuti za kutoa elimu na kuwashirikisha Wananchi katika shughuli za uhifadhi wa rasilimali za misitu ili kunusuru misitu yetu nchini; na

(iii) Serikali iweke mkakati wa kuvitambua, kuviendeleza na kuvitangaza vivutio vyote vya utalii nchini ikiwa ni pamoja na utalii wa malikale, utalii wa fukwe za bahari, uvuvi, utamaduni na maeneo mengine.

### 3.1.2 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

(i) Serikali ibuni njia zitakazowezesha utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini ili kusudi sekta ya ardhi iongeze mchango katika pato la taifa na kustawisha wananchi;

(ii) Serikali ibuni mbinu mbalimbali za kuhamasisha wananchi kulipa kodi za ardhi, kama vile kufanya matangazo kwenye mikusanyiko mbalimbali; na

(iii) Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuzingatia mpango wa matumizi ya ardhi sambamba na ushirikishwaji wa wananchi.

## 3.2 MAPENDEKEZO

### 3.2.1 Utaratibu wa Kubaki na Makusanyo (Retention) Katika Taasisi za TANAPA na NCAA

**KWA KUWA**, taasisi hizi zinakabaliwa na uhaba wa fedha katika utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi kutokana na ukomo wa bajeti na kuchelewa kupokea fedha kutoka hazina;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inazorotesha ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya kuwezesha shughuli za uhifadhi na utalii jambo ambalo linaweza kupunguza mchango wa sekta kwenye uchumi wa nchi;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ilete Bungeni Marekebisho ya Sheria ya Fedha **Na.8 /2020** kwa lengo la kuzifanya taasisi hizo kubaki na sehemu ya makusanyo yake (Retain) ili kuzisadia kutekeleza majukumu yake ya Uhifadhi na Kuhudumia Utalii kwa ufanisi.

### 3.2.2 Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA)

**KWA KUWA**, Miradi ya Kimkakati ya Ujenzi wa Hoteli ya Nyota tatu ya Burigi-Chato na Utengenezaji wa Kiwanja cha Golf katika Hifadhi ya Serengeti eneo la Fort Ikoma imechelewa kukamilika kamlika;

**NA KWA KUWA,** Ucheleweshaji huo:-

(i) Unaongeza gharama ya miradi kuliko ilivyokadiriwa awali; na

(ii) Unakwamisha uwezekano wa Taifa kunufaika ipasavyo na fursa zilizopo katika sekta ya utalii,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali:-

(i) Ifanye tathmini ili kubaini sababu za miradi hiyo kutokukamilika kwa wakati na taarifa hiyo iwasilishwe kwa Katibu wa Bunge ifikapo tarehe 10 Machi, 2025;

(ii) Ijipange kukamilisha miradi hiyo kabla ya tarehe 30 Juni, 2025; na

### 3.2.3 Mchakato Mrefu wa Malipo ya Kifutamachozi na Kifuta Jasho

**KWA KUWA**, Serikali imefanya uamuzi wa kutoa kifuta machozi na kifuta jasho kutokana na athari zinazo wapata wananchi kwa sababu ya migongano kati ya wanyamapori na binadamu,

**NA KWA KUWA**, mchakato wa malipo ya kifuta machozi na kifuata jasho umekuwa ukichukua muda mrefu hivyo kuongeza madhara kwa wananchi wanaokutwa na kadhia hiyo ikiwemo ulemavu, kuharibiwa mali na kupoteza maisha,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa inaboresha na kurahisisha mchakato wa malipo kwa wananchi walioathirika na migongano hiyo.

### 3.2.4 Kutokutekelezwa kwa Azimio la Bunge Kuhusu Uendeshaji wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA) na Mchakato wa kupandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania (TFS)

**KWA KUWA**, utekelezaji wa majukumu ya taasisi za TAWA na TFS unakosa ufanisi kutokana na changamoto ya muundo wa undeshaji,

**NA KWA KUWA**, athari za changamoto hizo zilizangatiwa na Bunge kwa kupitisha azimio mwaka 2023 na 2024 ili kutatua hali hiyo lakini utekelezaji haujafanyika,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ilete maelezo kwa Katibu wa Bunge kuhusu maazimio hayo ikifafanua mkakati uliopo wa kutekeleza maazimio hayo ifikapo 10 Machi, 2025.

### 3.2.5 Kutangaza vivutio vya Utalii Nchini kwa Njia ya Kidijitali

**KWA KUWA**, Serikali imetumia gharama kubwa katika ujenzi wa Kituo cha Kutangaza Utalii Kidijitali (DDMCC),

**NA KWA KUWA,** kituo hicho hakijaanza kufanya kazi licha ya kuwa kimekamilika takribani miaka mitatu (3), hivyo Taifa kushindwa kufaidika na manufaa ya kituo hicho,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye tathmini na uchuguzi wa kina ili kubaini sababu ya Kituo hicho kushindwa kufanya kazi na iwasilishe taarifa kwa Katibu Wa Bunge kabla ya tarehe 10 Machi, 2025.

### 3.2.6 Taasisi za Mafunzo zilizo Chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii

**KWA KUWA**, taasis hizi zinakabiliwa na changamoto za ufinyu wa bajeti, wanafunzi wake kukosa ufadhili katika Bodi ya Mikopo ya Eilimu ya Juu na kutofahamika miongoni mwa wananchi wengi,

**NA KWA KUWA**, hali hii inapelekea vyuo hivi kushindwa kuboresha miundombinu na kushindwa kufikia malengo ya udahili wa wanafunzi,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali: -

(i) Iandae mpango maalumu kuboresha miundombinu ya kufundisha na kujifunzia inayoendana na mahitaji ya sasa ya Kidijitali;

(ii) Kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ifanye tathmini ili kuwasaidia Wanafunzi wanaodahiliwa katika vyuo hivi kunufaika na fursa ya mikopo ya elimu ya juu; na

(iii) Iandae mpango madhubuti wa kuvitangaza vyuo hivi ili kuvutia wanafunzi wengi kujiunga na vyuo hivi.

### 3.2.7 Uchelewaji wa Maandalizi ya Kongresi ya 50 ya Shirikisho la APIMONDIA

**KWA KUWA,** uchelewaji huo unaweza kupelekea Tanzana kupokonywa nafasi ya kuwa mwenyeji wa Mkutano huo,

**NA KWA KUWA,** hali hiyo itaathiri nafasi ya nchi yetu katika mtandao wa Kimataifa na kukosa ujuzi toka nje kwa watalaamu wa sekta ya nyuki nchini,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ikamilishe taratibu za maandalizi ya Mkutano huo ikiwa ni pamoja na kupata fedha na eneo kwa ajili ya ujenzi wa Ukumbi. Taarifa ya hatua iliyofikiwa katika maandalizi hayo iwasilishwe kwa Katibu wa Bunge kabla ya tarehe 10 Machi, 2025.

### 3.2.8 Kuchelewa kwa Utekelezaji wa Mradi wa REGROW

**KWA KUWA,** utekelezaji wa shughuli zinazotekelezwa chini ya mradi huu umechelewa kukamilika kwa wakati,

**NA KWA KUWA,** ucheleweshaji huo unaathiri mradi kwa kuongeza gharama za utekelezaji na kuchelewa kupatikana kwa manufaa yake katika sekta ya utalii nchini,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali: -

(i) Ihakikishe kuwa shughuli zote zilizopangwa katika mradi huo zinakamilika hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2025;

(ii) Ichukue hatua za kimkataba wa Wakandarasi ambao hawajamaliza mradi ikiwa ni pamoja na kuwatoza gharama za upotevu wa muda (Liquidation Demages) ili kufidia ongezeko la gharama za mradi kwa sababu ya ucheleweshaji wa mradi.

### 3.2.9 Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF)

**KWA KUWA,** mfuko huu unakabiliwa na uhaba wa bajeti na majukumu yake kutofahamika miongoni mwa wananchi wengi nchini,

**NA KWA KUWA,** changamoto hizo zinawanyima fursa wananchi wengi kupata manufaa ya Mfuko huo,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali:-

(i) Ihakikishe inausimamia Mfuko ili kuongeza uwezo wake wa kuhudumia maombi yote ya ruzuku yanayowasilishwa kwake; na

(ii) Kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii ibuni mkakati wa kutangaza fursa zinazopatikana kupitia Mfuko ili kuongeza idadi ya wanufaika.

### 3.2.10 Hoteli na Loji Zilizobinafsishwa na Serikali kwa Wawekezaji

**KWA KUWA,** imebainika kuwa kuna baadhi ya hoteli na loji za Serikali ambazo wawekezaji wamekiuka masharti ya ubinafsishaji,

**NA KWA KUWA,** hali hiyo imesababisha hoteli na loji hizo kushindwa kufanya kazi kwa mujibu wa mikataba ya ubinafshaji na kupoteza manufaa ya kuwepo kwa hoteli hizo,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali: -

(i) Iandae taarifa kuhusu hatua iliyofikiwa katika majadiliano yanayoongozwa na Wakili Mkuu wa Serikali kwa ajili ya mchakato wa kuzirejesha hoteli na Loji hizo Serikalini na kuiwasilisha kwa Katibu wa Bunge kabla ya tarehe 10 Machi, 2025; na

(ii) Kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Ofisi ya Msajili wa Hazina, ifanye tathmini na ufuatiliaji kuhusu utendaji wa hoteli na loji zote zilizobinafsishwa nchini na kuwasilisha taarifa yake kwa Katibu wa Bunge kabla ya tarehe 10 Machi, 2025.

### 3.2.11 Hali ya Miundombinu Katika Maeneo ya Hifadhi Nchini

**KWA KUWA,** miundombinu ya barabara, madaraja na viwanja vya ndege katika maeneo ya hifadhi sio nzuri na fedha zinazotengwa kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa miundombinu hiyo hazitoshi,

**NA KWA KUWA,** hali hiyo inaathiri utekelezaji shughuli za Uhifadhi na kushindwa kuhudumia idadi ya watalii nchini inayozidi kuongezeka kila mwaka,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali:-

(i) Iandae Mpango madhubuti wa muda mrefu kwa kutenga Bajeti mahsusi kwa ajili ujenzi na ukarabati wa kudumu wa miundombinu hiyo;

(ii) Ihakikishe inapeleka fedha za matengenezo na ukarabati wa miundombinu katika mpango wa muda mfupi ili kunusuru miundombinu hiyo kwa sasa; na

(iii) Ihakikishe inaijengea uwezo Kampuni ya Ujenzi ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) ili iweze kuwa inafanya ujenzi na ukarabati wa mara kwa mara katika miundombinu ya hifadhi nchini.

### 3.2.12 Ujenzi wa Makumbusho ya Marais Nchini

**KWA KUWA,** hatua za awali za usanifu wa mradi huu unaolenga kuendeleza uhifadhi katika urithi wa asili ulitakiwa kuanza ndani ya mwaka wa fedha 2024/2025,

**NA KWA KUWA,** mradi huo unafaida ya kulifanya Taifa letu kuwa kitovu cha fikra na kutoa tafsiri ya maendeleo kupitia tawala za nchi yetu baada ya uhuru,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe inatoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo kama zilizoidhinishwa na Bunge ili usanifu wa mradi huo uanze mara moja.

### 3.2.13 Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi

**KWA KUWA**, imebainika kuwa zaidi ya **asilimia 65** ya vijiji nchini havina mipango ya matumizi ya ardhi,

**NA KWA KUWA**, hali hii inachangia migogoro baina ya watumiajii wa ardhi nchini,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae Mpango Madhubuti ambao utaiwezesha Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kupata fedha kwa ajili ya Kuandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi kwa vijiji vyote nchini.

### 3.2.14 Ucheleweshaji wa Maboresho ya Mfumo wa Usimamizi wa Ardhi Nchini

**KWA KUWA,** utekelezaji wa maboresho ya Mfumo wa Usimamizi wa Ardhi nchini umechelewa kwa zaidi ya mwaka mmoja;

**NA KWA KUWA**, ucheleweshaji huo umechangia kuendelea kuwepo kwa changamoto ya utunzaji wa kumbukumbu kwa wananchi kunakochangiwa na watumishi wasio waaminifu katika sekta hiyo;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ijipange kukamilisha mfumo huo ili kutatua changamoto ya utunzaji wa kumbukumbu za taarifa katika sekta ya ardhi nchini.

### 3.2.15 Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)

**KWA KUWA,** Shirika halijakamilisha baadhi ya miradi ya kimkakati kinyume na lengo la kuikamilisha kufikia mwaka 2025, huku kukiwa na malalamiko ya Shirika kujenga nyumba za bei ghali;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inachangia miradi hiyo kutekelezwa kwa gharama kubwa na kupunguza manufaa ya miradi hiyo kwa Shirika;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali:-

(i) Ilisimamie Shirika hilo kukamilisha mradi wa Kawe 711 kufikia tarehe 30 Juni, 2026 kwani utekelezaji wake umefikia **asilimia 50** tu kwa sasa;

(ii) Ihakikishe majadiliano kati ya Shirika na Wakandarasi katika miradi ya Golden Primier na Kiwanja Na. 300 Regent Estate yanafikia mwisho kufikia tarehe 30 Juni, 2025 ili kukwamua miradi hiyo ambayo utekelezaji wake umesimama tangu mwaka 2017;

(iii) Ilipe madeni kwa Shirika ikiwa ni malimbikizo ya kodi ya Pango na gharama ya huduma ya ukandarasi wa ujenzi wa majengo ya Wizara Nane; na

(iv) Ilisaidie Shirika kutimiza azma ya kujenga nyumba za gharama nafuu kwa kuondoa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa nyumba zinauzouzwa kwa bei isiyozidi **Shilingi milioni 100** badala ya **Shilingi milioni 50** ya sasa ili kuwafanya wananchi na wafanyakazi kuweza kumudu ununuzi wa nyumba hizo

### 3.2.16 Programu ya Kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa Vijiji 333 katika mwaka 2024/2025

**KWA KUWA,** muda wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025 umefikia asilimia 50 huku kukiwa hakujatolewa fedha za kutekeleza ya program hiyo ;

**NA KWA KUWA**, hali hii inayoweza kufanya lengo la Programu hiyo lisikamilke kama ilivyopangwa;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali:-

(i) Itoe kiasi cha Shilingi bilioni 5 kama ilivyoahidi ili kuhakikisha programu hiyo inatekelezwa kama ilivyopangwa; na

(ii) Itenge fedha zaidi katika bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 ili kufanya kazi ya mipango ya matumizi ya ardhi kuwa endelevu.

### 3.2.17 Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi Nchini

**KWA KUWA,** asilimia 70 ya halmashauri na taasisi zilizokopeshwa fedha kwa ajili ya kutekeleza program hiyo zimeshindwa kurejesha fedha zote tangu mwaka 2018,

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inakwamisha azma ya Serikali ya Kupanga na Kupima ardhi yote nchini,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali:-

(i) Kupitia Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI ihakikishe inazisimamia Halmashauri zote kurudisha kiasi cha **Shilingi bilioni 22.5** walizokopeshwa kwenye mradi huu ili ziweze kutumiwa na Wizara ya sekta katika kuendelea Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi kwenye Halmshauri zote nchini;

(ii) Kupitia Wizara ya Ardhi ihakikishe inafanya uchambuzi wa maandiko ya halmashauri zinazoomba mikopo kupitia programu hiyo ili kujiridhisha kama zinauwezo wa kurejesha fedha hizo; na

(iii) Kupitia Wizara ya Ardhi ihakikishe inalinda uhai wa Mfuko wa Mzunguko wa Maendeleo ya Ardhi (Plot Development Revolving Fund) ili uendelee kuwa chanzo cha uhakika cha fedha kwa ajili ya Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi nchini.

### 3.2.18 Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**KWA KUWA,** Serikali iliamua ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi (Land Rent) ufanywe na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na pango la Ardhi,

**NA KWA KUWA**, uamuzi huo umetoa matokeo hasi katika ufuatiliaji wa makusanyo hayo kwani Wizara haina fedha za kutosha kwa

ajili ya shughuli hiyo na halmashauri ambazo zimepewa jukumu hilo hazilitekelezi,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali: -

(i) Irudishe jukumu la ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi katika Wizara ya Ardhi ambayo ndio ina nyezo za kisheria na kimfumo katika kutekeleza jukumu hilo;

(ii) Iiwezeshe kifedha Wizara ya Ardhi katika kutimiza jukumu hilo kwa kuruhusu ibaki na **asilimia 20** ya makusanyo ya Kodi ya kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika zoezi hilo; na

(iii) Kupitia Wizara ya Ardhi ihakikishe inaongeza nguvu katika kukusanya maduhuli ili kufikia lengo la makusanyo katika mwaka wa fedha 2024/2025.

### 3.2.19 Ardhi ya Wawekezaji ambayo Haijaendelezwa

**KWA KUWA,** imebainika uwepo wa uhaba wa ardhi kwa wananchi wanaoishi kuzunguka baadhi ya maeneo ambayo yako chini ya wawekezaji wenye mashamba makubwa huku mashamba hayo yakiwa haijaendelezwa kwa mujibu wa Sheria,

**NA KWA KUWA,** hali hiyo huchangia migogoro inayopelekea maafa, majeruhi na uharibifu wa miundombinu kati ya wawekezaji na wananchi katika maeneo husika,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye tathmini ya wamaliki wa mashamba makubwa yote nchini ili kutambua ambayo hajaendelezwa na kuchua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria.

### 3.2.20 Utatuzi wa migogoro ya Ardhi jiji la Dodoma

**KWA KUWA**, Jiji la Dodoma ni moja ya sehemu zenye migogoro mingi ya ardhi nchini,

**NA KWA KUWA,** migogoro mingi inachangiwa na uwepo wa watumishi wasiowaaminifu na wasiozingatia sheria katika sekta ya ardhi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kuwa, Serikali:-

(i) Ihakikishe kuwa miamala yote ya ardhi katika jiji la Dodoma inafanyika katika Mfumo wa e-Ardhi ambao tayari unafanya kazi katika jiji hilo; na

(ii) Inafanya tathmini na uhakiki wa huduma zinazotolewa na kila mtumishi katika Ofisi ya Ardhi jijini Dodoma ili kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wasiowaaminifu.

### 3.2.21 Marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 *(Toleo la Mwaka 2023)*

**KWA KUWA,** Sera hiyo imebainisha changamoto ya kutokuwepo kwa mipango ya matumizi ya ardhi katika eneo la mipakani,

**NA KWA KUWA,** hali hiyo inawanyima wananchi wa mpiakani fursa ya kupata manufaa yanayopatikana katika sekta ya ardhi,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali:-

(i) Iandae Mpango wa Matumizi ya Ardhi katika maeneo ya mipakani kwa kuzingatia Usalama wa Nchi ili kuleta ustawi wa wananchi katika maeneo ya mipakani kupitia sekta ya ardhi;

(ii) Ifanye uwekezaji wa miundombinu ya barabara katika maeneo ya mipakani ili kuchochea shughuli za maendeleo na kurahisiha utekelezaji wa shughuli za ulinzi katika maeneo hayo.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 HITIMISHO NA KUFUNGA HOJA

## 4.1 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, Kwa namna ya kipekee napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako mafanikio ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii katika kutekeleza Shughuli zake kwa kipindi cha Februari 2023 hadi Januari, 2024 yametokana na juhudi, weledi pamoja na umahiri mkubwa wa Wajumbe katika kushiriki na kutoa maoni yenye tija wakati wote ambapo Kamati imekuwa ikiisimamia Serikali. Ni wazi kwamba, ufanisi wa utendaji wa Kamati hii unatokana zaidi na Ofisi yako kuwajengea uwezo Wabunge na kuwapa msaada stahiki wa kitaalam, na kiushauri wakati wote. Kwa heshima kubwa ningependa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge (Hansard). Majina hayo ni haya yafuatayo: -

1. Mhe. Timotheo P. Mnzava, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Alaudin Hasham Salim, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Askofu Josephat M. Gwajima, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Neema William Mgaya, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Innocent Bilakwate, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Maida Hamadi Abdallah, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Dkt Florence G. Samizi, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Emmanuel A. Mwakasaka, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Festo Richard Sanga, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Josephine Thabita Chagula, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Shaban Omari Shekilindi, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Ester Lukago Midimu , Mb - Mjumbe

22. Mhe. Asha Juma Abdallah, Mb - Mjumbe


**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Deogratius J. Ndejembi (Mb), na Naibu wake Mhe. Geofrey M. Pinda, (Mb) Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Balozi Dkt Pindi H. Chana (Mb) na Naibu wake Mhe. Dunstan L. Kitandula, (Mb) Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru Watunishi wote wa Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leonard, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote.

### 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji shughuli hizo, na pia maoni na mapendekezo ya Kamati, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.



Timotheo P. Mnzava, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**

7 Februari, 2025

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana, Mwenyekiti wetu wa Kamati, ahsante sana. Sasa

nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Mheshimiwa Jackson Kiswaga aje awasilishe maoni ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON G. KISWAGA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa shukrani zangu kwa kunipa fursa kutoa taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kwa kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema, uhai na kibali cha kuiona siku ya leo. Naomba taarifa hii yote iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninakushukuru kwa kunipa fursa ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2024 hadi Januari, 2025. Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne kama inavyoonekana katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inalenga kuliwezesha Bunge lako Tukufu kwa niaba ya Wananchi ambao ndiyo waliyolipa jukumu hili la kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kufuatilia hatua zilizochukuliwa katika utekelezaji wa masuala mbalimbali yaliyo chini ya Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira pamoja na kubainisha maeneo yenye mafanikio na yale yenye changamoto.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ilitekeleza

shughuli mbalimbali kama inavyoonekana katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa na Serikali wakati wa Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano wa azimio lililotekelezwa kwa ukamilifu kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira pendekezo la Serikali kutoa mafunzo kwa wataalamu wa ndani ili wawe na ujuzi wa kutosha wa kuandaa mapitio ya tathmini ya athari kwa mazingira ambapo katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Disemba, 2024 jumla ya wataalamu 75 walipatiwa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, mfano wa Azimio ambalo limetekelezwa kwa sehemu na utekelezaji wake unaendelea ni pendekezo la kufanya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191, ili iweze kuendana na Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021; ambapo Serikali iliwasilisha Muswada wa Marekebisho Madogo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 ili kutatua baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kutekeleza ahadi yake kwa Kamati ya kuwasilisha marekebisho makubwa ya sheria hiyo haraka iwezekanavyo ili kuendana na Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 na Mipango ya Muda mrefu ya Taifa katika uhifadhi wa mazingira ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 - 2050.

Mheshimiwa Spika, mfano wa azimio ambalo halikutekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira ni Serikali kuchukua hatua za haraka kufanyia marekebisho Kanuni zote ambazo zinaonekana kukinzana na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura, 191 na kuruhusu wakufunzi ambao ni washauri

elekezi wa mazingira kufanya majukumu yao kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati haijaridhishwa na majibu kwamba, kwa kipindi chote cha mwaka mzima ni rasimu pekee ya marekebisho ya kanuni hizo ndiyo imeandaliwa. Ni rai ya Kamati kwa Serikali kushughulikia suala hilo kwa haraka ili kutatua changamoto zilizojitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Maji. Mfano wa azimio lililotekelezwa kikamilifu ni pendekezo kwa Serikali kuchukua hatua madhubuti na za haraka ili kuhakikisha kuwa uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Maji unakamilika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Maji na kupitisha sera iliyopendekezwa ambapo pamoja na mambo mengine sera hiyo imeweka mkazo katika upangaji shirikishi, ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji, usimamizi na utoaji huduma za maji, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na usimamizi wa huduma za usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, mfano wa azimio linaloendelea kutekelezwa na Wizara ya Maji ni pendekezo kwa Serikali la kuainisha maeneo yote ya umma yenye changamoto ya ukosefu wa maji na kuyatafutia vyanzo vya kujitegemea ili kuhakikisha yanapata maji ya kutosha na kwa wakati wote. Kamati inasisitiza Serikali kuendelea na hatua hiyo ili kuimarisha huduma za maji katika maeneo yote ya umma.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati; maoni ya jumla. Kamati ina maoni ya jumla yafuatayo: -

(a) Bajeti inayotengwa kwa ajili ya Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ni finyu ikilinganishwa na mahitaji makubwa ya fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo; *(Makofi)*

(b) Usimamizi wa sheria, kanuni na miongozo hauridhishi;

(c) Watumishi kwa Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ni pungufu ikilinganishwa na mahitaji halisi;

(d) Elimu inayotolewa kwa umma juu ya uhifadhi wa mazingira haiwafikii walengwa wote; *(Makofi)*

(e) Hakuna programu za kutosha za utafiti na mafunzo ya umahiri kwa watalaam; *(Makofi)*

(f) Utekelezaji wa mwongozo wa kuratibu sekta za kiserikali zinazohusika katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira hauridhishi; na

(g) Utekelzaji wa sera ya kuwawezesha wakandarasi wa ndani hauridhishi.

Mheshimiwa Spika, maoni mahsusi kila sekta. Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira: -

(i) Kamati inatambua hatua ya Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ya kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Marekebisho madogo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2024;

(ii) Kuathirika kwa shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii kutokana na mabadiliko ya tabianchi kunasababishwa na kukwama kwa shughuli nyingi za kiserikali;

(iii) Uzagaaji wa takangumu nchini ni matokeo ya uzalishaji mkubwa wa takangumu ikilinganishwa na uwezo wa kukusanywa na kurejeleza taka hizo;

(iv) Utekelezaji wa mkataba wa Nairobi Kuhusu Uhifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi unachochea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kukuza uelewa kwa jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira;

(v) Utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2024 una lengo la kuchagia ukuaji wa uchumi kupitia matumizi endelevu ya Rasilimali za maji kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira na ushirikishwaji wa Jamii. Hata hivyo, Sera haijatungiwa Sheria yake;

(vi) Utiririshaji wa majitaka katika Ziwa Victoria umesababisha athari mbalimbali ikiwemo kupungua kwa rasilimali kama vile samaki, kuongezeka kwa viumbe vamizi, kuharibika kwa mifumo ya ikolojia muhimu ya viumbe hai vya majini, na kupungua kwa ubora wa maji;

(vii) Utolewaji usioridhisha wa fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendelea unaathiri utekelezaji wa miradi iliyopangwa; na

(viii) Usimamizi hafifu wa zuio la matumizi ya mifuko ya *plastic. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji:-

(i) Hatua ya Serikali kupitia Wizara ya Maji kukamilisha maboresho ya Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002 ni ya kupongezwa*; (Makofi)*

(ii) Kutotolewa kwa ukamilifu na kwa wakati fedha za Mfuko wa Taifa wa Maji zinazotokana na tozo ya mafuta ya dizeli na petroli ni ukiukwaji wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria ya Fedha Na. 16 ya Mwaka 2015;

(iii) Kiwango kikubwa cha upotevu wa maji nchini kinasababisha upotevu wa mapato ya Serikali na upungufu wa maji kwa matumizi ya nyumbani na shughuli za uzalishaji;

(iv) Uwekezaji wa ndani kupitia hati fungani umekuwa ni chanzo cha uhakika cha upatikanaji wa fedha katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(v) Msukumo mdogo katika utekelezaji wa Mwongozo wa Uvunaji wa Maji ya Mvua umesababisha jamii kutoshiriki katika uvunaji wa maji, uratibu hafifu katika ujenzi wa mabwawa ya maji na upatikanaji mdogo wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa;

(vi) Gharama za uzalishaji wa maji zimekuwa zikiongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo; kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)*, gharama za umeme, vipuri na mabomba pamoja na madawa ya kusafisha maji; na

(vii) Kukosekana kwa maji kwenye baadhi ya visima vinavyoendelea kuchimbwa licha ya kutumia rasilimali nyingi katika uchimbaji huo kunaiingizia Serikali hasara na wananchi kukosa maji.

Mheshimiwa Spika, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Naomba kutoa ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa namna itakavyowezesha Bunge kuazimia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mapendekezo kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira; tafiti za kimazingira na mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi:-

KWA KUWA, majanga mbalimbali ya kimazingira kama maporomoko ya ardhi, ukame na mafuriko yamesababisha madhara makubwa ikiwemo vifo, uharibifu wa miundombinu, upotevu wa mifugo kwa maeneo mengi ikiwemo Hanang, Kibiti na Rufiji.

NA KWA KUWA, kutokea kwa majanga hayo kumeathiri shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii kwa wananchi na Serikali;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Itungwe Sheria, Kanuni na Miongozo ya uanzishaji wa Mfuko wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi utakaogharamia utekelezaji wa Mipango na Mikakati ya usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi nchini.

(b) Serikali isimamie ipasavyo mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi kwa kuchukua hatua madhubuti katika utekelezaji wa Maazimio ya Kimataifa *(COP)* yanayolenga kuinua Uchumi wa Wananchi na kuhifadhi Mazingira kwa: -

(i) Kuandaa mwongozo wa kuwaongezea uwezo wa kiutendaji Watendaji wote wa sekta ya mazingira kwa kuwapa fursa sawa za kushiriki katika majukwaa mbalimbali ya kimazingira ikiwa ni pamoja na mikutano ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

(ii) Kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia hususan kwa maeneo ya vijijini ili kupunguza ukataji ovyo wa misitu. Aidha, hamasa katika Biashara ya Kaboni na manufaa yatakayopatikana iwe chachu katika kuhakikisha wananchi wa maeneo hayo wanapata nishati safi kwa gharama nafuu;

(iii) Kuandaa na kusimamia mwongozo utakaowawezesha wakulima wa tumbaku katika maeneo mbalimbali ya nchi kunufaika na kilimo hicho pasipo kuathiri misitu iliyo pembezoni; na

(iv) Kuandaa na kutekeleza program za utafiti, ubunifu na mafunzo ili Taifa liwe na uwezo mkubwa zaidi wa kukabiliana na athari za mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa taka ngumu:-

KWA KUWA, wastani wa takangumu zinazozalishwa nchini ni nyingi zaidi ikilinganishwa na zile zinazokusanywa na kurejelezwa;

NA KWA KUWA, pamekuwa na uelewa na mwitikio mdogo wa wananchi kuhusu utenganishaji wa taka katika ngazi ya kaya, uhaba wa miundombinu stahiki na udhibiti wa takangumu, uzingatiaji hafifu wa mipango miji inayopelekea kuwepo kwa

ujenzi holela, na mwamko hafifu wa matumizi ya mbolea itokanayo na taka;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali iharakishe mchakato wa kupata maeneo makubwa mbali na makazi ya watu kwa kuzingatia Kanuni za Mipango Miji ili kutumika kuhifadhi taka zinazozalishwa katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya jirani. Pengine, uzoefu unaopatikana kutokana na changamoto za kukabiliana na taka ngumu katika Jiji la Dar es Salaam utumike kunusuru miji na majiji mengine, ikiwemo Dodoma;

(b) Mchakato wa kukusanya chupa zenye rangi mfano *energy drinks* na kuzichakata kupitia viwanda vilivyoanzishwa uongezewe motisha ili kudhibiti kikamilifu uzagaaji wa chupa hizo;

(c) Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira iandae kanuni zitakazosimamia ubora wa madampo na vitendea kazi vinavyotumika katika zoezi la ukusanyaji wa taka ikiwa ni pamoja na matumizi ya magari ambayo katika kusafirisha taka yanachafua mazingira;

(d) Serikali iongeze jitihada katika kudhibiti utupaji hovyo wa taka ngumu kwa: -

(i) Kusimamia utengaji wa maeneo sahihi ya kuweka madampo wakati wa upangaji wa Miji;

(ii) Kuanzisha na kusimamia utaratibu wa kutenganisha taka *(Sorting)* kuanzia zinakozalishwa;

(iii) Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika eneo la taka ngumu;

(iv) Kuhakikisha miundombinu yote ya kuhifadhi taka inatumika kwa usahihi;

(v) Kushirikiana na TAMISEMI kuandaa mkakati wa kutoa mafunzo ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa viongozi wote kuanzia ngazi ya Watendaji wa Vijiji na Mitaa; na

(vi) Kuongeza msukumo katika utekelezaji wa zuio la matumizi ya vifungashio vya plastiki.

(e) Serikali iendelee kuhamasisha na kuwezesha vikundi vya wananchi wanaojihusisha na ukusanyaji wa taka ngumu kwa kutatua kero zao kwa wakati na kuwajengea uwezo zaidi wa kujikwamua kiuchumi;

(f) Uhifadhi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi upewe kipaumbele katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 – 2050;

(g) Serikali ihamasishe utenganishaji wa taka kwa kuanza na maeneo yenye mikusanyiko mikubwa ya watu, mfano vituo vya mabasi, reli, masoko, shuleni, hospitali, na baadaye kufikia ngazi ya kaya; na

(h) Serikali iongeze uwezo kwa Taasisi zake zinazojihusisha na biashara ya uzoaji taka kama Magereza na JKT, ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji, utenganishaji na usafirishaji wa taka ngumu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Nairobi.

KWA KUWA, Mikataba mingi ya Kimataifa kuhusu mazingira ukiwemo Mkataba wa Nairobi kuhusu Uhifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi inalenga kuhifadhi mazingira;

NA KWA KUWA, utekelezaji wa Mikataba hiyo umekuwa na manufaa mbalimbali kwa Taifa ikiwa ni pamoja na kupata fedha za utekelezaji wa miradi yenye mlengo huo, kuimarisha ushirikiano

wa Kikanda na nchi nyingine na kukuza uelewa kwa Jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira iendelee na jitihada za kutafuta fedha ili kuhakikisha kuwa, mipango na mikakati katika uandaaji na utekelezaji wa miradi mikubwa ya kuhifadhi mazingira ya Bahari inatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu:-

KWA KUWA, Tanzania imekuwa ikitekeleza shughuli za Uchumi wa Buluu kupitia Sekta mbalimbali zenye mnasaba na uchumi huo zikiwemo uvuvi, maliasili na utalii, maji, nishati, uchukuzi, madini, uwekezaji, viwanda na biashara na uhifadhi wa mazingira;

NA KWA KUWA, dhana ya Uchumi wa Buluu ni dhana inayochagiza ukuaji wa uchumi kupitia matumizi endelevu ya rasilimali za maji kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira na ushirikishwaji wa Jamii;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, ihakikishe mchakato wa kutunga Sheria ya Usimamizi wa Uchumi wa Buluu kwa kuzingatia malengo ya Sera Mpya ya Uchumi wa Buluu ya Mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udhibiti wa utiririshaji wa majitaka na taka za viwandani katika Ziwa Victoria:-

KWA KUWA, pamekuwa na shughuli zisizo endelevu za kibinadamu zikiwemo; uvuvi haramu, uharibifu wa maeneo oevu, kilimo kisichozingatia uhifadhi, uchimbaji madini usiokuwa endelevu pamoja na utiririshwaji wa majitaka katika maeneo yanayozunguka Ziwa Victoria;

NA KWA KUWA, hali hiyo imesababisha kupungua kwa rasilimali kama vile samaki, kuongezeka kwa viumbe vamizi, kuharibika kwa mifumo ikolojia ya viumbe hai vya majini, na kupungua kwa ubora wa maji;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kwa kushirikiana na Halmashauri zote zinazozunguka Ziwa Victoria kutekeleza mikakati iliyopo ya udhibiti wa taka katika Ziwa hilo, kwa kuzingatia ipasavyo Sheria ya Usimamizi wa Mazingira; na

(ii) Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira ichukue hatua za haraka zinazowezesha udhibiti endelevu wa usafirishaji wa majitaka katika Mto Milongo uliopo Jiji la Mwanza.

Mheshimiwa Spika, ushauri na mapendekezo kwa Wizara ya Maji kuhusu mahitaji makubwa ya fedha za utekelezaji wa miradi ya maji nchini.

KWA KUWA, kumekuwa na ongezeko kubwa la mahitaji ya maji kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kasi ya ongezeko la idadi ya watu, kasi ya ukuaji wa miji, na ongezeko la shughuli za uzalishaji;

NA KWA KUWA, ongezeko la mahitaji ya maji haliwiani na kiwango cha uzalishaji wa maji na hivyo kusababisha mahitaji makubwa ya fedha za utekelezaji wa miradi ya maji nchini;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali izingatie ongezeko la mahitaji makubwa ya maji nchini pamoja na ongezeko la mahitaji makubwa ya fedha za kutekeleza miradi ya maji wakati wa kuweka ukomo wa Bajeti ya Wizara ya Maji;

(ii) Kwa kuzingatia matakwa ya mabadiliko ya Sheria ya Fedha Na. 16 ya Mwaka 2015, Serikali iwasilishe kwa

ukamilifu na kwa wakati fedha zote za Mfuko wa Taifa wa Maji zinazokusanywa kutokana na tozo ya shilingi 50 kwa kila lita ya petroli na dizeli ili kupunguza pengo kubwa la mahitaji ya fedha lililopo katika Sekta ya Maji;

(iii) Kwa kuzingatia mwenendo wa bei ya mafuta duniani, Serikali iangalie uwezekano wa kutumia nafuu ya kupungua kwa bei ya mafuta duniani *(Windfall gain)* kwa kutunisha Mfuko wa Taifa wa Maji;

(iv) Serikali kupitia Wizara ya Maji ibuni vyanzo vipya vya mapato ya Mfuko wa Taifa wa Maji kwa mfano, *Tanga UWASA Green Bond* ili kupunguza utegemezi wa Mfuko huu kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali;

(v) Kwa kuzingatia mapinduzi makubwa ya uzalishaji Umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, na Rusumo, Serikali itafakari umuhimu wa manufaa ya kuweka bei maalum ya umeme *(Special Tariffs)* katika Sekta ya Maji, ili kupunguza gharama za uzalishaji wa maji;

(vi) Wizara ya Maji iandae Mpango wa Manunuzi ya pamoja *(Bulk procurement)* ili kutokana na faida ya kununua kwa wingi, nafuu itakayopatikana ipunguze gharama za uendeshaji na uzalishaji maji; na

(vii) Kwa kuzingatia umuhimu na unyeti wa huduma ya maji, Serikali iondoe kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* katika bidhaa na huduma muhimu zinazotumika wakati wa utekelezaji wa miradi ya Maji nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji na usambazaji wa maji katika Majiji ya Dodoma, Dar es Salaam, Tanga, Mbeya, Mwanza na Arusha:-

KWA KUWA, kumeendelea kuwepo na changamoto mbalimbali zinazokwamisha utendaji wa Mamlaka za Maji nchini zikiwemo, Mipango Miji kutozingatia uwepo wa miundombinu ya

majisafi na majitaka; uhujumu wa miundombinu ya majisafi na majitaka; na upotevu wa maji kutokana na mivujo, uchakavu wa miundombinu na ubovu wa dira za maji.

NA KWA KUWA, kuwepo kwa changamoto hizo kunakwamisha juhudi za Serikali katika kufanikisha azma ya kuwapatia wananchi wake majisafi na salama;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Wizara zishirikiane na kuchukua hatua madhubuti za kudhibiti ujenzi wa makazi holela kwa kuzingatia Kanuni za Mipango Miji, ili kuwezesha uwepo wa miundombinu muhimu kama vile miundombinu ya maji safi na maji taka katika maeneo yote yaliyopangwa;

(ii) Mikakati endelevu ibuniwe na kutekelezwa, ili kuhakikisha maeneo yote yenye vyanzo vya maji au miundombinu ya maji iliyokamilika yanapata maji ili kuleta tija ya fedha zilizowekezwa na Serikali;

(iii) Mamlaka za maji zishirikiane na kubadilishana uzoefu kuhusu namna bora zitakazowezesha upatikanaji wa maji safi kwa wananchi wa maeneo yote nchini; na

(iv) Serikali ihakikishe kuwa huduma ya maji katika maeneo yote ya umma zikiwemo shule, vituo vya mabasi, masoko, viwanja vya michezo, viwanja vya ndege, vyuo vikuu, maeneo ya ibada na vituo vya treni inapatikana kwa wakati wote, ili kukidhi mahitaji ya wananchi na vilevile kuchukua tahadhari juu ya magonjwa ya mlipuko katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya upotevu wa maji nchini:-

KWA KUWA, kiwango cha upotevu wa maji nchini ni 36.2% kikiwa ni juu ya wastani unaokubalika Kimataifa na Kitaifa wa 20%;

NA KWA KUWA, hali hiyo inasababisha athari mbalimbali zikiwemo upotevu wa mapato na upungufu wa maji kwa matumizi mbalimbali nyumbani na shughuli za uzalishaji;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali ihamasishe matumizi ya Mfumo wa Kisasa wa Kudhibiti Mivujo *(Integrated Leakage Management System)* kwa Mamlaka zote nchini ili kudhibiti kwa ukamilifu tatizo la upotevu wa maji nchini;

(ii) Kwa kushirikiana na Viongozi wa Mitaa, ichukue hatua za dharura za kudhibiti upotevu wa maji katika maeneo yote nchini pamoja na kutoa elimu kwa umma hususan kwa jamii za kifugaji kuhusu umuhimu wa kulinda miundombinu ya maji katika maeneo yote;

(iii) Ianzishe vitengo mahususi vitakavyoshughulikia masuala ya upotevu wa maji na kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa kubaini mivujo katika maeneo yote nchini, ili kuwezesha upatikanaji wa majisafi na kudhibiti hasara itokanayo na upotevu huo; na

(iv) Iandae mkakati wa pamoja utakaohusisha Wizara mbalimbali zikiwemo Wizara ya Nishati, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Uchukuzi, ili kudhibiti wizi wa miundombinu katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa shughuli za maji kupitia Hati Fungani:-

KWA KUWA, uwekezaji wa ndani katika Hati Fungani umekuwa ni chanzo cha uhakika cha upatikanaji wa fedha katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo;

NA KWA KUWA, hatua hiyo ni njia madhubuti na ya kimapinduzi kwa sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Maji nchini katika kuongeza kipato;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihamasishe uwekezaji katika Hati Fungani, ili kuimarisha zaidi uchumi wa wananchi wake na kutafuta changamoto za uwekezaji katika miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya mazingira;

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa mwongozo wa uvunaji wa maji ya mvua:-

KWA KUWA, mwongozo wa uvunaji wa maji ya mvua unalenga kuhakikisha uendelevu katika jitihada za kuongeza upatikanaji wa maji kwa mahitaji ya kijamii, kiuchumi na mazingira, pia kuzuia mafuriko ya maji ambayo yamekuwa yakitokea maeneo mengi nchini;

NA KWA KUWA, kumekuwa na msukumo mdogo katika utekelezaji wa mwongozo huo, hali ambayo inasababisha utayari mdogo wa jamii kushiriki kuvuna maji ya mvua, uratibu hafifu katika ujenzi wa mabwawa ya maji na upatikanaji mdogo wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali isimamie kuanzishwa kwa Kamati ya Kitaifa itakayoratibu shughuli za uchimbaji wa mabwawa ya maji kwa kuzingatia uhitaji wa maji kwa shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi; na

(ii) Ihamasishe ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji kwa kuanza na taasisi zake zikiwemo shule, zahanati na vyuo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shughuli zilizotekelezwa kwa kutumia mitambo 25 iliyonunuliwa na Serikali kwa ajili ya kuchimba visima na usambazaji wa maji:-

KWA KUWA, baadhi ya visima vinavyoendelea kuchimbwa nchini vimekuwa vikikosa maji licha ya kutumia rasilimali nyingi katika uchimbaji huo;

NA KWA KUWA, hali hiyo inasababisha hasara na kurudisha nyuma jitihada za kusaidia upatikanaji wa maji kwa maeneo yote nchini;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;

(i) Kwa kushirikiana na wadau wa utafiti Vyuo Vikuu, *TPDC* na kadhalika, Serikali iboreshe tafiti kwenye ufuatiliaji wa maji chini ya ardhi kwa kuwaongezea uwezo wataalamu wake pamoja na kutumia teknolojia za kisasa katika uchimbaji wa visima; na

(ii) Wizara ichukue hatua madhubuti zitakazowezesha kukamilika kwa uchimbaji wa visima vitano kwa kila Jimbo vilivyoahidiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa umahiri wako kwa kutuongoza vyema katika kuisimamia na kuishauri Serikali kwa kuzingatia sheria, taratibu na dhana nzima ya utawala bora kwa lengo la kuwaletea Watanzania maendeleo yenye tija. Tunakuombea afya njema, maisha marefu na mafanikio tele katika utekelezaji wa majukumu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge na Naibu Spika kwa kazi nzuri anayoifanya ya kukusaidia kuongoza na kusimamia Mhimili wa Bunge. Aidha, nawashukuru Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kuwashukuru Mawaziri, Mheshimiwa Jumaa Aweso Mbunge na Waziri wa Maji; na Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira; Naibu Mawaziri wake, Mheshimiwa Mhandisi Kundo Andrea Mathew, Mbunge na Naibu Waziri wa Wizara ya Maji; na Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, Mbunge na Naibu Waziri, Ofisi

ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zote zilizo chini yake wakiongozwa na Mhandisi Mwajuma Waziri, Katibu Mkuu Wizara ya Maji na Mhandisi Cyprian Luhemeja, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Natambua kuwa ushirikiano wao ndiyo uliofanikisha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa shughuli za Kamati. Natambua na kuthamini michango yao adhimu, makini na ya uzalendo wa hali ya juu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Kamati. Kwa heshima kubwa ninatamani kuwataja majina yao, hata hivyo kutokana na ufinyu wa muda, naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama yalivyoonekana katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, lakini siyo kwa umuhimu, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Bunge kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati, chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard kwa umakini na weledi katika kuratibu shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila kukwama na kuandaa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kwa kina shughuli zilizotekelezwa na Kamati, matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo na uchambuzi wake, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa liipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira na likubali Maoni na Mapendekezo yote ya Kamati kama yalivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**7 FEBRUARI, 2025**

# TAARIFA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA KWA KIPINDI CHA FEBRUARI, 2024 HADI JANUARI, 2025 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

*[Inatolewa Chini ya Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]*

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema, uhai na kibali cha kuiona siku ya leo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba Taarifa hii yote iingie kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (HANSARD).

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2024 hadi Januari, 2025.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Muundo wa Taarifa hii umezingatia matakwa ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 ambayo yanaainisha Sehemu Nne za Taarifa kama ifuatavyo: -

a) Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi wenye maelezo ya jumla pamoja na njia na mbinu zilizotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati;

b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati;

c) Sehemu ya Tatu inabainisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati na;

d) Sehemu ya Nne ni hitimisho.

**1.3 Madhumuni ya Taarifa**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inalenga kuliwezesha Bunge lako Tukufu kwa niaba ya Wananchi ambao ndiyo wamelipa jukumu hilo la kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kufuatilia hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa masuala mbalimbali yaliyo chini ya Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira pamoja na kubainisha maeneo yenye mafanikio na yale yenye changamoto. Aidha, Maudhui ya Taarifa yanalisaidia Bunge kuhakiki hatua zinazofikiwa na Serikali ili kukidhi matarajio ya Wananchi kwa shughuli za Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira.

**1.4 Msingi wa Utekelezaji wa Shughuli za Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 8(1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatambulisha Lengo Kuu la Serikali la kuwezesha Ustawi wa Wananchi. Vile vile, Ibara ya 63(2) ya Katiba imelipa Bunge jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya Wananchi.

Aidha, Ibara ya 96(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inatoa Mamlaka kwa Bunge kuunda Kamati mbalimbali za Bunge kadri litakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa Madaraka yake.

Ni kwa Muktadha huo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ni miongoni mwa Kamati Kumi na Nane za Kudumu za Bunge chini ya Kanuni ya 137 ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Vile vie Kamati hii ni miongoni mwa Kamati Kumi na Moja za Kisekta.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (6) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ina jukumu la kusimamia Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Nyongeza ya Nane 7 (1) (a - d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 imeainisha Majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta ikiwemo Kamati ya Maji na Mazingira kuwa ni pamoja na: -

a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia;

b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

c) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo pamoja na Taasisi zilizo chini yake; na

d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

**1.5 Njia na mbinu zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kuhusianisha matokeo ya shughuli za Kamati yanayoripotiwa na mapendekezo yatakayotolewa, naomba kubainisha njia na mbinu zilizotumika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 142 (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Njia hizo ni: -

a) Vikao vya kupokea na kujadili Taarifa za Utendaji wa Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira na Taasisi zilizo chini yake kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1) (c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 kwa lengo la kufahamu Utendaji, mafanikio na changamoto wanazokutana nazo;

b) Ziara za kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ili kujiridhisha kuhusu hatua za utekelezaji na ufanisi wake (*Value for Money*);

c) Vikao vya Uchambuzi wa Bajeti za Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa mujibu wa Kifungu cha 117(2) na 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge;

d) Ziara za kutembelea Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira ili kuona namna wanavyotekeleza Majukumu yao; Mafanikio yaliyopatikana, na changamoto zinazowakabili kisha kuishauri Serikali kwa lengo la kuboresha Huduma ya Maji na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa Mazingira.

e) Vikao vya pamoja na wadau wa Sekta ya Maji na Mazingira kwa lengo la kufahamu majukumu yao; Mafanikio yao na changamoto wanazokabiliana nazo ili kuishauri Serikali ipasavyo; na

f) Mafunzo na Semina kuhusu Sekta za Maji na Mazingira kwa lengo la kuwajengea uelewa Wajumbe juu ya Sekta hizo.

**Mheshimiwa Spika**, njia hizo ziliiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ya Kikanuni. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa maudhui ya Taarifa hii ni matokeo ya njia nilizozitaja.

**1.6 Shughuli zilizotekelezwa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira imetekeleza shughuli zifuatazo: -

**1.6.1 Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 inayozitaka Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha, Kamati ilitembelea na kukagua Miradi Nane (8) ambapo Miwili (2) ilitekelezwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na Sita (6) chini ya Wizara ya Maji. Naomba kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa ufafanuzi wa kina kuhusu miradi hii pamoja na Maoni na Ushauri ulitolewa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha, Kamati ilipata fursa ya kutembelea miradi mingine iliyo chini ya Wizara inazozisimamia ili kuona hatua za utekelezaji wake na thamani ya fedha (*Value for Money*).

Maelezo ya kina kuhusu miradi iliyotembelewa yanapatikana sehemu ya Pili ya Taarifa hii**.**

**1.6.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2024/2025.**

**Mheshimiwa Spika,** mwezi Machi, 2024 Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha 2023/ 2024 na kufanya ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 117 (2) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Maoni ya Kamati yaliyotokana na shughuli hii yaliwasilishwa Bungeni tarehe 24 Aprili, 2023 na tarehe10 Mei, 2023.

### 1.6.3 Kushiriki katika Mafunzo na Semina

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wa Kamati walipata fursa ya kushiriki katika Mafunzo na Semina zilizoandaliwa na Ofisi ya Bunge, Wizara na Taasisi zilizo chini ya OMRM na Wizara ya Maji pamoja na Taasisi zisizo za Kiserikali.

**Mheshimiwa Spika,** Mafunzo na Semina hizo zililenga kuongeza uelewa na ujuzi wa Wajumbe wa Kamati katika Nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwakumbusha majukumu na wajibu wa Kibunge katika kuisimamia na kuishauri Serikali.

### 1.6.4 Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa kwa Serikali wakati wa Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza Maazimio ya Bunge ambapo baadhi ya Maazimio yametekelezwa kwa sehemu na utekelezaji wake unaendelea. Hata hivyo, kuna baadhi ya maazimio ambayo hayakutekelezwa.

**(a) Ofisi ya Makamu wa Rais –Mazingira**

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa Azimio lililotekelezwa kwa ukamilifi ni **Pendekezo kwa Serikali kutoa Mafunzo kwa wataalamu wa ndani ili wawe na ujuzi wa kutosha wa kuandaa mapitio ya tathmini ya athari kwa mazingira** ambapo katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Disemba, 2024 jumla ya wataalamu 75 walipatiwa mafunzo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa Azimio ambalo limetekelezwa kwa sehemu na utekelezaji wake unaendelea ni **pendekezo la kufanyia marekebisho Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191, ili iweze kuendana na Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021.**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imewasilisha Muswada wa marekebisho madogo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 ili kutatua baadhi ya changamoto zilizojitokeza wakati wa

utekelezaji wake. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kutekeleza ahadi yake kwa Kamati ya kuwasilisha marekebisho makubwa ya Sheria hiyo haraka iwezekanavyo ili kuendana na Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 na Mipango ya Muda mrefu ya Taifa katika uhifadhi wa mazingira ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025-2050.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa Azimio ambalo halikutekelezwa na OMRM ni **Serikali kuchukua hatua za haraka kufanyia marekebisho Kanuni zote ambazo zimeonekana kukinzana na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura, 191 na iwaruhusu wakufunzi ambao ni washauri elekezi wa Mazingira kufanya Majukumu yao kwa mujibu wa Sheria.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haijaridhishwa na majibu kwamba, kwa kipindi chote cha mwaka mzima, ni rasimu pekee ya marekebisho ya Kanuni hizo ndio imeandaliwa. Ni Rai ya Kamati kwa Serikali kushughulikia suala hilo kwa haraka ili kutatua changamoto zilizojitokeza.

**(b) Wizara ya Maji**

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa Azimio lililotekelezwa kikamilifu chini ya Wizara ya Maji ni **pendekezo kwa Serikali kuchukua hatua madhubuti na za haraka ili kuhakikisha kuwa uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Maji unakamilika.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Maji kwa kupitisha Sera iliyopendekezwa ambapo pamoja na mambo mengine Sera hiyo imeweka mkazo katika upangaji shirikishi, ushiriki wa Sekta Binafsi katika utekelezaji, usimamizi na utoaji huduma za maji, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na usimamizi wa huduma za usafi wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Mfano wa Azimio linaloendelea kutekelezwa na Wizara ya Maji ni pendekezo kwa Serikali la kuainisha maeneo yote ya Umma yenye changamoto ya ukosefu wa maji na kuyatafutia vyanzo vya kujitegemea ili kuhakikisha

yanapata maji ya kutosha na kwa wakati wote. Kamati inaisisitiza Serikali kuendelea na hatua hiyo ili kuimarisha huduma za maji katika maeneo yote ya Umma.

**1.6.5 Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Majukumu ya OMRM na Wizara ya Maji**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia Kifungu cha 6 (6) (a) na (b) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (c) na (d) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025, Kamati ilipokea na kujadili taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya

Wizara inazozisimamia kama ifuatavyo: -

**(a) Ofisi ya Makamu wa Rais –Mazingira**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa OMRM, Kamati ilipokea na kujadili taarifa zifuatazo: -

(i) Tathmini ya athari kwa mazingira iliyotokana na mvua za El Nino kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na namna Ofisi ilivyokabiliana na athari hizo.;

(ii) Utekelezaji wa Maazimio ya Mkutano wa mabadiliko ya tabianchi (COP28) wa 2023;

(iii) Utekelezaji wa zoezi la urejereshaji wa Taka ngumu katika Jiji la Dar es Salaam;

(iv) Utekelezaji wa Mkataba wa Nairobi kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi (Convention for the Protection, Management, and Development of the Marine and Coastal Environment of the Eastern African Region;

(v) Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya Mwaka 2024;

(vi) Udhibiti wa utiririshaji wa Majitaka na taka za viwandani katika Ziwa Victoria;

(vii) Hatua iliyofikiwa katika Uanzishaji wa Mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa Taarifa za taka ngumu na hatarishi katika Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; na

(viii) Hali ya upatikanaji wa fedha na Utekelezaji wa Bajeti ya OMRM kwa Kipindi cha nusu mwaka Julai- Disemba, 2024.

**(b) Wizara ya Maji**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Wizara ya Maji Kamati ilipokea na kujadili taarifa zifuatazo: -

(i) Kiasi cha fedha za Mfuko wa Maji kilichopokelewa kwa miaka mitatu kuanzia 2021/2022 hadi 2023/2024 na Mgawanyo wa Fedha hizo kwa RUWASA, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira na Mabonde ya Maji;

(ii) Hali ya Upatikanaji na Usambazaji wa Maji katika Jiji la Dodoma, Mwanza, Arusha, Dar es salaam na Tanga;

(iii) Hatua zilizochukuliwa kukabiliana na hali ya upotevu wa Maji nchini kwa maeneo yenye upotevu zaidi wa Maji kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(iv) Utekelezaji wa shughuli za Mamlaka za Maji kupitia Hati Fungani;

(v) Utekelezaji wa Mwongozo wa Uvunaji wa Maji ya Mvua nchini;

(vi) Shughuli zilizotekelezwa kwa kutumia Mitambo 25 iliyonunuliwa na Serikali kwa ajili ya kuchimba visima;

(vii) Hatua iliyofikiwa katika usambazaji wa maji ya visima ambavyo vimechimbwa kwa nchi nzima;

(viii) Tathmini ya hasara iliyopatikana kutokana na Upotevu wa Maji na Uhujumu wa miundombinu ya maji kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Disemba 2024;

(ix) Hali ya upatikanaji wa fedha na Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Kipindi cha nusu mwaka Julai- Disemba, 2024; na

(x) Hali ya Upatikanaji wa Maji nchini hadi kufikia mwezi Disemba, 2024.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Pili ya Taarifa inahusu Matokeo ya Uchambuzi wa Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari,2024 hadi Januari,2025. Uchambuzi huo unafafanua shughuli zilizotekelezwa kwa kila Wizara na kubainisha mafanikio na changamoto kama ifuatavyo:-

### 2.2 Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Tangazo la Serikali la Majukumu ya Wizara la mwezi Julai 2021 (*Assignment of Ministerial Responsibilities Government Notice* No. 534 of 2nd July, 2021), majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais –Mazingira ni pamoja na: -

(a) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Mazingira;

(b) Kuratibu na kusimamia mabadiliko ya Tabianchi;

(c) Kuhamasisha uzalishaji unaozingatia hifadhi ya mazingira na uchumi wa kijani;

(d) Kuratibu hifadhi na usimamizi wa mazingira na kusimamia Sheria ya Mazingira Sura 191; na

(e) Kusimamia shughuli za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira inatekeleza majukumu yake ya kimuundo kwa kuzingatia maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (*SDGs* 2030), Ajenda ya Afrika 2063, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020, Mpango Kabambe wa Usimamizi wa Mazingira 2022-2032 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26.

**Mheshimiwa Spika,** kuanzia kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025 kwa upande wa OMRM, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa kwenye maeneo yafuatayo: -

(a) **Tathmini ya athari kwa mazingira iliyotokana na mvua za El Nino kwa mwaka wa fedha 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024 Mvua za El Nino zilinyesha katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Mikoa ya Tanga, Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Mtwara na Lindi katika Ukanda wa Mashariki, Mikoa ya Arusha na Manyara katika Ukanda wa Kaskazini, Mikoa ya Kigoma na Katavi katika Ukanda wa Magharibi, Mikoa ya Rukwa, Mbeya, Njombe na Songwe katika Ukanda wa Nyanda za Juu kusini na Mikoa ya Mwanza, Mara, Simiyu na Geita katika Ukanda wa Ziwa Victoria.

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya athari zilizotokana na Mvua hizo ilionesha Madhara makubwa kwa wananchi katika maeneo mbalimbali ikiwemo maporomoko ya tope kutoka milimani kwa maeneo kama Hanang na Mbeya Mafuriko yaliyosababisha

kuharibika kwa takribani ekari 600 za Mazao katika Wilaya ya Ludewa, Nyumba nyingi kuzingirwa na Maji mfano nyumba 230 zilizingirwa na Maji Mkoani Rukwa na upotevu mkubwa wa Mifugo.

**Mheshimiwa Spika;** kutokea kwa madhara mbalimbali yaliyosababishwa na Mvua za El Nino kwa Mwaka 2023/24 kumeonesha kuwa kuna haja ya Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kuwa na Mkakati Madhubuti utakaosaidia kunusuru wananchi pale watakapokumbwa na maafa yatokanayo na Mvua kubwa.

(b) **Utekelezaji wa Maazimio ya Mkutano wa mabadiliko ya tabianchi (COP28) wa mwaka 2023**

**Mheshimiwa Spika**, Mkutano wa Mataifa Wanachama kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi (COP 28) ulifanyika Dubai, katika Umoja wa Falme za Kiarabu mnamo mwaka 2023 ukiwa na lengo la kuendeleza jitihada mbalimbali za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika,** miongonio mwa Maazimio yaliyofikiwa na Nchi wanachama katika mkutano huo ni pamoja na: –

(i) Kuendelea kusaidia Nchi zinazoendelea katika kuandaa na kutekeleza Mipango ya Taifa ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi; na;

(ii) Nchi wanachama kupunguza ongezeko la gesijoto Duniani.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na OMRM katika jitihada za kuwezesha wananchi kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo, ni Rai ya Kamati kwa Serikali kuendelea kuchukua hatua thabiti zitakazosaidia kuongeza hamasa kwa Wananchi ili waweze kujihusisha kikamilifu katika utekelezaji wa Mipango na Mikakati ya uhifadhi wa mazingira.

(c) **Utekelezaji wa zoezi la urejeleshaji wa Taka ngumu katika Jiji la Dar es Salaam**

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuwa wastani wa tani 4,852 za taka ngumu huzalishwa kwa siku katika Jiji na Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam. Hata hivyo, ukusanyaji wa taka hizo ni wastani wa asilimia 63 ya kiasi cha taka kinachozalishwa ambapo asilimia 6.5 ya taka hizo ndizo hurejelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia umuhimu wa uhifadhi wa Mazingira ya Jiji la Dar es salaam, Serikali imechukua hatua mbalimbali katika kudhibiti kuzagaa kwa taka ngumu. Hatua hizo ni pamoja na: -

(i) Kuandaliwa kwa Mwongozo wa Udhibiti wa taka ngumu kwa kutumia dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza (*3Rs - Reduce, Reuse and Recycle*);

(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau imewezesha kujengwa kwa Kituo cha kuchakata na Uchambuzi wa taka ngumu (*Material Recovery Facility*) kilichopo eneo la Bonyokwa, katika Jiji la Dar es Salaam;

(iii) Kufanya mapitio ya Kanuni za usimamizi na udhibiti wa taka ngumu za Mwaka 2024 ili kuelekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kujenga vituo vya kuchakata taka ngumu kwa lengo la kupunguza kiasi cha taka zinazokwenda dampo;

(iv) Kujengea uwezo Viongozi na Wataalam katika ngazi za Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuboresha Mifumo ya usimamizi wa taka ngumu; na

(v) Kuandaa maandiko ya miradi ya usimamizi wa taka ngumu na kuwasilisha kwa Washirika wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya mikakati hiyo, pamekuwa na changamoto zinazokwamisha juhudi za Serikali za kudhibiti

uzagaaji wa taka ngumu kwa maeneo mengi. Changamoto hizo ni pamoja na;

(i) Uelewa na mwitikio mdogo wa Wananchi kuhusu utenganishaji wa taka katika ngazi ya Kaya;

(ii) Uhaba wa miundombinu stahiki ya udhibiti wa taka ngumu;

(iii) Uzingatiaji hafifu wa Mipango Miji inayopelekea kuwepo kwa ujenzi wa makazi yasiyozingatia Mipango husika; na

(iv) Mwamko hafifu wa matumizi ya mbolea itokanayo; na taka.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua zinazoonesha hali ya mafanikio katika udhibiti wa uzagaaji wa taka ngumu. Ni Rai ya Kamati kwamba Serikali iongeze jitihada zaidi katika kuhakikisha malengo ya kudhibiti taka hizo yanatimizwa kwa weledi na ufanisi unaostahili.

(d) **Utekelezaji wa Mkataba wa Nairobi kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi**

**Mheshimiwa Spika,** Mkataba wa Nairobi kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi (*Convention for the Protection, Management, and Development of the Marine and Coastal Environment of the Eastern African Region*) ulipitishwa mnamo tarehe 21 Juni, 1985. Aidha, Tanzania iliridhia Mkataba huu tarehe 1 Machi, 1996. Tangu hapo pamekuwapo na mabadiliko mbalimbali ya kimkataba yenye mrengo wa kuhakikisha changamoto mbalimbali katika maeneo lengwa zinatatuliwa kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mkataba huu unahusisha Nchi Kumi (10) ambazo ni Komoro, Kenya, Somalia, Madagascar,

Mauritius, Msumbiji, Shelisheli, Re-Union – Ufaransa, Afrika Kusini na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika Mkataba huu, Tanzania imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na: -

(i) Mradi wa kuimarisha Mfumo wa usimamizi unaozingatia uhifadhi wa mazingira na kuboresha maisha ya Jamii za wavuvi katika Wilaya ya Mkinga, Mkoa wa Tanga;

(ii) Mradi wa kutathmini ubora wa maji katika ukanda wa bahari eneo la Zanzibar;

(iii) Mradi kuhusu njia bora za uhifadhi shirikishi na uvunaji endelevu wa rasilimali za misitu ya mikoko katika Delta ya Mto Rufiji;

(iv) Mradi wa Kuimarisha Mbinu na Uwezo wa Kijamii katika Shughuli za Uvuvi kwa Wavuvi wadogo na Usimamizi wa Maeneo ya Hifadhi ya Chaneli ya Pemba Zanzibar;

(v) Mradi wa kuzuia uchafuzi wa mazingira ya bahari unaotokana na taka za plastiki "*Marine Litter Project*";

(vi) Mradi wa usimamizi endelevu wa Mito na kuboresha mitiririko yake katika Bonde la Rufiji; na

(vii) Mradi wa Kukuza Wigo na Uongezaji wa Kiwango cha Ufanisi wa Kusafisha Majitaka eneo la Msingini Chake Chake – Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mkataba huu umekuwa na manufaa mbalimbali kwa Taifa ikiwa ni pamoja na kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Nchi zingine za Ukanda wa Magharibi mwa Bahari ya Hindi katika nyanja ya hifadhi; Kukuza uelewa kwa Jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira ya bahari kupitia miradi na programu inayotekelezwa chini ya Mkataba; na Tanzania kupata nafasi ya kuongoza shughuli za Mkataba kwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati tendaji ya Mkataba wa Nairobi kwa kipindi cha Miaka

Miwili (2) hadi mwaka 2026. Hivyo, kutumia fursa hiyo kushawishi kupata miradi na programu zaidi za kuhifadhi mazingira ya Ukanda wa Pwani na Bahari.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya manufaa yanayopatikana kwa Tanzania kuwa Mwanachama katika Mkataba huu, zimekuwepo changamoto katika utekelezaji wake. Changamoto hizo ni pamoja na: -

(i) Ongezeko la uchafuzi wa mazingira ya bahari unaotokana na shughuli mbalimbali; ikiwemo taka zisizotibiwa, mtiririko wa mabaki yatokanayo na kilimo, uchafuzi unaotokana na taka za plastiki na uchafuzi wa taka za viwandani zinazoelekezwa baharini;

(ii) Ukosefu wa takwimu na ufuatiliaji hali ambayo huzuia usimamizi bora wa Mifumo ya ikolojia ya baharini; na

(iii) Mabadiliko ya tabianchi, ambapo vyanzo mbalimbali vimekuwa vikibainisha kuongezeka kwa mmomonyoko wa ardhi katika maeneo ya Pwani kwa kiwango kikubwa hali inayotishia Mifumo ikolojia.

(e) **Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya Mwaka 2024**

**Mheshimiwa Spika,** Uchumi wa Buluu ni dhana inayochagiza ukuaji wa uchumi kupitia matumizi endelevu ya Rasilimali za Maji kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira na ushirikishwaji wa Jamii. Tanzania imekuwa ikitekeleza shughuli za Uchumi wa Buluu kupitia Sekta mbalimbali zenye mnasaba na Uchumi huo ambazo ni pamoja na: Uvuvi, Maliasili na Utalii, Maji, Nishati, Uchukuzi, Madini, Kilimo, Misitu, Mifugo, Uwekezaji, Viwanda na Biashara, na Uhifadhi wa Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** kwa lengo la kuendelea kuchochea hali ya uzalishaji katika Sekta hizo, OMRM imeandaa Sera ya Uchumi wa Buluu ambayo inatarajiwa kuonesha uelekeo chanya wa

mapinduzi katika Sekta zenye mnasaba na Uchumi huo. Ni kwa muktadha huo, Kamati ililazimika kupata maelezo kuhusu Mkakati wa utekelezaji wa Sera hiyo ili iweze kushauri na kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Sera hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuimarika kwa ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kati ya Serikali na Wadau mbalimbali katika kutekeleza shughuli za uchumi wa buluu nchini, Kuongeza wigo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za uchumi wa buluu nchini na Kuimarisha uratibu wa shughuli za uchumi wa buluu nchini, pamekuwa na uelewa mdogo wa Jamii kuhusu dhana ya uchumi wa buluu na matumizi endelevu ya Rasilimali za uchumi wa buluu.

(f) **Udhibiti wa utiririshaji wa Majitaka na taka za Viwandani katika Ziwa Victoria**

**Mheshimiwa Spika,** Ziwa Victoria ni Ziwa la pili kwa ukubwa duniani kwa maziwa yenye maji baridi likiwa na ukubwa wa Kilomita za **mraba 68, 800** na Mita za ujazo **Kilomita 2,424**. Ziwa hilo linapatikana katika nchi tatu ambazo ni Tanzania (51%) Uganda (44%) na Kenya (5%).

**Mheshimiwa Spika,** Ziwa Victoria ndilo Ziwa kubwa zaidi duniani kwa shughuli za uvuvi wa maji ya baridi, ambapo kwa mwaka shughuli za uvuvi zinakadiriwa kuwa na thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 600. Bonde la Ziwa hilo limewezesha takriban asilimia 70 ya wakazi kujihusisha na shughuli za Kilimo. Aidha, huduma za Mifumo ikolojia ya Ziwa hilo imechangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la idadi ya watu pamoja na ukuaji wa shughuli za kiuchumi ikiwemo Viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwa Ziwa Victoria ni msingi wa kiuchumi kwa takriban watu Milioni 45, limeendelea kuathiriwa na shughuli zisizo endelevu za kibinadamu zikiwemo; uvuvi haramu, uharibifu wa maeneo oevu, kilimo kisichozingatia uhifadhi, uchimbaji madini usiokuwa endelevu pamoja na utiririshwaji wa majitaka kwenda ziwani. Hali hiyo imesababisha

kupungua kwa Rasilimali kama vile Samaki, kuongezeka kwa viumbe vamizi, kuharibika kwa Mifumo ikolojia muhimu ya viumbe hai vya majini, na kupungua kwa ubora wa maji.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya hatua mbalimbali zilizochukuliwa na OMRM, utiririshaji wa Maji taka na taka za viwandani katika ziwa hilo bado unaendelea kwa baadhi ya maeneo, ikiwemo mto Milongo.

(g) **Hatua iliyofikiwa katika Uanzishaji wa Mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa Taarifa za taka ngumu na hatarishi katika Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

**Mheshimiwa Spika,** kwa lengo la kuboresha usimamizi wa taka ngumu na taka hatarishi nchini, OMRM iliandaa Mpango wa kuanzisha Mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa taarifa za taka ngumu na taka hatarishi utakaowezesha kutoa taswira halisi itakayosaidia kufanya maamuzi sahihi kuhusiana na usimamizi wa taka zinazozalishwa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022-2032) umeeleza kuwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingiza litaanzisha Mfumo huo ifikapo mwaka 2025. Aidha, Mfumo huo unatarajiwa pamoja na masuala mengine kuwezesha ukusanyaji wa Taka kwa ufanisi, usimamizi wa Mikataba, uainishaji wa maeneo yanayohudumiwa, utunzaji wa takwimu za madampo na uchambuzi na utoaji wa takwimu.

**Mheshimiwa Spika**, Mfumo huu unaandaliwa chini ya mradi wa **"Kuimarisha Uwezo wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira"** unaotekelezwa na OMRM. Hadi sasa maandalizi ya Mfumo huo yamefikia asilimia sitini (60) na unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha ujao.

Kamati inaipongeza NEMC kwa kuanza utekelezaji wa maandalizi ya Mfumo huo ambao unatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika kuboresha huduma za usimamizi wa taka ngumu na taka hatarishi nchini. Aidha, Mfumo utaiwezesha

Serikali kupata taarifa sahihi za hali ya mazingira, changamoto zilizopo na jitihada za Serikali pamoja na wadau katika kuboresha Mfumo na hivyo kulinda mazingira na afya ya jamii.

(h) **Hali ya upatikanaji wa fedha na Utekelezaji wa Bajeti ya OMRM kwa Kipindi cha nusu mwaka Julai- Disemba, 2024.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 9,670,266,000.00** ikiwa ni Fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, jumla ya **Shilingi 21,207,841,000** iliidhinishwa kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,902,000,000** ni fedha za ndani, na **Shilingi 18,305,841,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Disemba, 2024 jumla ya **Shilingi 4,404,367,232.2** sawa na **asilimia 45.6** ya kiasi kilichotengwa, kilitolewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, hadi kufikia Disemba, 2024 Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira ilipokea **Shilingi 9,308,000,000.80** sawa na **asilimia 43.9** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, ulinganisho unaonesha kuwa **asilimia 10.1** ni fedha za ndani na **asilimia 49.2** ni Fedha za nje.

**2.3 Wizara ya Maji**

**Mheshimiwa Spika,** Hati idhini ya Wizara ya Maji inabainisha majukumu ya Wizara ya Maji kuwa ni pamoja na; Kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa Sera, Mikakati na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji; Kutayarisha na kusimamia Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Sekta ya Maji; Kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji; Kutoa miongozo ya kusimamia matumizi endelevu ya Rasilimali za maji na utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira Vijijini na Mijini; Kuendeleza tafiti kuhusu teknolojia bora zinazotumika katika kutoa huduma ya maji; na Kutekeleza ushauri wa Bodi ya Taifa ya Maji.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji inatekeleza majukumu yake ya kimuundo kwa kuzingatia maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali, sambamba na Mipango mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa kama ilivyoainishwa kwenye Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (*SDGs* 2030); Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020 - 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 inaelekeza kuwapatia Wananchi waishio Vijijini majisafi na salama katika umbali usiozidi **mita 400** kutoka kwenye makazi yao. Ili kufikia azma hiyo, Serikali imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa Wananchi waishio Vijijini kwa kujenga na kukarabati miradi ya maji kwa lengo la kufikia **asilimia 85** ya Wananchi wanaopata huduma ya maji safi na salama katika maeneo hayo na **asilimia 95** kwa Wananchi waishio Mijini ifikapo 2025.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia maelezo hayo, wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati, kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2024 hadi Januari, 2025 kwa upande wa Wizara ya Maji, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa kwenye maeneo yafuatayo: -

**(a) Kiasi cha fedha za Mfuko wa Maji kilichopokelewa kwa miaka mitatu kuanzia 2021/2022 hadi 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Taifa wa Maji unatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019. Lengo la kuanzishwa kwa Mfuko huu ni kuwa na Rasilimali fedha ya uhakika kwa ajili ya kusaidia kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji itakayoboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji nchini pamoja na kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa vyanzo vya maji.

**Mheshimiwa Spika,** vyanzo vya mapato katika Mfuko huu ni fedha zilizoidhinishwa na Bunge, Fedha zinazoweza kupokelewa kutokana na Michango, Ruzuku na Wasia (*bequests)* kutoka

katika chanzo chochote na Vyanzo vingine vya fedha baada ya mashauriano kati ya Waziri wa Maji na Waziri mwenye dhamana ya Fedha na Fedha nyinginezo zinazoweza kulipwa kwa Mfuko kwa mujibu wa Sheria yoyote nchini. Hadi sasa chanzo Kikuu cha fedha za Mfuko huu ni Tozo zinazotokana na mafuta ya petroli na dizeli.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya kuwa na chanzo cha uhakika cha fedha kutokana na Tozo ya Shilingi Hamsini (50) kwa kila Lita ya mafuta ya petroli na dizeli, utoaji wa fedha hizo kwa Mfuko wa Taifa wa Maji kwa kipindi cha Mwaka 2021/2022 hadi 2023/2024 bado hauridhishi. Mathalani kwa kipindi tajwa jumla ya **Shilingi 516,612,559,355.54** zilikusanywa na Serikali, hata hivyo kiasi kilichotolewa kwa ajili ya Mfuko wa Maji ni **Shilingi 467,080,540,583.61** sawa na **asilimia 90** ya fedha iliyokusanywa.

**(b) Hali ya Upatikanaji na Usambazaji wa Maji katika Jiji la Dodoma, Mwanza, Arusha, Dar es salaam na Tanga**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Mamlaka za Maji katika Majiji mbalimbali ikiwemo Dar es salaam, Dodoma, Mwanza, Arusha na Tanga imeendeleza jitihada za kuhakikisha Wananchi katika maeneo hayo wanapata majisafi na salama kwa matumizi ya kila siku. Kwa muktadha huo, hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa ili kuhakikisha uzalishaji na usambazaji wa maji katika Mamlaka hizo unaongezeka.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa jitihada zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na ujenzi wa Mabwawa, kuongeza maunganisho ya maji ili kuwafikia Wananchi wengi zaidi na kuanzishwa kwa Kituo cha Huduma kwa Mteja (*Call Center*) kwa simu bila malipo.

**Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyopatikana kutokana na jitihada za Serikali katika uendeshaji wa Mamlaka za Maji katika Majiji tajwa ni pamoja na: -

(i) Jiji la Dodoma, Serikali imefanikiwa kufanya yafuatayo: -

- Kuongeza mtandao wa mindombinu ya maji kutoka Kilomita **850** hadi Kilomita **1,580**;

- Kuongeza uzalishaji wa maji kutoka lita **Milioni 66** kwa siku mpaka lita **Milioni 79** kwa siku;

- Kuongeza maunganisho ya majisafi kutoka **56,266** mpaka **84,794**;

- Kuboresha huduma ya upatinakaji wa majisafi kwa masaa 24 kwa maeneo ya Nzuguni, Ilazo na baadhi ya maeneo ya Swaswa kupitia mradi wa Nzuguni na;

- Kuongezeka kwa huduma ya maji (*service coverage*) katika Jiji la Dodoma kutoka **asilimia 86** mpaka **asilimia 91.**

(ii) Jiji la Arusha, pamoja na mambo mengine Serikali imefanikiwa kufanya yafuatayo: -

- Kuongeza Uwezo wa uzalishaji maji kutoka wastani wa Lita **40,000,000** kwa siku hadi **200,000,000** kutokana na kukamilika kwa visima vilivyochimbwa kwenye mradi mkubwa katika maeneo ya Seedfarm, Valeska - Mbuguni na Majimoto;

- Kujenga mabwawa 18 Terrati ya kutibu majitaka;

- Kuongeza Idadi ya wateja waliounganishiwa huduma ya maji kutoka **80,037** mwaka 2021 hadi **127,087** mwezi Julai 2024; na

- Kuongeza ufanisi wa makusanyo kwa mwezi kutoka wastani wa **Shilingi Bilioni 1.8** mwaka 2021 hadi **Shilingi Bilioni 2.4** mwaka 2024.

(iii) Jiji la Mbeya, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: -

➢ Uboreshaji wa huduma ya maji katika Miji ya Tukuyu, Chunya, Rujewa na Kyela kwa kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji na kusimamia utendaji wa Mamlaka za Miji hiyo na;

➢ Usanifu na utekelezaji wa Mradi wa Kimkakati wa Kiwira pamoja na Miradi ya maji ya Mto Halinji na Mto Simba itakayozalisha Lita **Milioni 73** kwa siku.

(iv) Jiji la Mwanza, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:-

➢ Kuongeza uzalishaji wa maji kutoka Lita **Milioni 90** kwa siku mpaka Lita **Milioni 138** kwa siku;

➢ Kuongeza maunganisho ya Wateja wa majisafi kutoka **114,294** hadi **121,887** Julai, 2024; na

➢ Kuboresha huduma ya upatinakaji wa majisafi kwa masaa 24 kwa baadhi ya maeneo yaliyokuwa yakipata maji mara moja kwa wiki ikiwemo Kishiri, Sahwa ya chini, Igoma, Nyamhongolo, Bujora, Kisesa, Igudija, Luchelele na Buswelu.

(v) Jiji la Tanga, mafanikio yaliyopatikana ni Pamoja na: -

➢ Kuongeza uwezo wa uzalishaji wa Mtambo wa kutibu maji wa Mowe kutoka Lita **Milioni 30** hadi Lita **Milioni 45** kwa siku;

➢ Kusanifu mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na uondoshaji majitaka kwa ufadhili wa kuuza Hati Fungani ya **Shilingi Bilioni 53.12** iliyouzwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam na

➢ Kuongeza Vijiji vitatu (3) katika Mradi wa Utunzaji na Ulinzi wa Vyanzo vya Maji katika Vijiji vinavyozunguka Mto Zigi.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya mafaniko yaliyopatikana kwa Mamlaka mbalimbali za Majiji, Kamati ilibaini changamoto mbalimbali zinazozikabili Mamlaka hizi zikiwemo: -

i. Mipango Miji kutozingatia miundombinu ya majisafi na majitaka;

ii. Gharama kubwa za umeme katika uendeshaji wa shughuli za Mamlaka za Maji;

iii. Uhujumu wa Miundombinu ya Majisafi na Majitaka na;

iv. Upotevu wa Maji kutokana na Mivujo, Uchakavu wa Miundombinu na Ubovu wa Dira za Maji.

**(c) Hatua zilizochukuliwa kukabiliana na hali ya upotevu wa Maji nchini kwa maeneo yenye upotevu zaidi wa Maji kwa mwaka wa fedha 2023/2024;**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa viwango vya Kitaifa na Kimataifa, kiwango cha juu cha upotevu wa maji kinachoruhusiwa kinatakiwa kisizidi **asilimia 20** ya maji yote yanayozalishwa. Kiasi kidogo cha upotevu wa maji kinaruhusiwa kwa kuwa katika skimu za maji kuna maji yanayopotea bila kulipiwa ikiwemo maji yanayotumika kwenye shughuli za uendeshaji wa skimu hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kiwango cha upotevu wa maji kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini kimepungua kutoka **asilimia 36.2** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 hadi **asilimia 33.43** kwa mwezi Disemba 2024.

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Disemba, 2024, hali ya upotevu wa maji katika Mamlaka za maji **Nzega, Maganzo, Busega, Biharamulo, Shinyanga, Mwanhuzi, Kahama, MANAWASA, Kishapu, KASHWASA, Mbinga, Ruangwa, Namtumbo, Gairo, Igunga, Chunya, Iringa, Babati** na **Songea** umepungua hadi kufikia chini ya wastani wa **asilimia 20.** Hata hivyo, Mamlaka za maji nyingine zina upotevu wa maji juu ya viwango vinavyokubalika Kitaifa na Kimataifa. Miongoni mwa visababishi vya upotevu huo ni pamoja na uchakavu wa Miundombinu, uunganishaji haramu au wizi wa maji, usomaji wa

Dira za maji usio sahihi na uharibifu wa miundombinu ya maji unaotokana na shughuli za ujenzi wa miundombinu mingine mfano; ujenzi wa barabara, usambazaji wa njia za mawasiliano na usimikaji wa nguzo za umeme.

**Mheshimiwa Spika,** upotevu wa maji nchini umekuwa na athari mbalimbali kama vile upotevu wa mapato na upungufu wa maji kwenye maeneo ya huduma kwa matumizi mbalimbali majumbani na shughuli za uzalishaji. Licha ya mikakati mbalimbali inayoendelea kuchukuliwa ili kudhibiti changamoto hizo, Suala la upotevu wa maji nchini linahitaji kupewa kipaumbele ili kuwezesha upatikanaji wa majisafi na salama kwa Wananchi wengi zaidi.

**(d) Utekelezaji wa shughuli za Mamlaka za Maji kupitia Hati Fungani**

**Mheshimiwa Spika,** ili kuhakikisha fedha zinapatikana kwa wingi na kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maji nchini, Serikali imeanza utaratibu wa Hati Fungani kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Tanga (Tanga UWASA).

**Mheshimiwa Spika,** Hati Fungani hiyo imeuzwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam na imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni 54.72** ikiwa ni **asilimia 3** zaidi ya mahitaji ya fedha za kutekeleza miradi ambazo ni **Shilingi Bilioni 53.12**. Fedha zilizopatikana zinatarajiwa kutekeleza Mradi wa Kuboresha Miundombinu ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika maeneo ya huduma ya Jiji la Tanga, Miji ya Muheza na Pangani na baadhi ya Kata Saba za Wilaya ya Mkinga ikiwemo Miji ya Kasera, Horohoro na Maramba.

**Mheshimiwa Spika**, marejesho ya fedha za Wawekezaji yanatarajiwa kufanywa kwa utaratibu wa mkupuo mmoja baada ya miaka kumi (10) ya umri wa Hati Fungani kuisha. Hata hivyo, wawekezaji hao watalipwa riba katika utaratibu wa ‘‘*Coupon Payment*’’ kwa awamu mbili kila mwaka. Kamati inaipongeza

Serikali kwa hatua hiyo ambayo ni hatua ya mapinduzi kwa Sekta ya Maji nchini.

**(e) Utekelezaji wa Mwongozo wa Uvunaji wa Maji ya Mvua nchini Mheshimiwa Spika,** athari za mabadiliko ya tabianchi zimekuwa zikisababisha hali ya Ukame na Mafuriko ya mara kwa mara kwa maeneo mengi duniani ikiwemo nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 inatambua uvunaji wa maji kama hatua mojawapo itakayosaidia kuhakikisha uendelevu katika jitihada za kuongeza upatikanaji wa maji kwa mahitaji ya Kijamii, Kiuchumi na Mazingira na vile vile kuzuia mafuriko ya maji ambayo yamekuwa yakitokea maeneo mengi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kuwezesha utekelezaji wa zoezi la uvunaji wa maji ya mvua kwa kuzingatia teknolojia zilizopo, Wizara ya Maji iliandaa Mwongozo wa Uvunaji wa Maji ya Mvua (*Guideline for Rainwater Harvesting in Tanzania*) wa mwaka 2020. Mwongozo huo umeelekeza uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia mapaa ya nyumba (majumbani na kwenye majengo ya Taasisi pamoja na ujenzi wa malambo na mabwawa (*ground catchment*).

**Mheshimiwa Spika,** katika mwongozo huo Serikali imeelekeza:

a) Kila Wilaya kujenga Bwawa moja kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua;

b) TAMISEMI na RUWASA kuhamasisha uvunaji wa maji ya mvua kwenye mapaa katika Taasisi na maeneo wanayosimamia;

c) Kuzihamasisha Taasisi za Kijamii, Asasi na Watu Binafsi kujenga miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua kwenye majengo yao; na

d) Kupitia Bodi za Maji za Mabonde imeendelea kutoa elimu ya uvunaji wa maji ya mvua kupitia Jumuiya za Watumia Maji na majukwaa ya Wadau.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati kupitia taarifa ya Wizara ya Maji ilibaini uwepo wa msukumo mdogo katika utekelezaji wa Mwongozo huo hali ambayo imesababisha utayari mdogo wa Jamii kushiriki kuvuna maji ya mvua, uratibu hafifu katika ujenzi wa mabwawa ya maji na upatikanaji mdogo wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa.

**(f) Shughuli zilizotekelezwa kwa kutumia Mitambo 25 iliyonunuliwa na Serikali kwa ajili ya kuchimba Visima;**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji kupitia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 ilipokea **Shilingi Bilioni 139.4** ambapo sehemu ya fedha hizo kiasi cha **Shilingi Bilioni 34.92** zilitumika kununua **Seti 25** za mitambo ya uchimbaji wa Visima, **Seti tano (5)** za mitambo ya ujenzi wa mabwawa pamoja na **Seti mbili (2)** kwa ajili ya upimaji wa wingi wa maji (*pumping test unit*) kwa Visima vinavyochimbwa.

**Mheshimiwa Spika,** kununuliwa kwa mitambo hiyo kulilenga kuongeza kasi ya upatikanaji wa vyanzo vipya vya maji hususan kwenye maeneo yenye uhaba wa vyanzo vya maji juu ya ardhi; na kuhakikisha Vijiji visivyo na huduma ya maji vinapata huduma hiyo kwa haraka zaidi na kufikia zaidi ya **asilimia 85** ifikapo mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika,** hadi sasa matumizi ya Mitambo hiyo imeleta manufaa makubwa ikiwemo: -

(i) Kuongezeka kwa kasi ya upatikanaji wa vyanzo vya maji vya uhakika. Mathalani, kupitia mitambo hiyo jumla ya visima **882** vimechimbwa; na

(ii) Kuzalisha ajira rasmi **245** na zisizo rasmi takribani **150.**

Aidha, kutokana na changamoto zilizojitokeza wakati wa awali wa uendeshaji wa mitambo hiyo, Wizara ya Maji imeandaa Mwongozo Maalumu kwa ajili ya kutekeleza shughuli za uchimbaji Visima kwa ufanisi. Mwongozo huo, pamoja na mambo mengine umeelekeza uzingatiwaji wa matengenezo ili kuhakikisha uendelevu wa mitambo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza hilo, Mwongozo unaelekeza kuzuia (*ring fence*) **asilimia 10** ya fedha za mradi wa uchimbaji wa kisima ili kugharimia matengenezo madogo madogo (**service)** ya mitambo pamoja na ununuzi wa vifaa wezeshi (**consumables**).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara ya Maji kwa kuchua hatua ya kuandaa mwongozo unaoonesha dhamira ya dhati ya Serikali katika matumizi ya Mitambo hiyo kwa lengo la kuhakikisha Wananchi wake katika maeneo yote nchini wanapata majisafi na salama wakati wote. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua zitakazosaidia kuondoa dosari ya kukosekana kwa maji kwa baadhi ya visima vinavyoendelea kuchimbwa.

(g) **Taarifa ya hali ya upatikanaji wa Maji Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** lengo la Serikali kupitia Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2020-2025, Ukurasa wa 149 ni kuhakikisha kuwa huduma ya majisafi na salama inaendelea kuimarishwa na kuwafikia zaidi ya **asilimia 85** ya wakazi wa Vijijini na zaidi ya **asilimia 95** kwa Mijini ifikapo mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba, Wizara ya Maji imeendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji katika maeneo ya Mijini na Vijijini ili kufikia Malengo yaliyotarajiwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2020 hadi 2025.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Disemba 2024, kiwango cha uzalishaji wa maji nchini kwa maeneo ya Mijini kimeongezeka na

kufikia Mita za ujazo **457,162,193.80,** sawa na ongezeko la **asilimia 18.9** ikilinganishwa na Mita za ujazo **384,488,320.40** kwa kipindi cha mwezi Disemba 2023. Aidha, hatua hiyo imesababisha ongezeko la maunganisho ya wateja kutoka wateja **1,589,492** Disemba 2023 hadi wateja **1,625,669** kwa mwezi Disemba 2024 sawa na ongezeko la **asilimia 2.3**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa huduma ya maji kwa maeneo ya Vijijini, **Vijiji 10,532** kati ya **Vijiji 12,318** sawa na **asilimia 86** vimefikiwa na huduma hiyo. Ongezeko hili limechangiwa na kukamilika kwa miradi ya maji **218** ambayo inahudumia wakazi wapatao **1,426,940** katika maeneo ya Vijijini. Aidha, hadi kufika mwezi Disemba, 2024, hali ya uzalishaji wa maji kwa maeneo ya Vijijini umeongezeka kufikia Mita za ujazo **7,982,179,977.60,** sawa na ongezeko la **asilimia 7.9** ikilinganishwa na Mita za ujazo **7,395,224,412.00** kwa mwezi Disemba 2023.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla, Wizara ya Maji imefanikiwa: -

(i) Kukamilisha utekelezaji wa miradi **286** ikiwa miradi **68** ni ya Mijini na miradi **218** ni ya Vijijini;

(ii) Kuongeza uzalishaji wa maji kutoka Mita za ujazo **7,779,712,732.4** Disemba 2023 mpaka mita za ujazo **8,439,342,171.4** Disemba 2024 kwa maeneo ya Mijini na Vijijini;

(iii) Kuongeza hali ya upatikanaji wa majisafi na salama Vijijini kutoka **asilimia 79.6** Disemba 2023 hadi **asilimia 83** Disemba 2024 na kutoka **asilimia 90** Disemba 2023 hadi **asilimia 91.6** Disemba 2024 kwa Mijini.

(iv) Kupatikana kwa **Dola za Marekani Milioni 125** kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Farkwa ambapo utekelezaji wake umeanza kwa hatua za awali;

(v) Kuanza kwa utekelezaji wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda kwa kutumia fedha za ndani, ambapo utekelezaji wake umefikia **asilimia 27;** na

(vi) Kukamilika kwa ujenzi wa Mabwawa ya Manda, Mtamba, Paranga, Karema Kuu, Kambi ya Nyasa, Haneti, Masaka, Itamboleo, Zebeya na Muko.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilibaini uwepo wa changamoto zifuatazo katika utekelezaji wa shughuli za Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Upatikanaji wa Huduma za Maji nchini: -

(i) Mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya uwekezaji katika miradi mikubwa ya maji;

(ii) Kutosambazwa kwa maji kwa miradi iliyokamilika na kutokamilika kwa utekelezaji wa miradi mingi ya maji;

(iii) Ongezeko kubwa la shughuli za binadamu zinazosababisha uharibifu wa vyanzo vya maji;

(iv) Mabadiliko ya tabianchi yanasababisha vipindi virefu vya ukame na mafuriko;

(v) Madeni makubwa ambayo Mamlaka zinadai baadhi ya Taasisi za Umma;

(vi) Gharama kubwa za uzalishaji na uendeshaji na Upotevu wa Maji yasiyolipiwa (NRW); na

(vii) Uharibifu wa miundombinu ya maji na vyanzo vya maji;

**(h). Ziara za kutembelea miradi mbalimbali**

**Mheshimiwa Spika,** ikumbukwe kwamba, Kamati iliwasilisha Taarifa ya hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sambamba na bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 mbele ya Bunge lako Tukufu katika Mkutano wa **Kumi na Tano (15)** wa Bunge. Hata hivyo, kwa kipindi cha kuanzia Aprili hadi Januari, 2025, Kamati ilipata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali ili kujiridhisha na hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuwahudumia Wananchi.

**(i) Ziara katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Januari hadi Aprili, 2024 Wilaya ya Rufuji ilikabiliwa na mafuriko yaliyotokana na Mvua za El Nino. Mafuriko hayo yalisababisha athari mbalimbali ikiwemo; upotevu wa mali na mifugo, nyumba kubomoka, kuathirika kwa huduma za Zahanati na Shule, na kuharibika kwa miundombinu mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea maeneo mbalimbali ya Kata ya Muhoro ili kushuhudia athari za mafuriko hayo na kujiridhisha na hatua mbalimbali zilichochukuliwa na **OMRM** kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za Serikali na Binafsi katika kuhakikisha tathmini za athari kwa Mazingira zinafanyika kwa maeneo hayo na kutoa ushauri wa kitaalamu utakaosaidia kunusuru Wananchi kwa kipindi kijacho.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali na Wadau mbalimbali kwa kuchukua hatua za kusaidia waathirika wa Mvua hizo kwa kuwapatia makazi ya muda, vyakula na huduma nyingine muhimu. Vilevile, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa maeneo maalamu ya kuwahamishia wote waliothirika na Mafuriko. **Aidha, Kamati inasisitiza na kuhimiza Serikali kuzingatia uwepo wa Madampo katika maeneo hayo ili kulinda mazingira na afya za wakazi hao.**

**(ii) Mradi wa Maji taka katika Jiji la Dar es salaam.**

**Mheshimiwa Spika**, DAWASA inafanya kazi kwa Sheria ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira, Na.5 ya mwaka 2019. Hadi sasa idadi ya watu katika eneo la huduma la DAWASA inakadiriwa kuwa watu **Milioni 6.8**.

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 14 Septemba, 2024 Kamati ilitembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa Mitambo midogo 8 ya kuchakata majitaka katika eneo la Kigamboni na mradi wa majitaka katika eneo la Mbezi Beach Jijini Dar es Salaam ili

kujiridhisha na hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Mamlaka hiyo katika kudhibiti utiririshaji hovyo wa majitaka katika Jiji la Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Majitaka Mbezi Beach unahusisha maeneo ya Mbezi Beach, Mbezi Juu, Mbezi chini, Kilongawima na Salasala ambapo bomba lenye urefu wa **Kilomita 101** litalazwa. Ujenzi wa mradi huu utagharimu **Shilingi Bilioni 132.2** ambapo hadi kipindi cha ziara utekelezaji wa mradi ulifikia **asilimia 57.25**.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Kigamboni unaotekelezwa katika maeneo ya Vijibweni, Gezaulole, Kimbiji, Zingiziwa, Kisopwa, Mabwepande, Vikunai na Mtoni. Mradi huu umegharimu **Shilingi Bilioni 16.67** na unatarajiwa **kukamilika Mwezi Septemba 2025.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara ya Maji kupitia DAWASA kwa kusimamia ipasavyo utekelezaji wa mradi huo ambao kwa kiasi kikubwa utasaidia kuhifadhi mazingira na kuongeza usalama kwa afya za Wananchi.

**(iii) Ujenzi wa Miradi ya Maji kurejesha huduma katika Vijiji vilivyopata athari ya Maporomoko ya Mlima Hanang'**

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 03/12/2023, Wilaya ya Hanang' ilikumbwa na maporomoko ya tope ambayo yalisababisha uharibifu wa miundombinu ikiwemo miundombinu ya maji.

**Mheshimiwa Spika,** Miradi ya maji katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Hanang' inatekelezwa na Wakandarasi wa ndani hatua ambayo inaashiria dhamira ya Serikali kukuza Uchumi wa Wananchi wake.

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa miradi inayotekelezwa katika maeneo hayo ni pamoja na: -

(i) Mradi wa Usambazaji maji kwa makazi mapya ya Waret ulioanza mwezi Februari 2024 ikiwa ni upanuzi wa mradi wa maji wa Mogitu – Gehandu. Upanuzi wa mradi huu ulitekelezwa kwa kutumia Wataalam wa ndani (*force account*) kwa gharama ya **Shilingi 157,665,665.09**. Kazi zilizotekelezwa katika Mradi huu zinajumuisha ununuzi, uchimbaji na ulazaji wa bomba lenye urefu wa Kilomita **12.6** na ufungaji wa **vituo 109** vya kuchotea maji katika eneo la makazi mapya; na

(ii) Mradi wa Kurejesha huduma ya maji katika Vijiji Vitano (5) vya Gabadaw, Kinyamburi, Sarjanda, Nangwa na Basodagwargwe ulioanza kutekelezwa **tarehe 01 Oktoba 2024**. Mradi huu utagharimu kiasi cha **Shilingi 1,874,640,516.31** na unatarajiwa kukamilika tarehe **01 Oktoba, 2025.**

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua za haraka na muhimu ili kurejesha huduma ya miundombinu ya maji iliyoathirika katika maeneo yote. **(iii) Hali ya upatikanaji wa fedha na Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Kipindi cha nusu mwaka Julai hadi Disemba, 2024.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Maji iliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 627,778,217,840.00** kati ya fedha hizo, **Shilingi 69,662,838,840.00** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 558,115,379,000.00** ni fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha, kati ya fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo **Shilingi 340,463,656,000.00** ni fedha za ndani kupitia Mfuko wa Serikali na Mfuko wa Taifa wa Maji na **Shilingi 217,651,723,000.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Disemba, 2024, Wizara ya Maji ilipokea jumla ya **Shilingi 312,376,164,259.49** sawa na asilimia **49.76** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha zilizopokelewa **Shilingi 28,196,146,978.00** ni za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 284,180,017,281.49** ni fedha za Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** katika fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, hadi kufika Mwezi Disemba, 2024, Wizara ya Maji

ilipokea **Shilingi 182,877,595,953.38** sawa na **asilimia 53.7** ya bajeti iliyoidhinishwa kwa fedha za ndani na S**hilingi 101,302,421,328.11** sawa na **asilimia 46.4** ya fedha zilizoidhinishwa kutoka nje.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kamati imeridhishwa na mtiririko wa Fedha za maendeleo kwa Wizara ya Maji na hivyo, inapongeza jitihada za Serikali katika utoaji wa fedha hizo hususan katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

### 3.1 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** yafuatayo ni maoni ya Kamati kufuatia shughuli zilizotekelezwa katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025 ambayo yanaakisi kilichojadiliwa na Kamati wakati ikitekeleza majukumu yake. Maoni hayo ni kama yafuatayo**: -**

#### 3.1.1 Maoni ya jumla

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni ya jumla yafuatayo: -

(a) Bajeti inayotengwa kwa ajili ya Wizara ya Maji na OMRM ni finyu ikilinganishwa na mahitaji makubwa ya fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

(b) Usimamizi wa Sheria, Kanuni na Miongozo hauridhishi;

(c) Watumishi katika Wizara ya Maji na OMRM ni pungufu ikilinganishwa na mahitaji halisi;

(d) Elimu inayotolewa kwa Umma juu ya uhifadhi wa Mazingira haiwafikii walengwa wote;

(e) Hakuna programu za kutosha za utafiti na mafunzo ya Umahiri kwa Watalaam;

(f) Utekelezaji wa Mwongozo wa kuratibu Sekta za Kiserikali zinazohusika katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira hauridhishi; na

(g) Utekelzaji wa Sera ya kuwawezesha Wakandarasi wa ndani hauridhishi.

**3.1.2 Maoni mahsusi ya kila Sekta**

**a) Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira**

(i) Kamati inatambua hatua ya Serikali kupitia OMRM ya kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Marekebisho madogo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa mwaka 2024;

(ii) Kuathirika kwa shughuli nyingi za Kiuchumi na Kijamii kutokana na Mabadiliko ya Tabianchi kunasababisha kukwama kwa shughuli nyingi za Serikali;

(iii) Uzagaaji wa takangumu nchini ni matokeo ya Uzalishaji mkubwa wa takangumu ikilinganishwa na uwezo wa kukusanywa na kurejeleza taka hizo;

(iv) Utekelezaji wa Mkataba wa Nairobi kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi unachochea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na Kukuza uelewa kwa Jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira;

(v) Utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2024 una lengo la kuchagiza ukuaji wa uchumi kupitia matumizi endelevu ya Rasilimali za maji kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira na ushirikishwaji wa Jamii. Hata hivyo Sera haijatungiwa Sheria yake;

(vi) Utiririshaji wa majitaka katika Ziwa Victoria unasababisha athari mbalimbali ikiwemo kupungua kwa rasilimali kama

vile samaki, kuongezeka kwa viumbe vamizi, kuharibika kwa Mifumo ikolojia muhimu ya viumbe hai vya majini, na kupungua kwa ubora wa maji;

(vii) Utolewaji usioridhisha wa fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendelea unaathiri utekelezaji wa miradi iliyopangwa; na

(viii) Usimamizi hafifu wa zuio la matumizi ya mifuko ya plastic.

**b) Wizara ya Maji**

(i) Hatua ya Serikali kupitia Wizara ya Maji kukamilisha maboresho ya Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 ni ya kupongezwa;

(ii) Kutotolewa kwa ukamilifu na kwa wakati fedha za Mfuko wa Taifa wa Maji zinazotokana na Tozo ya Mafuta ya dizeli na petroli ni ukiukwaji wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria ya Fedha Na. 16 ya Mwaka 2015;

(iii) Kiwango kikubwa cha upotevu wa maji nchini kinasababisha upotevu wa mapato ya Serikali na Upungufu wa maji kwa matumizi ya nyumbani na shughuli za uzalishaji;

(iv) Uwekezaji wa ndani kupitia Hati Fungani umekuwa ni chanzo cha uhakika cha upatikanaji wa fedha katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo;

(v) Msukumo mdogo katika utekelezaji wa mwongozo wa uvunaji wa Maji ya Mvua umesababisha Jamii kutoshiriki katika uvunaji maji, uratibu hafifu katika ujenzi wa mabwawa ya maji na upatikanaji mdogo wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa;

(vi) Gharama za uzalishaji wa maji zimekuwa zikiongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo; kodi

ya ongezeko la thamani (VAT), gharama za umeme, vipuri na mabomba pamoja na madawa ya kusafisha maji, na

(vii) Kukosekana kwa maji kwenye baadhi ya visima vinavyoendelea kuchimbwa licha ya kutumia rasilimali nyingi katika uchimbaji huo kunaiingizia Serikali hasara na Wananchi kukosa maji.

**3.2 Ushauri na Mapendekezo ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii imebainisha matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025 kwa kuonesha mafanikio na changamoto zinazohitaji kupatiwa ufumbuzi kwa kuzingatia muundo wa hoja zinazowasilishwa Bungeni ulioelezwa katika Kanuni ya 61 (3) ya Kanuni za Bunge. Naomba kutoa ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa namna itakayowezesha Bunge kuazimia kama ifuatavyo: -

**3.2.1 Mapendekezo kwa Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira**

**1. Tafiti za kimazingira na mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi**

**"KWA KUWA,** majanga mbalimbali ya kimazingira kama maporomoko ya ardhi, ukame na mafuriko yamesababisha madhara makubwa ikiwemo vifo, uharibifu wa miundombinu, upotevu wa mifugo kwa maeneo mengi ikiwemo Hanang, Kibiti na Rufiji;

**NA KWA KUWA,** kutokea kwa majanga hayo kumeathiri shughuli nyingi za Kiuchumi na Kijamii kwa Wananchi na Serikali;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba"

a) Itungwe Sheria, Kanuni na Miongozo ya uanzishaji wa Mfuko wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi utakaogharamia

utekelezaji wa Mipango na Mikakati ya usimamizi wa mazingira na mabadilikoya tabianchi nchini.

b) Serikali isimamie ipasavyo mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi kwa kuchukua hatua Madhubuti katika utekelezaji wa Maazimio ya Kimataifa (COP) yanayolenga kuinua Uchumi wa Wananchi na kuhifadhi Mazingira kwa: -

(i) Kuandaa Mwongozo wa kuwaongezea uwezo wa kiutendaji watendaji wote wa Sekta ya Mazingira kwa kuwapa fursa sawa za kushiriki katika majukwaa mbalimbali ya kimazingira ikiwa ni pamoja na Mikutano ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

(ii) Kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia hususan kwa maeneo ya Vijijini ili kupunguza ukataji hovyo wa misitu. Aidha, hamasa katika Biashara ya Kaboni na manufaa yatakayopatikana iwe chachu katika kuhakikisha Wananchi wa maeneo hayo wanapata nishati safi kwa gharama nafuu zaidi;

(iii) Kuandaa na kusimamia Mwongozo utakaowawezesha wakulima wa tumbaku katika maeneo mbalimbali ya nchi kunufaika na Kilimo hicho pasipo kuathiri misitu iliyo pembezoni; na

(iv) Kuandaa na kutekeleza program za utafiti, ubunifu na mafunzo ili Taifa liwe na uwezo mkubwa zaidi wa kukabiliana na athari za mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

**2. Udhibiti wa taka ngumu**

**‘‘KWA KUWA,** wastani wa takangumu zinazozalishwa nchini ni nyingi zaidi ya zinazokusanywa na kurejelezwa;

**NA KWA KUWA,** pamekuwa na:-

a) Uelewa na mwitikio mdogo wa Wananchi kuhusu utenganishaji wa taka katika ngazi ya Kaya;

b) Uhaba wa miundombinu stahiki ya udhibiti wa taka ngumu;

c) Uzingatiaji hafifu wa Mipango Miji inayopelekea kuwepo kwa ujenzi; na

d) Mwamko hafifu wa matumizi ya mbolea itokanayo na taka.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba"

a) Serikali iharakishe mchakato wa kupata maeneo makubwa mbali na makazi ya watu kwa kuzingatia Kanuni za Mipango Miji ili kutumika kuhifadhi taka zinazozalishwa katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya Jirani. Pengine, uzoefu uliopatikana kutokana na changamoto za kukabiliana na taka ngumu katika Jiji la Dar es Salaam ukatumike kunusuru Miji na Majiji mengine ikiwemo Dodoma;

b) Mchakato wa kukusanya chupa zenye rangi mfano enegy drinks na kuzichakata kupitia Viwanda vilivyoanzishwa uongezewe motisha ili kudhibiti kikamilifu uzagaaji wa chupa hizo;

c) OMRM iandae Kanuni zitakazosimamia ubora wa madampo na vitendea kazi vinavyotumika katika zoezi la ukusanyaji wa taka ikiwa ni pamoja na matumizi ya Magari ambayo katika kusafirisha taka hayachafui mazingira;

d) Serikali iongeze jitihada katika kudhibiti utupaji hovyo wa taka ngumu kwa: -

(i) Kusimamia utengaji wa Maeneo sahihi ya kuweka madampo wakati wa upangaji wa Miji;

(ii) Kuanzisha na kusimamia utaratibu wa kutenganisha taka (*Sorting*) kuanzia zinakozalishwa;

(iii) Kuhamasisha Sekta binafsi kuwekeza katika eneo la taka ngumu;

(iv) Kuhakikisha miundombinu yote ya kuhifadhi taka inatumika kwa usahihi;

(v) Kushirikiana na TAMISEMI kuandaa Mkakati wa kutoa mafunzo ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa Viongozi wote kuanzia ngazi ya watendaji wa Vijiji; na Mitaa; na

(vi) Kuongeza msukumo katika utekelezaji wa zuio la matumizi ya vifungashio vya plastiki.

e) Serikali iendelee kuhamasisha na kuwezesha vikundi vya Wananchi vinavyojihusisha na ukusanyaji wa taka ngumu kwa kutatua kero zao kwa wakati na kuwajengea uwezo zaidi wa kujikwamua kiuchumi;

f) Uhifadhi wa Mazingira na mabadiliko ya tabianchi upewe kipaumbele katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025- 2050.

g) Serikali ihamasishe utenganishaji wa taka kwa kuanza na maeneo yenye mikusanyiko mikubwa ya watu, Mfano Vituo vya mabasi, Reli, masoko, Shuleni, Hospitali, na baadae kufikia ngazi ya Kaya.

h) Serikali iongeze uwezo kwa Taasisi zake zinazojihusisha na biashara ya uzoaji taka kama magereza na JKT ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji, utenganishaji na usafirishaji wa taka ngumu.

**3. Utekelezaji wa Mkataba wa Nairobi**

**"KWA KUWA,** Mikataba mingi ya Kimataifa kuhusu mazingira ukiwemo Mkataba wa Nairobi kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi inalenga kuhifadhi mazingira;

**NA KWA KUWA,** utekelezaji wa Mikataba hiyo umekuwa na manufaa mbalimbali kwa Taifa ikiwa ni pamoja na kupata fedha za utekelezaji wa miradi yenye mlengo huo, kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na nchi nyingine na Kukuza uelewa kwa Jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba''

OMRM iendelee na jitihada za kutafuta fedha ili kuhakikisha kuwa Mipango na Mikakati katika uandaaji na utekelezaji wa Miradi mikubwa ya kuhifadhi mazingira ya Bahari inatekelezwa.

**4. Utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu**

**''KWA KUWA,** Tanzania imekuwa ikitekeleza shughuli za Uchumi wa Buluu kupitia Sekta mbalimbali zenye mnasaba na Uchumi huo zikiwemo; Uvuvi, Maliasili na Utalii, Maji, Nishati, Uchukuzi, Madini, Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Uhifadhi wa Mazingira;

**NA KWA KUWA,** dhana ya Uchumi wa Buluu ni dhana inayochagiza ukuaji wa uchumi kupitia matumizi endelevu ya Rasilimali za maji kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira na ushirikishwaji wa Jamii;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba'' Serikali kupitia OMRM iharakishe mchaato wa kutunga Sheria ya usimamizi wa Uchumi wa Buluu kwa kuzingatia Malengo ya Sera mpya ya uchumi wa Buluu ya mwaka 2024.

**5. Udhibiti wa Utiririshaji wa Majitaka na Taka za Viwandani katika Ziwa Victoria**

**''KWA KUWA,** pamekuwa na shughuli zisizo endelevu za kibinadamu zikiwemo; uvuvi haramu, uharibifu wa maeneo oevu, Kilimo kisichozingatia uhifadhi, uchimbaji madini usiokuwa endelevu pamoja na utiririshwaji wa majitaka katika maeneo yanayozunguka Ziwa Victoria;

**NA KWA KUWA,** hali hiyo imesababisha kupungua kwa rasilimali kama vile samaki, kuongezeka kwa viumbe vamizi, kuharibika kwa Mifumo ikolojia ya viumbe hai vya majini, na kupungua kwa ubora wa maji;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba''

a) OMRM kwa kushirikiana na Halmashauri zote zinazozunguka Ziwa Victoria kutekeleza Mikakati iliyopo ya udhibiti wa taka katika Ziwa hilo kwa kuzingatia ipasavyo Sheria ya Usimamizi wa Mazingira; na

b) OMRM ichukue hatua za haraka zitakazowezesha udhibiti endelevu wa utiririshaji wa majitaka katika mto Milongo uliopo Jijini Mwanza.

**3.2.2 Mapendekezo kwa Wizara ya Maji.**

1) **Mahitaji makubwa ya fedha za utekelezaji wa miradi ya maji nchini**.

**''KWA KUWA** kumekuwa na ongezeko kubwa la mahitaji ya maji kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kasi ya ongezeko la idadi ya watu, kasi ya ukuaji wa Miji, na ongezeko la shughuli za uzalishaji;

**NA KWA KUWA** ongezeko la mahitaji ya maji haliwiani na kiwango cha uzalishaji wa maji na hivyo kusababisha mahitaji makubwa ya fedha za utekelezaji wa miradi ya maji nchini;

**KWA HIYO BASI**; Bunge linaazimia kwamba'' Serikali

(i) Izingatie ongezeko la mahitaji makubwa ya maji nchini pamoja na ongezeko la mahitaji makubwa ya fedha za kutekeleza miradi ya maji wakati wa kuweka ukomo wa bajeti ya Wizara ya Maji;

(ii) Kwa kuzingatia matakwa ya mabadiliko ya Sheria ya fedha Na. 16 ya mwaka 2015, Serikali iwasilishe kwa ukamilifu na

kwa wakati fedha zote za Mfuko wa Taifa wa Maji zinazokusanywa kutokana na Tozo ya **Shilingi 50** kwa kila lita ya petroli na Dieseli ili kupunguza pengo kubwa la mahitaji ya fedha lililopo katika Sekta ya Maji;

(iii) Kwa kuzingatia mwenendo wa bei ya mafuta duniani, Serikali iangalie uwezekano wa kutumia nafuu ya kupungua kwa bei ya mafuta duniani (*Wind fall gain*) kwa kutunisha Mfuko wa Taifa wa Maji;

(iv) Serikali kupitia Wizara ya Maji, ibuni vyanzo vipya vya mapato ya Mfuko wa Taifa wa Maji kwa mfano Tanga UWASA Green Bond ili kupunguza utegemezi wa Mfuko huu kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali;

(v) Kwa kuzingatia mapinduzi makubwa ya uzalishaji Umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, na Lusumo, Serikali itafakari umuhimu na manufaa ya kuweka bei maalum ya umeme (*Special Tarrif*) katika Sekta ya Maji ili kupunguza gharama za uzalishaji maji;

(vi) Wizara ya Maji iandae Mpango wa Manunuzi ya pamoja (*Bulk procurement*) ili kutokana na faida ya kununua kwa wingi nafuu itakayopatikana ipunguze gharama za uendeshaji na uzalishaji maji;

(vii) Kwa kuzingatia umuhimu na unyeti wa huduma ya maji, Serikali iondoe kodi ya ongezeko la thamani (VAT) katika bidhaa na huduma muhimu zinazotumika wakati wa utekelezaji wa miradi ya Maji nchini.

**2) Upatikanaji na usambazaji wa maji katika Majiji ya Dodoma, Dar es Salaam, Tanga, Mbeya, Mwanza na Arusha**

**"KWA KUWA,** kumeendelea kuwepo na changamoto mbalimbali zinazokwamisha utendaji wa Mamlaka za Maji nchini zikiwemo: -

a) Mipango Miji kutozingatia uwepo wa miundombinu ya majisafi na majitaka;

b) Uhujumu wa Miundombinu ya Majisafi na Majitaka; na

c) Upotevu wa Maji kutokana na mivujo, uchakavu wa miundombinu na ubovu wa Dira za Maji.

**NA KWA KUWA,** kuwepo kwa changamoto hizo kunakwamisha juhudi za Serikali katika kufanikisha azma ya kuwapatia Wananchi wake majisafi na salama;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba''

Wizara zishirikiane na kuchukua hatua Madhubuti za kudhibiti ujenzi wa makazi holela kwa kuzingatia Kanuni za Mipango Miji ili kuwezesha uwepo wa miundombinu muhimu kama vile miundombinu ya Maji safi na Maji taka katika Maeneo yote yaliyopangwa;

a) Mikakati endelevu ibuniwe na kutekelezwa ili kuhakikisha maeneo yote yenye vyanzo vya maji au miundombinu ya Maji iliyokamilika yanapata Maji ili kuleta tija ya fedha zilizowekezwa na Serikali;

b) Mamlaka za Maji zishirikiane na kubadilishana uzoefu kuhusu namna bora zitakazowezesha upatikanaji wa maji safi kwa Wananchi wa maeneo yote nchini; na

d) Serikali ihakikishe kuwa huduma ya maji katika maeneo yote ya Umma zikiwemo Shule, Vituo vya Mabasi, Masoko, Viwanja vya Michezo, Viwanja vya Ndege, Vyuo Vikuu, Maeneo ya Ibada na Vituo vya treni inapatikana kwa wakati wote ili kukidhi mahitaji ya Wananchi na vilevile kuchukua tahadhari juu ya magonjwa ya mlipuko katika maeneo hayo.

**3) Hali ya upotevu wa maji nchini**

**''KWA KUWA,** kiwango cha upotevu wa maji nchini ni **asilimia 36.2** kikiwa ni juu ya wastani unaokubalika Kitaifa na Kimataifa wa **asilimia** 20;

**NA KWA KUWA,** hali hiyo inasababisha athari mbalimbali zikiwemo upotevu wa mapato na upungufu wa maji kwa matumizi mbalimbali nyumbani na shughuli za uzalishaji;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba'' Serikali

a) Ihamasishe matumizi ya Mfumo wa Kisasa wa kudhibiti Mivujo (*Intergrated Leakage Management System* **(ILMS)** kwa Mamlaka zote nchini ili kudhibiti kwa ukamilifu tatizo la upotevu wa maji nchini;

b) Kwa kushirikiana na Viongozi wa Mitaa, ichukue hatua za dharura za kudhibiti upotevu wa maji katika maeneo yote nchini pamoja na kutoa elimu kwa Umma hususan kwa Jamii za kifugaji kuhusu umuhimu wa kulinda miundombinu ya Maji katika maeneo yao;

c) Ianzishe Vitengo mahsusi vitakavyoshughulikia masuala ya upotevu wa Maji na kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa kubaini mivujo (ILMS)katika maeneo yote nchini ili kuwezesha upatikanaji wa majisafi na kudhibiti hasara itokanayo na upotevu huo; na

d) Iandae Mkakati wa pamoja utakaohusisha Wizara mbalimbali zikiwemo Wizara ya Nishati, Wizara ya Mambo ya ndani, Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Uchukuzi ili kudhibiti wizi wa Miundombinu katika Sekta hizo.

**4) Utekelezaji wa shughuli za Mamlaka za Maji kupitia Hati Fungani**

**''KWA KUWA,** uwekezaji wa ndani kupitia Hati Fungani umekuwa ni chanzo cha uhakika cha upatikanaji wa fedha katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo;

**NA KWA KUWA,** hatua hiyo ni njia madhubuti na ya kimapinduzi kwa Sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Maji nchini katika kuongeza kipato;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba'' Serikali ihamasishe uwekezaji kwenye Hati Fungani ili kuimarisha zaidi uchumi wa Wananchi wake na kutatua changamoto za uwekezaji katika miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya Maji;

**5) Utekelezaji wa Mwongozo wa uvunaji wa maji ya mvua**

**''KWA KUWA,** Mwongozo wa uvunaji wa maji ya mvua unalenga kuhakikisha uendelevu katika jitihada za kuongeza upatikanaji wa maji kwa mahitaji ya Kijamii, Kiuchumi na mazingira, lakini pia kuzuia mafuriko ya maji ambayo yamekuwa yakitokea maeneo mengi nchini;

**NA KWA KUWA,** kumekuwa na msukumo mdogo katika utekelezaji wa Mwongozo huo hali ambayo imesababisha utayari mdogo wa Jamii kushiriki kuvuna maji ya mvua, uratibu hafifu katika ujenzi wa mabwawa ya maji na upatikanaji mdogo wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba'' Serikali

a) Isimamie kuanzishwa kwa Kamati ya Kitaifa itakayoratibu shughuli za uchimbaji wa Mabwawa ya Maji kwa kuzingatia uhitaji wa Maji kwa shughuli mbalimbali za Kijamii na Kiuchumi; na

b) Ihamasishe ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji kwa kuanza na Taasisi zake zikiwemo Shule, Zahanati na Vyuo.

**6) Shughuli zilizotekelezwa kwa kutumia mitambo 25 iliyonunuliwa na Serikali kwa ajili ya kuchimba visima na usambazaji wa maji katika maeneo yenye visima hivyo**

**"KWA KUWA,** baadhi ya visima vinavyoendelea kuchimbwa nchini vimekuwa vikikosa maji licha ya kutumia rasilimali nyingi katika uchimbaji huo,

**NA KWA KUWA,** hali hiyo inasababisha hasara na kurudisha nyuma juhudi za kusaidia upatikanaji wa maji kwa maeneo yote nchini,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba''

a) Kwa kushirikiana na wadau wa utafiti (Vyuo Vikuu, TPDC n.k), Serikali iboreshe tafiti kwenye utafutaji wa maji chini ya ardhi kwa kuwaongezea uwezo Wataalamu wake pamoja na kutumia teknolojia za kisasa katika uchimbaji wa Visima; na

b) Wizara ichukue hatua madhubuti zitakazowezesha kukamilika kwa uchimbaji wa visima vitano kwa kila Jimbo vilivyoahidiwa na Serikali.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa umahiri wako kwa kutuongoza vyema katika kuisimamia na kuishauri Serikali kwa kuzingatia Sheria, Taratibu na dhana nzima ya Utawala Bora kwa lengo la kuwaletea Watanzania maendeleo yenye tija. Tunakuombea afya njema, maisha marefu na mafanikio tele katika utekelezaji wa majukumu yako.

**Mheshimiwa Spika,** nitoe shukrani za dhati kwa Mhe. Azan Zungu (Mb), Naibu Spika kwa kazi nzuri anayoifanya ya kukusaidia kuongoza na kusimamia Mhimili wa Bunge. Aidha, niwashukuru Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee napenda kuwashukuru Mawaziri Mhe. Juma Aweso (Mb), Waziri wa Maji na Mhe Mhandisi HamadYussuf Masauni (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Manaibu Waziri, Mhe. Mhandisi Kundo Mathew (Mb), Naibu Waziri wa Wizara ya Maji, na Mhe. Khamis Hamza Khamis (Mb), Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Aidha, niwashukuru Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake wakiongozwa na Mhandisi Mwajuma Waziri, Katibu Mkuu Wizara ya Maji na Mhandisi Cyprian Luhemeja, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Natambua kuwa ushirikiano wao ndio uliofanikisha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee niwashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa shughuli za Kamati.

Natambua na kuthamini michango yao adhimu, makini, na uzalendo wa hali ya juu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Kamati.

Kwa heshima kubwa natamani kuwataja majina yao, hata hivyo kutokana na ufinyu wa muda. **Naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (HANSARD) kama ifuatavyo: -**

1. Mhe. Jackson Gedion Kiswaga, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Anna Richard. Lupembe, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Prof. Shukrani Elisha Manya, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Mhandisi Stella M. Manyanya, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Charles Mwijage, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Kavejuru Eliadory Felix, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb - Mjumbe

9. Mhe. Ritta Kabati Enespher, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Asya Sharif Omar, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Mohammed Jumah Soud, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Juma Usonge Hamad, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Haji Makame Mlenge, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Asya Mwadini Mohammed, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Regina Ndege Qwaray, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Suleiman Omar Mohamed, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Keneth Nollo, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Deo Kasenyanda Sanga, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Kasalali Emmanuel Mageni, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Robert Chacha Maboto, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Bunge kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati, chini ya Uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard kwa umakini na weledi katika kuratibu shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila kukwama na kuandaa taarifa hii.

### 4.2 Kutoa Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza kwa kina shughuli zilizotekelezwa na Kamati, matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo na uchambuzi wake, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa liipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira na likubali Maoni na Mapendekezo yote ya Kamati kama yalivyo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.



Jackson Gideon Kiswaga, (Mb),
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA.**

7 Februari, 2025

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo orodha hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia hoja hizi mbili za Kamati. Tutaanza na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mheshimiwa Asya Mohammed ajiandae.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi niweze kuchangia na kunipatia nafasi kuwa wa kwanza kuchangia taarifa za hizi Kamati mbili; ya Ardhi pamoja na Maji.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema chochote, kwanza nitumie nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati sana kwa Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na Ardhi kwa kutujaalia afya pamoja na uzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hili tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa sisi Wabunge kuwa na afya na uzima, lakini ziada ni kwako Mwenyezi Mungu kuendelea kukupatia afya njema pamoja na uzima na kuendelea kutusimamia sisi Waheshimiwa Wabunge katika muda wote ambao tupo hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ziada nitoe pongezi zangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kibamba kwa Viongozi wetu watatu wa Kitaifa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu wetu Maalum kuwa wagombea kwenye nafasi zao kwa uchaguzi wa 2025/2030, hasa kwa Dkt. Balozi Emmanuel John Nchimbi kuteuliwa na Chama chetu kuwa Mgombea wa nafasi ya Makamu wa Rais. Hawa wengine wanaendelea na nafasi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama Mjumbe wa ule Mkutano Maalum, ninaamini nilitenda haki kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kibamba kuwachagua wote hawa watatu kwa kura ya Ndiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi zangu hizo, nizungumzie maeneo mawili; la maji na hilo la ardhi. Hili la maji, moja kubwa ni mafanikio makubwa ambayo yamepatikana katika kipindi chote hiki cha miaka minne na miezi kama mitatu ya Chama chetu katika Ilani ya Uchaguzi ya 2020/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba mimi kama Mbunge wa Jimbo la Kibamba ninaendelea kutoa shukrani zangu za dhati sana kwa jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Awamu ya Sita pamoja na viongozi wote wa Wizara wakiongozwa na mdogo wangu Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, kwa kufanya kazi nzuri sana kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, katika muda wote nikisimama humu mwanzoni, nimekuwa nikisema kidogo kwa ukali juu ya changamoto kubwa ya maji ambayo toka ninaingia ilikuwa chini ya 40% au 30%, lakini leo ni ukweli tumeshafika zaidi ya 85%. Shukrani zangu hizi zipo wazi tu kwamba wananchi walio wengi sasa wanapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi mitatu mikubwa ya Wizara hii imeweza kuifanya kwenye Jimbo la Kibamba mikubwa kabisa. Mradi wa Tegeta A, tenki la ujazo wa lita 5,500,000. Ndani ya ujenzi wa takribani matenki makubwa matatu kwenye Mradi wa Changanyike - Bagamoyo, mradi ambao umetumia zaidi ya shilingi bilioni 64 za Benki ya Dunia. Kwa hiyo, sisi wananchi wa Jimbo la Kibamba eneo la Tegeta A, Goba na Goba nzima na viunga vyake sehemu kubwa wanapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tenki la pili, ni pale Mshikamano. Nimekuwepo humu, ndani ya mwaka 2021, fedha zile za UVIKO Mheshimiwa Rais, akatoa shilingi bilioni 4.8; Shilingi bilioni 2.5 fedha za ndani na shilingi bilioni 2.4 fedha za UVIKO kujenga lile tenki

kubwa la ujazo wa lita 6,000,000 pale Mbezi. Leo wananchi wengi wanapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba sasa hivi Mheshimiwa Rais anatekeleza mradi wa shilingi bilioni 42 chini ya Benki ya Dunia pale Pangulo ambao utawasaidia wananchi wengi wa Dar es Salaam ya Kusini ambao kwangu ni kule Mpakani, Msingwa, maeneo ya King'azi A na B, maeneo ya Kipera, Kwembe na maeneo mengine ya Malamba Mawili, Msigani. Sasa tenki limekamilika.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, juzi nilimwona kule na akatutaja Wabunge wahusika kwenye mradi ule na sasa wanaenda kwenye usambazaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na miradi niliyoisema hii, au mafanikio yetu ya Serikali yetu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwenye sekta ya maji, tunakubali changamoto bado ipo na changamoto kubwa ni usambazaji wa maji kwa muda mrefu kwenye haya matenki ambayo yametimia. Wananchi wanashaanga tu bado, kwa nini, hawayaoni wakati matenki yana maji.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuwaomba, yapo maeneo yamepelekwa mabomba, lakini hawajazamisha ndani. Yatoke maelekezo kwa sababu mabomba yale yanaibiwa, na wananchi wanashindwa kuelewa, hasa maeneo ya Mbezi, Torino, Kwa Mvungi, CCM ya Zamani Mpiji Magoe na maeneo machache mengine sehemu ya Jimbo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaomba sana Wizara itoe maelekezo mabomba ambayo wameyaleta jimboni yazamishwe ndani ili wananchi waone kweli yameletwa kwa ajili yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia changamoto nyingine ambayo nataka wananchi wajue, ni kwamba leo tunatumia chanzo cha Ruvu Juu. Ruvu Juu ndiyo inalisha Dar es Salaam na upande wetu huo Ruvu Chini inalisha upande wa Jimbo la Kawe na maeneo ya

mjini. Ni ukweli chanzo kile ni toka tunapata uhuru. Wananchi lazima wajue chanzo hakijawahi kubadilika, chanzo ni kile kile, na leo tunatengeneza tu vihifadhia maji. Kwa hiyo, nyakati kame ni kweli lazima tutakutana na upungufu wa uzalishaji wa maji kwenye vyanzo vyetu vikuu.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita katika kuliona hili, kwenye *long term* imekuja na Bwawa la Kidunda. Sijaliona kwenye taarifa inasemwa vizuri, lakini mradi unaoendelea na upo zaidi ya 46%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili bwawa ndiyo litakuwa ukombozi wa Morogoro na Dar es Salaam au Pwani kwa maana ya muda wote sasa kuwa na chanzo kinachotosheleza. Kwa hiyo, wananchi waendelee kuwa na subira kama walivyokuwa na subira nyakati za nyuma.

Mheshimiwa Spika, leo tumekuwa na vihifadhia maji kwenye maji machache yanayozalishwa, na tunaweza kuwapeleka walio wachache, wachache bado kweli hawayapati maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, siyo muda mrefu, hii ni awamu ya kwanza inakamilika. Mheshimiwa Mbunge Mtemvu, anamaliza, lakini ni imani yangu kwamba watanichagua tena kwa kura nyingi sana. Huu ni ukweli ambao nitaenda kukamilisha haya kwa sababu madirisha na milango ninaijua. Kwa hiyo, hilo lipo wazi na wenyewe wanaokuja wanajua, hili lipo vizuri sana kwa Mheshimiwa Mbunge Mtemvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo jambo la pili, ni jambo la migogoro ya ardhi. Hili nimekuwa nikilisema sana hata nikichangia kwenye Wizara za kisekta, lakini ukweli migogoro mingi imetatulika. Kuna maeneo machache sana ya mipaka haijasemwa sana kwenye Kamati, lakini kuna maeneo ambayo yanaingiliana, Wilaya ya Ubungo na Wilaya ya Kinondoni. Ule ambao tulikuwa nao Kisarawe na Ubungo imetatuliwa, na nitoe pongezi sana kwa viongozi wote wa Serikali Kuu wanaokuja na kupishana, kwa maana ya Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tunayo maeneo mawili ndani ya Ubungo na Kinondoni, moja ni eneo la Mpiji Magoe na Mabwepande kwa maana ya eneo ya Kibesa na Mabwepande eneo linaitwa Mji Mpya tukamilishe huu mgogoro Wizara mtusaidie kutatua.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni kule Msumi na Mbopo mtusaidie, kuna migogoro mikubwa na watu wanaumizana kwa sababu ya kutojua *GN* pale inasema nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa ambalo mara nyingi nimekuwa nikilisema hapa ni mgogoro wa Shamba la Malolo *(Malolo Farm)*. Nimewahi kulitolea historia yake jinsi lilivyopatikana, lakini lilikuwa chini ya *DDC* toka mwaka 1989 na hati wanayo, lakini wananchi wengi zaidi ya 70,000 wameingia humu.

Mheshimiwa Spika, nimewahi kueleza kwa historia kubwa sana na juzi Mheshimiwa Naibu Waziri ameniambia vizuri juu ya jambo hili. Nimtakie kila la heri ndugu yangu Mheshimiwa Ndejembi, akalimalize hili jambo kwenye Wilaya zetu hizi mbili ili wananchi waendelee kupimiwa ardhi wapate hati na mambo mengine ya kujiinua kiuchumi yaweze kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku ya leo sina maneno mengi zaidi, niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais na wateule wote wale. Sisi ni ahadi yetu kwao kwamba hatuwadai, zaidi wanatudai sisi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Kibamba wataenda kuonyesha jinsi gani ya kurudisha fadhila kubwa kwa kura nyingi sana kwa Wagombea wote Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Mbunge wao, Mheshimiwa Issa Bin Jumanne Mtemvu, kwenye Jimbo la Kibamba.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni walioingia baada ya tangazo la awali la wageni.

Tunao wageni waliokaa Jukwaa la Spika. Kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, Waziri wa Maliasili na Utalii, na huyu ni Ndugu Dkt. Hassan Abbas, ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni wageni saba wa Mheshimiwa Maryprisca Winfred Mahundi, ambaye ni Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, hawa ni watendaji katika Ofisi yake kutoka Mkoani Mbeya. Karibuni sana.

Tunao pia wageni 130 wa Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, hawa ni wanafunzi 126 na walimu wanne kutoka Shule ya Sekondari ya Wasichana Huruma ya Jijini Dodoma. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika wageni hawa nimeambiwa yupo mtoto wa Mheshimiwa Simon Songe, ambaye anaitwa Cafrine Simon Songe, karibu sana. Mheshimiwa George Malima, naye anao watoto wawili katika shule hii; wa kwanza ni Martha George Jacob. Karibu sana. Yupo na Mariam Manase Malima. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili mafunzo, yupo Ndugu Filberth Mkombwe kutoka Wilaya ya Songea Mjini, Mkoa wa Ruvuma. Karibu sana. Yupo pia mwingine ambaye ni Ndugu Halima Mbuguni kutoka Wilaya ya Moshi Mjini, Mkoa wa Kilimanjaro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Festo Richard Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Asya Mwadini Mohammed na Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Jambo la kwanza niunge mkono hoja ya Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa yale yote ambayo yamewasilishwa na nimpongeze Mheshimiwa Mnzava, kwa kuwasilisha vizuri sana maoni ya Kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitachangia mambo mawili nikiwa nimejikita kwenye suala la utalii, na pia kwenye Wizara ya Ardhi. Jambo la kwanza, kwa niaba ya wananchi wa Makete, nawapongeza sana Wagombea wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan; pia Dkt. Emmanueli Nchimbi na Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja, kati ya sifa ya Chama cha Mapinduzi, tuna Wagombea imara, tuna ilani inayotekelezeka, ni Chama ambacho kina wanachama wanaojitambua. Kwa hiyo, tupo tayari kwa uchaguzi na tumejipanga kweli kweli kuhakikisha mwaka huu tunashinda na hatuna mjadala.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jakaya Kikwete alisema ukitaka kujua nguvu ya CCM tangaza uchaguzi. Kwa hiyo, nasi tunaamini kwamba kwenye chama chetu, mwaka huu tumejipanga kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye sekta ya utalii, niungane na maoni yote ambayo yametolewa na Kamati na nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Utalii Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, na Mheshimiwa Deogratus Ndejembi, Waziri wa Ardhi kwa wanavyotuunga mkono sana kwa sababu tunafanyanao kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Sekta ya Utalii, Serikali tuliweka kusudio la kufikia watalii wengi zaidi ya 5,000,000. Nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara na Serikali kwa sababu tunavyozungumza leo kwenye ilani yetu, yale malengo ambayo tuliweka watu 5,000,000 tumeshavuka, tumefikia watu 5,360,000 zaidi ya 107% tumeweza kufikia watalii hao. Hii inaonesha kabisa kwamba *project* ya Mheshimiwa Rais ya *The Royal Tour* imeweza ku-*boost* utalii kwa kiwango kikubwa sana kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na Ripoti ya Shirika la Utalii Duniani linakiri wazi kwamba Tanzania imekuwa ni namba sita kwa ongezeko la watalii katikati ya Januari hadi Septemba, 2024. Tumekuwa namba sita duniani na namba moja barani Afrika. Maana yake ni

kazi kubwa sana ambayo Serikali imeifanya, na ninaunga mkono jitihada hizi na tuendelee kumshangilia Mheshimiwa Rais kwa sababu aliamua kuweka kabisa mguu wake na mkono wake kuhakikisha kwamba utalii wa nchi hii ambao unachangia zaidi ya 20% ya pato la Taifa. Ni kitu kikubwa ambacho Mheshimiwa Rais, amekifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu, nitachangia suala la miundombinu kwenye sekta ya utalii. Tuna takribani kilomita 6,950 ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho kwenye hifadhi zetu ili watalii wengi ambao Mheshimiwa Rais amepambana, wanapokuja waweze kuwa na maeneo mazuri ambayo yanapitika.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na changamoto sana kwenye hifadhi ya Serengeti na hifadhi zote mbalimbali nchini ambazo ukizijumlisha ni 10.2% ya ardhi ya Tanzania. Kwa hiyo, tunahitaji kuboresha miundombinu ya hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa sababu wameunda shirika ambalo linajihusisha na ujenzi wa barabara kwenye maeneo ya hifadhi na Serikali ilinunua mitambo mikubwa sana. Nami nikiunga mkono maoni ya Kamati, naomba sana Wizara na Serikali, shirika hili liweze kuwa na uwezo wa kujisimamia; pili, liweze kufuatilia maeneo yote ambapo barabara zimekuwa zikisumbua. Tufanye marekebisho haya kwa sababu sasa hivi gharama haitakuwa kubwa, kwani mitambo wanayo.

Mheshimiwa Spika, pili, vifaa mnavyo na kwa kuwa wataalamu pia wanao, waweze kujenga miundombinu ili iweze kupitika hususan barabara ambayo ni tegemeo kubwa. Tukifanikiwa kujenga barabara ya kuunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Mara, Mkoa ambao kwa kweli barabara ile ikiunganishwa, tunakuwa tumefungua lango la utalii kwenye eneo la Arusha na eneo la Serengeti yote.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwenye Kituo cha Utalii cha *DMCC*. Tumetumia zaidi shilingi 1,300,000,000/= kujenga kituo

hiki muhimu sana na Serikali ikalifanyia kazi kwamba hiki kituo sasa kianze kufanya kazi kwa sababu hii ni sehemu ambapo sisi tunategemea kitatupa *statistics* kwa maana ya takwimu nyingi za mwendelezo wa utalii kwenye nchi yetu, na baadaye kujua nini ambacho soko linahitaji?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni muhimu sana Serikali ikakifanyia kazi kituo hiki ambacho kipo pale Dar es Salaam. *DMCC* kwa maana ya *Digital Marketing Centre* cha Pale Dar es Salaam kwenye suala la utalii. Hayo yalikuwa ni maoni yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nilikuwa natamani sana Mheshimiwa Waziri kati ya hoja ambazo Mheshimiwa Rais amekuwa nazo kubwa kwenye sekta ya utalii ni suala pia la malazi. Tumeleta watalii wengi sana na kuleta huku watalii uhitaji wa malazi umekuwa kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, sasa naiomba Serikali, Kamati tulikutana na watu wa Wizara, lakini pia tulikutana na Msajili wa Hazina, ili kuzifanyia tathmini zile *lodge* na hoteli zote ambazo zipo kwenye maeneo *potential.* Bahati nzuri ni kwamba, hizi *lodge* na hoteli zipo kwenye maeneo mazuri ambapo zikifanikiwa kujengwa au kupata uwekezaji upya, zinaweza zikawa na tija sana kwenye Serikali.

Mheshimiwa Spika, sasa hizi *lodge* nyingi zimekwama na ndiyo mara nyingi nimekuwa nikitolea mfano hoteli ya *Embassy* iliyopo Dar es Salaam, ipo eneo zuri katikati pale Posta. Miaka 14 hoteli haifanyi kazi na pamekuwa kimya *as if* watu hawaoni kile kinachoendelea. Sasa ni muhimu Serikali ikazifuatilia hizi hoteli zote kwa sababu zipo kwenye maeneo muhimu, maeneo ambayo watalii wanatamani kuzitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, basi Serikali ingefuatilia kwa wale ambao wamekiuka umiliki, pia na uendelezaji, Serikali ikachukua hatua maeneo haya ya hoteli yakaweza kuchukuliwa na wawekezaji wapya wakapewa na ile nia ya Mheshimiwa Rais kwamba

wawekezaji wote wanaoingia Tanzania wasikose malazi, iweze kutimia.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo langu muhimu sana ambalo naisisitiza Serikali, na mwone tija *Embassy Hotel*, Dar es Salaam miaka 14 imelala haifanyi kazi, siyo jambo zuri na haileti faida kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwenye suala la hifadhi kwa maana Ngorongoro na hifadhi zetu za *TANAPA*. Sisi kama Kamati tulipeleka wazo Serikalini, kwamba hawa watu waweze kujikusanyia fedha na kuzitumia, lakini Serikali imekuwa na changamoto ya kuzuia hilo jambo. Hoja yao ni kubwa, kwamba kumekuwepo na matumizi ya mabaya kwenye suala hili kwa maana ya *TANAPA* na *NCCA* kukusanya fedha na kuzitumia wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Serikali imekuwa kwamba, matumizi *in a record* huko nyuma hakuwahi kuwa na matumizi mazuri kiasi kwamba wakafikia hatua ya kuzichukua hizi fedha. Sasa sisi tunamani haya maoni ya Kamati yangefanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, tusihukumu taasisi nzima kwa watu wachache ambao wame-*misbehave* tuka-*deal* na hawa wachache ambao wame-*misbehave,* lakini tukazisaidia hizi taasisi kwa sababu ukisaidia *TANAPA, NCCA* watapata fedha ambazo zitasaidia kwenye sekta ya utalii, kwa sababu 80% ya mapato ya utalii zinatoka na hizi shughuli ambazo zinafanywa na *TANAPA* pamoja na *NCCA*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vyema sana Serikali ikaangalia jinsi ya kuwawezesha hawa watu ili waweze kupata fedha, na pia waweze kufanya shughuli zao katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Spika, wazo langu lingine ni kwenye Wizara ya Ardhi. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri Ardhi kama nilivyosema, na pia Katibu Mkuu, kaka yangu Mhandisi Antony

Sanga kwa kazi nzuri ambayo anaifanya kwenye Wizara hii ya Ardhi. Ameleta utulivu mkubwa kwenye Wizara ya Ardhi na anafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa ni kuomba tu kwamba wakati anakuja kwenye Wizara, Mhandisi Antony Sanga, Waziri alisema huyu atakuja pia kutibu suala la mifumo kwenye Wizara. Sasa changamoto kubwa kwenye Wizara ya Ardhi ni mifumo kutokusomana, ndipo ambapo changamoto inajitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyu unakuta ana hati ya eneo hilo hilo, nami nina hati ya eneo hilo hilo, watu 10 tuna hati ya eneo moja. Hiyo ni kwa sababu mifumo haisomani, tunafanya *analogy way*. Ni vema Wizara ikachukua na ikifanya suala la mifumo kusomana, itakuwa imesaidia kuondoa *duplication* kwenye suala la upatikanaji wa viwanja, lakini pili itasaidia kwenye ukusanyaji wa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kitu muhimu sana Serikali ikalifanya hili ili migogoro ambayo ipo, ya wakulima na wafugaji; migogoro iliyopo kati ya wananchi kwa wananchi kwenye mipaka, itatatuliwa kwa mifumo kusomana na ujenzi wa mifumo. Hii imekuwa ndiyo kaulimbiu ya Mheshimiwa Rais, mifumo ya nchi isomane.

Mheshimiwa Spika, tunamtegemea Mheshimiwa Waziri Deogratus Ndejembi, kijana mzuri kabisa ambaye anaweza kuichapa kazi kwenye hili jambo, na anaweza akafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwenye suala la Tume ya Mipango ya Ardhi, wanahitajhi shilingi bilioni kama 170 tu kuweza kutatua changamoto za ardhi zote zilizopo nchini. Kwa hiyo, ni vyema Tume ya Mipango ikapewa fedha ikasaidiwe ili iweze kuratibu masuala ya upimaji wa ardhi nchini na kupanga matumizi ya ardhi. Hili ni muhimu sana na sisi tuseme kama Kamati tunaiombea sana Serikali yetu na hata bajeti ijayo tunatamani sana kwenye fungu namba tatu Tume ya Mipango ya Ardhi

iwezeshwe ili kutatua changamoto za mipango ya ardhi kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami sina mengi zaidi, naunga mkono hoja. Hivyo, ninawaahidi tu Wanamakete kwamba tutaendelea kuwa pamoja kwa sababu kazi njema ya Serikali yetu imefanyika na sisi tupo tayari kwa ajili ya mapambano. Niwahakikishie kwamba nipo imara na nguvu bado ipo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Haya. Mheshimiwa Asya Mwadini Mohammed, atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo na Mheshimiwa Riziki Said Lulida, ajiandae. *(Kicheko)*

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja za Kamati zilizo mbele yetu. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mdau mkubwa wa masuala mazima ya mazingira nchini. Mheshimiwa Rais ameonekana katika mikutano mbalimbali anajaribu kuchochea chachu kubwa na kuona mabadiliko makubwa ya kimazingira yanaendelea katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho kinashangaza, Mheshimiwa Rais anajitahidi kwa upande wake, lakini kwenye Wizara tunaona suala zima la bajeti la Ofisi ya Wizara ya Mazingira bado lipo chini sana. Kwa mfano, ukiangalia bajeti ya 2024/2025 fedha za maendeleo ambazo zimeletwa katika Wizara hii ya Mazingira ni shilingi bilioni 21; shilingi bilioni 18.3 ni fedha za nje, na shilingi bilioni 2.9 ndiyo fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, sasa unajiuliza kwa macho mawili; je, Serikali yetu ina nia madhubuti kwa ajili ya kulinda mazingira yetu?

Kwa sababu haiwezani fedha shilingi bilioni 18 kati ya bilioni 21 ni fedha ambazo tunategemea wahisani. Kwa hiyo, sisi mazingira yetu yatatunzwa na kulindwa na wahisani? Kwa sababu tunaamini, wahisani wanavyotuma fedha, wanatuma na utaratibu wao na matumizi yao ya kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa haya matatizo ambayo yapo ndani ya nchi yetu yanayojitokeza ambayo kama mabadiliko ya tabia ya nchi na vitu vingine vinajitokeza kwa haraka, tunawezaje kuvi-*solve* kama tunatarajia fedha za miradi ya maendeleo asilimia kubwa kama hii watupe wahisani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kwenye Kamati tulishauri na naendelea kushauri hapa kwamba bajeti lazima iongezwe na fedha za maendeleo ziongezeke. Isiwepo hii asilimia ndogo ambayo inaonekana hapa. *At least* ifike 60% ili tuweze kuyalinda na kuyatunza mazingira yetu na kupambana na changamoto ambazo zinajitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la taka ngumu. Mheshimiwa Mwenyekiti amewasilisha taarifa hapa vizuri sana, na ninampongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati. Amezungumzia kwamba wastani wa taka ngumu zinazozalishwa nchini, nyingi zinazokusanywa na kurejeleshwa, maana yake hapa ni zaidi ya hizo ambazo zinakusanywa na kurejeleshwa. Kwamba, inaonekana hakuna data maalumu ambayo inaonekana idadi ya tani ngapi tunakusanya taka kwa siku ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii inaleta masikitiko makubwa sana kwa sababu taka zinazalishwa kila siku na ndiyo maisha yetu. Kama tunapumua na taka ni lazima tutake tusitake tutazizalisha; lakini inaonekana ndani ya Wizara hakuna utaratibu au mpango mzuri sana wa kuzisimamia taka hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano hapa wamesema, kwa Jiji la Dar es Salaam wanakusanya taka kwa 63% tu. Sasa tujiulize, hiyo 37% ya taka zinakwenda wapi? Ni nani ambaye anazikusanya?

Maana haijulikani. Maana ukiangalia kwa makini zaidi, hii 37% ni taka ambazo zinaendelea kuzagaa na kutapakaa ndani ya nchi yetu. Hiyo ni kwa Dar es salaam, bado hatujachambua ndani ya mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya taka ni kubwa sana, kwa sababu kila siku ni lazima taka zizalishwe, na hii inasababisha taka kusambaa na hivyo inaweza kusababisha magonjwa mbalimbali ya mlipuko kuongezeka ndani ya Taifa letu. Hali kadhalika inaweza kusababisha uharibifu wa kimazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taka zinaweza zikabebwa na *wind force*. Kwa mfano, hapo Dar es salaam wapo katika kingo ya maji, na wapo katika Bahari, zina uwezo wa kuvutwa na kwenda baharini na *wind force,* lakini vile vile hayo mabadiliko ya tabia ya nchi tunayoyapigia kelele yanasababishwa na joto kali la ndani ya Taifa. Joto pia linatoka kwenye taka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unajiuliza, maana kama hiyo ni Dar es Salaam, huko kwingine tukija tukikaa chini tukachambua asilimia ni chache sana ya taka ambazo zinakusanywa. Sisi kwenye Kamati tulishauri Wizara na tunaendelea kushauri ndani ya Bunge lako Tukufu, kwamba ni wakati sasa wa Wizara kukaa na kutafuta wadau mbalimbali ambao wataweza kuanzisha, kama zilivyo taasisi nyingine binafsi zinazofanya kazi. Kwa mfano, ukienda nchi ya wenzetu jirani, Kenya wana kampuni inaitwa Takataka inafanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano ukija hapa ndani ya nchi yetu tuna changamoto kubwa ya mbolea. Kila siku hapa kilimo kikisimama watu wote wanapiga kelele, mbolea mbolea, ruzuku sijui inauzwa shilingi 70,000/= na kwingineko; huku ukiangalia ndani ya taka tuna uwezo wa kuzalisha mbolea nzuri ya mboji ambayo ni safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho kinasikitisha, Wizara ya Kilimo inapaswa ikae na Wizara ya Mazingira ili watafute namna

bora ya kutafuta wawekezaji ndani ya Taifa hili ili wawekeze viwanda vidogo vidogo, tuzalishe mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo kama mbolea inauzwa mfuko shilingi 70,000/= na kuendelea, huyo mkulima wa chini unategemea alime nini? Mabadiliko haya ya tabia ya nchi ambayo kila siku yanatokea huku na huku, ardhi zetu zimekuwa kame, mvua zimepotea, mambo ni shaghalabaghala? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi mimi nashauri kwenye sekta hii kwamba ni lazima kwenye vituo vyetu vya mabasi kukatengenezwa utaratibu wa ukusanyaji wa taka, wakaweka madampo, iwe mtu akifika anakuwa na hiyo taaluma ya kwenda na kufika. Pia waanzishe *radio, TV* ili kuonesha jinsi gani taka zinahitaji kuchambuliwa na watu waweze kupata elimu kwa ufanisi zaidi na waweze kuchambua taka hizo na zikusanywe zipelekwe katika madampo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara pia nayo wasijibebeshe kila mzigo. Kuna mambo mengine wanapaswa wasaidiwe. Sasa wao wajenge madampo, wakakusanye taka na mambo mengine. Kwa hiyo, wanatakiwa pia watoe hizi fursa kwa wawekezaji ili wawekezaji hao wajenge vituo vya kisasa waweze kuzirejelesha taka hizo na kuweza kupata bidhaa mbalimbali ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwa kumalizia, labda kwenye Wizara ya Maji. Kumekuwa na changamoto kubwa ya masuala ya taasisi za Serikali kutokurudisha fedha na kulipa ankara za bili za maji. Kwa mfano ukija katika Wizara hii ya Maji, wana miradi mingi sana ambayo haikamiliki kwa sababu hakuna fedha. Kama hakuna fedha, lakini mbona kuna hizi taasisi wana fedha wamezizuia? Kwa nini hawalipi maji? Kwa nini mwananchi wa chini aweze kulipa maji wao wasilipe maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaani wanatakiwa nao wawe na utaratibu wa kulipa maji. Hayo madeni ambayo wameyalimbikiza ambayo hapa tukisoma taarifa yanakaribia shilingi bilioni 80,

fedha ambazo zipo kwenye taasisi za Serikali, watu hawataki kulipa maji. Sasa walipe ili miradi ya maji ikamilike kwa wakati na wananchi wa Taifa hili wapate maji wasilalamike.

Mheshimiwa Spika, walipe ili fedha kwenye Wizara hii ziongezeke waweze kuchipua na miradi mingine. Mheshimiwa Mama Samia amesema ana nia ya dhati ya kumtua mwanamke ndoo kichwani. Sasa, anamtuaje ndoo ikiwa fedha wamezikalia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nije kwenye suala la uvunaji wa maji ya mvua. Tunashukuru Wizara imekuja na mpango mzuri na imetuonesha kwamba wapo tayari kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua, hususani mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, ushauri wetu kwa Serikali, kwa sababu tunaona changamoto kubwa inayoonekana hapa ni Wizara kwa Wizara kutokusomana. Maana hakuna mifumo maalumu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Wizara ya Maji watachimba mabwawa ya maji; Wizara ya Kilimo watachimba mabwawa; na wao wanataka hayo hayo maji. Wizara ya Kilimo na Wizara ya Maji, wote wanachimba maji; wavuvi nao wanachimba mabwawa ili waweze kupata maji wafuge samaki au waweze kulishia wanyama wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza hizo gharama, yaani fedha kwenda huku kwenda huku, walipaswa wakae meza moja waweze kutafakari namna nzuri ya kuchimba hayo mabwawa ya kisasa ili watu wa maji waweze kuchepua maji kutoka kwenye hayo mabwawa, watu wa kilimo wachepue maji kutoka kwenye hayo mabwawa na watu wa mifugo wachepue maji kwenye hayo mabwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nimalizie kwa kusema tutunze mazingira ili na sisi yaweze kututunza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo atafuatiwa na Mheshimiwa Lulida, Mheshimiwa Getere ajiandae.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyopo Mezani. Kwanza kabisa, niunge mkono hoja zote mbili. Nitumie fursa hii pia kupongeza kazi nzuri inayofanywa na Serikali yetu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maji na Mazingira; na kwa kweli naomba nijikite kwenye eneo moja kwa sababu muda ni mchache. Natambua kuwa kumefanyika kazi nzuri sana kwenye maji, hongera sana kwa Mheshimiwa Rais na Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji na mazingira, na hasa kwenye taarifa iliyowasilishwa leo, kwanza nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Rais ambaye ni kinara wa mazingira duniani. Hili wote tunatambua na limedhihirishwa kwanza kwa ule mkutano wa hivi karibuni uliohusu nishati ambao uliofanyika Dar es Salaam. Kwa kweli amekuwa ni kinara wa nishati safi ya kupikia; na hata kwenye taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni ya Kamati ya Nishati tumeona.

Mheshimiwa Spika, kwenye Kamati yao walisema takribani mitungi zaidi ya 400,000 ilishasambazwa, lakini tunaona namna ambavyo Mheshimiwa Rais amesimamia vyema maazimio ya *Cope 28,* hilo wala halina ubishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ule Mkutano wa Wakuu wa Nchi uliofanyika, na yale maazimio, tunaona namna ambavyo Mheshimiwa Rais ameendelea kuwa kinara. Hotuba zake nyingi, za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hakuna hotuba ambayo hajagusa suala la mazingira. Hata ile ya mwaka mpya alipozungumza na Waheshimiwa Mabalozi, alisisitiza suala la mazingira. Mheshimiwa Rais amekuwa pia akisisitiza suala la mabadiliko ya tabia ya nchi kuwekewa mikakati na namna

ambavyo tunaweza tukadhibiti. Pia suala la taka ngumu, namna ambavyo pia tunaweza tukadhibiti; vilevile na masuala mengine kimsingi ambayo yanaweza kuathiri mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hapa pia Serikali yake, hata katika rasimu ya Dira ya Taifa ya 2025 – 2050 ambayo sasa tunaitarajia izinduliwe suala la mazingira limepewa kipaumbele. Sasa nina uhakika kwamba Chama changu cha Mapinduzi katika ilani yake inayokuja ya 2025 – 2030 suala la mazingira na utunzaji wake litakuwepo. Hii ni kwa sababu hayo yote niliyoyasema yanaongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, nina uhakika kuwa chama changu kitaweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kazi nzuri hiyo na namna ambavyo sisi Wana-CCM tumeridhika, ndiyo maana Mkutano Mkuu ulimpitisha. Ninayo sababu ya kumpongeza yeye pamoja na mgombea mwenza pamoja na mgombea Urais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema, kwamba naunga mkono maazimio ya Kamati. Haya mambo yote ambayo Kamati yetu imewasilisha katika Bunge lako leo, naona ipo changamoto ambayo ni ya msingi sana ingewekewa mkazo. Hata katika mkutano uliopita kwenye sehemu ya maazimio ya Kamati, kuna jambo ambalo pengine linaendelea kutekelezwa, lakini naweza kusema pia bado halijatekelezwa, na lenyewe ndilo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati iliagiza mara kadhaa na kwenye taarifa pia limekuja, suala la kuharakisha mchakato wa kuleta mabadiliko makubwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Hili ni la msingi sana. Katika mabadiliko hayo makubwa ya sheria itakayobadilisha Sura Namba 191 ili iendene na sera mpya ya mazingira, tunaomba suala la *NEMC*, Baraza la Mazingira libadilishwe kuwa mamlaka. Hiyo itawezesha kuendana kwanza na sera mpya pamoja na kuifanya hilo baraza iwe mamlaka, iwe na meno au kuipa nguvu ya kuweza kusimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Baraza linasimamia mambo ambayo yanaanzishwa na Wizara nyingine. Kwa mfano tunapozungumzia labda masuala ya taka, au mifuko ya plastiki, ni suala ambalo pengine linasimamiwa na *TBS,* lakini wao wanakuja kudakia huku nyuma, na wakati mwingine masuala ya kelele. Kwa mfano, inaweza ikaweka katazo halafu mimi ni kiongozi nikawakataza. Kwa hiyo, ni vizuri hii sheria ikabadilika ili tuiondoe *NEMC* kuwa mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo imeonekana kwenye nchi za jirani, hata wenzetu wa Zanzibar tayari wanayo mamlaka. Ukienda Kenya wanayo mamlaka; ukienda Burundi wanayo mamlaka; Visiwa vya Shelisheli wanayo mamlaka. Sisi kizungumkuti kipo wapi ilhali tunaona *political will,* ama utashi wa kisiasa wa Mheshimiwa Rais upo wazi, dhahiri? Hili nadhani imebakia kwenye Wizara tu. Kwa hiyo, ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba kulikuwa na marekebisho madogo ya sheria ambayo pia na leo hayapo. Kwa hiyo, tunaamini itakapokuja, kutakuwa na mabadiliko hayo makubwa ya kuitoa *NEMC* kutoka kuwa baraza na kwenda kuwa mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, ni muhimu Wizara iharakishe mchakato wa kutunga Sheria ya Usimamizi wa Uchumi wa Buluu ili iweze kuendana na Sera mpya ya Uchumi wa Buluu ya 2024. Tukifanya hivyo, ni dhahiri pia kwamba tutakuwa tunafungamanisha masuala ya shughuli za kiuchumi hasa maliasili na utalii kama ambavyo imewasilishwa leo hapa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Tufungamanishe na Uchumi wa Buluu ili mambo yaweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu pia kwamba masuala yote hayo mawili yatawasilishwa katika Bunge lako Tukufu siku siyo nyingi ili Waheshimiwa Wabunge wote tuweze kuchangia vizuri, na ambapo tutaweza sasa kubadilisha sheria hiyo. Tunatambua kwamba iliyopo sasa inafanya kazi, lakini bado haiwezi kukidhi masuala ya mabadiliko ya tabia ya nchi, masuala ya hewa ya

ukaa *(carbon)* na masuala haya ya mamlaka kutoka kuwa baraza.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa kwamba Serikali ya Awamu ya Sita ni Serikali Sikivu. Sasa kama kuna mahali pengine kwenye ngazi ya Wizara hayo mambo yalikuwa hayajakaa vizuri, Bunge lako litafanya kazi hiyo kwa umakini mkubwa ili kuhakikisha mambo hayo yote yanaharakishwa na yanafanyiwa kazi sawasawa.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, kwa kweli naomba nitumie fursa hii kuamini kwamba katika eneo la tatu ambalo ninalipendekeza ni kuanzisha kituo mahususi na thabiti kitakachosimamia shughuli za hewa ya ukaa kuliko ilivyo sasa, kwa sababu tunajua kwamba kuna miongozo na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Spika, tunatamani wote tuingie kwa nguvu kwenye halmashauri, kwenye vijiji, ili kwa kweli tunapozungumzia masuala ya hewa ya ukaa, basi ijulikane kuwa kituo kipo mahali fulani, na hapo tutapata nyenzo zinazohitajika, na litasimamiwa pia kisheria ili kuhakikisha kuwa biashara hiyo inakuwa katika mikono salama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sitaki nigongewe kengele. Naomba nikushukuru tena, nirudie tena kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwa kinara wa nishati na kuharakisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Riziki Said Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia hii nafasi, lakini namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sisi sote kupata afya njema tukiwa katika hali ya usalama na amani katika nchi hii, Mwenyezi Mungu atubariki sana.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ujasiri aliokuwanao, Mwenyezi Mungu amempa kadari kubwa sana. Hii yote inatuonesha wanawake tuna uwezo mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe, kwa ujasiri uliokuwanao, unanitia nguvu na moyo sana, Mwenyezi Mungu azidi kukulinda. Tunakuiga katika mambo mengi, mifano mingi tunaipata, hasa kwetu sisi wanawake kwa kupitia wewe. Mwenyezi Mungu akuongoze zaidi na hayo unayoyafanya huko duniani, yawe tija na faraja kwa wanawake Tanzania nzima, kuwa wanawake tunaweza bila kuwezeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuja katika hoja tuliyokuwanayo mbele yetu. Mimi ni mdau, kwanza mimi ni balozi wa utalii, balozi wa maliasili, na pia mimi ni Mama Mjusi. Mimi ni balozi wa Selous, nimeisimamia Selous kwa muda mrefu, lakini vile vile ni Mama Tembo. Kwa hiyo, nitaondoka katika Bunge hili nikiwa na majina hayo matatu na yawepo katika rekodi, kwamba kulikuwa na Mama Mjusi, Mama Tembo, na Mama Selous, ni mimi Riziki Said Lulida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia hasa hali ya uchumi na hii Wizara ya Maliasili. Wizara ya Maliasili inahitaji kuongezewa *fund* za kutosha ili iweze kuiletea uchumi ambao utasaidia katika sekta za kiafya. Sekta zote za maendeleo ya jamii na elimu tunategemea fedha nyingi kutoka katika Wizara hii mojawapo.

Mheshimiwa Spika, naona katika tarakimu kwamba Wizara ya Maliasili inachangia pato la Taifa kwa 22.5%, lakini hii fedha ni ya kigeni. Ina maana Wizara hii ikiboreshwa na ikipewa *fund* ya kutosha, kama tulivyosikia kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati, ina maana tutaweza kupata faraja kubwa na huyu ng'ombe ambaye anakamuliwa maziwa atakuwa na maziwa ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi, mimi ni mwanaharakati wa mjusi, tangu mwaka 2005, nikiwa na mgombea mwenzangu Mama Mikidadi. Tulikuwa tunasimama tunaitwa Mama Mjusi, na

mjusi huyo nimeongelea humu Bungeni kwa miaka 20, lakini hakuna kinachoendelea. Kila anayekuja ananipa taarifa ambazo hazina matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupe taarifa. Mjusi huyu ambaye yupo Ujerumani, anafanyiwa biashara, na fedha zinazopatikana Tanzania hatupati *revenue* ya aina yoyote. Je, ni kwa faida ya nani? Kwa nini hatuonyeshi uzalendo wa kuhakikisha kuwa mapato yale yanaleta faida kwa Serikali Kuu, na yanaleta faida kwa Halmashauri ya Lindi?

Mheshimiwa Spika, hata pale lilipotoka jusi, hata shule hatujapata hadi leo, inasikitisha sana. Ninaondoka katika Bunge nikiwa na masikitiko kuwa masuala ya mjusi na faida ya mjusi haikupatikana mpaka leo. Kila anayekwenda inakuwa kama ngoma. Inachezwa ngoma, akirudi hakuna jibu linalopatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina imani hili utalisimamia ukishirikiana na Wizara ya Maliasili, Wizara ya Mambo ya Nje na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Hii fedha Tanzania tunaitaka tuifanyie kazi. Kuiachia hela iwe inatumika na Wajerumani, sisi tutapata nini kule kwetu?

Mheshimiwa Spika, wale wazee ambao wamechukua jusi kutoka Tendaguru, lilikuwa na tani 225, mpaka kule baharini, kilometa 120, wengine wamekufa na hatukupata faida yoyote, lakini wenzetu Namibia walidai mapato ya mafuvu na wamepata karibu shilingi trilioni nne. Sisi tunafanya nini hapa?

Mheshimiwa Spika, tufike mahali sisi tusiwe eneo la kuonewa. Tunataka fedha za mjusi ziingie hapa. Mwenyezi Mungu ajalie, nataka nikitoka hapa, mwezi wa Sita, *revenue collection* inayofanyika Ujerumani itengenezewe sheria kabisa, ili iweze kuwasaidia wanakijiji wa pale, hata watoto wa pale wapate shule. Hakuna shule, hakuna maji na hakuna chochote kinachoendelea kwa ajili yao ili kufaidika na mjusi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia suala la maendeleo ya urithi wa dunia. Katika urithi wa dunia, Kilwa haikuwa namba 21, lakini Kilwa ilikuwa na fedha yake ambayo iko Australia, ina zaidi ya miaka 1,000 haikufanyiwa kazi. Fedha nyingine ya Kilwa iko Zimbabwe, lakini leo Kilwa tukiangalia urithi wa Kusini, Lindi, Mtwara na Ruvuma tuna uwezo wa kuzalisha mapato makubwa na kuifanya nchi hii iweze kuibuka kiutajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utalii wa mikoa hiyo mitatu ya kusini unatosha kuweza kuongeza kutoka 22.5% mpaka hata kufikia 40% kwa vile ina uwezo mkubwa. Kwanza, vivutio vilivyoko kusini, tuna *beach sand* ambazo hakuna kabisa duniani. Alikuja balozi mmoja akasema *beach sand* ambayo inapatikana Mkoa wa Lindi na Mtwara hakuna duniani, lakini zile *beach sand* hazijatumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asilimia mbili kwa tatu ya Selous yote unayoiona inapatikana Lindi, lakini leo kuna nini kinafanyika Lindi, Mtwara na Ruvuma? Bado utalii.

Mheshimiwa Spika, fedha za *World Bank* zilitengwa kusaidia Mikoa ya Kusini, lakini lugha inayotumika hapa ni kuitenga kusini. Unaposema Kusini ni Lindi, Mtwara na Ruvuma, ile fedha imekwenda Kusini Nyanda za Juu. Mnapoipeleka Kusini Nyanda za Juu, Liwale, Namtumbo, Lindi; na wote katika hiyo mikoa mitatu hatukufaidika na fedha zile. Je, tuko tayari kuusaidia utalii? Nina imani na Katibu Mkuu na Mheshimiwa Waziri wake wana kazi ya ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Abbas, alifanya kazi kubwa sana kwenye michezo. Hivyo, ameingia huku. Nina imani kazi anayoifanya ni kubwa na Mwenyezi Mungu amlinde sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kuyapongeza mashirika yao, *TANAPA* na Ngorongoro, hayana mjadala. Haya mapato yote yanayopatikana *in forex* yanapatikana katika taasisi hizi. Je, kama hamjawasaidia hawa watu wakaweza kujikwamua

kiuchumi, wakalipeleka hili gurudumu vizuri, tunategemea mabadiliko ya kipato yatakuwa makubwa na nchi hii itakwenda vizuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaizungumzia *Royal Tour*. Mheshimiwa Rais ametuvalisha nguo katika *Royal Tour*. Nchi zote duniani zimetambua *Royal Tour* ya Tanzania, lakini kuna kipengele inabidi kifanyiwe kazi kwenye *Royal Tour* kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2014 Umoja wa Mataifa uliridhia na kupitia Sheria ya Watu wenye Ulemavu katika suala la utalii. Narudia, mwaka 2014, Sheria ya Utalii kwa Watu Wenye Ulemavu iliridhiwa na Tanzania. Kama mwanachama, inabidi na sisi tuifanyie kazi *Royal Tour* kwa watu wenye ulemavu, ili nasi tuonekane tumekubali maridhiano ya Umoja wa Mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka mwezi wa Sita, *at least* Waheshimiwa Mawaziri wangu wasikivu wa Maliasili, wote wawili, naomba waifanyie kazi *Royal Tour* kwa watu wenye ulemavu. Ipite na sisi turidhie, ili tunapokwenda katika *event* ya mwezi wa Sita, tuwe tumemalizana na masuala ya *Royal Tour* kwa watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna vivutio vikubwa katika mikoa ya kusini. Tanzania ndiyo ilikuwa nchi ya kwanza kwa ajili ya kusimamia ukombozi wa Afrika. Wilaya ya Nachingwea iliweza kuwaweka Waheshimiwa Marais wakubwa ambao waliingia kwa kuwekwa katika Kambi ya Nachingwea.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwao walikuwa ni Mondlane, Samora Machel, Augustino Netto na Savimbi. Morogoro na Mazimbu waliwekwa watu wa *ANC* ambao tumeona walikuwa Marais wa huko *South Africa*. Je, kumbukumbu zile ambazo zipo katika maeneo hayo tumezifanyia kazi?

Mheshimiwa Spika, kama hatujayafanyia kazi, basi tutengeneze *network* ya kuja kuyaona maeneo ya Mazimbu

ambayo tumewatoa Marais kwenda kwao na eneo la Nachingwea ambalo sasa hivi yamekaa kama magofu. Tunaomba, fedha ambazo zinawekwa zipelekwe kusini, ziangaliwe vizuri, ili utalii endelevu wa kumbukumbu za wapigania uhuru uwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, Putin amezungumza, alikuwa anakaa Bagamoyo kuisaidia nchi hii. Je, kumbukumbu zile ziko wapi?

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu hizi tuziweke katika *archives,* tuna mengi ya kuzungumza na tuna faraja kubwa ya kuishukuru nchi hii, lakini kwa sasa tunaomba zipatikane fedha za kutosha ili haya mabadiliko tunayoyataka ya urithi wa utalii kusini, yafanyiwe kazi. Nina imani fedha itakayopatikana ni kubwa na Mwenyezi Mungu atajalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina mengi ya kusema, ila haya machache ya mjusi. Wewe unanijua mimi nilikuwa mwanaharakati niliyewaita Waheshimiwa Wabunge humu ndani tukawa wanaharakati wa mjusi, Katibu wangu akiwa Mheshimiwa Omari Kigua na Mweka Hazina wangu alikuwa Mheshimiwa Reuben, lakini je, kwa nini mnatuacha hivi hivi, hatusimamii mjusi wetu?

Mheshimiwa Spika, huyu mjusi anatoka Lindi. Mimi natambua anatoka Lindi, na kama anatoka Lindi, tunahitaji Lindi yenye mabadiliko ya utalii ionekane. Isiwe Lindi ambayo inaonekana mjusi yuko Ujerumani, anafaidi Mjerumani, lakini ukienda pale hakuna shule. Natamani angalau twende Tendaguru ukaone.

Mheshimiwa Spika, Tendaguru imevamiwa na wafugaji na matokeo yake miti yote mizuri, kama mipingo, ambayo ilikuwa pale, inaisha. Mimi ni *champion* nasema, tungesimamia haya.

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu awabariki. Naunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati na Mheshimiwa Kavejuru Felix ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nazishukuru Kamati zote mbili na hasa Kamati ya Maliasili na Utalii. Kwa kweli, sisi Waheshimiwa Wabunge tunakaa humu tunaangaliana mambo mengi sana. Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Utalii, yule kijana anaitwa Mheshimiwa Mnzava yuko makini sana kwa kweli. Tumpigie makofi, kwani ni mmoja kati ya vijana wenye *talent* kubwa sana katika Bunge hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, katika Kamati ya Maji na Mazingira, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, amewakilisha hapa pamoja na Kamati nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kuzungumzia maliasili na utalii. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu wake na viongozi wengine wote wa Kamati hiyo, wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la fedha za *TANAPA, TAWA, TFS* na Ngorongoro kubaki kwenye maeneo yao, ni lazima Waheshimiwa Wabunge tufike humu ndani tuweke maazimio. Nafikiri Bunge lijalo, kwenye bajeti inayokuja, kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii kabla hatujaeleza hiyo bajeti, tuweke maazimio.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tutoe mwongozo wa kutaka kujadili, kwa nini Waheshimiwa Wabunge tumesema hizi fedha zibaki kwenye hizi taasisi ambazo ni taasisi mama kwenye Taifa letu?

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge ndio wasemaji na ndiyo tunatimiza majukumu ya Serikali. Katika Bunge lililopita tulifanya

maazimio humu ndani, tukasema fedha zibaki. Kwa nini hazijabaki?

Mheshimiwa Spika, nadhani kwenye Wizara hii, wakati tunakuja kwenye bajeti tutaambiwa kwa kina, kabla hatujaijadili, ni kwa sababu gani tuna hifadhi 22, mapori ya akiba karibu 49 na mambo mengi? Katika hifadhi zenyewe 22, hifadhi zenye fedha ni tano tu. Hivi kweli tunaweza kufanya mzaha katika kulinda mbuga na hifadhi zetu? Kwa sababu, mlolongo wa kupata fedha kutoka Hazina ni mkubwa sana, hivi kweli tembo atasubiri fedha zitoke Hazina ndiyo aje kulindwa? Haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesikia Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa anasema ilitokea kwamba hatukuiamini Wizara, Hapana. Lile tatizo la kupeleka zile fedha lilitokana na *COVID* – 19. Baada ya kuonekana kwamba watalii hawapo na hifadhi zinatakiwa kulindwa, basi zikapelekwa kule ili Serikali isaidie kulinda.

Mheshimiwa Spika, sasa *COVID* ilishaisha, mama alishatangaza, na sasa hivi watalii wamejaa Tanzania, kwa nini fedha zibaki? Hapana, nafikiri hili, Wizara inavyokuja kwenye bajeti, tutajadili ni kwa nini sisi Wabunge tukitoa maazimio hayatekelezwi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba sasa Wizara ya Maliasili na Utalii kuendelea kufanya mahusiano na majirani zao, waendelee kufanya mahusiano na vijiji Jirani. Zamani ilikuwa watu wanaenda kufanya makongamano na semina. Kwa mfano, sasa hivi Serikali za Vijiji zilizochaguliwa 2024 zote ni mpya. Inatakiwa *TANAPA, TFS,* Ngorongoro na *TAWA* waende wakafanye semina kuwapa elimu na mafunzo juu ya mahusiano na Serikali za Vijiji ambazo ni mpya. Waende huko wakajenge mahusiano, lakini pia, wakaone namna ya kufanya ulinzi wa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo tabia sasa ambayo imetokea, tunasema Wizara ya Maliasili ilinde, lakini kuna kitu kinaitwa *WMA,* wanapata mabilioni. Kwenye halmashauri kuna watu wanaitwa Maafisa Wanyamapori, wapo. Twende tukashirikiane kwa pamoja

tuweze kulinda wanyama waharibifu. Tushirikiane wote kwa Pamoja, hili ndilo agizo ambalo tunatakiwa kulifanya na pia, Maliasili na Utalii waendelee kujenga miradi ya majirani zao.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mimi pale Bunda kuna mradi wa jengo la upasuaji, wametoa shilingi milioni 55, wameliezeka, lakini sasa halina madirisha, milango na halina *finishing* yoyote. Kwa hiyo, naiomba ile shilingi milioni 50 ambayo tumeomba, ili waende wakamalize lile jengo kwa sababu, kituo cha afya kimejengwa, wametumia shilingi milioni 55 kujenga, lakini hawajamaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jengo la kuzalia la Zahanati ya Maliwanda ambalo watu wamekuja mpaka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tulizungumza na watu wa *TANAPA* kwenda kujenga lile jengo, wananchi wameweka viashiria vyote kwenye jengo la mama na mtoto la kujifungulia la Maliwanda. Waende wakajenge ile miradi. Kwa hiyo, naomba mahusiano ya Wizara ya Maliasili na Utalii yawe makubwa kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwenye Wizara ya Ardhi. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri wake ambaye ni mpya kabisa, na Mheshimiwa Naibu wake. Katibu wake ni mtu maarufu sana, anaitwa Sanga, ni mtu mzuri sana, aendelee. Nawaomba sasa kwenye Wizara ya Ardhi, Kamishna wa Ardhi achangamke.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani mimi Mbunge nimeshaenda kwao mara mbili, mara tatu. Kuna mgogoro uko pale Mikomarilo ambao labda pengine ilitakiwa Mheshimiwa Waziri angefika au hata mtu mwingine angefika. Wananchi wanapokuwa na migogoro viongozi wafike, wakaenao, wawaulize mgogoro ni wa nini? Waweze kutatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mgogoro mwingine umejitokeza hapo Kiumbu, kuna mwekezaji amekaa pale na wananchi hawana mahusiano naye. Nimekwenda ofisini kwao, lakini hakuna mtu aliyefika; hakuna Mheshimiwa Waziri wala kamishna aliyefika.

Mheshimiwa Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri Ndejembi, sina lawama naye, lakini Wizara ni ya kwake, tumezungumza sana. Atakapotoka hapa, nadhani kabla ya bajeti yake, awe yeye au Mheshimiwa Naibu wake au mtu yeyote, aje kule Bunda. Haiwezekani tukawa tunazungumza hapa na kila siku tunakwenda ofisini kwao, lakini hawatekelezi. Kwani Mheshimiwa Rais amewateua wafanye kazi gani? Amewateua watusaidie sisi Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati fulani huwa najiuliza maswali mengi sana. Mtu akiwa Mbunge wa kawaida anakuwa na akili nyingi sana, lakini akiwa Waziri anajisahaulisha. Kwa nini inakuwa hivyo? Tuwe pamoja, wanakuwa pamoja na sisi wakiwa Wabunge wa kawaida, kwa nini wakiwa Mawaziri wanajisahaulisha? Nawaomba sasa tulimalize hili tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale Bunda kuna suala la matumizi bora ya Ardhi ya Unyari, Kihumbu, Maliwanda na Sarakwa. Kwenye matumizi bora ya ardhi humo ndani kuna kitu kinaitwa *WMA* na kuna mashirika yanaitwa, sijui, *Frankfurt,* wanajiingiza humo kuwashawishi wananchi watengeneze *WMA* ambayo ni hewa. Tunaomba matumizi bora ya ardhi yabaki kama matumizi bora ya ardhi, tusiingize vigezo vingine vya kuwanyang'anya watu ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la Unyari, Maliwanda, Kihumbu na Sarakwa kuna mgogoro unaingia ingia humo ndani; waende wakafikirie, nataka kusikia maneno kama hayo.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa sababu wanaendelea kupima. Naomba Serikali iwape fedha kwa kweli, kwa sababu matumizi ya ardhi hii ni makubwa sana. Tunaomba Serikali iwape fedha za kutosha ili kutusaidia katika kupanga matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni Wizara ya Maji. Nilikuwa Mbunge wa kipindi kilichopita 2015 - 2020 na nimekuwa Mbunge mpaka sasa hivi. Katika jambo ambalo nimeondolewa aibu ni suala la Wizara ya Maji. Namshukuru sana Mheshimiwa Aweso,

ambaye kwa kweli Mheshimiwa Dkt. Samia alimteua akijua kwamba huyu kijana atafanya kazi. Ametoa maji ya Ziwa Victoria kutoka Butiama kuyaleta kwenye Jimbo langu la Nyamswa. Ametenga shilingi bilioni 8.7 ambazo tayari hizi fedha zinatafutwa ili ziende zikafanye hii kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilikuwa ni aibu, unatoka hapa Dodoma unaambiwa maji kutoka Ziwa Victoria yanakuja, unafika Tabora unaambiwa maji yamefika Tabora, unafika sijui wapi unaambiwa maji yamefika. Sisi Mkoa wa Mara, kilometa 20 kutoka Ziwa Victoria, hatuna maji. Yaani ilikuwa ni aibu kama vile Wabunge ni wapiga debe tu.

Mheshimiwa Spika, namwombea Mheshimiwa Aweso Mungu ambariki sana na ninamwombea wananchi wake wamrudishe na Mheshimiwa Rais aendelee kumteua aendelee kuwa kwenye Wizara hiyo, kwani amefanya kazi nzuri sana, na Katibu wake ni mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, sasa tunaiomba Serikali iwape fedha. Wanafanya miradi mikubwa ya maji, lakini fedha hakuna. Tunaiomba sana Serikali iwape fedha za kutosha ili waweze kumaliza kazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, palepale Bunda wametumia shilingi milioni 67 kutengeneza utafiti wa kujenga mabwawa sita. Wametumia *1.5 billion shillings* kujenga Bwawa la Nehingo, lakini halijakamilika, liko pale...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa malizia, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba na yale mabwawa sita ambayo wamejitayarisha kuyajenga, Wizara ya Maji, iende ikayakamilishe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Kavejuru Felix. Mheshimiwa Shukrani Manya, ajiandae.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kukupongeza wewe mwenyewe kwa kazi nzuri sana unayoifanya ya kutuongoza ndani ya hili Bunge, na kwa kazi nzuri sana unayoifanya huko kwenye Mabunge ya Dunia. Nawaomba Wanambeya, jamani msimwache Mheshimiwa Spika wetu, anafanya kazi ya nchi, mpeni kura nyingi sana ili aendelee kutuwakilisha kimataifa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pia, naendelea kuwapongeza Wenyeviti wote wawili waliowasilisha ripoti zao katika Bunge leo hii. Vilevile, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maji na Mazingira, naomba nitoe pongezi kubwa na kutambua mchango mzuri kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji, Jumaa Aweso na Naibu wake, Mheshimiwa *Eng.* Kundo, na Katibu Mkuu wake, Mwajuma Waziri. Tunashukuru sana Katibu Mkuu, Mwajuma kwa kweli, wamemwingiza jikoni. Hii sera anaitekeleza ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mazingira, Mheshimiwa Masauni, Naibu wake, Mheshimiwa Chillo, Katibu wake, Cyprian Luhemeja, pamoja na watendaji wote wa Wizara hizi mbili; Wizara ya Maji na Mazingira, kwa kazi nzuri sana ambayo wamekuwa wakiifanya, bila kuwasahau Mwenyekiti, Makamu na Wajumbe wa Kamati yetu ya Maji na Mazingira. Kwa kweli, wamekuwa wakishauri vizuri sana na ndiyo maana Wizara ya Maji inafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza mchango wangu, niomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa Sera ya Kumtua Mwanamke Ndoo Kichwani. Pia, nawapongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Dkt. Nchimbi na Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi wa

kule Zanzibar kwa kuchaguliwa kuendelea kupeperusha bendera ya Chama chetu cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba Watanzania wote, bila kujali itikadi ya vyama vyetu, tuunge mkono na tumchague kwa kura nyingi sana kwa kazi nzuri ambazo amekuwa akizifanya katika nchi hii. Naomba tusigombanie fito, mama anaweza na anaupiga mwingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaanza mchango wangu sasa kwa kuendelea kuunga mkono sera ya Mheshimiwa Samia ya kumtua mwanamke ndoo kichwani. Hali ya huduma ya maji vijijini hadi kufikia Desemba, 2024 idadi ya watu wanaopata maji ni 37,812,123 sawasawa na 83%. Ni vijiji 10,532 kati ya vijiji 12,318 ambavyo mpaka sasa hivi vinapatiwa maji, ambayo ni sawasawa na 36%, siyo kazi ndogo. Tunapongeza sana kwa kazi nzuri inayofanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo changamoto ambazo zinasababisha Serikali kutokufanya vizuri sana. Naishukuru Kamati yetu, imetoa sababu na changamoto nyingi sana ambazo zimekuwa zinasababisha kutofikiwa mapema au kutokumtua mwanamke ndoo kichwani kwa kata zile ambazo bado hazijafikiwa. Kwa hiyo, labda nitachangia changamoto chache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto ya kwanza ni madeni ya maji kwa taasisi za Serikali. Tumekuwa tukilizungumzia jambo hili kwa muda mrefu sana kama Kamati. Tunaomba sasa lichukuliwe kwa umuhimu wake. Kufikia Juni, 2024 deni lilikuwa shilingi 45,109,478,157, tunashukuru ilivyofika Desemba tuliongea sana angalau deni la shilingi 5,573,026,726 liliweza kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaona ulipwaji huu wa deni kama vile hauchukuliwi maanani sana, kutoka shilingi bilioni 45 zilipwe shilingi bilioni tano! Hizi taasisi ningeweza kuzitaja humu ndani, lakini kwa sababu ni Taasisi za Serikali zinajitambua, Waheshimiwa Mawaziri wapo humu, Makatibu Wakuu wanaelewa, walipe haya madeni

ili Wizara yetu ya Maji iweze kufanya kazi vizuri na miradi ya maji iweze kutekelezwa kwa wakati ili kusiwepo na changamoto kubwa katika utekelezaji wa hii miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba sasa Wizara ya Maji kupitia Mamlaka za Maji iendeleze na lile zoezi lake la kufunga dira za maji za malipo kabla ya kutumia *(prepaid meter)* hasa kwa hizi taasisi ili zisiendelee kuwa na madeni makubwa. Pia kwa wananchi hizi *prepaid meter* zifungwe ili wananchi waweze kulipa bili zao kama ilivyo *TANESCO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ambayo ipo kuhusiana na madeni ya wakandarasi wa miradi ya maji, mimi kwanza naipongeza Serikali, imeendelea kulipa madeni ya wakandarasi wetu nchini, lakini pia nitoe pongezi nyingi sana kwa Serikali ikishirikiana na Benki ya *CRDB* kwa kuanzisha Samia – *Bond*.

Mheshimiwa Spika, hii Samia *Bond* sasa tuna imani kabisa kwamba wakandarasi wetu watalipa kwa wakati na sasa miradi ya maji itakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitoe wito wangu mkubwa kwamba wananchi wote wakiwepo Waheshimiwa Wabunge wote, hebu tujiunge na hii *bond,* huu mfuko uweze kutuna zaidi ili tuendeleze kulipa wakandarasi wetu na miradi yetu ikamilike kwa wakati. Kwa sababu hii *bond* kwanza ina riba nzuri sana, hata mimi tayari nimeshajiunga, hivyo itaisadia sana Serikali yetu, wakandarasi wetu kukamilisha miradi yao kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza haya, basi namshukuru Mwenyezi Mungu na ninaomba, kwa kweli tunaenda kwenye uchaguzi tuombeane neema ili tuweze kurudi tena hapa Bungeni, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Shukrani Elisha Manya na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe ajiandae.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, nami kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Awali ya yote, nami niungane na wachangiaji wengine ambao mmeshatangulia kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupitishwa na Wajumbe wa Mkutano Mkuu kwa 100% kuwa Mgombea wa Urais, hongera sana Mama.

Mheshimiwa Spika, vile vile nampongeza na mteule, Mgombea Mwenza Dkt. Emmanuel Nchimbi. Hakika anatosha sana. Nimpongeze na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Hussein Mwinyi naye kwa kupata zaidi ya 98% ya kura kuwa mgombea wa Urais Zanzibar, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, sasa nawapongeza kwanza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yangu ya Maji na Mazingira na Mheshimiwa Makamu wake kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Sambamba na hilo, nawapongeza Wizara zote mbili ambazo tumekuwa tukishirikiana nazo tangu Januari, 2024 hadi leo Januari, 2025 nikianza na Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutupa Waziri wa Maji kijana na Makamu wa Wizara ya Maji kijana Mheshimiwa Aweso na Mheshimiwa Eng. Kundo, hongereni sana. Waheshimiwa Mawaziri hawa ni wasikivu mwanzo mwisho. Hutusikiliza, hupokea maoni na haya kwa ushirikiano mzuri na Wizara ndiyo yamechangia katika utendaji wao na maendeleo yanaonekana. Mwenye macho haambiwi tazama, miradi ya maji imesambaa katika nchi nzima, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi, niende kwenye Wizara ya Makamu wa Rais inayosimamia mazingira. Tunawashukuru kwa juhudi kubwa ambayo wameifanya hasa kwenye biashara ya *carbon* na ndipo mchango wangu utakapojikita.

Mheshimiwa Spika, biashara ya *carbon* ni fursa, ni chanzo kipya cha mapato ambacho kama tukikisimamia vizuri, kinaweza kikaleta mapato makubwa sana kwa nchi yetu na katika

Halmashauri zetu na katika vijiji vyetu. 32% ya nchi yetu ipo chini ya hifadhi za misitu na mbuga za Taifa. Biashara hii ni biashara ngeni, lakini inaonyesha kama tukiisimamia kwa umadhubuti kabisa, tunaweza tukapata pato kubwa sana. Mathalani tumeona mwaka 2024, halmashauri moja tu ya Tanganyika iliweza kupata zaidi ya shilingi bilioni 14. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa biashara hii kwetu hapa nchini ni ngeni, bado inahitaji tuone namna ambavyo tutaiendesha. Tunazo kampuni za ndani na za nje, lakini kampuni zetu, kwa wale ambao wana-*deal* na biashara hii, ambao ni wazawa kwenye biashara hii, wanafanya kazi kama *middle man.* Bado hatujawa na makampuni makubwa kutoka ndani ambayo yanaweza yakafikia masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunashauri sisi kama wanakamati, Wizara ijipange namna ya kusimamia suala hili muhimu sana ili makampuni yetu ya ndani, na kwa sababu itaongeza ajira na mapato kwa nchi, basi waweze kufikia masoko ya nje wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa ikisimamia mazingira kwa muda mrefu na tunaona jinsi ambavyo Mwenyezi Mungu ametuzawadia fursa nyingi, na rasilimali nyingi. Tunayo bahari, tunayo maziwa, tunayo misitu, tunayo mito. Haya yote yametengeneza mazingira mazuri ya nchi yetu. Tunalo Baraza la Mazingira ambalo limekuwa likisimamia juu ya uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia kwa fursa na rasilimali tulizonazo, wenzetu majirani zetu wameshasonga mbele. Sasa ni wakati ambao sasa tunatakiwa twende kwenye sheria yetu Na. 191 ya Mazingira ibadilishwe, ifanyiwe *amendment* ili iwezeshe Baraza la Mazingira kubadilika kuwa mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuwe na Sheria ambayo sasa itaenda kusimamia Sera ya Mazingira ya 2022 na Sera ya Uchumi wa Buluu 2024 pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ya pili ya mchango wangu kwenye Wizara ya Maji, niwapongeze sana, nimeshawapongeza, lakini cha zaidi nisisitize Wizara imefanya kazi moja nzuri, kubwa sana na tunaona ina changamoto ya upatikanaji wa fedha. Nawapongeza kwa kutafuta vyanzo vingine vya fedha hasa kwa kuanzisha Hati Fungani ambao mfano wake ni Tanga – *UWASA*.

Mheshimiwa Spika, mfano huu wa Tanga – *UWASA* ambao walipata shilingi bilioni 53 kwenye *green bond* yao na wakaiuza na wakapata shilingi bilioni 54, ambayo ni chanzo kipya kabisa ambacho kinaweza kikasaidia kutekeleza miradi mbalimbali ya maji bila kutegemea Mfuko Mkuu wa Serikali. Huu ni mfano mzuri na tunaiomba sasa Serikali isaidie mamlaka nyingine za maji ili ziingie kwenye matumizi, ziwezeshwe namna ya kuingia kutumia Hati Fungani ili kuweza kutekeleza miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya haya machache, naomba niunge mkono hoja kwa Kamati zote mbili, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Prof. Shukrani Elisha Manya, atafuataiwa na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, ajiandae.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja za Kamati mbili ambazo zimeweka taarifa zake za mwaka siku ya leo. Nami ni Mjumbe kutoka Kamati ya Maji na Mazingira na hivyo nitapenda kuzungumzia maeneo mawili tu katika taarifa yetu ya mwaka ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, natangulia kusema kwamba moja ya eneo ambalo Serikali yetu imefanya vizuri sana, napenda kuamini kwamba ni eneo ambao litaipeperusha vizuri bendera ya chama wakati wote, ni eneo la usambazaji maji mijini pamoja na vijijini.

Mheshimiwa Spika, taarifa yetu ya Kamati inaonesha kwamba, hadi sasa kati ya vijiji 12,318 vijiji 10,532 vimefikiwa na

huduma ya maji. Haya ni maendeleo, na ni hatua kubwa sana na kwa kweli, Wizara yetu ya Maji pamoja na mamlaka zote za usambazaji maji zinapaswa kupewa hongera na heko kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Serikali yetu imefanya vizuri sana ni katika ongezeko la nishati ambalo limetokana na kukamilika kwa mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Pamoja na kwamba siyo mitambo yote imewashwa, lakini pia na ule mradi wa Rusumo unaotoa *Megawatts* 80 na kugawanywa katika nchi wanachama watatu, hawa nao wamefanya kazi nzuri sana ya kuongeza nishati. Hao pia kwa kweli wanastahili pongezi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawaomba Wizara ya Nishati waendelee sasa na kazi kubwa kuendeleza vyanzo vingine vya nishati kama upepo, jotoardhi kule katika maeneo ya Tukuyu, nishati ya jua na hata makaa ya mawe ambayo vyote kwa pamoja vikijumuishwa, nchi yetu itapata nishati ya kutosha; na nchi inapokuwa imepata nishati ya kutosha pia huwa ni kigezo kikubwa cha hatua kubwa ya kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kujenga hoja yangu juu ya mafanikio haya katika sekta ya maji pamoja na sekta ya nishati. Tunaona kwamba pamoja na mafanikio haya makubwa, gharama za uzalishaji maji bado ni kubwa na sababu zinaleta ukubwa wa gharama katika uzalishaji maji ni pamoja na gharama kubwa za umeme, kodi ya ongezeko la thamani kwa uzalishaji huo na pia kwa vipuri, mabomba na madawa ya kusafisha maji.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni hivi, kwa sababu tumepata ongezeko kubwa la nishati, tunatamani tupate matunda ya nafuu iliyopatikana kwa sababu ya ongezeko kubwa hili la nishati katika nchi yetu. Sipo hapa kusema kwamba leo tupunguziwe gharama ya *unit* kwa kila mwananchi, huko siko ninapotaka Kwenda, lakini hoja yangu ni kwamba kwa sababu maji ni huduma, na kwa sababu maji yanapokuwa yamewafikia wananchi yanaleta furaha kwa wananchi, na ni kwa sababu pia ni kigezo chetu cha

maendeleo, tumependekeza katika Kamati yetu kwamba hebu Wizara ya Maji na Wizara ya Nishati, tunaelewa wameshaanza vikao lakini vikao vifikie mahali vikamilike na wakubaliane. Makubaliano tunayoyapendeleza ni kwamba, Wizara ya Nishati itoe bei maalumu kwa uzalishaji maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuliongea wakati uliopita, tunaendelea kuiongea tena, ni pendekezo letu la Kamati kwamba mamlaka za uzalishaji maji zipewe *special tariff* ili huduma ya maji iweze kutolewa kwa unafuu na kwa msingi huo maji yaweze kusambazwa na hatimaye tufikie malengo yetu ya kusambaza maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, gharama hizi zinapaswa zisihusishwe; kwa sababu huwa wanachaji bei inayotokana na kuwasha mitambo *KVA*, pia wanatoa na kodi ya ongezeko la thamani hapo hapo na hata kwa ile mitambo pamoja na mengine yote yanayohusu gharama za uzalishaji maji.

Mheshimiwa Spika, tulitamani kwamba *VAT* isiwe sehemu ya gharama inayochajiwa, pia gharama isichajiwe ile ya *KVA* wakati wa kuwasha mitambo. Kwa msingi huo, tunaomba Wizara ya Nishati iwakubalie, isiseme kwamba tuna hoja zetu, nasi tunatafuta fedha, hapana, tunatafuta unafuu ambao utakwenda kwa wananchi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya makubaliano baina ya Wizara ya Maji na Wizara ya Nishati, tumeweka katika mapendekezo yetu, na tunaomba yafikiwe haraka. Katika mwendo huo huo wa kupunguza gharama za uzalishaji maji, tunaiomba Wizara ya Maji iendeleze na kujiekeleza katika manunuzi ya pamoja *(bulk procurement)* ya mabomba, madawa ili kwamba iweze kufanikiwa katika kupunguza gharama za uzalishaji maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya mwisho ambayo natamani kuiongea, taarifa yetu inaonesha kwamba kumekuwa na uhujumu wa miundombinu ya maji na hasa ile mifuniko ya chuma

katika mamlaka mbalimbali za maji na mamlaka nyingine zimefikia mahali zinatafuta kuweka mifuniko ya zege ili kuepuka kuibiwa ile miundombinu ya chuma.

Mheshimiwa Spika, sasa hawa wanaoiba mifuniko ya chuma baada ya miradi kuwa imekamilika, wanaipeleka katika chuma chakavu. Katika mwendelezo wa biashara ya chuma chakavu ndiyo hao hao wanaoiba mafuta vya *transformer*, ni hao hao ambao wanakwenda kuvuta nyaya za *SGR,* ina maana hawa watu wanaturudisha nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi inakamilika, anaiba mifuniko ya chuma; miradi inakamilika anavuta nyaya ya *SGR;* hawa wanaturudisha nyuma. Maana yake hawafurahi kuona wananchi wanafurahia na kupata raha ya maendeleo yanayotokana na Serikali yao. Hawa sio wa kuvumiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pendekezo letu katika Kamati, tumesema kwamba, Wizara ya Nishati, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi wakae Pamoja, waje na mkakati wa pamoja wa kudhibiti wizi wa miundombinu katika sekta hizo. Pia wanapokuwa wamekamatwa hawa watu, tunaamini kwamba Wizara tano zikikaa haziwezi zikakosa njia ya kudhibiti wizi wa miundombinu. Udhibiti huu pia uelekezwe katika biashara ya chuma chakavu hapa nchini, kwa sababu ndiko wanakojificha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini kwamba watakapokuwa wamefanya hivyo, biashara ya chuma chakavu itadhibitiwa, pia tutakuwa tumedhibiti uhujumu wa miundombinu yetu katika Wizara ya Maji, katika Wizara ya Uchukuzi pamoja na Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, na ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, akimaliza Mheshimiwa Anna Richard Lupembe na Mheshimiwa Kasalali

Emmanuel Mageni, kwa sababu nilikuwa nimewataja kabla, Wabunge watakaofuatia hapo na wale walioomba nafasi kwa upande wa Serikali, watachangia kwa dakika tano.

Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni. Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi ajiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa naomba nimshukuru Mungu ambaye ametupa uzima na uhai, leo tupo mahali hapa kwa ajili yake.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nichukue fursa hii kukupongeza sana kwa kazi kubwa unayoendelea kuifanya na kusimamia majukumu ya Bunge. Vile vile una majukumu mengine ya dunia, unasimamia vizuri, unatufundisha sana, sana. Maana leo unakuta uko huko, lakini kesho uko Bungeni. Unatufundisha, tunapata somo kubwa kutoka kwako. Mwenyezi Mungu akusimamie kwa haya majukumu, nasi kazi yetu ni kuendelea kukuombea ili Mungu aendelee kukuimarisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii ya kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa Mgombea wa Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi, na Mgombea Mwenza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi. Vilevile naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Mwinyi kwa kuwa Mgombea kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi kwa upende wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri wetu wa Maji Mheshimiwa Jumaa Aweso kwa kazi kubwa na nzuri, pamoja na Naibu wake, wanafanya kazi kubwa sana kupitia miradi mbalimbali ya maji. Tusimsahau Katibu Mkuu wa Wizara Eng. Mwajuma, Naibu wake, pamoja na Menejimenti yote ya Wizara kwa kazi kubwa. Tusiwasahau pia Watendaji wakuu wa RUWASA pamoja na Mfuko wa Maji kwa kazi kubwa

wanayoendelea kuifanya. Tunaona jitihada zao, wanafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo yetu ya Kamati, naomba nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote wa Kamati yetu ya Maji na Mazingira kwa kazi kubwa ya kuendelea kuchambua utekelezaji wa Ilani ya mwaka mzima wa Wizara zote mbili; Maji pamoja na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, naenda kwenye kipengele cha magari. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kurahisisha kuwa magari yananunuliwa katika mikoa yote nchini, kuhakikisha visima vya maji vinachimbwa wakati wowote na muda wote. Naomba niipongeze Wizara kwa usimamizi wake pamoja na RUWASA ambao ndiyo waliopewa majukumu makubwa ya kuhakikisha kwamba visima vinachimbwa katika maeneo yetu ya vijiji pamoja na vitongoji katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi ni nzuri na Mheshimiwa Rais alinunua magari haya kwa ajili ya kuhakikisha kuwa Watanzania wote na akina mama wanatuliwa ndoo kichwani. Ni jitihada kubwa ya Mheshimiwa Rais, lakini kutokana na mfumo ambao ulikuwepo wa bajeti, kidogo hatuunganishi bajeti pamoja na visima.

Mheshimiwa Spika, visima vinachimbwa, lakini vinakaa muda mrefu ndipo vinakuja kujengwa na wananchi kupata maji. Sasa tunavyochimba vile visima tunawapa matamanio wananchi. Maji yanatoka kwa wingi, lakini yanafunikwa na tunakaa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba niishauri Serikali kuwa sasa hivi twende sambamba; uchimbaji wa visima na bajeti kwa sababu tunachimba visima, halafu tunakuwa hatuna bajeti, hatimaye tukipata bajeti yake ndiyo tunajenga miundombinu.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali kwamba sasa hivi twende kwa bajeti pamoja na kisima. Tukichimbe kile kisima na tukijenge ili yale matarajio ya wananchi yaweze kutimia. Vile

vile, ile hatima ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama iweze kutimilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya kupitia Wizara ya Maji. Wanafanya kazi kubwa, wanahakikisha usiku na mchana wanatafuta fedha kuhakikisha ile miundombinu inatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Mkurugenzi wa Mfuko wa Maji. Tuna Mfuko wa Maji ambao tunautegemea sana, lakini ule Mfuko wa Maji, fedha inayokusanywa na matarajio ya kwenda kwenye mfuko ni fedha ambayo haikidhi mahitaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukusanyaji mzuri ambao Serikali inaendelea kukusanya kupitia *TRA,* tulikuwa tunaomba kupitia yale malengo ambayo yalikuwa yamekadiriwa kupelekwa kwenye mfuko wa maji, yapelekwe ili ule mfuko uweze kufanya kazi vizuri, wakandarasi wetu waweze kulipwa na mambo yote yaweze kufanyika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina Wizara mbili, naomba nimpongeze sana Waziri wetu wa Mazingira, Mheshimiwa Masauni, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Menejimenti yote ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kwa kazi kubwa nzuri ambayo wanaifanya, na leo hii tumeona jitihada kubwa ya Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Mazingira; jitihada ambayo itawezesha sheria kubadilishwa na kuboresha sekta mbalimbali za mazingira kule ambako kulikuwa kuna tofauti, au ambako mwenendo ulikuwa siyo mzuri. Kutokana na hii sheria itakayokuja, tutapata mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona na mapitio ambayo Waheshimiwa Wabunge wamesema kwenye *carbon,* hewa ukaa ambako hakukuwa na sheria, lakini tunatamani sheria ikija ielekeze ili mambo yaweze kuwa vizuri. Naomba tumpongeze sana Mheshimiwa Waziri Masauni kwa kutuletea sheria ambayo itakuja humu Bungeni kuhakikisha tunaboresha zaidi.

Mheshimiwa Spika, nisiache kuzungumzia Wizara ya Maliasili. Mimi nina mbuga kule ya Katavi. Naomba nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili kwa kazi kubwa na nzuri anayoendelea kuisimamia Kamati, lakini nilikuwa naomba nimpongeze Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Pindi Chani.

Mheshimiwa Spika, Mbuga yetu ya Katavi bado haijatangazwa vizuri. Mbuga hii kwa sababu ni kubwa na ina wanyama wakubwa, tukiitangaza vizuri tutapata mafanikio makubwa sana. Tunaona jitihada za Mheshimiwa Rais, alitangaza nchi yetu kupitia utalii, na leo tunaona manufaa makubwa. Sasa naomba Wizara itangaze utalii wa mbuga ya Katavi ili tuweza kuendelea kupata mafanikio makubwa ya mapato katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja ya Kamati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, Mheshimiwa Angelina Mabula ajiandae.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na uzima.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema sana, nikipongeze Chama cha Mapinduzi kwa mkutano bora kabisa kuwahi kutokea na ambao umeonesha ni namna gani Chama cha Mapinduzi kimejipanga kuendelea kuwaongoza Watanzania na kuwatumikia.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, na Mgombea Mwenza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi kwa kuteuliwa na Mkutano huo bora kabisa wa CCM kuipeperusha Bendera ya Chama cha Mapinduzi. Pia nampongeza Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kwa kuteuliwa kwa kishindo na Mkutano huo

kupeperusha Bendera ya Chama cha Mapinduzi kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niko kwenye Kamati ya Maji na Mazingira, lakini kabla sijasema sana kwenye Kamati ya Maji na Mazingira, katika Kamati zote zilizowasilisha leo, Wenyeviti wameonesha umahiri mkubwa sana. Mheshimiwa Mnzava na Mheshimiwa Kiswaga wamewasilisha vizuri maoni ya Kamati zao; na kwa kweli hiyo ni dalili njema ya kwamba viongozi ndani ya Chama cha Mapinduzi ni wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Waziri wa Ardhi, ndugu yangu Mheshimiwa Deo. Nilimwona pale anateta na Mheshimiwa Jerry Silaa; najua amepokea kijiti kutoka kwake. Mazuri aliyoyafanya Mheshimiwa Jerry Silaa bado anaendelea kuyafanya, na kazi anaifanya vizuri sana. Mungu ambariki, aendelee kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwenye michango ya Kamati niliyomo ya Maji na Kamati ya Mazingira. Tunayo mambo mengi ambayo tumeyazungumza hapa. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya kwenye sekta ya maji na mazingira, lakini yapo mambo ambayo nilitamani Bunge hili sasa tuyajadili na tuishauri Serikali namna ya kuyafanya yawe mazuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, historia inaonesha Kamati imekuwa ikiishauri Serikali zaidi ya mara tatu hadi mara nne kuhusu Mamlaka ya Mazingira, kuhusu *NEMC* kuwa mamlaka kamili. Kamati imekuwa haishauri jambo hili, kwa bahati mbaya, imekuwa ikilishauri kwa makusudi kwamba tupate mamlaka ambayo itasimamia mazingira kwa ubora na bila kuingiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira ni jambo la muhimu sana, lakini kwa bahati mbaya tumekuwa tukilichukulia poa, tunachukulia kama jambo la kawaida, lakini mazingira ni jambo ambalo linahusu uhai wetu na usalama wa nchi yetu, na ni jambo

ambalo tusipolipa ukubwa wake na umuhimu wake tunaweza tukaishia pabaya sana. Sasa naomba kupitia nafasi hii kuishauri Serikali ielewe kwamba upo umuhimu wa kuja na sheria nzuri ambayo inaifanya *NEMC* kutoka kuwa chombo tu cha kuzungumza kuhusu mazingira, sasa kiwe chombo chenye mamlaka kamili inayosimamia mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuwa na *NEMC* ambayo, na sisi sote ni mashahidi. Mimi sijakuwepo muda mrefu lakini nilikuwepo; wakati ninakua kulikuwa kuna vitu vinaitwa *night clubs.* Wakati nasoma *UDOM* hapa tulikuwa tunaenda *Club Fifty-Four, Club* la Aziz, *Club Seven*; yaani ukitaka kwenda *Club* unakwenda kwenye chumba ambacho kimefungwa, unapigiwa kelele wewe mwenyewe mwenyewe mle, ukimaliza unatoka nje.

Mheshimiwa Spika, tumebadilika ghafla kutokana na kutokuwa na mamlaka, na sasa hivi *clubs* ziko nje. Yaani mtu akiamua kupiga muziki, anapiga muziki mpaka asubuhi, na majirani wote hamlali, na yeye halali. Sheria ipo, lakini kwa sababu *NEMC* haina meno, leo inafunga *club*, kesho Mkuu wa Wilaya anasimama anafungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakuwa tunatengeneza Taifa la watu ambao hawalali; watu ambao siyo kwamba hawalali kwa sababu wamekwenda *club,* ila hawalali kwa sababu kuna watu wameamua wasilale, na nchi ipo, na mambo yapo. Sisi tunawaambia tengenezeni *NEMC* ambayo ita-*regulate* hivi vitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, duniani kote haya mambo yanasimamiwa vizuri. Hatuwezi kuwa na nchi tunasema kwamba tuna miji mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza kuna uchafu tunaukusanya. Yale magari yanayobeba uchafu na yenyewe ni uchafu.

Mheshimiwa Spika, nafikiri wote ni mashahidi na mnaona. Yaani suala la mazingira tunalichukulia poa. Ni lazima tupate

mamlaka kamili inayosimamia suala la mazingira. Nadhani nchi yetu itakuwa na nafuu sana kuanzia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwenye suala la maji. Mimi naweza kuwa shahidi dhahiri wa mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita kwenye suala la maji. Mimi ni Mbunge wa Sumve, ninatoa mfano wa Sumve ili tuelewane vizuri. Mimi Mbunge wa Sumve kabla Mheshimiwa Dkt. Samia hajawa Rais wa nchi yetu, kulikuwa kuna vijiji sita tu kati ya 60 kwenye Jimbo la Sumve ambavyo wananchi walikuwa wanaweza wakaenda kwenye bomba wakafungua maji yakatoka.

Mheshimiwa Spika, leo ninapozungumza, vijiji ambavyo tukienda tunafungua maji yakatoka viko 26 ndani ya huo muda mfupi. Vijiji ambavyo wakandarasi wako *site* ili na vyenyewe tufungue maji, acha kupampu hivi, kufungua, ambavyo wakandarasi wako *site* na wanaendelea na kazi ni vijiji 13. Kwa hiyo, ukiangalia katika muda huu kutoka vijiji sita mpaka 39 ni mafanikio makubwa sana ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unakumbuka nilisimama hapa nikasema Jimbo la Sumve liko Mkoa wa Mwanza, lakini ni jimbo pekee ambalo ladha ya maji ya Ziwa Victoria hatuijui. Hivi ninavyozungumza ipo miradi miwili; mradi wa kwanza una thamani ya shilingi bilioni 32, uko 30%, utekelezaji unaendelea. Mheshimiwa Rais ametupa shilingi bilioni 32 sisi watu wa Sumve. Mradi wa pili Mheshimiwa Rais ametoa shilingi bilioni 20.5 na wenyewe uko 25% ya utekelezaji, ni hatua kubwa sana kwenye sekta ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Aweso, Naibu wake mdogo wangu Mheshimiwa Eng. Kundo pamoja na Katibu Mkuu Mwajuma, wanamsaidia vizuri sana Mheshimiwa Rais kwenye sekta ya maji. Wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, ambacho nataka niiombe Serikali ili tuendelee na hatua hii na mafanikio haya, kwanza fedha za

mfuko wa maji zisichezewe, yaani fedha ya Mfuko wa Maji iende kwenye maji ili miradi ya maji iende vizuri. Vilevile tuongeze fedha kuwalipa wakandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii miradi mingi ya maji pia kwa asilimia kubwa kwa sababu ndiyo mingi, imechangia sana kufilisi wakandarasi wazawa wa Kitanzania kwa sababu wakandarasi wanakwenda kujenga miradi, wanakomea kuikopesha Serikali na inawalipa baada ya miaka kadhaa, wakati huo huo wana mikopo kwenye mabenki, wanadaiwa riba.

Mheshimiwa Spika, sasa ni wakati Serikali, fedha ya maji ipewe kipaumbele na bajeti ya maji inapopitishwa na Bunge lako Serikali itekeleze kama tulivyoelekeza; na fedha Mfuko wa Maji tunayoitunza ambayo inaelekezwa inatoka wapi na ikatumike na na kadhalika, iendelee kutumika inavyopaswa. Vinginevyo, tunaweza kupunguza *speed* ya Mheshimiwa Rais ya kuwaangalia Watanzania kwenye suala la maji, ambayo imeonekana dhahiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya mazungumzo hayo, naomba kuunga mkono haoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi atafuatiwa na Mheshimiwa Angeline Sylivester Mabula, na Mheshimiwa Haji Makame Mlenge ajiandae; na hao watakuwa wakichangia kwa dakika tano.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia taarifa za Kamati hizi mbili. Niungane na wenzangu kuwapongeza Chama cha Mapinduzi kwa kufanya maamuzi ya busara na makini kabisa ya kuwapitisha wagombea wetu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kwa kura 100% kuendelea kuwatumikia wananchi wa nchi hii. Vile vile nampongeza Mgombea Mwenza, Mheshimiwa Balozi Dkt. Nchimbi kwa

kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kwa kuteuliwa kuwa Mgombea wa Urais Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mawaziri wa Wizara hizi zote mbili, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote ambao wamesababisha haya mazuri tunayoyaongea katika Wizara hizi; Wizara ya Ardhi, Maliasili, na Maji kwenda vizuri kama ambavyo wote tumeona Wizara hizi zimefanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kuipongeza Wizara ya Maliasili kwa kuendelea kuboresha mapato, lakini kuendelea kutimiza lengo la watalii. Wote tumejionea, sasa tumefika lengo la watalii milioni 5.3 kuingia nchini. Hii ni kwa sababu ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia picha ya *Royal Tour;* amekuwa kinara wa utalii na matokeo tumeyaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona Wizara hii inachangia pato la Taifa kwa 22.5%, kwa kuingiza Dola za Kimarekani bilioni 3.6 kwa mwaka. Haya ni mafanikio makubwa sana, hatupaswi kuyafumbia macho, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, nitatoa ushauri kidogo kwenye Wizara hizi. Wote tunafahamu umuhimu wa kupanga matumizi bora ya ardhi ya vijiji vya nchi hii. Kupitia taarifa ya Mwenyekiti wetu makini, Mheshimiwa Timotheo Mnzava, mmeona vijiji 65% bado havijafanyiwa mipango ya matumizi bora ya ardhi, hali inayochangia migogoro ya ardhi kwenye mipaka ya vijiji, mipaka ya wilaya, lakini migogoro ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi imepokea shilingi bilioni tano kwa ajili ya fedha za maendeleo, ambayo ni 42% tu ya pesa ambazo walizitegemea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali iendelee kupeleka fedha kwenye Tume ya Mipango, ili iweze kupanga vijiji vya nchi hii, 65% ambayo bado.

Mheshimiwa Spika, Tume hii inahitaji shilingi bilioni 120 tu kuipanga nchi nzima. Kwa hiyo, naomba niishauri Serikali iipelekee Tume shilingi bilioni 120, ili vijiji vyetu viweze kufanyiwa mipango ya matumizi bora ya ardhi, ili kuepusha migogoro hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, tunayo programu ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kupitia Wizara yetu ya Ardhi. Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa shilingi bilioni 50 kwenye halmashauri 57 ili ziweze kufanya mpango huo.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha kabisa, fedha zile zilitakiwa zirejeshwe. Fedha hizi zimetolewa mwaka 2018, lakini ni zaidi ya miaka sita sasa halmashauri hizi hazijaweza kurejesha fedha. Halmashauri zilizorejesha ni halmashauri 17 tu. Tunaiomba Wizara ya TAMISEMI isimamie halmashauri hizi ili ziweze kurudisha hizi fedha. Kiasi cha shilingi bilioni 22.5 bado hakijarudishwa.

Mheshimiwa Spika, hizi fedha ni kwa ajili ya kurudi kwenye mfuko ambao uliandaliwa na Wizara ili ziwe zinazunguka, ili sasa halmashauri zote ziweze kupimwa. Tunaomba TAMISEMI itusaidie, tukishirikiana na Wizara ya Ardhi fedha hizi ziweze kuja, kwa sababu kwa kweli Wizara hii jukumu lake kubwa ni kupanga na kupima ardhi yetu, na bila fedha hawataweza. Kwa hiyo, fedha hizi shilingi bilioni 22 zirudishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa Serikali iangalie Wizara yetu ya Ardhi iweze kuipatia fedha ili iweze kupanga nchi hii na kupunguza migogoro, ili Mawaziri badala ya kushinda na kutatua migogoro, basi waendelee kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naounga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Mabula, atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Makame Mlenge. Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi ajiandae.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, kwa dakika hizi zilizopunguzwa, naomba Mungu anijaalie angalau niweze ku-*cover* machache niliyokuwa nimepanga kuyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono mada zote mbili, au hoja zote mbili zilizoko Mezani. Nawapongeza Wenyeviti, wamefanya kazi nzuri pamoja na Wajumbe wao. Pia, naomba kupongeza Wizara zenyewe husika, ambazo zinahusika kwa kazi nzuri walizofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la changamoto ambazo zimeonyeshwa na Kamati ya Ardhi na Maliasili kwamba, pengine wanashindwa kufikia bajeti zao walizowekewa katika utendaji kutokana na mwingiliano wa kazi kama ambavyo imeonyeshwa na Kamati yenyewe.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi pamoja na TAMISEMI kuna mwingiliano mkubwa katika suala zima la utendaji. Matokeo yake sasa inakuwa ni ngumu, nani umkamate, nani ambaye amefanya vibaya, na nani kafanya vizuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mchakato wa kugatua madaraka, hasa pale walipofanya kwenye Wizara ya Maji, wakaanzisha *RUWASA*, na kwenye miundombinu *TARURA* ikatengwa peke yake, na ardhi ilitakiwa kuwa pia imetengwa kwa ajili ya kuwa na Wakala atakayesimamia Sekta ya Ardhi mwanzo mwisho, na mchakato ulikuwa umeshaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani tunafikiria pengine Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi ingeweza kuongezewa majukumu, na ikapewa jukumu hilo la kuhakikisha ardhi ya nchi hii inasimamiwa vizuri, kwa sababu Tume inafanya vizuri. Watalaamu walikuwa wanafanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Serikali iangalie suala zima la kugatua madaraka katika suala zima la usimamizi wa ardhi, na kuweka Wakala atakayefanya kazi nzuri kama wanavyofanya

*TARURA* pamoja na Maji, kwa sababu Serikali tayari ilishatoa Waraka wa kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili lilikuwa ni hatua nzuri ya kuwa na ule Mradi wa Uboreshaji wa Usalama wa Milki, ambapo nasikitika kwamba mradi huo umesimama. Mradi huo ulikuwa unakwenda kuimarisha hasa miundombinu katika idara nzima, au Wizara nzima, kuanzia wilayani, mikoani, na mpaka Taifa, lakini naona kama mradi ule umeondolewa, pamoja na kusitishwa kwa kurasimisha viwanja 1,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale tulikuwa tunakwenda kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuwapa umiliki wa maeneo yao. Sasa unapositisha maana yake mwananchi huyu alishajenga bila utaratibu, lakini tulimwachia akajenga mpaka akafikia hapo alipo. Leo hii anataka kumilikishwa ili angalau hata katika uboreshaji awe na kitu ambacho atasimama nacho. Leo tunasema wasiwezeshwe hivyo. Kwa kweli katika kusimamisha miradi ile ni makosa makubwa ambayo sijui kwa nini ilifanyika hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia watu tunakwenda katika halmashauri zetu. Tunaangalia Idara za Ardhi jinsi zilivyo na ofisi duni katika utendaji, ukiacha zile ambazo wamejenga majengo, lakini unaingia kwenye ofisi mpaka unasikitika. Chumba kimoja wamekaa watu saba au nane, halafu leo tunasema wasijengewe ofisi, na pesa ilikuwa imepatikana. Hata nyaraka nyingine zinapotea kwa sababu ya namna ya kulundikwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba ku-*declare interest* kwamba wakati niko Wizarani tulikwenda Tabora. Tulikuta wamekaa kwenye chumba kimoja kama *corridor*, na mafaili yamejaa mle. Kutafuta tu faili la mtu mmoja linachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, sasa kama leo tunasema hatuwezi kuwapa nafasi ya miundombinu wakawa na ofisi nzuri, sijui tunataka nini kifanyike pale? Nadhani katika hilo tumekwenda vibaya katika suala zima la kuwawezesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mradi wa KKK ambao ulikuwa umepangwa, Kupima, Kupanga na Kumilikisha, nao naomba pia tuangalie vizuri. Serikali iangalie namna ambavyo pesa za Serikali zinatoka. Mwaka 2018/2019 zilitoka zaidi ya shilingi bilioni sita kwa halmashauri 24, lakini zilizokamilisha kulipa ni halmashauri 13 tu. 10 zote hazijalipa, na moja haijalipa kabisa. Halmashauri ya Nzega haijalipa hata senti tano. Sasa sijui wana mpango gani? Maana yake zile fedha zingeweza pia kwenda kwa wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zile pesa zinakuwa ni *seed money* kwao, lakini ukizitumia vizuri unaweza ukajikuta umepima wilaya yako kwa 100%, kwa sababu zinazalisha fedha nyingi kuliko hata maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2021/2022 zimetoka shilingi bilioni 50 kwa halmashauri 57. Kati ya hizo ni halmashauri 19 tu zimelipa 100%; halmashauri 38 zimelipa nusu, nyingine hazijalipa. Kama fedha ya Serikali inatoka kwa utaratibu huo, halafu hairudishwi, na mpango wa Serikali ni kuhakikisha nchi nzima inapimwa, sasa kwa *style* hii hatuwezi kumaliza.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme, kama fedha hizi zikitumiwa vizuri, ni mradi mmoja mzuri ambao unawezesha kupima ardhi hii kwa haraka sana. Naweza kutolea mfano wa wilaya ninayotoka, Manispaa ya Ilemela. Hii imebakiza kama 12% kuipima kwa 100%, kwa sababu ya kuwezeshwa na Mfuko huu, na walilipa kwa 100% na halmashauri nyingine zilifanya vizuri. Kwa hiyo, nasema mradi huu usimamiwe vizuri ili uweze kuona ni jinsi gani ambavyo tunaweza tukaipima ardhi hii. *(Makofi)*

*(Hapa, kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, upande wa Tume ya Matumizi ya Ardhi, naomba kusema wamefanya kazi vizuri.

**SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ni ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilifikiri ya kwanza. Ahsante, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi. Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo ajiandae.

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuweza kunipatia nafasi hii. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupatia uzima wa kuweza kufika katika Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawapongeza viongozi wetu wakuu wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Samia, Dkt. Nchimbi na Mheshimiwa Dkt. Hussein, kwa kuteuliwa kwao. Hii inaonyesha wazi kwamba wamefanya kazi ipasavyo, na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wakaridhika kwa kazi yao ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba Watanzania, kazi zao zinaonekana, hazikujificha, wawaone na wawatambue, ikifika mwezi wa Kumi mwaka huu wawape tu kura zote za Ndiyo viongozi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepata bahati ya kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Maji na Mazingira. Kwa hiyo, niseme tu kwamba, Kamati zote ambazo leo zimeweka ripoti zao za mwaka, naunga mkono hoja zote ambazo zimezungumzwa na Kamati zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na kusema bajeti ndogo ya Wizara ya Maji. Maji ni uhai. Maji ni muhimu sana katika shughuli zetu za siku zote. Maana yake hakuna siku ambayo utakosa maji ukafurahi. Maji yanatakiwa kupatikana kila siku, lakini bajeti ambayo inatengewa na Serikali ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka 2024/2025 haikuridhisha, na tulisema sana wakati wa bajeti. Kwa hiyo, tunaikumbusha Serikali mapema, kuona Bajeti ya mwaka 2025/2026 iweze kutimiza angalau zile ndoto za Wizara na Kamati.

Mheshimiwa Spika, sisi Kamati tunaishukuru sana Wizara kwa sababu inafanya kazi kubwa sana. Kwa ushauri wangu, kipindi hiki wapewe fedha nyingi ili tuwaone wanafanya kazi zaidi, kwa sababu muda ambao wanafanya kazi hautoshi kutokana na fedha wanazopewa. Tuwape fedha nyingi ili watimize shughuli ambazo wamepangiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kulionyesha hili, nimekuja na bajeti za miaka mitatu, kuonyesha kwamba badala ya kuwa tunaenda mbele, bajeti iongezeke, lakini bajeti imepungua. Tukiangalia mwaka 2022/2023, bajeti ya maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 657.9. Bajeti ya maendeleo ya mwaka 2023/2024 ilikuwa shilingi bilioni 695.8. Bajeti ya mwaka 2024/2025 ilikuwa shilingi bilioni 558. Hapa imepungua, na mahitaji yameongezeka *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inaongezeka mahitaji kila siku. Watu wanaongezeka kila mwaka, maana yake bajeti iweze kuongezeka. Tunapokwenda kupunguza bajeti, maana yake hatujawafanyia vizuri wananchi; kwa sababu wananchi wanaongezeka, lakini sisi tunapunguza bajeti. Kwa hiyo, tunashauri bajeti ya mwaka 2025/2026 iongezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia suala la upotevu wa maji. Suala hili limezungumzwa na wadau wenzangu, lakini suala la upotevu wa maji, mara nyingi yanapotea katika mitazamo miwili tofauti. Kuna ule wa kibinadamu ambao watu wanatumia maji isivyo halali, lakini kuna ule wa miundombinu, ambayo yote ukiiangalia inarudi nyuma kwenye bajeti ndogo.

Mheshimiwa Spika, unapokuwa na bajeti ndogo, na huku una miundombinu chakavu, maana yake huwezi kwenda kutatua matatizo ya miundombinu chakavu. Kwa hiyo, maji yanapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitazama upotevu wa maji unavyotakiwa Kitaifa na Kimataifa, maana yake usizidi 20%, lakini leo maji yanapotea kwa 36.2%. Maana yake maji yanapotea kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah. Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso ajiandae.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuchangia mada iliyopo Mezani. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, na leo tuko hapa Bungeni. Napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kuwa mgombea pekee wa Chama cha Mapinduzi. Pia, nampongeza Mgombea Mwenza, Mheshimiwa Balozi Dkt. Nchimbi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nirudie kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kupata tuzo ambayo inaitwa *The Gates Goal Keeper Award*, ambayo ni tuzo pekee iliyotolewa kwa huku Afrika. Hongera sana kwake Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote wa sekta zote, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Kitandula, pia Wizara ya Ardhi, Mheshimiwa Ndejembi, pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Geofrey Pinda, pamoja na watendaji wote wa Wizara zote, Maliasili na Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, ninayo mambo ya kuchangia. Tumeona jinsi gani *Royal Tour* ambayo ilifanyika Tanzania chini ya Mheshimiwa Rais, ilivyoweza kuleta watalii wengi nchini Tanzania. Tumekuwa na watalii wengi, wamependa kuja

Tanzania kwa sababu Mheshimiwa Rais ameitangaza nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo ni ukosefu wa vitanda, nikiwa na maana ya malazi. Malazi siyo ya kutosha nchini Tanzania, hasa kwenye mbuga zetu. Hivyo basi, inasababisha ukosefu wa vyumba vya kutosha, hasa kwenye mbuga zetu ambazo watalii wanapenda kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilibinafsisha hoteli takribani 23 nchini Tanzania, mwaka 1992, ilipokuwa na Sera ya Ubinafsishaji. Katika hoteli hizo, hoteli 17 zilikuwa zinamilikiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwa hiyo, utaona ni jinsi gani hoteli hizo zingekuwa bado zinamilikiwa na Wizara hii, zingeweza kuisaidia nchi yetu kupata malazi kwa wageni ambao wameongezeka sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maazimio ya Kamati, azimio mojawapo ni kurudisha hoteli ambazo zilibinafsishwa kwa wabinafsishaji ambao hawajatekeleza masharti ya ubinafsishaji. Hoteli hizo ni nyingi.

Mheshimiwa Spika, ziko hoteli pamoja na *lodge* ambazo ziko mbugani, na nyingine kama vile ziko Serengeti, ziko Ngorongoro, na pia nyingine ziko Dar es Salaam. Mfano, Hoteli ya *Embassy* haijafanya kazi toka mwaka 2008. Takribani miaka 17, moja kwa moja unaona kwamba mwekezaji huyu hawezi kujenga tena hiyo hoteli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, sioni haja ni kwa nini Serikali inashindwa kuzirudisha hoteli hizi mikononi mwake kwa sababu, moja kwa moja, hata kama una nyumba yako, mpangaji akishindwa kukulipa kodi, nadhani unachukua jukumu la kumtoa kwenye nyumba yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii ni suala la kuboresha miundombinu iliyoko kwenye hifadhi zetu, ambazo

wageni wanakwenda. Ukifika kule Serengeti kipindi cha mvua zinapokuwa zinanyesha, madaraja yale ni madogo, miundombinu ni mibovu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iongeze bajeti, lakini iweze kufikiria sula la kuboresha miundombinu yetu iliyoko kwenye uhifadhi ili wageni wetu wanapokuja wasikwame kipindi cha mvua. Wizara ya Maliasili na Utalii inao uwezo wa kuingiza watalii wengi nchini, kama itarekebisha miundombinu kwenye hifadhi zote, lakini pia kama itaongeza vitanda vya malazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye Wizara ya Ardhi. Wizara ya Ardhi imefanya kazi katika kuhakikisa wananchi wanapata milki kwenye baadhi ya maeneo. Wizara ya Ardhi ilijenga mfumo wa kuwawezesha wananchi kupata bili zao kwenye simu. Mfumo huu haujafanya kazi vizuri, na iko kwenye Maazimio ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfumo huu umefanya kazi kwa 10% tu. Katika halmashauri 184 zilizoko nchini Tanzania, Wizara ya Ardhi imeweza kufunga mfumo kwa 10.6% tu. Kwenye bajeti yake ya mwisho ilisema kwamba mpaka kufika mwaka 2024 ingekuwa imefunga mifumo kwenye halmashauri zote. Naona suala hili linakwenda taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini *TANESCO* wanaleta bili mkononi? Kwa nini Wizara ya Maji imeweza kufunga mfumo, na tunapata bili kwenye simu zetu? Kwa nini Wizara ya Ardhi mnashindwa kufunga mfumo wananchi wapate bili kwenye simu zao? *(Makofi)*

*(Hapa, kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ...

**SPIKA:** Kengele imeshagonga.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, haya ahsante. Nakushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Soud Mohamed Jumah atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, ajiandae.

**MHE. SOUD MOHAMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia ripoti za Kamati zetu mbili hizi. Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na ripoti ya Maji na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, nitajikita zaidi katika ripoti ya Kamati ya Maji na Mazingira, na nitaanza na Mazingira. Kwanza, nakushukuru na nawashukuru Wenyeviti kwa kuwasilisha vizuri ripoti zote. Hata hivyo, napenda vilevile kuwashukuru sana Watendaji wa Wizara hizi mbili zikiwemo Wizara ya Maji na Mazingira pamoja na Wizara ya Mazingira kwa ujumla, wamefanya vizuri sana katika uwasilishaji na utayarishaji wa kazi ambazo zimesababisha sisi kuandika ripoti hizi mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza tu, Mheshimiwa Mwenyekiti amezungumza hapa kuhusu masuala ya maazimio ambayo yamefanyiwa kazi na yale ambayo hayakufanyiwa kazi vizuri. Sasa nitajikita zaidi katika maazimio ambayo hayakufanyiwa kazi, na Azimio hili moja kubwa ambalo halikufanyiwa kazi, ni Azimio la kuifanya *NEMC* kuwa mamlaka.

Mheshimiwa Spika, hili ni agizo la Bunge lako Tukufu hapa na tulikaa kwa pamoja na tukakubaliana kwamba kutokana na changamoto za kimazingira, ambazo hivi sasa zinaathiri nchi yetu, basi ni vyema *NEMC* itoe neno ili iweze kufanya kazi vizuri. Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri alikuja hapa na akaahidi japo siyo Mheshimiwa Waziri huyu ni yule ambaye ameondoka.

Mheshimiwa Spika, hivyo, aliahidi kwamba katika marekebisho makubwa yanayokuja ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, basi suala la *NEMC* kuwa mamlaka litazingatiwa. Kwa

hiyo, tunategemea sana kwamba sheria itakayokuja, basi italizingatia hili.

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima la sheria hizi ambazo zimekuja kurekebishwa na kuweza kuzisaidia hizi kampuni za kufanya wa *Environmental Impact Assessment* kuweza kuwa na masharti ambayo yatazingatia uwepo wao.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna shida ambayo vilevile imejitokeza kwa sababu makampuni ambayo hapo mwanzo yalikuwa yamesajiliwa kuweza kufanya kazi za *Environmental Impact Assessment,* mengi yao kutokana na masharti ambayo yameletwa, yamefanya kwa kiasi fulani, yasiweze kuzingatiwa, na hili limesababisha kusitisha baadhi ya kampuni, ikiwa ni pamoja na vyuo vikuu ambavyo vina wanafunzi wanaofanya kazi katika makampuni hayo kwa ajili ya kufanya tathmini ya athari ya mazingira *(Environmental Impact Assessment)*.

Mheshimiwa Spika, naomba tu kwamba, kwa sababu ilikuwa ni takwa la Azimio kwamba waje na kanuni wazipitie, kanuni ambazo zina ukakasi na zinakwamisha makampuni haya kufanya usajili, basi naomba sana Mheshimiwa Waziri zile kanuni ambazo zilikuwa zimeainishwa na Bunge na zikaonekana zina ukakasi na mpaka leo hazikufanyiwa marekebisho, basi zikafanyiwe marekebisho ili turuhusu hizi kampuni hasa za Vyuo Vikuu na zile kampuni ambazo vijana wetu ndio wanatafuta ajira kutokana na shughuli hizi, basi waweze kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala zima la hii Sheria yenyewe ya Usimamizi wa Mazingira ambayo vilevile ilikuwa ni miongoni mwa maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, pia tulitegemea kwa sababu imeshasomwa kwa mara ya kwanza, hivyo, tunategemea itakapokuja, hapa vilevile itazingatia yale mambo muhimu ambayo Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba yatakuwemo katika hii sheria.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, ni suala zima la kufanya uratibu wa hewa ukaa au *carbon* itazingatiwa kwa kuwa na Mamlaka ya hewa ukaa, hili nafikiri litazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi. Kuna Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi ambao upo sasa hivi, lakini hauzingatii mabadiliko ya tabianchi, unazingatia tu masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, sasa tulitegemea kwamba sheria hii itakaporekebishwa, itakuja na marekebisho ambayo mfuko huu utakuwa umeongezwa *element* ya mabadiliko ya tabianchi ili tuweze kusaidia kupata rasilimali fedha za kusaidia shughuli mbalimbali za mazingira na mabadiliko ya tabianchi ambazo hivi sasa nyingi zinakwama kutokana na uchache wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie la mwisho katika suala la sekta ya maji. Kama tunavyofahamu kwamba sekta ya maji, ni sekta muhimu na zaidi ya miradi 1,000 hivi sasa inaendelea kutekelezwa katika nchi yetu na kutokana na uwasilishwaji, wenzetu wanasema kwamba ni miradi 240 tu ambayo ndiyo imekamilika na zaidi ya miradi 700 bado haijamalizika, iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri na hasa Waziri wa Fedha awapatie fedha ili miradi iweze kukamilika, kwa sababu kutokana na bajeti kuwa ndogo inaonekana wazi kwamba hii miradi inasuasua.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya. Naibu Waziri wa Maji ajiandae.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika taarifa za Kamati

zilizopo Mezani. Nami niungane na Wabunge wengine kuwapongeza Wenyeviti wote kwa uwasilishaji mzuri wa ripoti za Kamati. Nitachangia katika maeneo matatu. Kwanza ni kwenye sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana umuhimu wa sekta ya utalii katika nchi yetu, kwa maana ya kukuza uchumi wa nchi, lakini kuingizia nchi fedha za kigeni. Siyo hilo tu, katika sekta hii pia tumeona utayari wa kisiasa wa Mheshimiwa Rais, ambaye kwa yeye mwenyewe kujitolea kutoka ofisini na kwenda uwandani, katika maeneo ya vivutio, na kutengeneza filamu maarufu ya *Royal Tour* ili kutangaza Tanzania huko duniani, kuelezea tuna nini na nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa utayari huu wa Mheshimiwa Rais, kama Mkuu wa Nchi, maana yake sekta hii ni muhimu sana na inapaswa sasa wale ambao ni wasaidizi wake wahakikishe kwamba sekta hii inakua. Pia, kwa sababu sasa tunaona kuna ongezeko kubwa la watalii, maana yake nasi tuwe na mazingira ambayo tayari tumeshayaandaa kuwapokea watalii hawa.

Mheshimiwa Spika, jitihada hizi zinaenda kuongeza utalii. Hivyo, baada ya ile filamu, tutarajie baada ya miaka miwili mitatu ijayo ambayo sasa ndiyo tunaanza kuifikia hili ongezeko, litakuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, pia tutarajie kwamba mtalii huyu atakapofika, anapokwenda kwenye hiyo miundombinu iliyoko kule, iwe rafiki na imfikishe kwa urahisi ili aone kile ambacho amekiona na Mheshimiwa Rais ameitangazia dunia kwamba Tanzania tuna nini na nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa miundombinu yetu hasa kwenye hifadhi ambayo inajulikana kama hifadhi bora Barani Afrika ambayo ni hifadhi ya Serengeti na imepata tuzo miaka sita mfululizo kwamba ni hifadhi bora iliyoko barani Afrika. Barabara za kule kwa kweli ni mbovu, na nyakati za masika, kupita ni changamoto.

Mheshimiwa Spika, tunaomba na kuishauri Serikali, ilichukulie jambo hili kwa uzito kuhakikisha kwamba tunaimarisha hizi barabara hasa hii ya Serengeti na barabara nyingine zote zilizoko katika hifadhi zetu, ili hizi jitihada zilizofanywa na Mheshimiwa Rais zisiende bure, watalii hawa wakija waweze ku-*enjoy* na kuona yaliyomo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, tuhakikishe utoaji wa huduma pia uwe bora. Siyo tu utoaji wa huduma, upungufu wa malazi tuliyonao leo tuone namna gani ya kuimarisha na kuboresha na kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa vyumba vya malazi kwa ajili ya wageni kwa mwaka mzima bila kuwepo na changamoto yoyote. Kwa hiyo, huo ni ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, tulishauri mara nyingi, kwenye hizi taasisi zetu, lazima wabakiwe na fedha, kitu kinachoitwa *retention.* Hii ni kwa sababu hizi taasisi zinafanya kazi za *operation,* wakati mwingine doria mara kwa mara ni muhimu, kuliko fedha zote zikusanywe ziingie kwenye mfuko mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana baadhi ya fedha wakabakiwa nazo ili pale panapotokea na mambo ambayo yanatakiwa kufanyika kwa haraka, hizi fedha waweze kupatiwa na kubaki kufanya kazi. Kwa mfano, hawa wanaofanya *operation* wakisikia kuna ujangili umetokea mahali, hawawezi kusubiria fedha ziletwe kutoka Hazina wakapambane na ujangili mahali fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni muhimu wawe na hizi fedha. Tumesema mara nyingi na tumeshauri mara nyingi, tunaomba hili lifanyike. Hizi taasisi zetu *TANAPA,* Ngorongoro, *TAWA* na wengineo waweze kubakia na hizi fedha kwa ajili ya kufanikisha majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, pamoja na faida za kiutalii, kuna changamoto kwa upande wa wananchi. Wanyama hawa wanaenda kuvamia maeneo ya wananchi, wanaharibu,

na wananchi hawapewi fidia. Tunapongeza kwamba kuna jitihada zimefanyika, angalau wananchi wamepewa fidia.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ni vema mkaendelea kuhakikisha kwamba wananchi wale ambao tayari wako kwenye *list* ya kupewa fidia kwenye baadhi ya maeneo, kwa maana ya nchi nzima, waweze kulipwa fidia zao kutokana uharibifu walioupata kwa wanyama kuvamia kwenye mashamba yao, kuwajeruhi, wengine kufariki na vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kazi nyingine kubwa ya Wizara hii ni kulinda shoroba. Tumeona na kupitia ripoti mbalimbali huko nyuma shoroba zinaendelea kuvamiwa. Kwa hiyo, ni muhimu sana hizi shoroba zikaendelea kulindwa na kutunzwa kwa kiwango kinachotakiwa ili wanyama wanapohama kutoka eneo moja kwenda lingine, basi wahame bila kuwa na usumbufu wowote. Muda umeisha?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, kengele imeshagonga.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, atafuatiwa na Naibu Waziri wa Maji, Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote, nianze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuyafanya haya, lakini pia nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Wenyeviti wa Kamati hizi mbili kwa uwasilishaji wao mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, hata yale yaliyoandikwa humu kwa kweli yamegusa maeneo mazito ambayo wananchi wengi wangetamani kuyasikia.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea na mchango wangu, nami niungane na Watanzania wenye mapenzi mema, na wanachama wa Chama cha Mapinduzi, kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa kuwa katika kinyang'anyiro cha kugombea Urais itakapofika muda 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. John Emmanuel Nchimbi kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza. Sisi wana Nyasa, wana Ruvuma tumefurahi na kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili yake kwamba nasi sasa tunaenda kuchukua nafasi ya kuisaidia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tumefurahi kwa sababu mwanzo alikuwa Makamu wa Rais ambaye hakuwa kama Mgombea Mwenza, lakini Makamu wa Rais alitokea kule Kigoma na sasa imekuwa Magharibi, tena kule Kusini, hususan Wilaya ya Nyasa. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Dkt. Hussein Mwinyi, naye pia kwa kupata nafasi yake ya kuendelea kuwa Mgombea kwa ajili ya Urais Zanzibar. Pia siyo kwa udogo wake, nampongeza sana mzee wetu Mheshimiwa Stephen Wasira, kwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, hakika tumeona cheche zake, siku hizi chache alizokaa, anatosha, yaani kwenye Kiti ametosha na kujaa. Kweli mji bila wazee unapwaya, lakini pia mwenyewe ametuhakikishia kuwa yeye ni injini yenye uhai, nguvu na siyo bodi. Kwa hiyo, tunategemea atakisaidia Chama chetu na atamsaidia sana Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, kwanza nawapongeza hawa Mawaziri wote waliowasilishiwa taarifa kupitia Kamati zetu. Suala la mazingira limeitwa ni suala mtambuka *(cross-cutting issue)* na lipo katika kila Wizara. Linapokuwa halina chombo madhubuti cha kusimamia, kuna

maeneo tunakuwa kama hatuendi vizuri. Ndiyo maana Kamati yetu imekuwa ikisimamia sana suala hilo, na tunalizungumza wote mara kwa mara. Hadi humu maazimio yamepitishwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuweka sauti yangu ya kusisitiza, na bahati nzuri Waziri wa Wizara ya Mazingira amekuwa msikivu pamoja na Katibu wake Mkuu tulipowashauri kwenye Kamati yetu, na hivyo kuwaahidi kuleta sheria hii mapema iwezekanavyo. Tunaomba atusaidie kuwezesha hilo ili kweli chombo hicho Madhubuti kiweze kupatikana na mazingira yaweze kusimamiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tungetamani kuona sasa wataalamu wa mazingira na wenyewe wawe na bodi yao ya utaalamu kama ilivyo Bodi ya Wahandisi. Bodi mbalimbali sasa hivi zipo nchini za kusimamia utaalamu, na kwenye mazingira tungehitaji iwe hivyo.

Mheshimiwa Spika, pia tumezungumzia masuala yanayohusu maji. Hivi tunavyoenda kwenye uchaguzi, wanawake wanafurahi, wanamshukuru Mheshimiwa Rais, kwa miradi ya maji mingi ambayo imetekelezwa katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bahati mbaya miradi mingine haijaweza kutoa maji, matenki yameshajengwa, njia zake kuu za maji zimeshajengwa, nyingine ndiyo zinangoja hizo njia, lakini fedha hazipo za kutosha. Tunaomba sana fedha zipelekwe na mfuko wa maji upewe fedha zake zote ili maji yaweze kuwafikia wananchi hasa wanawake wanaoteseka kutafuta maji mbali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, kengele imeshagonga.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, mwisho namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kuwasadia watu wangu waliokufa kwa kukamatwa na mamba ili waweze kulipwa fidia.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Waziri wa Maliasili na Utalii, ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia kwenye Taarifa ya Kamati mbili. Hata hivyo, nitajikita katika Kamati ya Maji na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, vilevile nawapongeza sana Wenyeviti wote wa Kamati kwa mawasilisho mazuri, lakini hasa Mwenyekiti wa Kamati ya Maji na mazingira Jackson Kiswaga, Mbunge wa Kalenga na Makamu wake Anna Lupembe, Mbunge wa Nsimbo kwa kazi nzuri pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya Maji na Mazingira kwa kuendelea kutushauri na kutoa maoni na kuhakikisha kwamba sekta hii inaendelea kuimarika kwa maslahi mapana ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, nami niungane na Watanzania kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa kuwa Mgombea kupitia tiketi ya Chama cha Mapinduzi na Mgombea Mwenza Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi pamoja na Dkt. Hussein Mwinyi kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kuunga mkono hoja, na vilevile mapendekezo ya Kamati yetu ya Mazingira na Maji. Sisi kama Serikali tunapenda kuyatekeleza kwa kadiri ambavyo Kamati hii imeshauri.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo machache ambayo ningependa kutoa ufafanuzi kidogo. Kwa upande wa kuwezesha wakandarasi wetu wa ndani na wakandarasi wengine, Serikali

imeendelea kutoa fedha kuhakikisha kwamba wakandarasi hawa wanaendelea kulipwa.

Mheshimiwa Spika, pia wakandarasi wa ndani wameendelea kulipwa hadi kufikia 2024, tayari Serikali ilikuwa imeshapokea kiasi cha shilingi bilioni 285 kwa ajili ya kulipa wakandarasi, lakini shilingi bilioni 87 hizi zimelipwa kwa kipindi cha mwezi Januari. Katika fedha hizi, zinaendelea kuhakikisha kwamba *local content* tunaizingatia, wakandarasi wetu kuwawezeshwa ili waweze kuondokana na madeni ambayo yanawasumbua katika mabenki, kuwa na mwendelezo mzuri katika utekelezaji wa majukumu.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais. Tutakumbuka mwaka 2021 Mheshimiwa Rais wakati anaingia madarakani, upatikanaji wa huduma ya maji ulikuwa 72% kwa vijijini, na hivi tunavyoongea sasa, upatikanaji wa maji umefikia 87%.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mjini upatikanaji wa maji ulikuwa 86% hivi tunavyoongea ni 91.6%. Upatikanaji wa maji vijijini tulikuwa na vijiji takribani 9,737, hivi tunavyoongea, kuna vijiji 10,532 tayari vimefikishiwa huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba upatikanaji wa maji unaendana pia na kudhibiti namna bora ya kuhakikisha kwamba upotevu wa maji usiwe changamoto kwa Watanzania. Tunaelewa kwamba maji yanaweza yakapotea kwa watumiaji, maana yake wateja kutumia mbinu ambazo siyo salama ambazo haziruhusiwi, lakini vilevile kuna miundombinu inaweza ikasababisha upotevu wa maji, kuna miundombinu ya utunzaji wa maji ambayo inaweza ikasababisha uvujaji wa maji.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba sisi Wizara ya Maji tunakuja na mfumo wa kidijiti kuhakikisha kwamba tunaenda kudhibiti upotevu wa

maji nchini. Mfumo huu unaenda kutengenezwa na wazawa kupitia Chuo chetu cha Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfumo huu utaweza kutoa taarifa ya kwamba maji yanavuja katika eneo la tenki au katika eneo la usambazaji wa maji au katika usomaji wa dira au kuna mtu ambaye amechepusha maji ambayo yanaweza kutusababishia upotevu. Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba mfumo huu utaweza kutoa taarifa ya namna gani tunaweza kwenda kuchukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti upotevu wa maji, tunaenda kuongeza mapato kutokana na maji ambayo yanawafikia wateja. Napenda kusema kwamba Serikali tumeendelea kujipanga kuhakikisha kwamba lengo kubwa tuweze kuwa na uendelevu katika ujenzi wa miundombinu, lakini tukiwa tunadhibiti upotevu wa maji kwa sababu ni hasara kubwa kwa Taifa iwapo tutaruhusu maji yaweze kupotea.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele imegongwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba tumeshaujaribisha mfumo huu na kuna maeneo ambayo tayari tuna 33% tumeshusha mpaka 10%. Sasa tunaendelea kuhakikisha kwamba upotevu wa maji unaenda kukomeshwa kabisa katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Baada ya

kumshukuru Mwenyezi Mungu, naomba nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuzidi kuniamini na kunipa majukumu mengine ya kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, pia, nichukue fursa hii kuishukuru Kamati ya Maji na Mazingira pamoja na Kamati ya Katiba na Sheria ingawa leo ni kwa sababu tunazungumzia Kamati ya Maji na Mazingira. Naomba kipekee nimshukuru Mwenyekiti, Mheshimiwa Kiswaga na Mheshimiwa Mwakamo; Mwenyekiti Mheshimiwa Lupembe na Wajumbe mahiri kabisa wa Kamati hii ambayo nimeweza kukutana nayo kwa muda mfupi sana toka nipewe dhamana hii.

Mheshimiwa Spika, naipongeza kwa sababu kwa kweli ni Kamati ambayo inaoneka kwanza kuwa na ushirikiano mkubwa. Pia, ni Kamati ambayo ina maono sana na kutaka kuona mabadiliko ya kweli katika sekta ya mazingira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuthibitisha hayo, ni kwamba wakati nilivyokwenda kwenye kikao changu cha kwanza cha Kamati pamoja na timu yetu ya Wizara kwa ujumla wake waliweza kunipa ushauri mzuri sana na leo hapa nimedhihirisha hapa yale ambayo walikuwa wametushauri wameyarudia tena hapa na tuliwaahidi kwamba tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumewaahidi kwenye Kamati, naomba mbele yako na mbele ya Bunge hili Tukufu niwaahidi kwamba yale yote ambayo wametushauri tutayafanyia kazi kama ambavyo tumeahidi na hakuna kitu kitabadilika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa ufupi niseme yale maoni yote ambayo yametolewa leo hapa kupitia Taarifa ya Kamati na michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge ikiwemo Wajumbe wa Kamati na Wabunge wengine ni kwamba tumeyapokea na tutakwenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, katika maoni mengi yaliyotolewa hapa, yamejikita zaidi katika maeneo makubwa matatu. Naomba niyagusie kwa haraka haraka ili kuonesha kwamba kama Serikali, tumedhamiria kuweza kushughulika na hizi changamoto ambazo zimezungumzwa.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumza na Kamati imeliwasilisha, ni jinsi ambavyo wanakerwa sana na utaratibu wa mabadiliko ya sheria katika maeneo makubwa matatu. Moja, ni eneo la Baraza la Mazingira *(NEMC),* wamezungumza kwa sauti kubwa sana kuhusu umuhimu wa kutaka kulifanya Baraza letu la Mazingira *(NEMC)* kuwa mamlaka. Hii ni hoja ambayo kwa kweli imesisitizwa sana hapa leo na ni hoja ya kipaumbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo wameizungumzia sana leo na wameizungumzia kipindi chote tangu nimeanza kuielewa Kamati hii na Wabunge hapa, ni juu ya umuhimu wa kutunga Sheria ya Uchumi wa Buluu. Hoja nyingine ambayo wameizungumzia ni kuhusiana na namna ambavyo Kituo chetu cha Kaboni kitaweza kutambulika kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wamewasilisha hoja hizi mara ya kwanza, nilipokutananao nami niliwaahidi kwamba tutazichukua kama ndiyo kipaumbele changu cha kwanza. Kiukweli tumefanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tumeshaandaa mpango kazi kabambe toka siku ambayo tumetoka kwenye Kamati. Mpango kazi ule mpaka leo hii tunapozungumza hakuna kipengele hata kimoja ambacho hatujakitekeleza kama tulivyojipangia. Kwa hiyo, tunakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili, nataka nikupongeze sana wewe binafsi, kwa sababu kulikuwa kuna mabadiliko madogo ya sheria ambayo yanahusu mabadiliko ya Sheria ya Mazingira ambayo yalipangwa kuwasilishwa katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya mabadiliko haya madogo hayakuwa yamegusa kwa upana wake matarajio ya Waheshimiwa Wabunge, lakini baada ya kazi ya kuhakikisha kwamba tunafanyia kazi maoni ya Waheshimiwa Wabunge, ambayo tumeifanya kwa muda mfupi, tuliona kuna mambo mengine ni vema tukayapenyeza kabisa sasa hivi bila kukiuka taratibu za Kibunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mwongozo wako, tunakushukuru sana, na leo hii tutaweza kukaa na Kamati ya Bunge kuipitisha ili uone *seriousness* yetu kama Serikali kwamba hata yale mambo ambayo tumedhani hayahitaji kusubiri tuweze kuyawahisha kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunakushukuru sana na tunaamini kwamba mpango wetu ambao tumejiwekea na dhamira yetu kama Serikali ambayo naizungumza hapa hadharani ya kuhakikisha haya mabadiliko yote makubwa ambayo Waheshimiwa Wabunge wanayataka katika maeneo haya matatu, ikiwezekana katika Bunge lijalo bila kukiuka taratibu zozote nyingine zilizopo katika misingi ya uendeshaji wa Bunge letu na Serikali, tuweze kupitisha na kukidhi matarajio ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, naamini kwa jinsi ambavyo umetupa ushirikiano mkubwa katika kufikisha haya mabadiliko madogo na makubwa, utatusaidia kuweza kutimiza azma hiyo, kwa yale ambayo yanahusu mamlaka yako. Yanayohusu mambo ya Kiserikali tutayapeleka kwa mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla nimalizie kwa kusema kwamba, hoja hizi ni za msingi sana.

Mheshimiwa Spika, hoja za Uchumi wa Buluu, hoja za Kituo cha Kaboni, na hoja za Baraza la Mazingira *(NEMC)* kuwa mamlaka ni hoja zenye maslahi mapana ya Taifa na zitasaidia sana kuleta mabadiliko makubwa sana hususan katika sekta ya mazingira na sekta mtambuka ya Uchumi wa Buluu ambayo

inakwenda kuchangia kwa kiwango kikubwa mapato ya nchi hii na kuongeza mchango katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, watoa hoja wajiandae.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, natoa shukrani za dhati kupata nafasi hii. Niungane na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu kuendele kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupewa dhamana ya kupeperusha bendera. Tunasema hongera sana Mheshimiwa Rais umetuheshimisha duniani, tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, vilevile, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Nchimbi pamoja na Dkt. Hussein Ali Mwinyi kule Zanzibar. Sisi Watanzania tunaunga mkono hoja hizi za chama tawala na tunasema tuko bega kwa bega kupeperusha bendera yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba naungana na michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge, lakini nashukuru kwa maoni ya Kamati ikiongozwa na Mwenyekiti, Mheshimiwa Mnzava na timu nzima ya Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Wabunge wote. Michango yote tumeisikia na hii ni Serikali sikivu. Tutahakikisha tunaleta ufafanuzi kwenye *point* moja mpaka nyingine.

Mheshimiwa Spika, tumeweza kufanikiwa kuongeza idadi ya watalii. Idadi hii ya watalii imeongezeka kuzidi hata ile ambayo ilikuwepo kabla ya UVIKO 19. Sasa hivi tuna watalii milioni 5.3 wanaoingia nchini na ndiyo maana tulikuja na ile *plate number* tukasema T503 *USD.* Hapa tulitaka tuwapongeze Watanzania, kwamba unaposema utalii, dereva *tax* anahusika, anapoenda kulala, muuza vocha, anayelima kule shambani mchicha tunahitaji pamoja na matunda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni Watanzania wote milioni 62 na zaidi kwa mujibu wa idadi ya watu wameshiriki kuhakikisha idadi ya watalii inaongezeka chini ya uongozi mahiri kabisa wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tukasema tunakuja na T503 *USD* tukimaanisha tumevuka zaidi ya idadi ambayo ilikuwepo kabla ya UVIKO, lakini hata upande wa fedha, sasa hii mapato yetu, ni Dola za Kimarekani bilioni 3.9 na chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kweli yajayo ni neema tele, tunamshukuru.

Mheshimiwa Spika, watu wanapoenda kutalii nchi fulani lazima wajihakikishie amani, utulivu, na uongozi bora; watu ambao tunawapokea na kuwahudumia. Kwa hiyo, haya yote yanachangia kuleta watalii wa kutosha. Siyo hilo tu, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tumekuwa na mikutano mikubwa sana. Utalii ni pamoja na kwenda kuangalia wanyama, utalii wa malikale na sasa hivi tuna utalii wa mikutano, tunaita *conference tourism.*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na mikutano mikubwa sana ya Waheshimiwa Marais, wamekuja hapa kwenye Mkutano wa Nishati. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Hivi sasa tuna mkutano mkubwa sana wa viongozi wakubwa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na *SADC*. Hii yote ni chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, viongozi wameingia kujadili ili kutatua matatizo ya nchi mbalimbali ikiwemo *DRC*. Hii yote ni ishara kwamba Tanzania tuko imara chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na ndiyo maana tunasema mitano tena, Mheshimiwa rais wetu anastahili. Tunasema ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hivyo vigezo vyote, 2027 tutakuwa wenyeji wa Mkutano wa Apimondia. Huu ni mkutano maalumu ambapo wadau wote wa masuala ya nyuki watakuja

ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati imetupa ushauri na sisi tunashukuru.

Mheshimiwa Spika, Kamati imesema, ujenzi wa eneo la kufanyia Mkutano wa Apimondia tuukamilishe haraka. Tumelipokea na tuwahakikishie Kamati tayari eneo la ekari 48 pale Arusha limeshapatikana. Tunashirikiana na *Foreign Affairs* kumpata mkandarasi na kwa haraka sana *structure* itakwenda kuwepo mahali pale.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia utalii ni pamoja na miundombinu. Waheshimiwa wamesema na wamesisitiza, tunasema ahsante. Miundombinu ni muhimu, masuala ya barabara, na masuala ya malazi lazima tuyape kipaumbele. Chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, niseme tu kwamba *UNESCO* tayari wameshatupatia kibali cha kuridhia tujenge barabara ya tabaka gumu kutoka Nabi hadi Fort Ikoma Eneo la Ngorongoro na tutaendelea kuhakikisha miundombinu tunaizingatia.

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe tunakushukuru sana unatuheshimisha kama Rais wa *IPU*. Unapoenda kwenye mikutano ya huko unatuletea wageni wengi na hiyo sisi kwetu tuna *package* kama sehemu ya utalii na umeendelea kuwa balozi wetu mzuri sana wa utalii, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na masuala yote tutaendelea kuyafafanua, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya makazi, Mwenyekiti wa Ardhi, Maliasili na Utalii atafuatia.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nami naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge, Mawaziri wenzangu, kutoa pongeza kwa Kamati za Kudumu za Bunge ambazo zimefanya mawasilisho ya taarifa zake leo.

Mheshimiwa Spika, kipekee, napenda kutoa pongezi kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Timotheo Mnzava, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Najma Giga pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii ambao wanafanya kazi kubwa ya kukuwakilisha wewe katika kuisimamia Serikali na kusimamia sekta yetu hii ya ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba tunapokea maoni yote yaliyotolewa na Kamati. Tunapokea michango yote iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge leo humu ndani katika kuchangia Taarifa hii ya Kamati. Nami niseme kwamba, naunga mkono Taarifa hiyo ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali tutakwenda kuhakikisha tunatekeleza maazimio yote yaliyotolewa kwenye Taarifa hii ya Kamati na kuhakikisha kwamba tunaleta Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio hayo. Kama ulivyojionea wewe mwenyewe, jitihada kubwa imekuwa ikifanyika katika kuhakikisha kwamba katika Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi tunatekeleza maazimio yanayotolewa na Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, Maazimio hayo ya Bunge maana yake ni sauti za wananchi ambao wanaishauri Serikali nini kifanyike katika sekta hii. Tutaweka mkazo katika kuhakikisha mifumo inakuwa inasomana. Tunaenda kuweka mkazo katika kuhakikisha halmashauri zote 184 zinaenda kupata Mfumo wa Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, ni kilio cha muda mrefu cha kuhakikisha kwamba vijiji vyetu vyote nchini vinapimwa. Tutahakikisha tunaweka nguvu kama ambavyo Kamati imeshauri na imeelekeza.

Mheshimiwa Spika, tutaweka nguvu kupima vijiji zaidi ya 330 mara moja, kwa sababu juzi tu tumefanya kikao cha Wizara ya Fedha, sisi Wizara ya Ardhi pamoja na Kamati hii ya Kudumu ya Bunge na kuna *commitment* hiyo ya kuhakikisha kwamba tunaenda kupima vijiji hivi mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengine tutaendelea kupeana miongozo na maelekezo mbalimbali kupitia vikao mbalimbali vya Bunge na kupitia Kamati yako, nasi tuko tayari kuendelea kutekeleza maelekezo na maazimio yoyote yale ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa kupewa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Timotheo Mnzava aje ahitimishe hoja yake.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika kuhitimisha hoja yetu, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia. Takribani Wabunge 22 wamechangia hoja za leo; na katika hao Wabunge 12 wamegusa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Waheshimiwa Wabunge tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri sehemu kubwa ya michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge imeendelea kusisitiza mambo ambayo kwa ujumla wake ndiyo tumeyaweka kwenye maazimio ya Kamati. Kwa upande wa Wizara ya Maliasili na Utalii kuna mambo makubwa manne yamesemwa. Moja, ni utaratibu wa makusanyo wa taasisi zetu zile za uhifadhi, pia suala la miundombinu kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana na Waheshimiwa Wabunge na tunashukuru wenyewe wamelisema vizuri sana kwamba, shughuli za uhifadhi kwa asili yake zina namna ya tofauti kidogo. Ukisema taasisi zikae kwa kutegemea OC kutoka Serikalini, ikichelewa ni changamoto. Kwa hiyo, ndiyo maana tumeweka azimio lile na tunashukuru kwamba Waheshimiwa Wabunge wameonesha kuliunga mkono.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana na tunampongeza Mheshimiwa Rais, amefanya kazi nzuri sana. Mafanikio makubwa tunayoyaona kwenye sekta ya utalii sasa huwezi kumwondoa Mheshimiwa Rais. Tunasema huwezi kuuboresha utalii, ukaongeza watalii halafu miundombinu ikawa hai-*support* ongezeko hilo la watalii wanaoongezeka. Ndiyo maana tumesema, ni vizuri tuweke azimio hili ili kuhakikisha kwamba taasisi zetu, Wizara na Serikali kwa ujumla zinaendelea kufanya ukarabati wa miundombinu ili iendelee kufaa kwenye maeneo yetu na watalii waendelee kufurahia kutembelea maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa jambo la mazao mapya ya utalii, amesema vizuri Mheshimiwa Lulida na Mheshimiwa Waziri amesema na kwenye Taarifa pia tumeweka azimio la kuitaka Serikali kuendelea kuvigundua, lakini kuendelea kuvitangaza vivutio vyetu. Tunaamini Serikali ikitekeleza azimio hilo, mipango, ndoto na matamanio haya ya Waheshimiwa Wabunge yatakuwa yamefikiwa.

Mheshimiwa Spika, liko moja hili la hoteli limesemwa vizuri. Tumeweka azimio kwa namna tulivyoliweka na tunashukuru kwa Wabunge wameliunga mkono kwa sababu jambo hili ni la kisheria na lina taratibu zake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba tutahitaji hoteli zirudi Serikalini, lakini hatuhitaji kuiingiza nchi kwenye changamoto ya kisheria. Kwa hiyo, tunaamini likitekelezwa hili azimio kwa namna tulivyoliweka kwenye taarifa yetu tutakuwa tumeisaida Serikali, na nchi kwenye kutatua changamoto hii ya maradhi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya ardhi, jambo kubwa ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelichangia ambalo pia kwenye taarifa yetu limeoneshwa ni migogoro ya ardhi. Sisi kama Kamati tunajua suluhisho pekee la migogoro ya ardhi, moja, ni kuwa na mfumo wa ku-*manage* ardhi ya nchi yetu, kwamba leo mtu popote alipo akitaka kiwanja au eneo, anajua kwamba nikiingia hapa najua hiki ni kiwanja cha mtu au hiki hakina mtu. *Management* ya ardhi ikiwa kwenye mfumo, ni rahisi kuzuia

migogoro ya ardhi, kwa sababu ni rahisi kutotoa viwanja kwa mtu zaidi ya mmoja, lakini pia na mambo ya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la kusaidia kupunguza migogoro ya ardhi ni kwenye kupanga mipango ya matumizi ya ardhi kwenye maeneo yetu hasa kwenye maeneo ya ardhi ya vijijini. Ziko tafiti nyingi zinaonesha hivyo kwamba moja ya njia ya kutatua changamoto ya migogoro ya ardhi hasa kwenye maeneo ya vijijini ni kupanga mipango ya matumizi ya ardhi. Ndiyo maana kwenye taarifa yetu tumetilia mkazo na msisitizo sana kwenye jambo hili na tumeweka azimio na tunaamini kama Serikali ikitimiza na ikitekeleza azimio hili, itatusaidia sana kupunguza changamoto tuliyonayo kwenye migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha, naomba nitumie fursa hii kukushukuru sana wewe kwa namna unavyotuongoza kwenye Bunge lako Tukufu, na sisi wenyeviti na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kweli tunajifunza mengi sana kwako na tunanufaika sana na uongozi wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee niungane na wengine wote, mwisho lakini siyo kwa umuhimu kuendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Leo tunasherehekea mafanikio makubwa kwenye sekta ya utalii kama nilivyosema, huwezi kumtoa Mheshimiwa Rai, na ninaamini kwa hili na mengine mengi makubwa yaliyofanywa kwenye nchi yetu. Ndiyo maana Chama cha Mapinduzi kilimpitisha kwa kauli moja kuwa mgombea wa nafasi ya Urais kupitia Chama cha Mapinduzi kwenye Uchaguzi Mkuu wa Mwaka huu 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika tunampongeze Dkt. Balozi Emmanuel Nchimbi kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza wa Chama cha Mapinduzi na Dkt. Hussein Mwinyi kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa Urais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Chama cha Mapinduzi. Tunaamini kwa kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Serikali zetu viongozi hawa wanastahili kuchaguliwa tena ili kupata nafasi ya kuiongoza nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naendelea kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kupokea na kujadili taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji, wanaoafiki Hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

Wote mmeafiki. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024, yalipitishwa na Bunge kuwa Maazimio ya Bunge kwa Serikali)*

**SPIKA:** Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Mheshimiwa Jackson Kiswaga, aje ahitimishe hoja yake.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA (MWENYEKITI WA KAMATI YA MAJI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuja kuhitimisha hoja ambayo tuliileta Mezani leo mapema. Kwanza, nawashukuru Wabunge wote waliochangia. Nilikuwa nafuatilia michango, katika wachangiaji wote tangu tumeanza Kamati, Kamati yangu ya Maji na Mazingira ndiyo imepata wachangiaji wengi zaidi. Imepata jumla ya wachangiaji 15, inaonesha umuhimu wa Kamati hii ya Maji na Mazingira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mambo mengi yamezungumzwa. Kwanza nami nianze kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kupitishwa na Chama chetu cha Mapinduzi kuwa Mgombea wa Urais. Pia, mwenza wake Dkt. Nchimbi na Makamu Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Wasira pamoja na Mheshimiwa Mwinyi pale Zanzibar kwa kuwa Rais kwa kupitia CCM katika eneo lile la Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pia, nawashukuru Mawaziri wangu wawili, kwanza kwa kukubaliana na hoja za Kamati. Kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Masauni, amekuwa mgeni, ana wiki chache, lakini amekubaliana na mambo yote na ameielewa Kamati inataka nini kwa muda mfupi sana. Mheshimiwa Dkt. Masauni nakushukuru kwa kuielewa Kamati na kujua inataka nini kwa maslahi mapana zaidi ya nchi yetu ya Tanzania na mustakabali mzima wa mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna Mawaziri wawili ambao ni wasikivu sana, wenye heshima, wanyenyekevu na watii kwa Kamati. Huwa tunasigana, lakini mwisho tunaelewana na mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa nakuja kwenye hoja. Yamezungumzwa mambo mengi, lakini kwa sababu ya muda ambao tumepewa, nitakwenda kuyafupisha. Kikubwa ambacho kimezungumziwa ni ulipaji madeni kwenye miradi yetu ambayo inaendelea nchini. Wizara ya Maji inatekeleza miradi ipatayo 1,342. Kwa kipindi cha miaka miwili imetekeleza miradi hiyo. Ni miradi mingi, ukiijumlisha kwa pamoja, fedha zake zinafika shilingi trilioni na zaidi.

Mheshimiwa Spika kwa hiyo, unaweza ukaona kwamba, ni kazi kubwa ambayo inafanywa na Wizara ya Maji. Sasa, kwa miradi hii yote ni ngumu wakati mwingine kuwa na *resources* za kutosha kuweza kulipa madeni katika miradi hii yote.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, *RUWASA* peke yake kuna miradi 1,095 ambapo miradi 247 imekamilika. Kwenye miji miradi

218 na 68 imekamilika, ni miradi mingi, kwa hiyo, inahitaji fedha nyingi. Sasa, kwenye eneo hilo tunachoiomba Serikali kwa kweli, pamoja na nia nzuri ya kuendelea kuwapatia maji wananchi ni vema ikaona umuhimu na tunamwomba Waziri wetu wa Fedha, kama alivyoaminiwa na Mheshimiwa Rais kuitafutia Serikali fedha, basi hata hili eneo la maji huko tunakokwenda atutafutie fedha, ili angalau tukwamue miradi kadhaa ambayo bado haijaweza kulipiwa.

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia suala la *NEMC* kuwa mamlaka. Siyo tamaa ya Kamati, hapana. Tumejaribu kuangalia kwa mapana yake namna mazingira yanavyosimamiwa, na pia tumeangalia hata wenzetu wa nchi za jirani wanaotuzunguka, hata Zanzibar hapo.

Mheshimiwa Spika, vilevile hata matakwa, wakati mwingine ya wale ambao tunashirikiana nao, hawa ambao pengine tunawaita wafadhili, wanatamani sana kuona tuna taasisi imara zenye nguvu na wanapenda zaidi wakati mwingine kufanya kazi moja kwa moja na hizi taasisi kuliko Wizara.

Mheshimiwa Spika, tumeiona hiyo mara nyingi, kwa hiyo, tulitamani sana tuwe na hii taasisi ambayo ni imara, ambayo pia inaweza ku-*access* fedha ambazo ziko huko duniani na zipo zinatakiwa.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia kwenye kituo cha usimamizi wa biashara ya *carbon,* nacho kinatakiwa kitungiwe sheria. Kikiwa na sheria ni rahisi hata wale wanaokuja kuona, ni taasisi ambayo inaeleweka na kutambulika na Serikali. Pia, kwenye eneo la Uchumi wa Buluu, ni eneo kubwa ambalo Serikali inaweza kupata fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi yanaweza kufanyika. Kuna madini kwenye bahari kule, kuna mazao ya mwani na mengine yote na pia, kuna uvuvi kwenye bahari kuu. Kule nako tukiwa na chombo imara ambacho kinaweza

kusimamia, nchi hii tutakuwa na vyanzo vingi za kuweza kupata fedha za kukwamua shughuli zetu nyingi za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pia, tumezungumzia masuala mengine ambayo wenzangu hapa wameyasema kwenye upande wa mazingira. Tumezungumzia kushirikiana katika kupanga miji. Kwa mfano, unakuta miji inafanyiwa mpango, lakini hawaweki mpango wa kuhakikisha mabomba ya majisafi na majitaka yanapita.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukasema kwamba, ni vizuri sasa, wakati tunaweka mipango miji, wenzetu waweze kushirikiana na Wizara ya Maji, TAMISEMI na watu wa mipango miji waende pamoja, ili tusiwe na sababu wakati mwingine ya kuendelea kuharibu mipango miji na miundombinu ambayo tayari imeshawekwa. Kwa hiyo, tukasema jambo la ushirikiano ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, yapo mengi yamezungumzwa, lakini naunga mkono hoja zote ambazo zimetolewa na wenzangu, ziko nyingi. Kwa kuwa, wenzetu katika Serikali wamesema wamepokea, basi waende wakayafanyie kazi, ili tuwapatie Watanzania mazingira mazuri na pia tuwape maji kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache naomba kutoa hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji, wanaoafiki Hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira Kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

*(Hoja ilitolewa iamulilwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira Kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024 yalipitishwa na Bunge kuwa Maazimio ya Bunge kwa Serikali)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya taarifa hizi mbili za Kamati na kuwahoji yale ambayo Kamati imeyasema kwenye taarifa hizi, hakuna Mheshimiwa Mbunge au upande wa Serikali ambaye amependekeza marekebisho yoyote kwenye azimio lolote, ama kwenye mapendekezo yoyote yaliyokuwepo awali na sasa kwenye azimio lolote.

Kwa muktadha huo, taarifa hizi mbili na mambo yote yaliyoandikwa humo ndani, hasa yale ambayo yalikuwa yamesemwa na Wenyeviti kwenye zile taarifa kwamba, Bunge linaazimia, yale mwanzo yalikuwa mapendekezo sasa ni maamuzi ya Bunge na yakishakuwa maamuzi ya Bunge, kwa kuwa ni maazimio, ni maagizo kwa Serikali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, natumia fursa hii kuwashukuru sana Mawaziri ambao wamepata nafasi ya kueleza namna ambavyo wamepokea maagizo haya ambayo Bunge limeyatoa. Tunaamini kwamba, mtaenda kuyafanyia kazi kwa kadiri walivyopendekeza.

Nimeipitia taarifa zote za Kamati, lakini Kamati mojawapo imeweka na tarehe kabisa na sikusikia upande wa Serikali ukisema pengine zile tarehe zimekaa kwa sura ambayo haitawezekana. Kwa hiyo, ninaamini na yale mmeyaona na tarehe ambazo Kamati imesema mmeziona. Kwa hiyo, mkayafanyie kazi yale Maazimio ya Bunge kwa namna hiyo. Kamati imeweka ile tarehe maalum kabisa, ili iweze kuyapitia hayo kabla ya kuanza vile vikao vingine vinavyokuja.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuishukuru Serikali kwa hayo ambayo wametoa ufafanuzi hapa, nawashukuru pia kwa

ushirikiano. Hakuna taarifa ambayo Kamati imeonyesha kwamba pengine walihitaji kukutana na upande wa Serikali kwa ufafanuzi wa hoja fulani au kukubaliana jambo fulani wakapata changamoto. Kwa hiyo, nawashukuru sana upande wa Serikali kwa ushirikiano, Mawaziri na Naibu Mawaziri, tunawashukuru sana.

Wakati huo huo, nawashukuru Waheshimiwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti kwa kufanya kazi hii nzuri ya kuzisimamia Kamati hizi, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hizi. Ahsanteni sana kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya kwa niaba ya Bunge lote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa uvumilivu ambao mmeuonyesha, ahsanteni sana. Maana tumevuta sana muda, lakini wote mmekuwepo na tumeweza kufanya kazi hii kwa ukamilifu kabisa, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Sasa, nilikuwa namsikiliza hapa Mheshimiwa Mwenyekiti wa mwisho kabisa kuzungumza, Mheshimiwa Jackson Kiswaga, wakati anasema tushirikiane kupanga miji, nikawa nimesikia kama amesema kupanga mechi. Nikawa nawaza sasa mambo ya kupanga mechi tena, utakuwa mtihani. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ahsanteni sana na ninawatakia mwisho mwema wa wiki, tutaonana Jumatatu. Kwa hiyo, ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka Jumatatu, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 8.48 Mchana, Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 10 Februari, 2025, Saa Tatu Asubuhi)*